

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Arobaini na Moja – Tarehe 1 Juni, 2021**

*(Bunge Lillianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge leo ni Kikao cha Arobaini na Moja katika Mkutano wetu wa Tatu ambao unaendelea.

Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**MHE. VITA R. KAWAWA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Vita Kawawa. Kwenye Kamati hii ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Vita Kawawa ni moja ya Wabunge wakongwe kabisa kwenye Kamati ile, alikuwa Mjumbe wakati huo Mwenyekiti wa Kamati akiwa ni Mama Anna Abdallah, kwa hiyo, mpaka leo ni mzoefu kwenye Kamati ya Mambo ya Nje. Ahsante sana Mheshimiwa Vita Kawawa, tunafurahi kuwa nawe. *(Makofi/Kicheko)*

Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 341

**Maprofesa wa Kigeni Kufanya Kazi Nchini**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaboresha Sheria ya Ajira na kuweka mazingira mazuri ili maprofesa wa kigeni waweze kufanya kazi nchini?

**SPIKA:** Ahsante sana, majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, aah Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,  
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kuboresha utoaji ajira kwa wageni ilitunga Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni, Namba 1 ya mwaka 2015 pamoja na Kanuni za Kuratibu Ajira za Wageni za mwaka 2016 ili kuratibu ajira za raia wa kigeni wanaokuja kufanya kazi nchini ikiwa ni pamoja na kulinda ajira za wazawa na kuruhusu ujuzi adimu kutoka nje kuingia na kurithishwa nchini. Serikali kwa sasa inaendelea na mapitio ya sheria ili kuifanyia maboresho kwa kuzingatia mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Spika, ili kuweka mazingira mazuri ya kuruhusu uwepo wa wafanyakazi wa kigeni nchini, Serikali imeanzisha mfumo wa kielektroniki wa kushughulikia maombi ya vibali vya kazi na ukaazi kwa raia wa kigeni wanaokuja kufanya kazi nchini na mfumo husika umeanza kutumika kwa majaribio (*piloting*) kuanzia tarehe 23 Aprili, 2021. Mfumo huu utaongeza Ufanisi katika kushughulikia maombi husika.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu pia utaondoa changamoto ya upatikanaji wa taarifa unganishi za kissekta za kurahisisha upatikanaji wa vibali vya wageni wakiwemo Maprofesa kwa wakati kwa kuzingatia uhitaji.

Mheshimiwa Spika, kulingana kwa taarifa zilizopo mpaka sasa jumla ya vibali vya kazi 74 vimetolewa kwa Maprofesa na Wahadhiri wa Vyuo Vikuu nchini vikiwemo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino (*St. Augustine University*) na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph Tanzania na vinginevyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea nimekuona, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibuyake, lakini niseme tu kwamba mpaka sasa vyuo vikuu vina shida sana ya wahadhili na mfumo huo unachukua muda mrefu mno, yaani mtu anaomba kibali inachukua miezi sita na zaidi.

Ni lini watarekebisha na kuona kwamba huo mfumo unakuwa mwepesi ili tupate wahadhili wa kutosha katika vyuo vikuu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimpongeze sana Dkt. Thea Ntara ni mwakilishi wa vyuo vikuu hapa ndani ya Bunge na kwa kweli anaitendea haki sana nafasi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulitambua kwamba mifumo ambayo tulikuwa nayo nyuma ndiyo iliyokuwa ikileta matatizo na kusababisha ucheleweshaji mkubwa sana wa upataji wa vibali vya wageni. Mfumo ambao ninauzungumza ambao upo kwenye *piloting* kwa sasa ni mfumo mpya na tulipoanza kufanya majaribio kibali kina uwezo wa kutoka ndani ya siku moja ama siku mbili.

Naomba tu Mheshimiwa Mbunge awe na amani, tutausimamia vizuri mfumo hu una kuondoa tatizo la upatikanaji wa vibali kwa maprofa, wahadhili, lakini na wageni wote wanaotaka kupata vibali hapa nchini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante tunaendelea, nimekuona Mheshimiwa uliza swali la nyongeza. *(Kicheko)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, katika siku za hivi karibuni tumeshuhudia kuona wasomi, wahadhiri, maprofa wakiondoka katika taasisi za kufundisha na kuingia katika utumishi mwingine tofauti.

Je, upi umekuwa mkakati wa Serikali kama *succession plan* kwamba ikimuondoa profesa fulani mwenye uzoefu fulani katika chuo anaweza kuwa *replaced* ili kuondoa lile pengo ambalo linakuwa linajitokeza?

**SPIKA:** Waliondoka wachache sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi majibu ya swali hilo tafadhali. Wakina AG wanapoondoka huko. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Serikali na hasa kupitia Sheria za Utumishi wa Umma ipo mipango ya *succession plan* kuhakikisha kwamba ikama za utumishi wa umma zinazingatia mahitaji tuliyonayo nchini.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi, tutaendelea kusimamia mifumo tuliyoiweka ya kuzingatia na kulinda ikama ya utumishi wa umma nchini ili kuhakikisha kwamba mapungufu hayapatikani pale ambapo wataalam wanahamia katika masuala mengine ya kiutendaji. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaenda TAMISEMI Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile.

Na. 342

### **Gari la Wagonjwa Katika Kituo Cha Afya Mgololo**

**MHE. DAVID M. KIHENZILE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italeta gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Mgololo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri - TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Mgololo kilipatiwa gari la kubeba wagonjwa mwaka 2018 ambalo linalotumika kwa sasa kuhudumia wagonjwa wa dharura kwenye kituo hicho. Hata hivyo, kutokana na udogo wa gari hilo na ugumu wa jioografia ya eneo husika, gari la kubebea wagonjwa lililopo Kituo cha Afya Kasanga hutumika kuhudumia wagonjwa wa dharura inapohitajika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya uhaba wa magari ya kubebea wagonjwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi na kwa kulizingatia hilo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri imenunua gari ya wagonjwa kwa kutumia mapato yake ya ndani lenye thamani ya shilingi milioni 174.

Aidha, Halmashauri imefanya matengenezo ya magari mawili ya wagonjwa ambayo yalikuwa mabovu kwa muda mrefu na kufanya Halmashauri kuwa na jumla ya magari matano ya kubebea wagonjwa. Magari haya yanatumika kubeba wagonjwa mara tu dharura zinapotokea katika vituo vya afya vilivyopo Wilayani Mufindi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari ya wagonjwa ili kuboresha huduma za rufaa Wilayani Mufindi na nchini kwa ujumla, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kihenzile swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Mheshimiwa Naibu Waziri anisaidie kujibu, hicho kituo cha afya kipo mbali sana, kimejitenga ndio kila siku napigia kelele habari za barabara. Atuambie ni lini sasa Serikali itapatia kituo cha afya pale gari ya kubebea wagonjwa kwa sababu ipo mbali sana, ni tofauti na maeneo mengine anayosema?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI tafadhali.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kituo cha afya ambacho gari hilo linatoa huduma kipo mbali na kituo hiki ambacho kinahitaji gari lingine la nyongeza kwa ajili ya kusaidia gari dogo lililopo. Kwa kutambua hilo, Serikali imeona ni busara gari lile liwe *standby* wakati wowote kusaidia ikitokea kuna dharura pamoja na umbali wakati tunaendelea kutafuta fedha, Serikali kwa kushirikiana na wadau ili tuweze kupata gari kwa ajili ya kuhakikisha linapelekwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge jukumu ambalo limechukuliwa na Serikali ni la muda mfupi la kuondoa changamoto ya kukosa magari ya wagonjwa, lakini mpango ni kutafuta fedha na nikuhakikishie kwamba fedha zikipatikana, tukipata magari ya wagonjwa tutakupa kipaumbele katika Jimbo la Mufindi Kusini.

**SPIKA:** Bado tupo TAMISEMI, swali la Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka Adamson, uliza swali lako Mheshimiwa Mbunge wa Tabora Mjini.

Na. 343

**Miundombinu ya Barabara Iliyoharibiwa**

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukarabati barabara zilizoharibika hasa barabara za vijijini?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri bado tupo kwako.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua adha kubwa inayotokana na kuharibika kwa miundombinu ya barabara uliosababishwa na mvua nyingi zilizonyesha msimu wa mwaka 2019/2020 na msimu wa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeongeza bajeti ya matengenezo ya barabara ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (*TARURA*) kutoka shilingi bilioni 275.03 iliyotengwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 hadi shilingi bilioni 400 iliyotengwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 ambalo ni ongezeko la Shilingi bilioni 124.97 sawa na aslimia 45.4. Ongezeko hili litaiwezesha *TARURA* kufanya matengenezo ya miundombinu ilyoharibika kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti ya ujenzi na matengenezo ya barabara kadri ya upatikanaji wa fedha, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mwakasaka swali la nyongeza.



**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali; kwa kuwa tulishawahi kupata mafanikio katika kuunganisha baadhi ya shughuli za taasisi fulani kwa mfano tuliunganisha *TRL* pamoja na *RAHCO*, lakini pia kwa ufanisi kabisa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imeweza kuunganishwa.

Je, Serikali haioni sasa kwamba imefika mahali kwamba tulete mabadiliko ya sheria ambayo tutaunganisha sasa *TARURA* pamoja na *TANROADS* ili waweze kufanya kazi pamoja tuweze kuondoa hii kero ambayo hii kila siku kunakuwa na mapungufu ya fedha?

Mheshimiwa Spika, Tabora Mjini ina kata 29 na vijiji visivyopungua 41, imeathirika sana pembezoni Kata za Tambuka Reli, Ntarikwa, Uyui, Ifucha na kata nyingi za pembezoni.

Je, Serikali haioni sasa kwamba ni muda muafaka pamoja na kwamba imetenga bajeti ya nyongeza kuweza kufanya haraka kutengeneza zile barabara kwa sababu nyingine hazipitiki? Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana umeeleweka Mheshimiwa. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme dhumuni la Serikali kuanzisha Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini ilikuwa ni kuiwezesha Mamlaka hii kuwa karibu zaidi na wananchi na barabara za vijijini na mijini ili tathmini ya kina na ya haraka iweze kufanyika na kuhakikisha kwamba barabara hizi zinajengwa mapema iwezekanavyo kuliko ilivyokuwa inasimamiwa na *TANROADS* kutokana na ukubwa wa nchi na majukumu ambayo *TANROADS* ilikuwa nayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba *TARURA* inafanya kazi yake vizuri na kwa kushikirina kwa karibu sana na *TANROADS* tunaendelea kuhakikisha barabara zetu za mijini na vijijini zinapitika vizuri na changamoto ya fedha haitakuwa na suluhu kama tutaunganisha *TANROADS* na *TARURA* kwa sababu Serikali ni moja na vyanzo ni vilevile. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuhakikisha kwamba *TARURA* inafanya kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusiana na suala la barabara za Tabora Mjini; ni kweli nchini kote tumepata changamoto ya uharibifu wa barabara nyingi na nimhakikishie kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, tayari fedha zimetengwa zaidi ya mara moja na nusu ya fedha za mwaka wa fedha uliopita ili kuhakikisha kwamba fedha zile zinatumika kurekebisha miuondombinu mingi ya barabara na katika Jimbo la Tabora Mjini barabara Mama Onyango, Kilimbika, Jobodo, Mkoani, Lubatuka, Manolelo, Inala, Shule ya Msingi Jamhuri na nyingine tayari kazi za mrekebisho zinaendelea na nimhakikishie zitaendelea kufanyiwa marekebisho, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Condester.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; nilikuwa nasema kwa kuwa barabara nyingi za vijijini ambazo zinahudumiwa na *TARURA* zimeonekana kutokuwa na uteshelevu wa bajeti na angalau *TANROADS* kuonekana wana bajeti ya kutosha.

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha barabara nyingi ambazo zipo vijijini zinazochelewa kupandishwa hadhi kwenda *TANROADS* ili angalau ziweze kusaidiwa kwa sababu barabara za vijijini tunapata shida sana na bajeti ya *TARURA* ni ndogo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Nabu Waziri - TAMISEMI, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Condester Sichalwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bajeti ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Wakala wa Vijijini na Mijini imeendelea kuboreshwa mwaka hadi mwaka. Kama nilivyojibu kwenye swali la msingi katika mwaka wa fedha 2019/2020, 2020/2021 bajeti ilikuwa bilioni 275.034 lakini mwaka ujao wa fedha ni shilingi bilioni 400, ongezeko la zaidi ya shilingi bilioni 125. Jitihada hizi zote ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kuboresha uwezo wa *TARURA* kuhudumia barabara zetu za vijijini.

Mheshimiwa Spika, na naomba nichukue hoja yako, tutaendelea kufanya tathmini kwenye barabara hizo ambazo zinahitaji kusajiliwa wa *TARURA* lakini zile ambazo zinahitaji kupandishwa hadhi kwenda *TANROADS* kuna utaratibu ambao Serikali imeelekeza naomba tuufuate huo ili tuweze kupata barabara zenye hadhi hiyo na kufanyiwa matengenezo kwa wakati, ahsante.

**SPIKA:** Bado tupo TAMISEMI, Mheshimiwa Daudi Protas Venant, Mbunge wa Igalula uliza swali lako.

Na. 344

### **Ujenzi wa Barabara ya Igunga – Iyumbu Singida**

**MHE. VENANT D. PROTAS** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya Igunga – Miswaki – Loya – Migongwa – Magulyati hadi Iyumbu Singida yenye urefu wa kilometa 89?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, bado tupo TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daudi Protas Venant, Mbunge wa Jimbo la Igalula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Igunga – Miswaki – Loya – Migongwa – Magulyati hadi Iyumbu Singida ni barabara inayouganisha Wilaya za Igunga na Uyui. Kwa upande wa Wilaya ya Igunga, barabara hii inajulikana kama barabara ya Igunga – Itumba – Buhekela – Simbo na ina urefu wa kilometa 107. Kwa upande wa Wilaya ya Uyui barabara hii inaunganisha barabara tatu ambazo ni Simbo - Miswaki - Loya – Migongwa – Magulyati yenye urefu wa kilometa 72.8, hivyo kufanya urefu wa barabara ya Igunga – Miswaki – Loya – Migongwa – Magulyati hadi Iyumbu Singida kuwa na urefu wa kilometa 179.8.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 *TARURA* Halmashauri za Wilaya ya Igunga na Uyui zimetenga jumla ya shilingi milioni 361.99 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida, kilometa 27, maeneo korofi kilometa 8.7 na matengenezo maalumu kilometa tano na ujenzi unaendelea. Aidha, katika mwaka 2021/2022 *TARURA* Halmashauri za Wilaya ya Igunga na Uyui zimetenga jumla ya shilingi milioni 235 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida kilometa 35 na ujenzi wa daraja dogo (*box culvert*) mawili, makalvati mistari minne ili kuimarisha maeneo korofi ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga na kuzifanyia matengenezo barabara katika maeneo mbalimbali nchini kulingana na upatikanaji wa fedha, nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Igalula, swali la nyongeza.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, ahsante; pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, barabara hii ambayo inatoka Wilaya ya Igunga kuja Loya mpaka Magulyati ni barabara muhimu kwenye uchumi wa wananchi wa Jimbo la Igalula, lakini barabara hii ina mito zaidi ya tisa,

kwa tafiti ya mkandarasi inasema kila mto mmoja kwa kujenga *box culvert* inagharimu takribani shilingi milioni 100. Leo Waziri ananiambia ametenga milioni 200 maana ma-*box culvert* mawili tu hela itakuwa imekwisha.

Je, Serikali haioni haja ya kuitilia kipaumbele kuiongezea fedha hii barabara ili wananchi waweze kupita masaa yote? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili, barabara hii ina vigezo na imekidhi vigezo vya kupandishwa hadhi ihudumiwe na *TANROADS* kwa sababu inaunganisha Wilaya mbili ya Igunga na Halmashauri ya Wilaya ya Uyui, lakini vilevile inaunganisha na Mkoa wa Tabora na Singida. Kwa nini Serikali isipitie mchakato kuipandisha hadhi iweze kuhudumiwa na *TANROADS* ili kuepuka bajeti ndogo ya *TARURA*? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Venant Daudi Protas, Mbunge wa Igalula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa wananchi wa Igalula na barabara hii imepitiwa na mito mingi na kama ambavyo nimeongea kwenye jibu langu la msingi, Serikali imetenga zaidi ya shilingi milioni 600 katika mwaka wa fedha 2021 tunaomaliza lakini katika mwaka wa fedha unaokuja. Jumla ya shilingi milioni 600 kwa ajili ya kutambua umuhimu wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie pamoja na ma-*culvert* ambayo tumeendelea kujenga lakini tathmini itafanyika katika maeneo mengine yote ya barabara ile ambayo yanahitaji kujengewa ma-*culvert* lakini pia na

madaraja ili fedha iweze kutafutwa na iweze kutengwa kwa ajili ya kujenga madaraja hayo kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, barabara zote ambazo zinahitaji kupandishwa hadhi kwenda kuwa barabara za *TANROADS* utaratibu upo wazi unaanza katika ngazi ya Halmashauri husika *DCC* tunakwenda *RCC* na baadae unawasilisha katika Wizara za TAMISEMI na Ujenzi.

Kwa hiyo, naomba nimshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba wafuate utaratibu huo ili tuweze kuona kama inakidhi vigezo iweze kupata hadhi inayotakiwa, nashukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri mwenyewe Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Ummy Mwalimu tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini nilitaka kuongeza kwenye majibu yake kwa mara ya kwanza Serikali imesikia kilio cha Waheshimiwa Wabunge kwa sababu fedha za *TARURA* zilikuwa zinatoka katika Mfuko wa Barabara, kwa mara ya kwanza tumepata fedha shilingi bilioni 172 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu fedha hizi tumezipata haraka haraka na bajeti zilishapitishwa na Kamati za Halmashauri, kwa hiyo tumetumia maamuzi ya jumla kila Jimbo tunapeleka shilingi milioni 500 *TARURA* kwa ajili ya ujenzi wa barabara. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Halmashauri au Waheshimiwa Wabunge mtaamua milioni 500 kujenga kilometa moja ya barabara ya lami au milioni hiyo 500 kujenga kilometa 10 kupandisha barabara ya udongo kuwa ya changarawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeiweka hii chini ya uamuzi wa Mabaraza ya Madiwani kuamua milioni hii 500

kwa kila Jimbo sio kwa kila Halmashauri. Kwa hiyo, kama Halmashauri ina Majimbo matatu kila Halmashauri itapata milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Na hii ndiyo kazi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan amesikia kilio chenu Waheshimiwa Wabunge na Waziri wa Fedha ananiambia bado wanaangaliaangalia kwa hiyo mambo yanaweza yakawa mazuri zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rais Samia oyeeee.

**WABUNGE FULANI:** Oyeeee. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, angalau kila Mbunge ataondoka hapa kurudi akiwa anatoka kwenye Bajeti ya Serikali, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo.

Na. 345

### **Mgogoro Kati ya Jeshi la Magereza na Wananchi wa Ukondamayo - Urambo**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kutatua mgogoro wa mipaka kati ya Jeshi la Magereza na wananchi wa Kata ya Ukondamayo hususan Kijiji cha Tumaini, Wilayani Urambo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kukujulisha kwamba kwa sasa hakuna mgogoro wa ardhi kati ya Kata ya Ukondamoyo hususani Kijiji cha Tumaini na Gereza la Kilimo Urambo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli hapo awali ulikuwepo mgogoro baina ya vijiji vinne mojawapo Kijiji cha Tumaini. Mgogoro huo ulitatuuliwa na kuhitimishwa mwaka 2000 kwa kushirikishwa viongozi kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Ardhi, Jeshi la Magereza, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Tabora, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Urambo na Serikali ya vijiji vyote vinne vilivyokuwa na mgogoro kikiwemo Kijiji cha Tumaini.

Mheshimiwa Spika, hitimisho la mgogoro huo ni baada ya Jeshi la Magereza kukubali kutoa eneo la jumla ya ekari 3,218 kwa vijiji vilivyokuwa na mgogoro mojawapo Kijiji cha Tumaini kupewa ekari 505, Kijiji cha Imalamakoye ekari 195, Kijiji cha Nsendakanoge ekari 1,655 na Kijiji cha Itebulanda ekari 860.

Mheshimiwa Spika, aidha, hati ya makubaliano ya hitimisho la mgogoro ilisainiwa na viongozi wa vijiji vyote vinne vilivyokuwa na mgogoro kikiwemo Kijiji cha Tumaini na mawe ya mipaka (*beacons*) yakawekwa upya kwa utambulisho wa Namba Uv 66, Uv 69, Uv 107, Uv 35 na Uv 108, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mama Sitta wanasema hakuna mgogoro, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa heshima naomna niseme maneno machache kabla sijauliza maswali yangu ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha Serikali inapoacha migogoro inakua miaka na miaka na hili suala sio mara yangu ya kwanza kuuliza humu Bungeni, Mheshimiwa Masauni alipokuwa Naibu Waziri alijibu majibu ya hivyo hivyo. Kwa hiyo, naomba Wizara ikasome mafaili yake ya maswali itakuta ni hayo hayo majibu ni hayo na maswali ni hayo.



Maswali yangu ya nyongeza ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mgogoro huu umedumu tangu mwaka 1998 baada ya mipaka iliyokuwa halali kuondolewa na kupunguza maeneo ya wananchi ya kulima na kufuga mifugo yao, nini kauli ya Serikali kuhusu kumaliza mgogoro huu? Naomba Serikali itoe kauli yake lini inamaliza mgogoro uliodumu tangu mwaka 1998?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kama kweli Serikali ina nia ya kumaliza mgogoro huu ambao unawasikitisha sana wananchi wa Ukondamoyo na Tumaini, je, Waziri yupo tayari twende naye akaone yeye mwenyewe na ndiyo atakuja kuthibitisha kama kweli majibu yanayotolewa na Serikali ni ya halali? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mimi nadhani kwa kuwa Mbunge anasema kuna mgogoro, Wizara inasema hakuna mgogoro, kwa hiyo Naibu Waziri..., aah Waziri mwenyewe, haya ahsante.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu na naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge yote mawili kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kama ulivyosema kwamba majibu ya msingi ya Serikali, mgogoro unaonekana haupo, ushahidi wa namna ambavyo Magereza walitoa lile eneo na kuligawanya kwa idadi ya heka ambapo Kijiji cha Tumaini kilipata heka 505, maelezo haya yanaonekana Mbunge hakubaliani nayo, ninaomba nikuhakikishie kwamba nipo tayari baada ya Bunge kwenda nikajionee mwenyewe na kuwasikiliza wananchi, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa George Simbachawene.

Mheshimiwa Stanslaus Nyongo nimekuona, swali la nyongeza.

**MHE. STANSALUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuwa Magereza nyingi zipo katikati ya mji kwa mfano Mji wa Maswa ipo katikati ya mji na majengo na maeneo yao yanaingiliana sana na makazi ya watu na maeneo hayo yanaonekana kuwa ni *potential* hata kwa uwekezaji mwingine.

Je, ni lini Serikali itaamua basi kujenga Magereza nje ya mji kwa mfano Maswa tumeshatoa na eneo na kuwapa Magereza ili wajenge nje ya mji na kuachia maeneo ya katikati ya mji kwa ajili ya uendelezwaji wa shughuli zingine za kibiashara? Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri mwenyewe.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nyongo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa asili zamani huko kidogo maeneo haya yalikuwa pembeni ya miji, lakini kadri miji inavyokua tumejikuta sasa wakati mwingine maeneo haya ya Magereza na hata majeshi yakiwa katikati ya miji, jambo hili sio la kulijibu kwa haraka haraka kwa sababu ni mpango mkubwa unaohusisha Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Magereza au vyombo kama hivyo ambavyo vina changamoto kama hiyo.

Mheshimiwa Spika, wacha tulichukue tuone namna tunavyoweza kulifanya lakini si jambo jepesi kwa haraka kuhamisha gereza kwa mara moja na miundombinu yake, uwekezaji uliopo pale ni mkubwa lakini ni hoja ambayo kwa kweli Mheshimiwa Mbunge acha tuichukue tuitafakari.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Tuhamie Wizara ya Maji, Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni. Mbunge wa Sumve.

Na. 346

## Uhaba wa Maji Sumve

**MHE. KASALALI E. MAGENI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kupeleka maji ya Ziwa Victoria katika Jimbo la Sumve?

**SPIKA:** Majibu ya swali hili Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer* Maryprisca Mahundi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mbunge wa Sumve kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, huduma ya upatikanaji wa maji katika Wilaya ya Kwimba kwa kutegemea visima virefu ni asilimia 72 ambapo Vijiji vya Mwabaratulu, Nyashana na Sumve Mantare, Ishingisha, Mwabilanda, Nyambiti, Isunga, Kadashi na Malya vinapata huduma ya maji kutoka kwenye vituo 122 vya kuchotea maji na wateja wa majumbani ni 1,208.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali itakamilisha usanifu wa kina wa mradi wa maji kwa ajili ya kuhudumia Miji Midogo ya Malampaka, Malya na Sumve na vijiji katika maeneo hayo ambavyo huduma ya maji haitoshelezi. Usanifu huu unatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Desemba, 2021 na utekelezaji wa mradi utaanza kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru, kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa ahadi ya kuanza upembuzi yakinifu tangu mwaka wa fedha 2019/2020, 2020/2021 na leo mwaka 2021/2022 lakini upembuzi yakinifu

huu hauishi na umechukua zaidi ya miaka mitatu kwa mradi huu wa maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria kwenda kwenye Miji ya Malya, Sumve na Malampaka.

Je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuwaambia uhalisia watu wa Sumve ili wajue ni lini wanapata maji haya ya bomba kutoka Ziwa Victoria?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria yameshafika kwenye Mji wa Ngudu na Serikali imejenga pale tenki la maji la lita milioni mbili na Naibu Waziri aliwahi kutembelea tukiwa naye; na katika mradi ule usanifu unaonesha maji yanatakiwa yafike katika Jimbo la Sumve katika Kata za Lyoma, Malya, Mwagi, Nyambiti na Wala.

Je, Serikali inasema nini kuhusu kusambaza maji haya ya bomba kwenye Kata hizo za Jimbo la Sumve?

**SPIKA:** Ahsante sana, majibu ya maswali hayo mawili, Naibu Waziri wa Maji, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kasalali Emmanuel kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mradi wa maji wa Ziwa Victoria kufikia Kata ambazo zipo ndani ya Jimbo la Sumve, tayari Wizara inaendelea kuona uwezekano wa kukamilisha hilo na mara fedha itakapopatikana suala hili tunakwenda kulitimiza.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili tenki ambalo limekamilika usambazaji wa maji katika maeneo yale ya wakazi, suala hili tayari linafanyiwa kazi. Wizara tumeshaagiza mamlaka husika pale Mwanza na wataendelea kufanyia kazi kwa haraka sana kwa sababu tayari fedha nyingi ya Serikali imeshatumika, hivyo tunahitaji kuona kwamba wananchi wale wanakwenda kunufaika na kufaidi maji haya ambayo tunatarajia yatoke bombani.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum - Kagera.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naomba niulize Serikali ni lini kupitia Wizara ya Maji itapeleka maji kutoka Ziwa Victoria katika Mji wa Bihalamuro kama alivyoahidi Hayati Rais Magufuli mwaka jana akiwa anaomba kura kwa ajili ya kuwataua ndoo wakina mama? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo kutoka kwa Mheshimiwa Oliver Semuguruka, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oliver, Mbunge wa Viti Maalum, Kagera kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, maji kutoka Ziwa Victoria yanatarajiwa pia kunufaisha wakazi wa Jimbo la Biharamulo na hii binafsi nilishaenda kufanya ziara maeneo ya Biharamulo na mipango mikakati inakwenda ukingoni sasa ili tuweze kuona mwaka ujao wa fedha kadri ambavyo fedha itakuwa ikipatikana, Biharamulo nao wawe wanufaika namba moja.

Mheshimiwa Spika, nipende kumpongeza Mheshimiwa Oliver amekuwa mfuatiliaji mzuri na sisi hatutakuwa kikwazo, tutahakikisha wote ambao mnafuatilia kwa kina hii kazi ya usambazaji maji na kuleta maji kutoka Maziwa yetu Makuu ikiwa ni mpango mkakati wa Wizara kutumia Maziwa Makuu inakwenda kutimia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, bado tupo Wizara ya Maji, tumsikilize Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu. Mheshimiwa uliza swali lako.

Na. 347

**Mradi wa Maji Katika Mji wa Kakonko**

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA** aliuliza:-

(a) Je, ni kwa nini miradi ya maji katika Mji wa Kakonko kwa muda mrefu haijakamilika?

(b) Je, ni lini Mji wa Kakonko na vitongoji vyake vitapata maji safi na salama ya kutosha?

**SPIKA:** Majibu ya swali hili, Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Maryisca Mahundi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi Desemba, 2020 miradi 15 ilikuwa inatekelezwa katika Wilaya ya Kakonko ambapo miradi 14 imekamilika na inatoa huduma ya maji kwa wananchi, mradi mmoja uliobaki ni mradi wa Kakonko ambao utekelezaji wake umefikia asilimia 65 na unatarajiwa kuhudumia Mji wa Kakonko pamoja na kijiji cha Kasuga.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Kakonko unatekelezwa na *RUWASA* kwa kutumia Wataalam wake wa ndani kwa ajili ya kuukamilisha. Utekelezaji wa mradi huu unafanyika kwa awamu ambapo awamu ya kwanza ambayo inahusisha ulazaji wa bomba kilometa 35 na ujenzi wa matanki mawili yenye ujazo wa lita 500 kila moja utakamilika mwezi Desemba mwaka 2021 na kunufaisha Mji wa Kakonko pamoja na vijiji jirani vya Kasuga, Mbizi, Kanyonza pamoja na Kata ya Kiziguzigu yenye Vijiji vya Kiziguzigu, Kibingo, Kiyobera na Ruyenzi.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili itahusu kufanya upanuzi kwa kulaza mabomba urefu wa kilometa 78 kuelekea vijiji vya Njoomlote, Muganza, Kihomoka na Nyakayenzi ambapo itakamilika mwezi Juni, mwaka 2022.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali pia imepanga kujenga miradi mipya katika Vijiji vya Chilambo na Kinonko, ukarabati na utanuzi wa mradi wa Muhange kwenda Muhange Juu na Shule ya Sekondari Ndalichako pamoja na kuchimba visima virefu viwili katika Vijiji vya Chilambo na Nyakayobe.

**SPIKA:** Mheshimiwa muuliza swali tafadhali, Mheshimiwa Kamamba,

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika majibu ambayo ameyatoa ametaja mradi wa maji katika Kijiji cha Muhange ambao unapata maji kutoka Mto Mgendezo kwenda *Muhange Centre* na kwenda Muhange ya Juu. Hata hivyo mradi huu sasa maji yanayotoka hayafai kwa matumizi ya binadamu kwasababu ni machafu. Lakini vilevile mradi huu haukukamilika kama ilivyokusudiwa. Je, nini kauli ya Serikali kuhusiana na mradi huu?

Pili, kutokana na mradi wa maji na changamoto hizi ambazo nimezitaja, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufuatana nami ili akazione hizo changamoto na hatimaye kutoa suluhu ya miradi hii?

**SPIKA:** Majibu ya maswali haya mawili Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aloyce Kamamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nipende kusema nimesikitika kuona kwamba Mheshimiwa Mbunge anasema maji ni machafu na mradi haujakamilika vizuri kwa sababu swali lake la pili ni ombi la kuambatana na mimi nipende kukuhakikishia Mheshimiwa Mbunge mara baada ya Bunge hili tutakwenda pamoja na nitakwenda kujihakikishia na wakati tunaendelea kukamilisha *session* hii ya Bunge ninatoa maagizo kwa Meneja wa eneo lile aweze kuwajibika haya maji yaweze kufanyiwa *treatment* kadri ya utaalumu wetu wa Wizara ili wananchi waweze kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa.

Na. 348

### **Kukamilika kwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza:-

Je, lini Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe itakamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi wa Mkoa wa Songwe?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo na sasa nimkaribishe Waziri mwenyewe wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dkt. Dorothy Onesphoro Gwajima.

**WAZIRI WA AFYA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe kwa kujenga majengo mawili ikiwa ni Jengo la Huduma za Uchunguzi wa Maabara ambalo limefikia asilimia 98 na Jengo la Huduma za Wagonjwa wa Nje (*OPD*) ambalo ujenzi umefikia asilimia 96. Majengo haya



mawili yanatarajiwa kuanza kutoa huduma ifikapo mwezi Julai, 2021.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza ujenzi wa Jengo la Huduma za Afya ya Uzazi pale pale ambao utakamilika mwezi Februari, 2022 na kiasi cha shilingi bilioni tano kimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri ambayo yanatoa matumaini kwamba hospitali hii sasa itaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ili hospitali iweze kuanza kufanyakazi inahitaji matayarisho ya kuwa na vifaa tiba vya kutosha ikiwemo *ultrasound, x-ray* na vinginevyo vyote.

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba inapofika Julai vifaa tiba vitakuwa vimeshapatikana ili wananchi wa mkoa huu waweze kupata huduma?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa ujenzi wa majengo haya mawili ambayo ameyasema umechukua muda mrefu sana kutokana na mfumo uliokuwa unatumika wa *force account* ambao haukuleta tija sana kwa sababu ya usimamizi hafifu.

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba majengo yaliyobaki sasa wanatumia mkandarasi badala ya *force account* ili yakamilike kwa viwango vinavyokubalika?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Gwajima.

**WAZIRI WA AFYA MAENDELEO YA JAMII JINSIA WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Japhet Hasunga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa vifaa tiba hivi ikiwemo *x-ray*, *ultrasound* na vingine vyote kwa ajili ya kuhakikisha kwamba huduma zinaanza Julai napenda kumhakikishia kwamba tayari tulishapewa fedha *MSD* inaendelea na manunuzi na ufuatiliaji unafanyika na *x-ray* itakayokuja na *ultrasound* tumelenga kuelekeza kwenye hizi hospitali kubwa ambazo tayari zimeshakamilika kwa ajili ya kuanza huduma.

Mheshimiwa Spika, aidha kwa sababu swali lingine la pili la nyongeza ni kuhusu mfumo huu wa *force account* kuchukua muda mrefu ni kwa sababu gani tusihamie kwenye utaratibu wa mkandarasi. Naomba kulichukua hili nikaangalie na kabla ya Bunge hili kwisha nitafika pale mimi mwenyewe nikaone uhalisia wa kasi jinsi unavyoendelea sasa hivi kwa ajili ya kufanya maamuzi hayo ambayo ameyapendekeza, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Anastazia James Wambura, kwa niaba yake Mheshimiwa Mtenga nadhani Mheshimiwa Esther Matiko, muulizie.

Na. 349

**Kuharibika Mara Kwa Mara Barabara ya  
Kibiti - Lindi**

**MHE. ESTHER N. MATIKO K.n.y. MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

(a) Je, nini sababu ya barabara ya Kibiti – Lindi kuharibika mara kwa mara licha ya kufanyiwa ukarabati?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatiza hilo ili kuzuia ajali za mara kwa mara katika barabara hiyo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kibiti – Lindi kwa sasa inabeba magari mengi na yenye uzito mkubwa zaidi ya ilivyokusudiwa wakati wa usanifu uliotumika kujenga barabara hiyo. Hali hiyo inatokana na uwekezaji mkubwa wa viwanda na migodi katika Mikoa ya Kusini na Nyanda za Juu Kusini uliojitokeza miaka ya hivi karibuni baada ya ujenzi wa barabara hii kukamilika.

Aidha, ujenzi wa viwanda vikubwa kama cha Dangote, Mkoani Mtwara na uwepo wa migodi mikubwa ya Makaa ya Mawe, Mkoani Ruvuma kumechangia ongezeko la magari yanayobeba uzito mkubwa kuliko ilivyotarajiwa wakati barabara hii inafanyiwa usanifu.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hiyo kwa sasa, Serikali inaendelea na mpango wa ukarabati mkubwa utakaowezesha barabara hiyo kustahimili wingi na uzito wa magari kwenye barabara hii. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya shilingi milioni 7,500 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo. Aidha, pamoja na juhudi za Serikali zinazoendelea, ninaomba nitoe wito kwa wasafirishaji kutumia Bandari ya Mtwara ambayo upanuzi wake umekamilika na hivyo kuwa na uwezo wa kupokea meli nyingi na kubwa kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, kutumia bandari hii ya Mtwara itasaidia sana kupunguza usafirishaji wa mizigo mikubwa kwa njia ya barabara na hivyo kunusuru barabara hiyo kuharibika mara kwa mara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko nimekuona, uliza swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru; ni barabara nyingi sna Tanzania hii unakuta zimeharibika na zinasababisha ajali. Nilitaka kujua mpango mkakati maana yake Waziri amekiri kwamba ni kwa sababu ya malori yenye mizigo mizito yanapita yanasababisha uharibifu wa barabara.

Mheshimiwa Spika, mpango mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba barabara zinajengwa kwa kiwango cha lami ambayo itastahimili haya malori ambayo yanakuwa yanapita na mizigo mikubwa na kuharibu barabara na hivyo kusababisha ajali nyingi na kupoteza maisha ya watu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa sababu Serikali ina *project* ambayo inaendelea ya *SGR* na vitu vingine. Ni lini itakamilika sasa ili mizigo mingi iweze kusafirishwa kwa njia ya reli na siyo kutegemea barabara ili barabara ziweze kutumika kwa usafiri wa mabasi na magari mengine madogo madogo? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati wote tunapofanya *design* ya barabara tunategemea na kiasi cha mizigo itakayopita na ukubwa wa barabara. Lakini kwa sababu ya mabadiliko ya uchumi kumekuwa na mabadiliko makubwa sana ya uchumi ambayo yanapelekea magari ambayo yalikuwa yamepangiwa kupita barabara hiyo hayabadiliki na hivyo lazima tubadilishe *design* na ndiyo maana tunafanya matengenezo na tunapofanya matengenezo kwenye barabara hizi tunahakikisha tunapofanya matengenezo

ambayo sasa magari makubwa na mazito yatapita kwenye barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mkakati wa Serikali ni kufanya *rehabilitation* kubwa kwenye hizi barabara ambazo tunaamini zitachukua magari makubwa na yenye mizigo mizito.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba Serikali imekuwa ikisimamia na imeendelea kutoa fedha na ni mpango wa Serikali kuanzisha ujenzi wa *SGR* ili kunusuru barabara zetu na kuhakikisha kwamba mizigo mikubwa sasa badala ya kupita kwenye barabara ipite kwenye reli ya kisasa ambayo *SGR* na ndiyo maana tayari sasa barabara inaendelea kujengwa na fedha zinaendelea kutolewa ili kupunguza mizigo mikubwa itakayopita kwenye barabara zetu na kunusuru hizo barabara, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kusini ile tunayoita ya Kilwa-Mtwara nilizungumzia hapa ni barabara mbovu kuliko barabara nyingine zote. Sambamba na hilo tunawashukuru Serikali kwa kututengea hizo pesa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo. (*Makofi*)

Sasa swali langu ni kwamba Serikali imesema imetoa ushauri tusafirishe hiyo mizigo kwa njia ya bandari; je, meli ya mizigo kwa ajili ya kusafirisha hiyo *cement* iko tayari au lini itakuwa tayari?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi *Engineer* Godfrey Kasekenye Msongwe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Kikwete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ni kuboresha usafirishaji na ndiyo maana Bandari ya Mtwara imepanuliwa ili iweze tu si kusafirisha mizigo mikubwa lakini pia kufungua Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti na tumesema tutakuwa na ujenzi wa meli kubwa itakayokuwa inafanya pwani ya Bahari ya Hindi, lakini nilichosema kwenye jibu langu la msingi, ni kuwahamasisha wafanyabiashara wa ndani na wa nje sasa kutumia bandari yetu, kutumia meli mbalimbali za kibiashara ambapo bandari hii ya Mtwara ina uwezo wa kupokea meli kubwa na uwezo wa kushusha shehena kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge na wale ambao wanafanyabiashara; kupitia Bunge lako napenda kuwataarifu kuwa Bandari ya Mtwara sasa iko tayari kupokea mizigo mbalimbali kwa ajili ya kusafirisha hiyo mizigo na kupunguzia uzito barabara yetu ambayo sasa inaharibika mara kwa mara, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ngoja nilipeleke hili swali huko huko Kusini maana yake hii barabara imeambiwa ni mbovu sana, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri vumilia kidogo maswali. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Kuchauka tutamalizia na Mheshimiwa Nape.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa na mimi nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyojibu kwenye jibu la msingi kwamba barabara hii inaharibika sana kutokana na malori hasa ya Dangote na malori ya *gypsum*. Lakini usafirishaji kama anavyosema ni kweli Bandari ya Mtwara imeboreshwa kwa kiwango kikubwa, lakini gharama ya usafirishaji wa mzigo kutoka kwenye Bandari ya Mtwara na Bandari ya Dar es Salaam ni sawa sawa na ndiyo maana

wafanyabiasha wana *option* kusafirisha mzigo kwa barabara kuja kusafirisha kwa Bandari ya Mtwara na ndiyo maana hata mafuta watu wa mafuta wameambiwa wachukulie Mtwara, lakini bado malori ya mafuta yanatoka Tunduru, yanatoka Liwale, yanatoka Nachingwea yana *option* kuja Dar es Salaam badala ya kuchukulia Mtwara.

Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali sasa Serikali wataangalia namna yaku-*adjust* hizi bei ili iwe kivitio kwa Bandari ya Mtwara? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo:-

Kwanza majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri mwenzangu ni sahihi lakini niongezee tu kusema kwamba tumeshafanya mazungumzo ni kweli barabara imeharibika kwa sababu ya mzigo mzito wa Dangote lakini pia na tungependa pia hata korosho zisafirishwe kupitia Bandari ya Mtwara. Tumefanya ziara pale, tulikuwa na changamoto ya gharama ambayo Dangote alilalamika tumefanya *negotiation* tumekubaliana kupunguza gharama hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili wenzetu wa korosho wanasema kwamba kulikuwa hamna makontena tumewapa nafasi katika Bandari ya Mtwara ili waweze kuhifadhi korosho zao na kwa sababu hiyo tunaamini kwamba hata mazungumzo yakikamilika mzigo utapita sehemu kubwa pale. Tumeboresha Bandari ya Mtwara lakini pia na uwanja wa ndege unaboreshwa, kwa kweli barabara ile kwa namna ilivyo ikiendelea kutumika vile ilivyo watu wa Kusini wataendelea kupata gharama kubwa ya mizigo yao.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna shida kwamba hata uiharibifu wa barabara gharama yake ambayo inachangiwa

hatuwezi ku-*replace* kwa hiyo *alternative* njia nzuri ni kuhakikisha kwamba bandari ile inatumika vizuri na imeshaboreshwa tumetumia gharama kubwa zaidi, hayo mengine mazungumzo ya kiutawala itakamilika ili mizigo iweze kupita kwenye eneo hilo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nape Nnauye nilikuona

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, suala la barabara hii ya Kusini liko *serious* kuliko namna ambavyo Serikali wanafanya kulijibu hapa na niwasihi sana Serikali hayo majibu mnayoyotoa hapa si sawa; ni kuwakejeli wananchi wa Kusini. Hii barabara imeharibika sana, kuna fedha mnapeleka kwa kweli ni uhujumu wa uchumi wa watu wa Kusini. Mtakumbuka mpaka ilifikia wakati Rais Magufuli akaja akafukuza watu yaani mpaka Rais anakuja anapita anaona ubovu anafukuza watu.

Mheshimiwa Spika, kinachoendelea kwenye ukarabati ni kuongeza ubovu ndani ya ubovu yaani kwa kweli Kusini kwa sasa kumefungika.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kwamba ni lini Serikali watakuwa *serious* waache kutumia rasilimali za nchi hii kuharibu zaidi ile barabara badala yake waende kufanya jambo la kuonyesha wako *serious* na kukarabati hii barabara badala ya majibu haya mnayotoa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Waziri muachie Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Jenista Mhagama, tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimesikiliza sana, sana hoja zilizojengwa na Wabunge na hasa katika eneo la Ujenzi wa barabara hii inayokwenda huko Kusini



(Mtwara - Lindi) na inafika mpaka huko kwenye Mkoa wa Ruvuma kwa jografia yake.

Mheshimiwa Spika, na ninaendelea kukumbuka na kurejea maelezo ya Serikali na hasa viongozi wa juu ambavyo walikuwa na *concern* kubwa na barabara hiyo na hiki ambacho Waheshimiwa Wabunge wanakieleza kwa sasa ndani ya Bunge lako tukufu, ninaomba sana jambo hili tulichukue turudi ndani ya Serikali, tukafanye majadiliano na kwenda kufanya tathmini ya kina ya kujua nini kinachofanyika na hii itatusaidia kuokoa fedha za wananchi wa Tanzania walipa kodi katika kutekeleza miradi ambayo hailingani na thamani ya fedha na uhalisia unaotakiwa katika eneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hapa hatuwezi kupata nafasi ya kufanya haya majadiliano ya kina na kutoa tathimini ya uhakika naomba uridhie tulichukue Serikali na tukalifanyie kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa kauli hiyo inatia moyo tunashukuru.

Mheshimiwa Cecil vumilia tunaendelea, tunashukuru sana kwa kauli hiyo tunaamini Serikali itafanyia kazi kwa sababu visingizio vya malori ya Dangote havitoshi, kwa sababu malori haya yanavyotoka kiwandani yanapimwa kilo. Kwa hiyo, yanaingia barabarani yakiwa na uzito ambao ni *acceptable* ni kwamba barabara yenyewe ndiyo iko chini ya kiwango. *(Makofi)*

Wizara ya Fedha na Mipango swali la Mheshimiwa Jerry William Silaa. Mbunge wa Ukonga.

Na. 350

**Ucheleweshaji wa Uteuzi wa Bodi za Taasisi**

**MHE. JERRY W. SILAA** aliuliza:-

(a) Je, ni taasisi ngapi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango hadi sasa hazina Bodi au Bodi zake zimemaliza muda wake?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha benki ya waliopekuliwa ili muda wowote uteuzi ufanyike haraka kusaidia Taasisi hizo kwenda na kasi ya Mheshimiwa Rais kwani kwa sasa upekuzi imekuwa kisingizio cha kuchelewesha uteuzi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hili, Waziri wa Fedha mwenyewe, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, tafadhali.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mbunge wa Ukonga lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha na Mipango ina jumla ya Taasisi 28 ambazo inazisimamia na kati ya hizo Taasisi tisa Bodi zake zimemaliza muda wake na mapendekezo ya majina kwa ajili ya kujaza nafasi za Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi hizo yamewasilishwa kwenye Mamlaka za Upekuzi.

Mheshimiwa Spika, upekuzi kwa ajili ya kujaza nafasi mbalimbali hufanyika kwa wakati husika kutokana na ukweli kwamba utendaji na mienendo ya maafisa hubadilika kutoka wakati mmoja hadi mwingine. Hivyo, siyo sahihi kuwa na kanzidata ya upekuzi (benki ya waliopekuliwa) ili kurahisisha mchakato wa upekuzi kwa kuwa utendaji na mienendo ya maafisa hubadilika kuendana na wakati husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Silaa nimekuona.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha nimeridhika, sina swali la nyongeza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mwangozo wa Spika.

**SPIKA:** Ahsante sana haya tuanze na huo Mwangozo.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwangozo wako kwa Kanuni ya 170 naomba niisome; Mbunge anayeingia kwenye ukumbi wa Bunge au ukumbi mwingine wowote ambao Kikao cha Kamati kinafanyika au maeneo mengine yoyote ambapo shughuli za Bunge zinafanyika atawajibika kuvaa mavazi nadhifu na yenye kuifadhi heshima yake, hadhi ya Bunge na utamaduni wa nchi kama inavyoainisha katika kanuni hii.

(a) Katika mavazi ya dada zetu wanawake; vazi lolote la heshima yaani ambalo si la kubana mwili, lisiloonesha maungo ambayo kwa mila na desturi za Kitanzania hayapaswi kuoneshwa na ni refu kuvuka magoti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mwangozo wako kwa sababu Bunge ni kioo cha wananchi, kioo cha Tanzania; kuna dada zetu wanavaa nguo za ajabu ambao ni Wabunge tunaonesha nini kwenye jami?

Mheshimiwa Spika, ninaomba baadhi ya dada zetu Waheshimiwa Wabunge mavazi yao kwa kweli yanalivunja heshima Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwangozo wako.

**SPIKA:** Tunaweza tukapata mifano Mheshimiwa Amar? *(Makofi)*

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, upo.

**SPIKA:** Nakuruhusu uendelee kuniambia.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, unaniruhusu eeh?

Mheshimiwa Spika, nitakapomtaja kama utaniruhusu aje hapo itakuwa ni vizuri, unaniruhusu nimtaje? (*Kicheko*)

**SPIKA:** Nakuruhusu endelea Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, mfano kuna dada yangu niliposimama hapa, mkono wa kulia ana shati ama *t-shirt* ya njano angalia suruali aliyovaa, aje hapo, huyo ni mmoja, amevaa miwani nyeusi.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa kwa *concern* hii nikuombe Mheshimiwa ukavae vizuri zaidi halafu utajiunga nasi baadaye, ahsante sana. (*Makofi*)

*(Hapa Mbunge aliyetajwa alitoka ndani ya ukumbi wa Bunge)*

**SPIKA:** Kuna mwongozo mwingine wowote? Na nichukue nafasi hii basi kuwaambia Waheshimiwa Wabunge akinamama hasa kuwa makini sana na masuala ya mavazi na kwa hatua hii..., naomba tusikilizane.

Kwa hatua hii nawaagiza *Sergeant-At-Arms* na timu yako yote inayokaa kwenye mageti ya Bunge kuanzia sasa Mbunge yeyote ambaye amevaa mavazi yasiyo stahili mumrudishie getini huko huko. Kwa sababu hili silo lalamiko la kwanza tumepata mara kwa mara, *consistently* baadhi ya Wabunge, wengine watu wazima kidogo, lakini bado wanavaa vitu..., sijui wanatafuta nini. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tujitahidi kwa sababu ndiyo kanuni zetu jamani na hasa kwa mila zetu na desturi kwa wanawake *it is even more* kuzingatia nidhamu ya mavazi. Nawashukuruni sana. (*Makofi*)

Sasa nina wageni wengi leo kwa hiyo naomba tuvumiliane na mniazime masikio yenu. Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane na ninawaona wale mnaopiga piga makelele, naomba tusikilizane.

Naomba nitambulisha wageni tukianza na mgeni mashuhuri ambaye mwenyeji wake Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naye siyo mwingine bali ni mgeni wetu ambaye ni Balozi wa Utalii (*Tourism Goodwill Ambassador to Tanzania*) ambaye ni mchezaji mpira wa miguu maharufu duniani ambaye ni Ndugu Mamadou Sakho, ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, makofi hayatoshi naomba na mke wake asimame. *His wife if she is around*, ahsante sana. (Kicheko/Makofi)

Mamadou ni raia wa Ufaransa mwenye asili ya kutoka Mali, ni mchezaji wa mpira wa miguu kama nilivyosema maarufu duniani kuchezea timu ya Taifa ya Ufaransa, lakini amewahi kuchezea ile timu ya *PSG (Paris Saint Germany)* ya Ufaransa na timu ya Liverpool na sasa hivi anachezea *Crystal Palace* katika ligi kuu ya Uingereza na Serikali yetu imempa heshima ya kuwa balozi wetu katika masuala ya utalii wa nchi yetu. Karibu sana Mamadou, ahsante sana, karibu sana Tanzania, karibu Bungeni. Ahsante sana. (*Makofi*)

Sasa wageni wengine nilionao wageni wa Spika kutoka kwenye *gallery* kubwa ya Spika ninaanza na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Kamishna wa Polisi Salumu Hamdun. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge ni mara ya kwanza Kamishna wa TAKUKURU anafika hapa, kwa hiyo makofi hayo hayatoshi tumkaribishe Bungeni, ahsante sana, tunakupongeza sana kwa kuteuliwa kwako, tunakuhakikishia ushirikiano kutoka Bungeni, karibu sana Bungeni wewe na maafisa wako. (*Makofi*)

Amefuatana na Naibu Mkurugenzi Mkuu, Ndugu Neema Mwakalyeye, karibu sana. (*Makofi*)

Pia amefuatana na Mkurugenzi wa Huduma za Sheria Ndugu George Barasa, amefuatana na Mkurugenzi Msaidizi

wa Utawala na Rasilimali Watu, Ndugu Damas Sutta. Karibuni sana, mnaweza kukaa sasa. (*Makofi*)

Tuna wageni wengi kidogo wa Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambao ni familia yake wakiongozwa na mume wake Mhandisi Dkt. George Mulamula. (*Makofi*)

Ehe wale pale, karibuni sana, karibuni sana wanafamilia, karibuni sana Dodoma shemeji yetu Dkt. George yuko wapi? Ahsante sana, yuko kule kwenye *gallery* ya Spika, ahsante sana, karibu sana, mama ameshafika tuko naye, kwa hiyo, tukimaliza mambo hapa wewe unaweza kwenda tu (*Kicheko/Makofi*)

Wageni wengine 21 wa Mheshimiwa Balozi Mulamula, Waziri wa Mambo ya Nje ni Watendaji Wakuu wa Wizara ya Mambo ya Nje wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ya Mambo ya Nje ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki Balozi Joseph Sokoine. Balozi Joseph Sokoine, karibu sana Mheshimiwa Balozi, karibu sana. (*Makofi*)

Pia wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Balozi Mulamula ambao ni Watendaji Wakuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Dkt. Peter Mathuki, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Dkt. Peter Mathuki amewekwa upande gani? Kamera mnisaidie ku-*allocate* haraka ili tuweze kuwaona kama wapo kule. Kamera yenu ipelekeni kule zaidi na Mhandisi Steven Mlote, Naibu Katibu Mkuu, karibu sana. (*Makofi*)

Naomba watu wa kamera peleka kule kwa Mabalozizi kule badala ya kuonesha Bunge.

Sasa naanza kupitia Mabalozizi 37 ambao ni wageni wetu leo. Huyu mtu wa kamera sijui yukoje huyu!

Naanza na *Ambassador and Dean of Diplomatic Corps Comoro, Ahmada EL Badaoui Fakih*, karibu sana. (*Makofi*)

*Ambassador Malawi - Glad Munthali, Ambassador Burundi - Gervais Abayeho, Ambassador Zimbabwe - Lieutenant General (Rtd) A. N. Sanyatwe, Ambassador Cuba - Lucas Domingo Hernandez Polledo, High Commissioner Rwanda - Major General Charles Karamba, High Commissioner Pakistan - Mohammed Saleem, Ambassador Ethiopia - Yonas Yosef Sanbe, Ambassador Algeria - Ahmed Djellal, High Commissioner Namibia - Lebbius Thobias, Ambassador Turkey - Mehmet Gulluoglu, Deputy High Commissioner British - Erick Shern, Charge D'Affairs Nigeria – Bintu Ekikor, Charge D'Affairs Mozambique - Hipolito Roia, Charge D' Affairs Saharawi - Eluali Ramdan, Defense Attachee Angola - Jose Trindade, Country Representative Aga Khan Development Network - Amin Kurji, Political Counselor China - Yang Zhiyu, Minister Plenipotentiary Morocco - Lahosine Rahmouni, Minister Counselor/HOC Kenya - Justina Miriti, Counsellor and Attachee Iran - Seyed Reza, Honorary Consul Lithuania - Sheikhar Kanabar, Head of Development Cooperation Germany Embassy - Katrin Bournerman, Liaison Officer Dodoma Germany Embassy - Richard Shaba, Social Policy Specialist UNICEF - Zena Amour, UNCR-Project Control Officer UNHCR - Adele Man Ho. Guidita, Minister Counselor Cuba - Meylin Alvares, First Secretary Trade and Economics Zambia - Nombuleo Mbuli, Third Secretary Turkey - Onur Yay, Communication Specialist UNICEF - Usia Ledama, Assistant Representative UNFPA - Dkt. Majaliwa Marwa, Attaché China - Wang Haonan, Commercial Attaché Honorary Consulate of Seychelles - Paul Siniga, Financial Attaché Uganda High Commission Representative - Victoria Asea, akifuatana na Afisa wa Ubalazi wa Uganda, Jirian Laizer. (Makofi)*

Pia wapo Wawakilishi wa Mabalazi Wastaafu 10 wakiongozwa na Balozi Mstaafu Celestine Liundi, mwenyewe Celestine Liundi kwanza pale walipo Waheshimiwa Mabalazi, karibu sana, nakuona pale. (Makofi)

Yupo Balozi Mstaafu Balozi David Kapya, Balozi Begum Taj, Balozi Bertha Somi, Balozi Victoria Mwakasege, Balozi Alex Muganda, Balozi Ammy Mpungwe, Balozi Ali Karume, Balozi

Amina Ali, Balozi Mohamed Hamza na Balozi Mahadhi Maalim, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tunao Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki; Mheshimiwa Lemoyan Sebastian, Mbunge wa Afrika mashariki, nitawataja mmoja mmoja. Mheshimiwa Lemoyan Sebastian, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Maasay Simon, ahsante sana; Mheshimiwa Lugiko Elias, ahsante sana; hata wasukuma wako huko. Mheshimiwa Dkt. Abdullah Makame, ahsante; Mheshimiwa Yahya Ussi, ahsante; Mheshimiwa Nkuhi Haji, ahsante. Haya majina wameandika kidogo sio vizuri watu wangu. Mheshimiwa *Engineer* Mohamed Mnyaa, ahsante sana na Mwenyekiti wao wa Wabunge wao wa Afrika Mashariki Mheshimiwa Kimbisa Omar; ahsante sana. *(Makofi)*

Ahsanteni sana Wabunge wetu wa Afrika Mashariki, tunafarijika kuwa nanyi leo na tunaridhika na kazi ambayo mnaendelea kuifanya kule Afrika Mashariki, karibuni sana mwakani shughuli hapa kwa hiyo wale wengine muanze kutoa shikamoo kwa Waheshimiwa Wabunge mapema. Wabunge watageuka kuwa ni wajumbe wakati huo na wajumbe ni noma. *(Makofi/Kicheko)*

Pia tunao wageni wa Waziri wa Mambo ya Nje ambao ni Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo Mkurugenzi Mwendeshaji Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha - A/CC Ndugu Elishilia Kaaya, ahsante. *(Makofi)*

Yupo pia Kaimu Mkurugenzi Chuo Cha Diplomasia Balozi Dkt. Abdulrahman Kaniki, karibu; Katibu Mwendeshaji APRM Dkt. Rehema Twalib, karibu. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Nje Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk ambao ni Mtafiti Mchambuzi wa Masuala ya Uchumi, Siasa na Mahusiano ya Kimataifa na Diplomasia katika Ofisi ya Naibu Katibu Mkuu CCM Zanzibar Ndugu Mohamed Nassor, karibu sana. *(Makofi)*



Yuko Katibu Mkuu wa Asasi ya Kukuza Urafiki Kati ya Tanzania na China Ndugu Joseph Kahama, karibu sana. *(Makofi)*

Pia yupo Mkurugenzi wa Bodi ya Asasi ya Kukuza Urafiki kati ya Tanzania na China Ndugu Victoria Mwanziva *(Makofi)*

Pia kuna wanafunzi 21 kutoka Chuo cha Diplomasia - Kurasini, Dar es salaam wakiongozwa na Jeremiah Shigongo. Wanafunzi wa chuo cha Diplomasia, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wako wageni wengine watatu wa Mheshimiwa Kasalali Mageni ni ndugu zake kutoka Sumve, wageni wa Mheshimiwa Kasalali karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 41 wa Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Gekul na Mheshimiwa Atupele Fred Mwakibete wakiongozwa na Mchungaji Clement Nkita, karibuni huenda wengine wamekosekana kwenye *gallery* maana imejaa. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambaye ni Ndugu Dkt. Frank Manase, karibu. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimwa Jumanne Sagini, Ndugu Zena Munyaga na Mariam Sagini, karibuni. *(Makofi)*

Wako wageni 23 wa Mheshimiwa Jumanne Sagini ambao ni wapiga kura wake nadhani watakuwa mahali kwa sababu wataingia baada ya maswali wengine wale pale, ahsanteni na karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Jackson Kiswaga, ambao ni Ndugu Wiliam Kusga na Fred Isowe, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa 51 wa Mheshimiwa Aloyce Kamamba ambao ni wanachuo wanaosoma Chuo cha *UDOM* wakitoka Buyungu, karibuni sana. Eeh, wote mnatoka Buyungu ninyi, kweli nchi hii sasa hivi tumeendelea kielimu. *(Makofi)*

Wageni 12 wa Mheshimiwa Simon Songe ambao ni wanafunzi nane wa Chuo Kikuu cha Dodoma na wapiga kura wake wanne kutoka Jimbo la Busega, Simiyu, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa wanne wa Mheshimiwa Atupele Mwakibete karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Rashid Shangazi wakiongozwa na Rugayah Said, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 36 wa Mheshimiwa Yahaya Massare ambao ni wanafunzi wa huo cha Biblia Sanjaranda kutoka Itigi wakiongozwa na Elibariki Chima, karibuni wale kule. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimwa Boniventure Kiswaga ambao ni wananchuo Chuo Kikuu cha Dodoma wakifuatana na Lusia Nandi, karibuni popote pale mlipo. *(Makofi)*

Wageni watano wa Constantine Kanyasu ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha UDOM pia wakiongozwa Emmanuel Bwire, karibuni sana na;

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma Ndugu John Mlyambate, karibuni sana. *(Makofi)*

Sio kwa umuhimu lakini ninao wageni wa Spika ambao ni wanafunzi 83 na walimu 11 jumla yao ni 94 kutoka Shule ya Sekondari ya Mnyakongo kutoka kule Kongwa wakiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Shule nNugu James Nkini na Makamu wa Shule Jacob Malando. Wale wanafunzi kutoka Myakongo naomba msimame na walimu karibuni sana. *(Makofi)*

Jamani hawa ni watoto wangu kutoka kule Kongwa, karibuni sana watoto wetu. *(Makofi)*

Sasa tunaendelea yako matangazo mawili/matatu mengine; Katibu wa Bunge anatutangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba Maafisa kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya

Ngorongoro watakuwepo katika viwanja vya Bunge kuanzia jana hadi tarehe 4 Juni kwa ajili ya maonesho maalum ya kutoa elimu kuhusu uhifadhi na utalii. Waheshimiwa Wabunge wote pale nyuma ya ukumbi wa Msekwa wako Ngorongoro kwa ajili ya kuwapa habari za Hifadhi hiyo ya Ngorongoro, ni vizuri kufika na kuona kilichopo.

Katibu wa Bunge pia anatutangazia kwamba Maafisa kutoka Idara ya Uhamiaji wako hapa Bungeni hadi tarehe 11 Juni kwa ajili ya kutoa huduma za kupata *pass* za kusafiria nje ya nchi kwa Waheshimiwa Wabunge, huduma hiyo inatolewa katika ukumbi namba 9 *ground floor* ya jengo la utawala; palepale jengo la utawala ukiingia tu, *groud floor* pale.

Lakini pia ningependa kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa mujibu wa sheria inapotokea nafasi ya Mbunge yeyote kuwa wazi huwa ni jukumu la Spika kupeleka barua kwa Mwenyekiti wa Tume; kwa hiyo, nataka kutaarifu tu nimeshapeleka barua kwa Mwenyekiti wa Tume kuhusiana na nafasi ya kiti cha Mbunge wa Jimbo la Konde ili kuziba nafasi ya Mheshimiwa Khatib ambaye alifariki hivi karibuni.

Kwa hiyo, Tume ya Uchaguzi wanaendelea na taratibu za kuandaa uchaguzi mwingine kule Pemba wakati utakapofika kule Konde. Nawashukuruni sana.

Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA  
MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI  
KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**SPIKA:** Ahsante sana, sasa moja kwa moja nikuite Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika

Mashariki Mheshimiwa Waziri Mulamula ili uje kupitia hotuba yako kwa muda wa nusu saa. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge nawasalimia kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**WABUNGE FULANI:** Kazi lendelee.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na pia lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, aidha naomba hotuba yangu yote kama ilivyo kwenye kitabu cha bajeti iingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge yaani *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu siku ya leo. Kwa kuwa hotuba hii ya bajeti ni ya kwanza nikiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniadini na kuiteua kuongoza Wizara hii.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa nitafanya kazi kwa uwezo wangu wote na kwa kudra za Mwenyezi Mungu nitatekeleza majukumu yangu ipasavyo katika kuleta maendeleo ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba tarehe 17 Machi, 2021 Taifa lilipata msiba mzito wa kuondokewa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Taifa letu limepoteza viongozi wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Balozi Mhandisi John William Hebert Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kuungana na Waheshimiwa Mawaziri wenzangu waliotangulia kuwasilisha hotuba zao kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais, familia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa ujumla kwa misiba hii mizito. Wizara yangu inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa viongozi hawa katika kukuza kidiplomasia yetu.

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii pia kutoa shukrani za dhati kwa nchi marafiki na jumuiya ya kimataifa kwa kuonesha mshikamano, kutufariji na kushiriki nasi katika kipindi cha majonzi makubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba kutoa shukrani kwa Umoja wa Mataifa kwa uamuzi wake wa kuitisha kikao rasmi cha Baraza Kuu la Umoja huo kwa ajili ya kumuenzi na kumkumbuka Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kupitia kikao hicho nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa zilielezea mafanikio makubwa ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yaliyopatikana chini ya Uongozi wa Hayati Dkt. Magufuli katika kuboresha huduma za jamii kama vile elimu, maji, afya, nishati na miundombinu ya usafirishaji. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba kutoa pole kwako na Bunge lako Tukufu kufuatia vifo vya Waheshimiwa Khatib Said Haji aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde, Mhandisi Atashasta Justus Nditiye aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambwe Mkoa wa Kigoma, na Martha Jachi Umbulla

aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara, Mwenyezi Mungu azipumzishe roho za marehemu mahala pema.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa na kwa moyo mkunjufu napenda kutumia nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge kwa kuaminiwa na kuendelea kushika nafasi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, nampongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman Sharif kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna imani kuwa uongozi mpya utaendelea kudumisha tunu za Taifa na kuimarisha diplomasia nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeweka historia ya kujivunia na kuigwa duniani kwa namna ilivyopata uongozi mpya wa juu wa Serikali na kuzingatiwa misingi ya Katiba kufuatia vifo vya viongozi wakuu waliokuwa madarakani. Hatua hii ni kielelezo cha ukomavu, uimara wa demokrasia na kuzingatiwa misingi ya utawala wa sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumpongeza tena Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake aliyowasilisha hapa Bungeni ambayo imetoa dira na mwongozo wa utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Nawapongeza

pia Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walionitangulia kuwasilisha hotuba zao katika Bunge hili la Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa uongozi wako madhubuti katika uendeshaji wa shughuli za Bunge. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson - Mbunge na Naibu Spika; Wenyeviti wa Bunge na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi nzuri wanazozifanya kukusaidia kusimamia na kuendesha shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee tena napenda kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu - Mbunge, pamoja na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo - Mbunge, kwa kazi nzuri na ya kizalendo ya kuishauri Serikali hususan Wizara yangu. Naomba nikiri kuwa miongozo na ushauri wao katika masuala mbalimbali umekuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwapongeza Waheshimiwa Eliadory Felix Kavejuru na Dkt. Florence George Samizi kwa kuchaguliwa hivi karibuni kuwa Wabunge wa Majimbo ya Buhigwe na Muhambwe, mtawalia. *(Makofi)*

Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa kuaminiwa kuwawakilisha wananchi katika Bunge hili Tukufu. Vilevile nitumie nafasi hii kuwapongeza viongozi wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa mbalimbali Serikalini. Kuteuliwa kwao ni kielelezo cha kuaminiwa na Mheshimiwa Rais katika kuwaletea maendeleo wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, historia ya nchi yetu imesheheni misingi imara inayoiwezesha kuendelea kuwa miongoni mwa nchi zilizo na ushawishi mkubwa kimataifa tangu Uhuru. Misingi ya nchi yetu iliyopelekea kuheshimika kimataifa iliwekwa na Waasisi wa Taifa letu kwa kupinga na kulaani ubabe, uonevu

na ukandamizaji popote pale ulipotokea duniani bila hofu. Hivyo katika kusimamia misingi hiyo, tumeendelea kulinda uhuru wetu; kujiamulia mambo yetu wenyewe bila kuingiliwa; kulinda mipaka ya nchi yetu; kutetea haki; kuimarisha ujirani mwema; na kutekeleza Sera ya Kutofungamana na Upande Wowote kama dira na msimamo wetu kwenye uhusiano na nchi nyingine katika jumuiya ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hali ya siasa, ulinzi na usalama imeendelea kuimarika katika maeneo mengi Barani Afrika. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 nchi za Benin, Burkina Faso, Côte d'Ivoire, Chad, Ghana, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Niger, Shelisheli, Guinea, Uganda na Jamhuri ya Kongo zilifanya uchaguzi. Tunawapongeza Waheshimiwa Marais wa nchi hizo kwa kuchaguliwa na tunaahidi kuendelea kushirikiana na Serikali zao kwa lengo la kudumisha uhusiano baina ya nchi zetu. Taarifa ya kina inapatikana kwenye aya ya 20 hadi 35 katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara yangu iliendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyo ainishwa katika muundo wa Wizara toleo la 7 la tarehe 7 Julai, 2018. Majukumu hayo yameainishwa kwenye aya 36 katika kitabu cha hotuba yangu ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara uliongozwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi; Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001; pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025; na Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na miongozi mingine kama ilivyoainishwa kwenye aya ya 37 katika kitabu cha hotuba yangu ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ilipanga kukusanya shilingi 2,550,879,000. Kati ya kiasi hicho shilingi 47,170,000 ni makusanyo ya Makao Makuu ya Wizara na shilingi 2,503,709,000 ni makusanyo kutoka Balozi za Tanzania. Vyanzo vya mapato hayo ni uhakiki wa nyaraka,



pango la majengo ya Serikali nje ya nchi na mauzo ya nyaraka za zabuni.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili 2021, Wizara ilikusanya jumla ya Shilingi milioni 756,182,081.71 sawa na asilimia 29.6 ya lengo lililopangwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kupungua kwa mapato hayo kumetokana na kukosekana kwa wapangaji katika baadhi ya majengo ya Serikali kwenye Balozi za Tanzania kutokana na athari za uwepo wa janga la UVIKO-19 ambayo imesababisha kukosa wapangaji kutokana na kutokuweko kwa biashara.

Mheshimiwa Spika, katika kuiwezesha Wizara kutekeleza malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha shilingi 199,750,684,000 kati ya fedha hizo, shilingi 179,750,684,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 20,000,000,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, shilingi 167,717,723,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 12,032,961,000 ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 Wizara ilipokea kutoka Hazina kiasi cha shilingi 127,648,549,514 kiasi hicho cha fedha ni sawa na asilimia 63.9 ya fedha zote za bajeti zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2020/2021. Kati ya fedha hizo, shilingi 118,893,319,946 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 70.9 na shilingi 8,755,299,568.18 ni kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 72.8.

Mheshimiwa Spika, katika fedha zilizotolewa Wizara ilitumia kiasi cha shilingi 106,601,250,300 sawa na asilimia 83.5 ya fedha zilizopokelewa. Kati ya fedha hizo, shilingi 97,846,020,731.93 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 8,755,229,568.18 ni mishahara.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nitumie fursa hii ili kueleza kwa kifupi mapitio ya utekelezaji na majukumu ya

Wizara katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwezi Mei, 2021 Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya Kitaifa ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Kenya kufuatia mwaliko wa Mheshimiwa Uhuru Muigai Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ziara hiyo ya kwanza ya Kitaifa tangu kuapishwa kwa Mheshimiwa Rais lilenga kuimarisha uhusiano wa kidugu na ujirani mwema kati ya nchi hizi mbili. Wakati wa ziara hiyo, Mheshimiwa Rais alihutubia kikao maalum cha pamoja cha Bunge la Taifa na Bunge la Seneti la Kenya na kukutana na wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwezi Aprili mwaka huu pia Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan nchini Uganda. Wakati wa ziara hiyo Mheshimiwa Rais na mwenyeji wake Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda, walishuhudia uwekaji saina mikataba mitatu ya utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Tanga. Mikataba iliyosainiwa imeainishwa kwenye aya ya 50 katika kitabu cha hotuba yangu ya bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwezi Januari, 2021 Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Filipe Jacinto Nyusi, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji hapa nchini kwa mwaliko wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Katika ziara hiyo, viongozi hao walikubaliana kuimarisha ushirikiano baina ya nchi hizi mbili na kukuza kiwango cha biashara na uwekezaji pamoja na kuimarisha ujirani mwema.

Mheshimiwa Spika, mwezi Januari, 2021 Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Sahle-Work Zewde, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia iliyofanyika nchini. Tanzania na Ethiopia zilikubaliana kuongeza kiwango cha biashara na uwekezaji, na

kubadilishana utaalum na uzoefu katika uendeshaji wa viwanda vya kuongeza thamani ya ngozi za mifugo na Tanzania kuisaidia Ethiopia kufundisha lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Addis Ababa na Chuo cha Diplomasia cha Ethiopia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba, 2020 Wizara iliratibu ziara rasmi ya Mheshimiwa Dkt. Lazarus Chakwera, Rais wa Jamhuri ya Malawi iliyofanyika nchini. Katika ziara hiyo pamoja na mambo mengine, Tanzania na Malawi zilikubaliana kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Huduma kwa Pamoja Mpakani cha Songwe/Kasumulu na ujenzi wa barabara ya Mpemba - Isongole - Mbozi Chitipa - Mbilima; na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania kufungua ofisi nchini Malawi. Nchi hizi pia zilikubaliana kushirikiana katika utekelezaji wa miradi ya mipango ya kufua umeme na umwagiliaji katika Bonde la Mto Songwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba, 2020 Wizara iliratibu ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda iliyofanyika nchini. Katika ziara hiyo, Tanzania na Uganda zilisaini hati ya makubaliano kuanza ujenzi wa mradi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Tanga. Maelezo ya kina ni kama inavyoonekana kwenye aya ya 46 hadi 60 katika kitabu cha hotuba ya bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwezi Januari, 2021 Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Wang Yi, Mjumbe wa Baraza la Taifa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Watu wa China, iliyofanyika hapa nchini. Pamoja na masuala mengine, Serikali ya nchi hiyo ilitoa msaada wa shilingi milioni 350 kwa ajili ya kununua vifaa vya karakana ya fani ya uvuvi katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi VETA, huko Chato na mwezi Mei, 2021 imetoa msaada wa shilingi bilioni 35.37 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba, 2020 Wizara ilifanikisha kusainiwa kwa mkataba kati ya Tanzania na China

utakaowezesha Tanzania kuuza maharage aina ya soya katika soko la China. Kupitia mkataba huo, Tanzania inakuwa nchi ya 12 kuruhusiwa kuuza maharage hayo ambayo yana soko kubwa nchini humo. Kampuni 49 za Tanzania zimepata vibali vya kuuza maharage hayo katika soko hilo. Hadi kufikia mwezi Mei, 2021 zaidi ya tani 120 za soya zimekwisha kuuzwa chini ya mpango huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu na kufanikisha upatikanaji wa Kampuni ya PT Indesso ya nchini Indonesia iliyojenga kiwanda cha kutengeneza mafuta yatokanayo na majani ya mimea katika eneo la Mgelema, Pemba kwa kushirikiana na Shirika la Taifa la Biashara la Zanzibar kwa gharama ya dola za Marekani milioni 1.4. Kiwanda hicho kilizinduliwa mwezi Septemba, 2020 na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein aliyekuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Maelezo ya kina ni kama inavyoonekana kwenye aya ya 62 hadi 72 katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, kufuatia utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi, Wizara imefanikisha Tanzania kuruhusiwa kuingiza nyama na bidhaa za nyama katika masoko ya nchi za Oman, Kuwait na Qatar. Naomba Waheshimiwa Wabunge msikilize. *(Makofi)*

Vilevile bidhaa hizo zitaanza kuuzwa nchini Saudi Arabia baada ya kukamilika kwa taratibu za kupata ithibati kutoka kwenye mamlaka za nchi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, mwezi Januari 2021, Wizara ilifanikisha upatikanaji wa vibali kwa kampuni nane za Tanzania kuuza minofu ya samaki aina ya sangara katika nchi ya Saudi Arabia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwezi Januari, 2021 Wizara ilifanikisha uwekaji saini hati ya makubaliano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mamlaka ya Uwekezaji ya Oman kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Mangapwani, Zanzibar. Mradi huo utajumuisha ujenzi wa eneo la kuhudumia mizigo;

gati la meli za uvuvi; gati la meli za mafuta na gesi; chelezo kwa ajili ya matengenezo ya meli; na mji wa kisasa katika eneo la Mangapwani. Mradi utakapokamilika utachochea ukuaji wa biashara na usafirishaji Zanzibar. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwezi Agosti, 2020 Wizara ilifanikisha kusainiwa kwa mkataba wa mkopo wa dola za Marekani milioni 15.3 kutoka kwenye Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait kwa ajili ya mradi wa kilimo cha umwagiliaji kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 3,000 katika Bonde la Mto Luiche, mkoani Kigoma. Mradi huo utaongeza uzalishaji wa mazao ya mpunga, mahindi na mbogamboga na hivyo kuinua kipato cha wakulima wa eneo hilo. Maeneo ya kina ni kama inavyooneshwa kwenye aya ya 73 hadi 81 katika kitabu changu cha bajeti. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwezi Februari, 2021 Wizara iliratibu uwekaji saini Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Kampuni ya *Tangen & Intertorco Group* ya nchini Hispania kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri, Unguja na Bandari ya Mkoani, Pemba; na mradi wa kufua umeme kwa kutumia gesi. Hafla ya uwekaji saini makubaliano hayo ilishuhudiwa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwezi Desemba, 2020 Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 111 wa Baraza la Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya *OACPS* uliofanyika kwa njia ya mtandao chini ya Uenyekiti wa Tanzania. Kupitia Mkutano huo, Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi 10 za Jumuiya hiyo zitakazonufaika na utekelezaji wa mradi wa kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao ya samaki ujulikanao kama *FISH4ACP* unaogharimu shilingi bilioni 110. Katika mradi huo Tanzania imetengewa kiasi cha shilingi bilioni nane kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao ya samaki aina ya migebuka na dagaa kutoka mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba, 2020 Wizara iliratibu na kufanikisha kusainiwa kwa mkataba kati ya Tanzania na Uswiss wa msaada wa shilingi bilioni 39.15 kugharamia utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini nchini na mkataba wa shilingi bilioni 4.95 ikiwa ni msaada wa kuchangia Mfuko wa Pamoja wa Afya. Pia Wizara iliratibu kusainiwa kwa mkataba kati ya Tanzania na Uswiss wa shilingi bilioni 15.8 ikiwa ni msaada kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kitaifa ya Kutokomeza Malaria Awamu ya Kwanza; na Mkataba wa shilingi bilioni 24.76 ikiwa ni msaada kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kuimarisha Mfumo wa Kutoa Huduma za Afya Awamu ya Tatu. Misaada hiyo imeendelea kuchangia jitihada za Serikali katika kupunguza umaskini na kuboresha huduma za afya. Maelezo zaidi yanapatikana katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika kuratibu masuala ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, mwezi Februari, 2021 Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 21 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika kwa njia ya mtandao. Katika Mkutano huo, Wakuu wa Nchi waliidhinisha lugha za Kiswahili na Kifaransa kutumika rasmi kwenye shughuli za Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 Tanzania ilitoa vyeti 37,111 vya uasilili wa bidhaa kwa wafanyabiashara wadogo wadogo wa Tanzania wanaofanya biashara katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vyeti hivyo vimewasaidia wafanyabiashara kupata unafuu wa kodi kwa kutolipa ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazozalishwa nchini na zinazokidhi vigezo vya uasilili wa bidhaa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika maandalizi ya Rasimu ya Katiba ya Fungamano la Kisiasa la Afrika Mashariki kama hatua ya mpito kuelekea Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 zoezi la kukusanya maoni na kutoa elimu

kwa Umma limefanyika katika nchi za Burundi na Uganda. Timu ya wataalam ya Jumuiya inayokusanya maoni kuhusiana na rasimu ya katiba hiyo itatembelea Tanzania mwezi Agosti, 2021. Maelezo ya kina yanapatikana kwenye hotuba yangu ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika; mwezi Aprili, 2021 Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa nchi na Serikali wa Troika Mbili wa SADC uliofanyika Jijini Maputo, Msumbiji. Katika Mkutano huo, nchi wanachama zilizimia kuendelea kushirikiana kuimarisha hali ya ulinzi na usalama kaskazini mwa Msumbiji, hususan kwenye Jimbo la Cabo Delgado.

Mheshimiwa Spika, mwezi Machi, 2021 Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa SADC uliofanyika kwa njia ya mtandao. Pamoja na masuala mengine, mkutano huo uliridhia kuongeza wigo wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mikutano ya kisekta ya SADC. Maelezo ya kina yanapatikana katika hotuba yangu ya bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Umoja wa Afrika; mwezi Februari, 2021 Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 34 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika kwa njia ya mtandao. Mkutano huo uliridhia ombi la Tanzania la kujumuisha lugha ya Kiswahili na uanzishaji wa Kituo cha Urithi wa Afrika - jijini Dar es Salaam katika programu ya kutekeleza kaulimbiu ya mwaka 2021 inayosema; "Sanaa, Tamaduni na Urithi katika kufikia Azma ya Afrika Tuitakayo."

Mheshimiwa Spika, maamuzi hayo yamejumuishwa kwenye shughuli za programu hiyo zinazotekelezwa na Umoja wa Afrika katika mwaka 2021. Maelezo zaidi yanapatikana katika hotuba yangu ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa kimataifa; Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Kikao cha 46 cha Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa kilichofanyika

mwezi Machi, 2021. Katika Kikao hicho, Tanzania ilipata fursa ya kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa haki za binadamu nchini ikiwa ni pamoja na hatua zilizofikiwa katika kutoa haki ya elimu, huduma za afya, maji safi na salama pamoja na nishati.

Mheshimiwa Spika, Tanzania pia ilitumia kikao hicho kuielezea jumuiya ya kimataifa kuhusu Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba, 2020 ambao kwa mara ya kwanza katika historia ya Taifa letu uligharamiwa kwa fedha za ndani; na kuwa uchaguzi huo ulikuwa wa haki, huru na wazi uliozingatia misingi ya demokrasia na utawala bora, na ulifanyika katika mazingira ya amani na utulivu. Hatua hizi zimesaidia kujenga mtazamo chanya kwa jumuiya ya kimataifa kuhusu Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Kikao cha 75 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kilichofanyika kuanzia mwezi Septemba hadi Desemba, 2020. Tanzania ilitumia fursa hiyo kuieleza jumuiya ya kimataifa kuhusu hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha huduma za kijamii na kutengeneza fursa za kiuchumi kwa kuimarisha miundombinu ya reli, barabara, maji, nishati, afya na elimu.

Mheshimiwa Spika, vilevile Tanzania ilieleza kuhusu hatua zinazochukuliwa katika kupambana na rushwa na ubadhirifu wa mali za umma; kusimamia nidhamu kwenye utumishi wa umma; na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Maelezo ya kina yanapatikana katika hotuba yangu ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara iliratibu na kushiriki katika majadiliano na kusimamia uwekaji saini mikataba na hati za makubaliano mbalimbali ya Kimataifa kama ilivyoainishwa kwenye aya ya 165 hadi 166 katika kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mahusiano ya Tanzania na nchi nyingine, Wizara imeendelea kuandaa na



kuratibu ziara mbalimbali za viongozi wakuu wa Kitaifa nje ya nchi. Aidha, Wizara imeratibu na kufanikisha ziara za viongozi wa mataifa mbalimbali na mashirika ya kimataifa waliokuja Tanzania kwa ziara rasmi kushiriki katika mikutano, makongamano na kutekeleza majukumu mbalimbali ya Kitaifa. Maelezo ya kina yanapatikana kwenye aya ya 167 hadi 178 katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee sasa uratibu wa Watanzania wanaoishi nje ya nchi (*diaspora*); Wizara imeendelea kuratibu masuala yanayohusu jamii za *diaspora* ili kuongeza mchango wao katika maendeleo ya Taifa. Kupitia jukumu hili Tanzania imeendelea kunufaika na *diaspora* ambapo kwa mujibu wa Benki Kuu ya Tanzania fedha zilizotumwa na *diaspora* nchini kwa mwaka 2020 zilikuwa ni dola za Marekani milioni 189.13. Vilevile katika kipindi hiki *diaspora* wamenunua nyumba kupitia Shirika la Nyumba la Taifa zenye thamani ya shilingi milioni 423.8.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa za ajira, elimu, biashara, uwekezaji na utalii zitokanazo na uanachama wa Tanzania katika Jumuiya za Kikanda...

**SPIKA:** Bado dakika tano.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

...na Kimataifa pamoja na mahusiano na nchi nyingine. Fursa hizo hutangazwa kupitia vyombo mbalimbali vya habari kama inavyoonekana kwenye kitabu changu cha bajeti.

Mheshimiwa Spika, utawala na maendeleo ya watumishi; Wizara imeendelea kusimamia masuala ya utawala na maendeleo ya watumishi kwa lengo la kuboresha na kuimarisha utendaji wa kazi. Wizara ina jumla ya watumishi 455 wa kada mbalimbali; kati yao watumishi 228 wapo Makao

Makuu ya Wizara na watumishi 227 wapo kwenye Balozi za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika utoaji wa mafunzo na upandishaji vyeo, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake ambapo jumla ya watumishi 219 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani mbalimbali ndani na nje ya nchi. Watumishi wanane walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 211 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi. Maelezo zaidi yanapatikana katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Wizara na taasisi zilizo chini yake katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ilitengewa bajeti ya maendeleo ya shilingi 20,000,000,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo iliyopo ndani na nje ya nchi. Wizara inaendelea kufuatilia utekelezaji huo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya taasisi zilizo chini ya Wizara; katika kipindi hiki, Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha kimeendelea kuendesha biashara ya mikutano; upangishaji wa nyumba na ofisi; na kutoa huduma ya afya kupitia hospitali inayomilikiwa na kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Chuo cha Diplomasia pia kimeendelea na mafunzo na kutoa mafunzo ya Lugha saba za kigeni ambazo ni Kiarabu, Kifaransa, Kihispania, Kiingereza, Kichina, Kikorea na Kireno.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora ulifanya tathmini kuhusu utawala bora nchini na kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa *APRM* nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha 30 cha wakuu wa nchi na Serikali zinazoshiriki Mpango wa *APRM*, kilichofanyika mwezi Machi, 2021 kwa njia ya mtandao kilimteua Mheshimiwa Balozi Ombeni Yohana Sefue, Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu kuwa Mwenyekiti wa Jopo la Watu

Mashuhuri wa *APRM*, Barani Afrika. Tunapenda kumpongeza Mheshimiwa Sefue kwa uteuzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla hujaniondoa hapa, naomba nitumie fursa hii kuzishukuru Balozi, Mashirika ya Kimataifa na taasisi za kikanda, kimataifa na washirika wa maendeleo kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa kufanikisha mipango mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nazitambue nchi za Algeria, Australia, Austria, Brazil, Jamhuri ya Korea, Poland, Romania, Saudi Arabia, Singapore, Uganda na nyingine zote, pamoja na Mashirika ya Kimataifa yakiwemo *ACBF, AfDB, AU, FAO, GiZ, UN, UNAIDS, USAID, UNCTAD, UNEP, UNESCO, UNFPA, UNICEF, INIDO, UNWOMEN, WHO* na *WFP* na mengine mengi, pamoja na Benki ya Dunia; *Bill* na *Melinda Gates, Global Fund, Investment Climate Facility for Africa* na *Red Cross*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa moyo mkunjufu, napenda niwashukuru watendaji na watumishi wa Wizara na taasisi zake kwa kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ipasavyo. Kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Balozi Joseph Edward Sokoine, Katibu Mkuu; Balozi Fatma Mohammed Rajab, Naibu Katibu Mkuu; Waheshimiwa Mabalazi wa Tanzania; Wakuu wa Idara na Vitengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuwashukuru Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Kabudi, aliyekuwa Waziri; Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro na Mheshimiwa William Tate Olenasha waliokuwa Naibu Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya pekee kabisa, napenda kumshukuru mume wangu mpendwa Mhandisi Dkt. George Steven Mulamula; watoto wangu pamoja na familia

yangu yote kwa ujumla kwa uvumilivu wao na kuwa karibu nami wakati wote wa kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ni malengo ya Wizara ambayo yameainishwa kwenye kitabu changu cha bajeti ambayo ni kuendelea kutekeleza diplomasia ya uchumi na kuendelea kuboresha mahusiano mazuri na nchi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika malengo hayo naoba niseme kwamba kuna mpango mkakati wa Chuo cha Diplomasia, *AICC, APRM* ambayo yote yameainishwa kwenye kitabu changu cha hotuba ya bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba uniruhusu niseme kwamba katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 Wizara Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 2,550,879,000 ikiwa ni mapato ya Serikali yatakayopatikana kutokana na vyanzo vilivyopo Makao Makuu ya Wizara na Balozi za Tanzania ambavyo ni pango la nyumba za Serikali zilizopo nje ya nchi na kuthibitisha nyaraka.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara imetengewa bajeti ya kiasi cha shilingi 192,265,438,000. Kati ya fedha hizo shilingi 178,765,438,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida zinazojumuisha shilingi 167,937,219,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo; shilingi 10,828,219,000 kwa ajili ya mishahara; na shilingi 13,500,000,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe jumla ya shilingi 192,265,438,000. Kati ya fedha hizo shilingi 178,765,438,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 13,500,000,000 ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii adhimu kukushukuru tena wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja; kazi iendelee.  
(Makofi)

**HOTUBA YA MHESHIMIWA BALOZI LIBERATA RUTAGERUKA  
MULAMULA (MB), WAZIRI WA MAMBO YA NHE NA  
USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI AKIWASILISHA BUNGENI  
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA  
MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## 1.0 UTANGULIZI

1. *Mheshimiwa Spika*, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na pia lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

2. *Mheshimiwa Spika*, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu siku ya leo. Kwa kuwa Hotuba hii ya Bajeti ni ya kwanza nikiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniadini na kunitaua kuongoza Wizara hii. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa nitafanya kazi kwa uwezo wangu wote na kwa kudra za Mwenyezi Mungu nitatekeleza majukumu yangu ipasavyo katika kuleta maendeleo ya Taifa letu.

3. itakumbukwa kwamba, tarehe 17 Machi, 2021 Taifa lilipata msiba mzito wa kuondokewa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, tarehe 24 Julai, 2020

tulimpoteza Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na tarehe 17 Februari, 2021 tuliwapoteza Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Balozi Mhandisi John William Hebert Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Naomba kutumia nafasi hii kuungana na Waheshimiwa Mawaziri wenzangu waliotangulia kuwasilisha Hotuba zao kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais, familia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa ujumla kwa misiba hii mizito. Wizara yangu inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa viongozi hawa katika kukuza taswira ya nchi yetu kimataifa na mahusiano ya kidiplomasia baina yetu na nchi mbalimbali.

**4. Mheshimiwa Spika**, natumia nafasi hii pia kutoa shukrani za dhati kwa nchi marafiki na jumuiya ya kimataifa kwa kuonesha mshikamano, kutufaraji na kushiriki nasi katika kipindi cha majonzi makubwa kwa Taifa letu.

**5.** kwa namna ya pekee naomba kutoa shukrani kwa Umoja wa Mataifa kwa uamuzi wake wa kuitisha kikao rasmi cha Baraza Kuu la Umoja huo kwa ajili ya kumuenzi na kumkumbuka Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kilichofanyika tarehe 16 Aprili, 2021 Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa jijini New York, Marekani. Kupitia kikao hicho, Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa zilizielezea mafanikio makubwa ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yaliyopatikana chini ya Uongozi wa Hayati Dkt. Magufuli katika kuboresha huduma za jamii kama vile elimu, maji, afya, nishati na miundombinu ya usafirishaji. Tunawashukuru sana.

**6. Mheshimiwa Spika**, vilevile, naomba kutoa pole kwako na Bunge lako Tukufu kufuatia vifo vya Waheshimiwa Khatibu Said Haji aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde, Zanzibar aliyefariki tarehe 20 Mei, 2021; Mhandisi Atashasta Justus Nditiye aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambwe Mkoa wa Kigoma, aliyefariki tarehe 12 Februari, 2021; na Martha Jachi Umbulla aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa

Manyara, aliyefariki tarehe 21 Januari, 2021. Mwenyezi Mungu azipumzishe roho za marehemu mahala pema peponi. Amina.

7. kipekee kabisa na kwa moyo mkunjufu napenda kutumia nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), kwa kuaminiwa na kuendelea kushika nafasi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tuna imani na uongozi mpya ulioingia madarakani kuendelea kudumisha amani na Muungano wetu, kusukuma mbele gurudumu la maendeleo na kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia na jumuiya ya kimataifa.

8. **Mheshimiwa Spika**, nampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Othman Masoud Othman Sharif kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar; na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

9. **Mheshimiwa Spika**, nchi yetu imeweka historia ya kujivunia na kuigwa duniani kwa namna ilivyopata uongozi mpya wa juu wa Serikali kufuatia vifo vya Viongozi Wakuu waliokuwa madarakani. Mabadiliko hayo yalifanyika kulingana na misingi ya Katiba. Hatua hii ni kielelezo cha ukomavu, uimara wa demokrasia na misingi ya utawala wa sheria.

10. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kumpongeza tena Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake aliyowasilisha hapa Bungeni ambayo imetoa dira na mwongozo wa utekelezaji wa kazi za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Nawapongeza pia

Waheshimiwa Mawaziri wenzangu waliionitangulia kuwasilisha hotuba zao katika Bunge hili la Bajeti.

**11. Mheshimiwa Spika**, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa uongozi wako madhubuti katika uendeshaji wa shughuli za Bunge. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb), Naibu Spika; Wenyeviti wa Bunge; na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi nzuri wanazozifanya kukusaidia kusimamia na kuendesha shughuli za Bunge. Naomba Mwenyezi Mungu azidi kuwajalia afya njema, busara na hekima katika kuongoza Mhimili huu muhimu kwa Taifa letu.

**12. Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb), pamoja na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo (Mb), kwa kazi nzuri na ya kizalendo ya kuishauri Serikali hususan Wizara yangu. Naomba nikiri kuwa miongozo na ushauri wao katika masuala mbalimbali umekuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

**13. Mheshimiwa Spika**, naomba pia kuwapongeza Waheshimiwa Eliadory Felix Kavejuru na Dkt. Florence George Samizi kwa kuchaguliwa hivi karibuni kuwa Wabunge wa Majimbo ya Buhigwe na Muhambwe, mtawalia. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa kuaminiwa kuwawakilisha wananchi katika Bunge hili Tukufu. Vilevile, nitumie nafasi hii kuwapongeza viongozi wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa mbalimbali Serikalini. Kuteuliwa kwao ni kielelezo cha kuaminiwa na Mheshimiwa Rais katika kuwaletea maendeleo wananchi.

## **2.0 MISINGI YA SERA YA TANZANIA KATIKA UHUSIANO WA KIMATAIFA**

**14. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ina jukumu la kusimamia uhusiano wa



Kimataifa, Kikanda na baina ya Tanzania na nchi moja moja duniani. Aidha, Wizara ina jukumu la kuratibu ushiriki wa Tanzania katika Taasisi na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa. Lengo kuu la uhusiano na ushirikiano huo ni kutetea na kulinda maslahi ya Tanzania ndani na nje ya nchi. Pamoja na masuala mengine, utekelezaji wa majukumu ya Wizara unaongozwa na Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 inayoweka msisitizo katika dhana ya Diplomasia ya Uchumi. Msisitizo wa dhana hiyo umejikita katika kukuza biashara na kutafuta fursa mpya za masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini; kuvutia wawekezaji; kuvutia watalii; kutafuta fursa za misaada na mikopo yenye masharti nafuu; na kutafuta fursa za ajira na ufadhili wa masomo nje ya nchi.

**15. *Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kujenga taswira nzuri ya nchi na kuhakikisha sauti ya Tanzania inasikika katika medani za Kimataifa. Vilevile, imeendelea kuimarisha uhusiano baina ya nchi yetu na nchi moja moja pamoja na Mashirika mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa. Lengo kuu ni kuhakikisha kuwa Tanzania inaendelea kunufaika na fursa mbalimbali zinazopatikana kupitia uhusiano huo sambamba na kuendelea kuwa mstari wa mbele katika kusimamia na kutetea misingi ya Taifa letu.

**16. *Mheshimiwa Spika***, historia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesheheni misingi imara inayoiwezesha kuendelea kuwa miongoni mwa nchi zilizo na ushawishi mkubwa kimataifa tangu Uhuru. Misingi ya nchi yetu kuheshimika kimataifa iliwekwa na Waasisi wa Taifa letu kwa kupinga na kulaani ubabe, uonevu na ukandamizaji popote pale ulipotokea duniani bila hofu. Hivyo, katika kusimamia misingi hiyo, tumeendelea kulinda uhuru wetu; kujiamulia mambo yetu wenyewe bila kuingiliwa; kulinda mipaka ya nchi yetu; kutetea haki; kuimarisha ujirani mwema; na kutekeleza Sera ya Kutofungamana na Upande Wowote kama dira na msimamo wetu kwenye uhusiano na nchi nyingine katika jumuiya ya kimataifa.

### 3.0 TATHMINI YA HALI YA UCHUMI, SIASA, ULINZI NA USALAMA DUNIANI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

17. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa taarifa fupi kuhusu hali ya uchumi, siasa, ulinzi na usalama duniani kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama ifuatavyo:

#### 3.1 Hali ya Uchumi

18. *Mheshimiwa Spika*, kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia ya mwezi Januari 2021, ukuaji wa uchumi wa dunia kwa mwaka 2020 ulipungua kwa asilimia 4.3 kutokana na athari za ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na Virusi vya Korona (UVIKO-19) ambao uliathiri sekta nyingi za uchumi hususan uwekezaji, uzalishaji, upatikanaji wa huduma na biashara ya kimataifa. Kasi ya kupungua kwa ukuaji wa uchumi ilikuwa ndogo kwa asilimia 0.9 ikilinganishwa na makadirio ya awali ya asilimia 5.2.

Aidha, kwa mwaka 2021 uchumi wa dunia unakadiriwa kukua kwa asilimia 4 kutokana na kuanza kurejea kwa shughuli za kiuchumi katika nchi mbalimbali. Ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia, Benki hiyo inahimiza kuimarisha huduma za afya, elimu, miundombinu ya TEHAMA, uwekezaji na biashara. Hatua hizi zina mchango mkubwa katika kujenga uchumi jumuishi na kupunguza umaskini.

19. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na ukuaji wa uchumi wa dunia kupungua kutokana na athari za UVIKO - 19, mwezi Julai, 2020 Benki ya Dunia iliitangaza Tanzania kukidhi vigezo vya kuwa nchi yenye uchumi wa kati. Hatua hiyo inatoa fursa kwa nchi yetu kuaminiwa kimataifa katika juhudi zake za kuinua uchumi na kuvutia wawekezaji kwa maendeleo yetu.

#### 3.2 Hali ya Siasa, Ulinzi na Usalama

##### A. Afrika

20. *Mheshimiwa Spika*, hali ya siasa, ulinzi na usalama imeendelea kuimarika katika maeneo mengi barani Afrika. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 nchi za Benin, Burkina Faso, Côte d'Ivoire, Chad, Ghana, Jamhuri ya

Afrika ya Kati, Niger, Shelisheli, Guinea, Uganda na Jamhuri ya Kongo zilifanya chaguzi. Tunawapongeza Waheshimiwa Marais wa nchi hizo kwa kuchaguliwa na tunaahidi kuendelea kushirikiana na Serikali zao kwa lengo la kudumisha uhusiano baina ya nchi zetu.

**21. Mheshimiwa Spika**, vilevile, naomba kutumia fursa hii kutoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Lt. Gen. Mahamat Idriss Déby, Rais wa Mpito wa Chad na wananchi wa nchi hiyo kwa ujumla kufuatia kifo cha Mheshimiwa Idriss Déby ltno aliyekuwa Rais wa nchi hiyo kilichotokea tarehe 20 Aprili 2021. Dunia itamkumbuka Hayati Idriss Déby ltno kwa kujitoa na kuwa mstari wa mbele katika juhudi za kuimarisha usalama na utulivu katika eneo la ukanda wa Sahel na Afrika kwa ujumla. Tunatoa rai kuimarishwa kwa amani nchini humo na kurejeshwa utawala wa kiraia kama Katiba ya Umoja wa Afrika (AU) inavyoeleza.

**22. Mheshimiwa Spika**, pamoja na hali ya kisiasa kuwa ya kuridhisha, uwepo wa tishio la ugaidi, uharamia, vikundi vya waasi, biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, dawa za kulevya na utakasishaji wa fedha bado ni changamoto kwa baadhi ya nchi barani Afrika kama ifuatavyo:

### **Ethiopia**

**23. Mheshimiwa Spika**, nchini Ethiopia hususan kwenye jimbo la Tigray lililopo Kaskazini mwa nchi hiyo kumekuwa na mvutano wa kisiasa tangu mwaka 2019. Mvutano huo ulisababisha kuibuka mapigano kati ya Jeshi la Serikali ya Shirikisho na Jeshi la jimbo hilo. Mapigano hayo yalisitishwa mwezi Februari 2021 na pande zote mbili zimeanza mazungumzo ya amani.

### **Jamhuri ya Afrika ya Kati**

**24. Mheshimiwa Spika**, hali ya kiusalama katika Jamhuri ya Afrika ya Kati imeendelea kuwa ya wasiwasi kutokana na mwendelezo wa mashambulizi ya vikundi vya waasi dhidi ya majeshi ya Serikali na raia, licha ya kufikiwa kwa makubaliano ya amani na kukamilika kwa zoezi la Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Desemba 2020. Tanzania inaendelea

kuunga mkono juhudi zinazofanywa na jumuiya ya kimataifa katika kutafuta suluhu ya mgogoro huo ikiwemo kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi hiyo kwa kuchangia vikosi vya kijeshi kwenye misheni ya Umoja wa Mataifa ya ulinzi wa amani (MINUSCA).

### **Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo**

**25. Mheshimiwa Spika**, mwezi Desemba 2020, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) iliingia kwenye mgogoro wa kisiasa baada ya kuvunjika kwa Serikali ya Mseto iliyoundwa na muungano wa *Cap Pour le Changement* (CACH) unaoongozwa na Mheshimiwa Felix Tshisekedi Tshilombo, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na muungano wa *Front Commun Pour le Congo* (FCC) unaoongozwa na Rais Mstaafu, Mheshimiwa Joseph Kabila Kabange. Kufuatia kuvunjika kwa Serikali ya mseto, Mheshimiwa Rais Tshisekedi aliunda Serikali mpya mwezi Aprili 2021.

**26. Mheshimiwa Spika**, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo pia inaendelea kukabiliwa na changamoto za kiusalama katika eneo la Mashariki mwa nchi hiyo ambapo vikundi vya waasi vyenye silaha vimeendelea kufanya mashambulizi ya mara kwa mara dhidi ya raia na majeshi ya nchi hiyo. Tanzania inaendelea kuunga mkono juhudi zinazofanywa na jumuiya ya kimataifa katika kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi hiyo kupitia misheni ya kulinda amani ya Umoja wa Mataifa (MONUSCO) inayojumuisha vikosi vya kijeshi kutoka Tanzania.

### **Msumbiji**

**27. Mheshimiwa Spika**, Msumbiji inaendelea kukabiliwa na changamoto za kiusalama katika eneo la Kaskazini mwa nchi hiyo hususan jimbo la Cabo Delgado kutokana na mashambulizi ya mara kwa mara yanayodaiwa kufanywa na vikundi vya kigaidi dhidi ya Serikali na raia. Tanzania kama ndugu na jirani wa Msumbiji inaendelea kuwa sehemu ya juhudi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) katika kudhibiti na kuimarisha hali ya usalama kwenye eneo hilo.

## **B. Mashariki ya Kati**

**28. *Mheshimiwa Spika***, hali ya siasa, ulinzi na usalama katika ukanda wa Mashariki ya Kati imeendelea kuimarika isipokuwa kwa baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:

### **Yemen**

**29. *Mheshimiwa Spika***, hali ya usalama nchini Yemen bado siyo ya kuridhisha kutokana na mapigano yanayoendelea kati ya jeshi la Serikali na kundi la wanamgambo wa *Houthi*. Mapigano hayo yamekuwa na athari kwa ustawi wa nchi hiyo. Tanzania inaunga mkono msimamo wa Umoja wa Mataifa unaozitaka pande mbili zinazopigana kujadiliana na hatimaye kupata suluhu ya mgogoro huo.

### **Lebanon**

**30. *Mheshimiwa Spika***, Lebanon imeendelea kukabiliwa na changamoto ya uwepo wa makundi yenye itikadi kali zinazokinzana. Hali hii ikijumuishwa na mdororo wa uchumi, mifumo dhaifu ya utawala na uhasama baina yake na Israel imechochea kuendelea kuwepo kwa machafuko ya mara kwa mara nchini humo na kusababisha mgogoro wa kisiasa na kiusalama. Tanzania imeendelea kuunga mkono juhudi za jumuiya ya kimataifa katika kuleta amani na usalama, ikiwemo kuchangia vikosi vya kijeshi katika misheni ya kulinda amani ya Umoja wa Mataifa nchini humo (UNIFIL).

### **Israel na Palestina**

**31. *Mheshimiwa Spika***, hivi karibuni mgogoro kati ya Israel na Palestina umeongezeka na kusababisha madhara makubwa ikiwemo vifo na uharibifu wa mali na miundombinu muhimu katika miji ya Gaza, Jerusalem, Tel Aviv na Ukingo wa Magharibi. Tanzania inaunga mkono maazimio ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika kuhusu mgogoro huo yanayozitaka pande husika kuheshimu makubaliano ya kuwepo kwa nchi mbili ikiwa ni Palestina huru na Israel salama.

### **Syria**

**32. *Mheshimiwa Spika***, Syria imeendelea kukabiliwa na mapigano ya ndani kati ya majeshi ya Serikali na vikundi vya uasi. Mgogoro huo uliodumu kwa muda wa muongo mmoja

sasa umekuwa na athari kubwa za kiuchumi na kijamii na kusababisha raia wengi kuikimbia nchi yao na kutafuta hifadhi ya ukimbizi katika nchi mbalimbali duniani. Tanzania inaunga mkono jitihada za kutafuta suluhu ya mgogoro huo kwa njia ya majadiliano ili kurejesha amani ya kudumu katika nchi hiyo.

### C. Ulaya na Amerika

**33. *Mheshimiwa Spika***, hali ya siasa, ulinzi na usalama katika nchi za Ulaya na Amerika imeendelea kuwa tulivu na Tanzania imeendelea kuimarisha uhusiano wake na nchi hizo.

### Uingereza

**34. *Mheshimiwa Spika***, tarehe 9 Aprili, 2021 Uingereza ilipata msiba mkubwa kwa kuondokewa na Prince Phillip, *Duke of Edinburgh*, mwenza wa Mtukufu Malkia Elizabeth II wa Uingereza na Mkuu wa Jumuiya ya Madola. Tanzania inatoa pole kufuatia msiba huo na inaungana na Familia ya Kifalme, Serikali, Waingereza na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Madola kuomboleza kifo chake. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Amina.

### Marekani

**35. *Mheshimiwa Spika***, mwezi Novemba 2020, Marekani ilifanya Uchaguzi Mkuu ulioleta mabadiliko ya utawala kutoka Chama cha Republican kwenda Chama cha Democratic. Licha ya Rais aliyekuwepo madarakani kupinga matokeo ya uchaguzi kwa madai ya kuwepo kwa udanganyifu katika baadhi ya majimbo, nchi hiyo iliweza kukamilisha zoezi la uchaguzi na kumuapisha Mheshimiwa Joseph Robinette Biden Jr. wa Chama cha Democratic mwezi Januari 2021. Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Wamarekani kwa ukomavu wa demokrasia na Rais Biden kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 46 wa Marekani. Tanzania itaendelea kushirikiana na Serikali yake na kudumisha uhusiano baina ya nchi zetu.

#### 4.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**36. Mheshimiwa Spika**, kabla ya kueleza utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, naomba nitaje majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kama yalivyoainishwa katika Muundo wa Wizara Toleo la tarehe 7 Julai, 2018 kama ifuatavyo:

i. Kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje;

ii. Kusimamia na kuratibu masuala ya uhusiano baina ya Tanzania na nchi nyingine;

iii. Kusimamia na kuratibu masuala ya mikataba na makubaliano ya kimataifa;

iv. Kusimamia masuala yanayohusu kinga na haki za wanadiplomasia waliopo nchini;

v. Kusimamia na kuratibu masuala ya itifaki na uwakilishi;

vi. Kuanzisha na kusimamia huduma za kikonseli;

vii. Kuratibu masuala ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa;

viii. Kuratibu na kusimamia masuala ya Watanzania waishio ughaibuni; ix. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

x. Kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo ya taasisi zilizo chini ya Wizara; na

xi. Kusimamia utawala na maendeleo ya watumishi Wizarani na katika Balozi za Tanzania.

**37. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa majukumu ya Wizara uliongozwa na nyaraka mbalimbali ikiwemo Ilani ya Chama

cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015; Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025; Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 2020/21); Ajenda ya 2063 ya Umoja wa Afrika; Ajenda ya 2030 ya Umoja wa Mataifa ya Malengo ya Maendeleo Endelevu; Mkakati wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 2017/2018 2021/2022; Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 1999 kama ulivyorekebisha na Itifaki zake; Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika wa mwaka 1992 kama ulivyorekebisha na Itifaki zake pamoja na mikataba mingine ya Kikanda na Kimataifa; maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili Mpango na Bajeti ya Wizara kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; Mpango Mkakati wa Wizara wa mwaka 2020/2021 – 2024/2025; na maagizo yaliyotolewa kwa nyakati tofauti kwa Wizara na Viongozi wa Kitaifa, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali.

## Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

### Mapato

**38. Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ilipanga kukusanya **shilingi 2,550,879,000**. Kati ya kiasi hicho **shilingi 47,170,000** ni makusanyo ya Makao Makuu ya Wizara na **shilingi 2,503,709,000** ni makusanyo kutoka Balozi za Tanzania. Vyanzo vya mapato hayo ni uhakiki wa nyaraka, pango la majengo ya Serikali nje ya nchi na mauzo ya nyaraka za zabuni.

**39. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2020 hadi tarehe 30 Aprili 2021, Wizara ilikusanya jumla ya **shilingi 756,182,081.71** sawa na asilimia **29.6** ya lengo lililopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Kupungua kwa mapato hayo kumetokana na kukosekana kwa wapangaji katika baadhi ya majengo ya Serikali kwenye Balozi za Tanzania kutokana na athari za uwepo wa janga la UVIKO-19. Nchi



nyingi duniani zilichukua hatua za kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huo kwa kufunga shughuli muhimu za kijamii na uzalishaji zilizosababisha kampuni na ofisi nyingi kufungwa na kufanyia kazi zake kutokea nyumbani.

**40. Mheshimiwa Spika**, mapato yaliyokusanywa na Wizara katika kipindi cha mwezi Julai 2020 hadi Aprili, 2021 yaliingizwa moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kama taratibu zinavyoelekeza.

#### **Fedha Zilizoidhinishwa**

**41. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, kiasi cha **shilingi 199,750,684,000** kiliidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **shilingi 179,750,684,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 20,000,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika fedha zilizoidhinishwa kwa Matumizi ya Kawaida, **shilingi 167,717,723,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **shilingi 12,032,961,000** ni kwa ajili ya Mishahara.

#### **Fedha Zilizopokelewa na Kutumika**

**42. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 Wizara ilipokea kutoka Hazina kiasi cha **shilingi 127,648,549,514.76**. Kiasi hicho cha fedha ni sawa na asilimia **63.9** ya fedha zote za bajeti zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021. Kati ya fedha hizo, **shilingi 118,893,319,946.58** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo sawa na asilimia **70.9** na **shilingi 8,755,299,568.18** ni kwa ajili ya Mishahara sawa na asilimia **72.8**.

**43. Mheshimiwa Spika**, Wizara ilitumia kiasi cha **shilingi 106,601,250,300.11** sawa na asilimia **83.5** ya fedha zilizopokelewa. Kati ya fedha hizo, **shilingi 97,846,020,731.93** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **shilingi 8,755,229,568.18** ni mishahara.

**44. Mheshimiwa Spika**, baada ya kutaja majukumu ya Wizara, Miongozo mbalimbali iliyozingatiwa na Wizara pamoja na taarifa ya mapato na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha

2020/2021, naomba sasa nitumie fursa hii kueleza kwa kifupi mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi husika kama ifuatavyo:

#### **4.1 Kusimamia na Kuratibu Masuala ya Uhusiano Baina ya Tanzania na Nchi Nyingine**

##### **4.1.1 Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi**

**45. *Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza Diplomasia ya Uchumi kwa lengo la kuchangia maendeleo ya Taifa letu, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta imeendelea kutafuta masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini; kuongeza idadi ya watalii na wawekezaji; kuongeza fursa za mafunzo nje ya nchi; kutafuta misaada na mikopo ya masharti nafuu pamoja na kuimarisha ushirikiano katika nyanja nyingine za kiuchumi na kijamii. Matokeo mahsusi katika utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi yanatokana na kuendelea kuimarika kwa ushirikiano baina ya Tanzania na Jumuiya ya kimataifa.

##### **4.1.2 Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Afrika**

**46. *Mheshimiwa Spika***, mwezi Mei 2021, Wizara iliratibu ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda hapa nchini. Wakati wa ziara hiyo, Mheshimiwa Museveni na mwenyeji wake Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walishuhudia uwekaji saini Mkataba wa Uenyeji kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kampuni ya Mafuta Ghafi ya Afrika Mashariki (EACOP) kuhusu Ujenzi wa Mradi wa Bomba la kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima, Uganda mpaka Chongoleani, Tanga.

**47. *Mheshimiwa Spika***, mwezi Mei 2021, Wizara iliratibu Ziara ya Kitaifa ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, nchini Kenya kufuatia mwaliko wa Mheshimiwa Uhuru Muigai Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya. Ziara hiyo ya kwanza ya Kitaifa tangu kuapishwa kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ililenga kuimarisha uhusiano wa kidugu na ujirani mwema kati

ya Tanzania na Kenya. Wakati wa ziara hiyo, nchi hizi mbili zilikubaliana kuharakisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya lami ya Bagamoyo - Tanga - Horohoro - Lungalunga - Mombasa - Malindi (Km 454) na mradi wa kusafirisha umeme kV 400 kutoka Singida (Tanzania) hadi Isinya (Kenya).

**48. Mheshimiwa Spika**, aidha, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na mwenyeji wake Mheshimiwa Rais Uhuru Muigai Kenyatta walishuhudia uwekaji saina Hati ya Makubaliano ya Kusafirisha Gesi Asilia kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kenya na Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano katika Masuala ya Utamaduni, Sanaa, Mahusiano ya Jamii na Urithi wa Taifa. Vilevile, walishiriki jukwaa la wafanyabiashara wa Tanzania na Kenya lililofanyika jijini Nairobi na kuwahakikishia kuwa Serikali za nchi zote mbili zitaendelea kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na biashara.

**49. Mheshimiwa Spika**, kadhalika wakati wa ziara hiyo, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan alihutubia Kikao Maalum cha pamoja cha Bunge la Taifa na Bunge la Seneti la Kenya, ambapo pamoja na masuala mengine alieleza nia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuendelea kudumisha uhusiano wa kihistoria, kidugu na kirafiki kati ya nchi hizi mbili.

**50. Mheshimiwa Spika**, mwezi Aprili 2021, Wizara iliratibu ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Uganda. Wakati wa ziara hiyo, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na mwenyeji wake Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda walishuhudia uwekaji saina mikataba mitatu ya utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Tanga. Mikataba iliyosainiwa ni:

i. Mikataba wa Uenyeji wa mradi kati ya Serikali ya Uganda na kampuni za *TOTAL Limited* ya Ufaransa na *China National Offshore Oil Corporation (CNOOC)* ya China zilizowekeza kwenye mradi;

ii. Mkataba wa Wanahisa kati ya Serikali ya Uganda, Serikali ya Tanzania na wawekezaji (TOTAL na CNOOC); na

iii. Mkataba wa Tozo ya Usafirishaji wa Mafuta kati ya Serikali ya Uganda na wawekezaji.

**51. Mheshimiwa Spika**, mwezi Machi 2021, Wizara iliratibu Mkutano wa Sita wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Burundi uliofanyika mjini Kigoma, Tanzania. Katika Mkutano huo, Tanzania na Burundi zilikubaliana kuimarisha na kukuza ushirikiano katika maeneo mbalimbali ikiwemo siasa na diplomasia; ulinzi na usalama; uendelezaji wa miundombinu ya uchukuzi inayounganisha nchi hizi mbili; na biashara na uwekezaji.

**52. Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano huo, nchi hizi pia zilikubaliana kushirikiana katika ufundishaji wa lugha za Kiswahili na Kifaransa na Burundi kutumia masoko na mitambo ya kuchenjua madini hapa nchini. Vilevile, Chama cha Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) na Chama cha Wafanyabiashara wa Burundi vilisaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano ambayo inatoa fursa kwa wafanyabiashara wa nchi hizi mbili kufanya biashara bila vikwazo.

**53. Mheshimiwa Spika**, mwezi Januari 2021, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Filipe Jacinto Nyusi, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji iliyofanyika nchini kwa lengo la kufanya mazungumzo maalum na Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika ziara hiyo, viongozi hao walikubaliana kuimarisha ushirikiano baina ya nchi hizi mbili na kukuza kiwango cha biashara na uwekezaji pamoja na kuimarisha ujirani mwema.

**54. Mheshimiwa Spika**, mwezi Januari 2021, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mheshimiwa SahleWork Zewde, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia iliyofanyika nchini. Tanzania na Ethiopia zilikubaliana kuimarisha na

kukuza uhusiano wa kiuchumi hususan kuongeza kiwango cha biashara na uwekezaji; na kubadilishana utaalum na uzoefu katika uendeshaji wa viwanda vya kuongeza thamani ya ngozi za mifugo. Nchi hizo pia zilikubaliana kuwa Serikali ya Tanzania itatoa msamaha kwa wafungwa 1,789 raia wa Ethiopia ili warejeshwe kwao; na Tanzania kuisaidia Ethiopia kufundisha lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Addis Ababa na Chuo cha Diplomasia cha Ethiopia.

**55. Mheshimiwa Spika**, mwezi Desemba 2020, Wizara iliratibu ziara ya Mheshimiwa Dkt. Netumbo Nandi-Ndaitwah, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Jamhuri ya Namibia iliyofanyika nchini. Katika ziara hiyo, nchi hizi mbili zilikubaliana kuendelea kuimarisha ushirikiano kwenye sekta za uvuvi hususan uvuvi wa bahari kuu, mifugo, biashara, uwekezaji na kilimo. Vilevile, Mheshimiwa Nandi-Ndaitwah alihudhuria Mahafali ya 50 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam yaliyofanyika tarehe 8 Desemba, 2020 na kutunukiwa shahada ya heshima ya uzamivu ya falsafa kwa kutambua mchango wake katika kupigania uhuru, kutetea haki za binadamu na ustawi wa watu wa Namibia na Afrika kwa ujumla.

**56. Mheshimiwa Spika**, mwezi Desemba 2020, Wizara iliratibu ushiriki wa ujumbe wa Tanzania katika mkutano wa ujirani mwema kati ya mikoa ya Kagera na Kigoma ya Tanzania na majimbo ya Makamba, Rutana, Cankuzo na Rumonge ya Burundi uliofanyika mjini Kigoma. Katika Mkutano huo, Tanzania na Burundi zilikubaliana kuimarisha ushirikiano katika masuala ya usalama, biashara, utamaduni na michezo katika maeneo ya mpakani. Mikutano ya aina hii ni muhimu katika kuimarisha ujirani mwema na kutatua changamoto za kiusalama na kibiashara katika maeneo ya mipaka.

**57. Mheshimiwa Spika**, mwezi Novemba 2020, Wizara iliratibu ziara ya Mhe. Dkt. Mohamed Hemed Shaker Elmarkabi, Waziri wa Nishati wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri na Mhe. Dkt. Asim Abdelhamid Hafiz Elgazar, Waziri wa Makazi wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri iliyofanyika nchini. Viongozi hao walijumuika na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushuhudia uzinduzi wa uchepushaji wa maji katika mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere.

**58. Mheshimiwa Spika**, mwezi Oktoba 2020, Wizara iliratibu ziara rasmi ya Mheshimiwa Dkt. Lazarus McCarthy Chakwera, Rais wa Jamhuri ya Malawi iliyofanyika nchini. Katika ziara hiyo, pamoja na mambo mengine, Tanzania na Malawi zilikubaliana kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Huduma kwa Pamoja Mpakani (OSBP) cha Songwe/Kasumulu; ujenzi wa barabara ya Mpemba - Isongole - Mbozi (km 51)/Chitipa - Mbilima (km 32); na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania kufungua ofisi nchini Malawi. Nchi hizi pia zilikubaliana kushirikiana katika utekelezaji wa miradi ya pamoja ya kufua umeme na umwagiliaji katika Bonde la Mto Songwe.

**59. Mheshimiwa Spika**, mwezi Oktoba 2020, Wizara ilifanikisha uwekaji saina Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano Kuanzisha Ofisi ya Uhusiano ya Mamlaka ya Bandari ya Tanzania nchini Burundi. Ofisi hiyo ambayo imeanza kufanya kazi, inarahisisha utoaji wa huduma za uagizaji na usafirishaji wa bidhaa kwenda nchini Burundi kupitia Bandari ya Dar es Salaam kwa kuzingatia kuwa zaidi ya asilimia 95 ya bidhaa zinazolingizwa nchini Burundi kutoka nje zinapitia bandari hiyo. Hatua hii ni sehemu ya utekelezaji wa maazimio ya mkutano wa viongozi wakuu wa nchi hizi mbili uliofanyika mwezi Septemba 2020.

**60. Mheshimiwa Spika**, mwezi Septemba 2020, Wizara iliratibu ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda iliyofanyika nchini. Katika ziara hiyo, Tanzania na Uganda zilisaina Hati ya Makubaliano Kuanza Ujenzi wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Tanga.

**61. Mheshimiwa Spika**, mwezi Septemba 2020, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Meja Jenerali Évariste Ndayishimiye, Rais wa Jamhuri ya Burundi iliyofanyika nchini. Katika ziara hiyo, Tanzania na Burundi zilikubaliana kushirikiana kujenga reli yenye urefu wa kilomita 200 kutoka Uvinza,

Tanzania hadi Gitega, Burundi; kuanza ujenzi wa Kituo cha Huduma kwa Pamoja Mpakani Manyovu/Mugina; na Burundi kuuza madini yake katika masoko ya madini nchini Tanzania. Nchi hizi zilikubaliana pia kuimarisha ushirikiano katika masuala ya ulinzi na usalama; biashara na uwekezaji; na ujirani mwema.

#### 4.1.3 Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Asia na Australasia

**62. Mheshimiwa Spika**, mwezi Januari 2021, Wizara na Benki ya NMB ziliandaa mpango wa kuwezesha wafanyabiashara wa Tanzania kuuza bidhaa zao katika soko la China. Kupitia mpango huo, Wizara itatafuta masoko na Benki ya NMB itatoa mikopo kwa wafanyabiashara Watanzania kwa ajili ya mitaji ya kuuza bidhaa nchini China. Benki ya NMB pia imekubali kufadhili ushiriki wa Tanzania katika maonesho ya nne ya bidhaa za nje yatakayofanyika China mwezi Novemba 2021 kwa kutoa shilingi milioni 100 kwa ajili ya kujenga banda la Tanzania kwenye maonesho hayo.

**63. Mheshimiwa Spika**, mwezi Januari 2021, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mhe. Wang Yi, Mjumbe wa Baraza la Taifa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Watu wa China iliyoanyika hapa nchini. Kufuatia ziara hiyo:

i. Serikali ya China ilitoa msaada wa shilingi milioni 350 kwa ajili ya kununua vifaa vya karakana ya fani ya uvuvi katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi VETA, Chato;

ii. Serikali ya China imeahidi kutoa misaada ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji; upanuzi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete; na ujenzi wa barabara kuu za Zanzibar zenye urefu wa kilometa 148;

iii. Serikali ya China imeahidi kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la Umeme la Ruhudji (MW 358) na njia ya kusafirishia umeme kutoka Ruhudji hadi Kidasa (km 170, kV400); na ujenzi wa Bwawa la Umeme la Rumakali (MW 222) na njia ya kusafirishia umeme kutoka Rumakali hadi Mbeya (Km 150, kV400);

iv. Serikali ya China ilitoa msaada wa Dola za Marekani 20,000 kwa ajili ya kusaidia ununuzi wa vifaa vya uvuvi kwa jumuiya ya wavuvi wa mwalo wa Chato; na

v. Mwezi Mei, 2021 Serikali ya China imetoa msaada wa Shilingi Bilioni 35.37 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo hapa nchini.

**64. Mheshimiwa Spika**, katika ziara hiyo, Mhe. Wang Yi pia alishuhudia uwekaji saini mkataba wa ujenzi wa awamu ya tano ya reli ya kisasa ya kiwango cha kimataifa (SGR) kipande cha Mwanza hadi Isaka chenye urefu wa kilometa 341.

**65. Mheshimiwa Spika**, mwezi Desemba 2020, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa wadau wa biashara wa Tanzania na China kuhusu soko la mabondo ya samaki nchini China uliofanyika kwa njia ya mtandao. Mkutano huo ulizikutanisha kampuni za Tanzania zinazojihusisha na biashara ya samaki pamoja na kampuni ya Alibaba ya China. Kampuni ya Alibaba imeonesha nia ya kutangaza mabondo ya samaki katika mtandao wake pamoja na kununua mabondo kutoka Tanzania.

**66. Mheshimiwa Spika**, mwezi Desemba 2020, Wizara ilifanikisha kusainiwa kwa mkataba utakaoiwezesha Tanzania kupata mkopo wa masharti nafuu wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 300 kutoka Mfuko wa Ushirikiano wa Kiuchumi wa Korea. Miradi itakayogharamiwa na fedha za mkopo huo ni ujenzi wa vituo vya kupoozea umeme katika njia ya kusafirishia umeme ya Kigoma – Nyakanazi kwa kiasi cha shilingi bilioni 102.9; uboreshaji wa huduma za majitaka jijini Dodoma kwa kiasi cha shilingi bilioni 160; na uimarishaji wa huduma za upimaji na ramani kwa kiasi cha shilingi bilioni 148.6. Fedha nyingine za mkopo huo kiasi cha shilingi bilioni 91.4 zitatumika kwa ajili ya kukabiliana na athari za kiuchumi zilizotokana na janga la UVIKO-19; na shilingi bilioni 74.5 ni nyongeza katika mradi wa ujenzi wa Daraja la Tanzanite linalojengwa jijini Dar es Salaam.



**67. Mheshimiwa Spika**, mwezi Desemba 2020, Wizara ilifungua Ofisi ya Mwakilishi wa Heshima wa Tanzania jijini Mumbai, India. Ofisi hiyo imerahisisha utoaji huduma za kikonseli kwa watazania wanaoishi katika jiji hilo. Ofisi hiyo pia itakuwa kiungo muhimu katika masuala ya biashara kati ya wafanyabiashara wa Tanzania na wafanyabiashara wa jiji la Mumbai.

**68. Mheshimiwa Spika**, mwezi Novemba 2020, Wizara ilifungua Ofisi ya Mwakilishi wa Heshima wa Tanzania katika jiji la Jakarta, Indonesia. Ofisi hiyo itaratibu masuala ya biashara, uwekezaji na utalii pamoja na kutoa huduma za kikonseli kwa watazania wanaoishi Indonesia na wageni wanaotaka kutembelea Tanzania.

**69. Mheshimiwa Spika**, mwezi Novemba 2020, Wizara ilifanikisha kusainiwa kwa mkataba kati ya Tanzania na China utakaowezesha Tanzania kuuza maharage aina ya soya katika soko la China. Kupitia mkataba huo, Tanzania inakuwa nchi ya 12 kuruhusiwa kuuza maharage hayo ambayo yana soko kubwa nchini humo. Kampuni 49 za Tanzania zimepata vibali vya kuuza maharage hayo katika soko hilo na tayari mwezi Mei 2021, Tanzania imepeleka shehena ya soya yenye uzani wa zaidi ya tani 120.

**70. Mheshimiwa Spika**, mwezi Oktoba 2020, Wizara ilifanikisha kusainiwa kwa Mkataba Maalum wa muda mfupi wa ushirikiano katika usafiri wa anga kati ya Tanzania na India. Kupitia mkataba huo, ndege za ATCL zimefanya safari 36 ikiwemo kuwarejesha Watanzania wapatao 1,770 kutoka nchini India katika kipindi cha UVIKO-19.

**71. Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu na kufanikisha upatikanaji wa kampuni ya PT Indesso ya nchini Indonesia iliyojenga kiwanda cha kutengeneza mafuta yatokanayo na majani ya mimea katika eneo la Mgelema, Pemba kwa kushirikiana na Shirika la Taifa la Biashara la Zanzibar kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 1.4. Kiwanda hicho kilizinduliwa mwezi Septemba 2020 na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, aliyekuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti

wa Baraza la Mapinduzi. Kiwanda kina uwezo wa kuzalisha tani 1.2 za mafuta ghafi ya majani ya mkarafuu kwa mwaka.

**72. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Ubalozi wa Tanzania katika Jamhuri ya Korea imeendelea kutangaza utamaduni wa Tanzania kwa kufundisha lugha ya Kiswahili nchini humo kwa hatua ya awali, kati na juu. Mpaka sasa wanafunzi 150 wamehitimu mafunzo hayo. Vilevile, Ubalozi umekamilisha machapisho ya kufundisha lugha hiyo kwa ngazi ya awali, kati na juu yaliyoanza kutumika mwezi Oktoba 2020.

#### **4.1.4 Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Mashariki ya Kati**

**73. Mheshimiwa Spika**, kufuatia utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi, Wizara imefanikisha Tanzania kuruhusiwa kuanza kuingiza nyama na bidhaa za nyama ya ng'ombe, mbuzi na kondoo katika masoko ya nchi za Oman, Kuwait na Qatar. Vilevile, bidhaa hizo zitaanza kuuzwa nchini Saudi Arabia baada ya kukamilika kwa taratibu za kupata ithibati kutoka kwenye mamlaka za nchi hiyo.

**74. Mheshimiwa Spika**, mwezi Mei 2021, Wizara iliratibu ziara ya Mwana Mfalme Faisal bin Farhan Al Saud, Waziri wa Mambo ya Nje wa Saudi Arabia. Mwana Mfalme huyo alifanya mazungumzo na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo walikubaliana kuendelea kukuza zaidi uhusiano na ushirikiano kati ya Tanzania na Saudi Arabia hususan katika kuvutia uwekezaji na kuimarisha biashara ya mazao ya mifugo, uvuvi na kilimo. Vilevile, Mheshimiwa Rais aliomba Serikali ya Saudi Arabia kufungua ofisi ya Ubalozi Mdogo Zanzibar.

**75. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Mwana Mfalme huyo alikutana nami pamoja na Mawaziri wenye dhamana za Viwanda na Biashara; Uwekezaji; Mifugo na Uvuvi; Mawasiliano na Uchukuzi; na Fedha na Mipango wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo tulikubaliana kuendeleza ushirikiano baina ya Tanzania na Saudi Arabia katika sekta hizo.

**76. Mheshimiwa Spika**, mwezi Januari 2021, Wizara ilifanikisha upatikanaji wa vibali kwa kampuni nane za Tanzania kuuza minofu ya samaki aina ya sangara katika nchi ya Saudi Arabia. Vibali hivyo vimetolewa na Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Saudi Arabia baada ya kukidhi vigezo. Kampuni hizo kwa sasa zipo kwenye maandalizi ya kuanza kupeleka minofu hiyo nchini humo. Aidha, Saudi Arabia imeanza kununua maparachichi kutoka hapa nchini.

**77. Mheshimiwa Spika**, mwezi Januari 2021, Wizara ilifanikisha uwekaji saine Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mamlaka ya Uwekezaji ya Oman kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Mangapwani, Zanzibar. Mradi huo utajumuisha ujenzi wa eneo la kuhudumia mizigo; gati la meli za uvuvi; gati la meli za mafuta na gesi; chelezo kwa ajili ya matengenezo ya meli; na mji wa kisasa katika eneo la Mangapwani. Mradi utakapokamilika utachochea ukuaji wa biashara na usafirishaji Zanzibar.

**78. Mheshimiwa Spika**, mwezi Desemba 2020, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Tamasha la Kumi la Mashindano ya Majahazi lililofanyika nchini Qatar. Tamasha hilo lililohudhuriwa na nchi za Afrika, Mashariki ya Kati na Asia ni jukwaa muhimu katika kutangaza mila na tamaduni za nchi zenye historia ya safari za kale za majahazi. Tanzania ilitumia fursa ya ushiriki kwenye tamasha hilo kutangaza bidhaa zinazozalishwa nchini hususan korosho, asali, kahawa, pilipili, viungo na mafuta.

**79. Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza jitihada za Serikali za kuleta mapinduzi ya kilimo nchini, Wizara inaendelea kuratibu mpango wa mafunzo ya kilimo na mifugo kwa vitendo kwa vijana 100 wa Tanzania kwenda kusoma nchini Israel kila mwaka. Kwa mwaka wa masomo 2020/2021 vijana 36 wanashiriki mafunzo hayo na vijana 64 waliobaki wanatarajiwa kwenda Israel pindi hali ya maambukizi ya UVIKO-19 itakapodhibitiwa. Inatarajiwa kuwa vijana hao watakaporejea wataweza kujiajiri na kuajiri wengine katika sekta za kilimo na mifugo.

**80. Mheshimiwa Spika**, mwezi Agosti 2020, Wizara ilifanikisha kusainiwa kwa mkataba wa mkopo wa Dola za Marekani milioni 15.3 kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait kwa ajili ya mradi wa kilimo cha umwagiliaji kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 3,000 katika Bonde la Mto Luiche mkoani Kigoma. Mradi huo utaongeza uzalishaji wa mazao ya mpunga, mahindi na mbogamboga na hivyo kuinua kipato cha wakulima wa eneo hilo.

**81. Mheshimiwa Spika**, mwezi Septemba 2020, Wizara iliratibu na kufanikisha ziara ya ujumbe maalum kutoka kwa Sheikh Saud bin Saqr al Qasimi, Mtawala wa Ras Al Khaimah kutembelea Zanzibar. Ujumbe huo ulioongozwa na Mohammed Ally Musabbeh, Mshauri Mkuu wa Mtawala wa Ras Al Khaimah uliwasilisha taarifa kuhusu maendeleo ya utafiti wa rasilimali ya gesi na mafuta katika visiwa vya Unguja na Pemba kwa Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Awamu ya Saba wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

#### **4.1.5 Ushirikiano wa Tanzania na Nchi za Ulaya na Amerika**

**82. Mheshimiwa Spika**, mwezi Mei 2021, Wizara iliratibu ziara ya Kikazi ya Mhe. James Philip Duddridge, Waziri wa Uingereza anayesimamia masuala ya Afrika katika Wizara ya Mambo ya Nje, Jumuiya ya Madola na Maendeleo. Wakati wa ziara hiyo Mhe. Duddridge alifanya mazungumzo na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kukubaliana kuimarisha ushirikiano katika masuala ya maendeleo na kijamii. Aidha, Mheshimiwa Rais alieleza kuwa Tanzania inaendelea kuboresha zaidi mazingira ya biashara na uwekezaji na kuiomba Serikali ya Uingereza kuendelea kuiunga mkono Tanzania katika juhudi za maendeleo na uimarishaji wa huduma za kijamii ikiwemo elimu, afya na masuala ya mazingira.

**83. Mheshimiwa Spika**, wakati wa ziara hiyo, Waziri huyo alifanya pia mazungumzo na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambapo walikubaliana kuimarisha ushirikiano katika masuala ya maendeleo na kijamii.

**84. Mheshimiwa Spika**, vilevile, ziara hiyo iliongeza msukumo wa kukamilika kwa majadiliano kati ya Timu ya Tanzania na wawekezaji wa Kiwanda cha Sukari cha Kilombero ambapo wawekezaji hao wamepata idhini ya Serikali (kama mwekezaji mwenza) kuongeza uwekezaji katika kuzalisha sukari hapa nchini utakaogharimu takriban kiasi cha Shilingi bilioni 570. Serikali inamiliki hisa asilimia 25 na mwekezaji anamiliki hisa asilimia 75. Ongezeko la uzalishaji wa sukari litakalotokana na uwekezaji huo litasaidia kupunguza uagizaji wa bidhaa hiyo nje ya nchi.

**85. Mheshimiwa Spika**, mwezi Mei 2021, Wizara iliratibu ziara ya Kikazi ya Mhe. Mikhail Bogdanov, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Urusi na Mjumbe Maalum wa Mheshimiwa Vladimir Putin, Rais wa Shirikisho la Urusi. Kiongozi huyo alikutana na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo pamoja na masuala mengine ya ushirikiano baina ya nchi zetu mbili alimfahamisha kuhusu maandalizi ya Mkutano wa Pili wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika na Urusi unaotarajiwa kufanyika barani Afrika mwaka 2022.

**86. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Mjumbe huyo alikutana nami pamoja na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango na Viongozi wa Vyombo vya Ulinzi ambapo tulikubaliana kuendelea kuimarisha ushirikiano kwenye sekta za biashara, uwekezaji, ulinzi, utalii na fursa za mafunzo kwa Watanzania nchini Urusi.

**87. Mheshimiwa Spika**, mwezi Februari 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha kusainiwa kwa mikataba sita ya msaada kati ya Tanzania na Umoja wa Ulaya kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Umoja huo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hapa nchini yenye thamani ya shilingi bilioni 307.9. Miradi hiyo ambayo itatekelezwa katika kipindi cha miaka minne ni: mradi wa maboresho ya sekta ya nishati wenye thamani ya shilingi bilioni 96.7; mradi wa matumizi endelevu ya nishati mbadala ya kupikia wenye thamani ya shilingi bilioni 82.8; mradi wa kuongeza mnyororo wa thamani katika ufugaji wa nyuki wenye thamani ya shilingi bilioni 27.6;

mradi wa uboreshaji wa huduma za afya ya mimea na usalama wa chakula wenye thamani ya shilingi bilioni 27.6; mradi wa kusaidia uboreshaji wa mazingira ya ukuaji wa biashara na ubunifu wenye thamani ya shilingi bilioni 63.5; na programu ya ushirikiano wa kitaalam yenye thamani ya shilingi bilioni 9.7.

**88. Mheshimiwa Spika**, mwezi Februari 2021, Wizara iliratibu na kufanikisha kusainiwa kwa Mkataba kati ya Tanzania na Ujerumani kuhusu msaada wenye thamani ya shilingi bilioni 18 kwa kipindi cha miaka minne kuanzia 2021 hadi 2024. Msaada huo unahusisha ununuzi wa vifaa tiba na ujenzi wa hospitali ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania jijini Dodoma.

**89. Mheshimiwa Spika**, mwezi Februari 2021, Mhe. Prof. Palamagamba J. A. M. Kabudi (Mb.), aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki alifanya ziara ya kikazi nchini Ufaransa. Kufuatia ziara hiiyo:

i. Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika lake la Maendeleo (AFD) ilikubali kuongeza kiasi cha fedha za mkopo wa masharti nafuu Euro milioni 178 na hivyo kufanya jumla ya mkopo kuongezeka kutoka Euro milioni 600 hadi Euro milioni 778 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo nchini;

ii. Tanzania na UNESCO kukubaliana kuanza taratibu za kuwa na siku rasmi ya kuadhimisha lugha ya Kiswahili duniani kila mwaka. Tanzania imependekeza tarehe 7 Julai ya kila mwaka kuwa siku rasmi ya maadhimisho. Serikali kupitia Wizara inaendelea na majadiliano na UNESCO kufikia lengo hilo; na

iii. Kampuni 11 za Ufaransa zimeonesha utayari wa kutekeleza miradi hapa nchini kwa kutumia fedha kutoka Serikali ya Ufaransa. Kampuni hizo zinalenga kuwekeza kwenye sekta za viwanda, kilimo, maji, elimu, uvuvi, utalii na miundombinu ya reli na barabara.

**90. Mheshimiwa Spika**, mwezi Februari 2021, Wizara iliratibu uwekaji saina Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kampuni ya Tangen & Intertorco Group ya

nchini Hispania kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri, Unguja; Bandari ya Mkoani, Pemba; na mradi wa kufua umeme kwa kutumia gesi. Hafla ya uwekaji saina makubaliano hayo ilishuhudiwa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

**91. Mheshimiwa Spika**, mwezi Januari 2021, Wizara iliratibu uwekaji saina Mkataba kati ya Serikali ya Tanzania na kampuni ya LZ Nicol ya nchini Uingereza kwa ajili ya uchimbaji wa madini ya *nickel*/yanayopatikana eneo la Kabanga wilayani Ngara, Kagera. Katika Mkataba huo pande zote mbili zilikubaliana kuunda kampuni ya ubia ambayo itapewa jina la Tembo Nickel Corporation ambapo Serikali ya Tanzania itamiliki asilimia 16 ya hisa za kampuni hiyo. Aidha, Serikali na kampuni ya LZ Nicol zilikubaliana kujenga kiwanda cha kuchenjua madini ya *nickel*, dhahabu na shaba katika wilaya ya Kahama, Shinyanga. Utekelezaji wa mkataba huo utaongeza fursa za ajira kwa watanzania, uhaulishaji wa teknolojia ya uchimbaji madini na ongezeko la fedha za kigeni.

**92. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia tarehe 31 Agosti, 2020 hadi tarehe 31 Januari, 2021, Tanzania ilipewa heshima ya kuwa Rais wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific (OACPS). Hiyo ilikuwa ni mara ya tatu kwa nchi yetu kushika nafasi hiyo tangu ilipojiunga na Jumuiya hiyo mwaka 1975. Miongoni mwa sababu za kuchaguliwa kushika nafasi hiyo ni kuongezeka kwa ushawishi wake kwenye Jumuiya ya OACPS, sera na hatua thabiti zinazochukuliwa na Tanzania katika kusimamia masuala ya kitaifa na kimataifa pamoja na utendaji madhubuti wa Wizara katika kusimamia Sera ya Mambo ya Nje ikiwemo ushiriki mahiri katika masuala yanayogusa maslahi ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya OACPS.

**93. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha uongozi wetu kwenye Baraza hilo, Tanzania imesimamia ukamilishwaji wa majadiliano ya Ubia Mpya wa Ushirikiano kati ya Nchi za Jumuiya ya OACPS na Umoja wa Ulaya. Vilevile, imeimarisha

ushirikiano miongoni mwa Nchi Wanachama; na ushirikiano baina ya Nchi Wanachama na wadau wa maendeleo katika masuala ya biashara na uwekezaji. Aidha, katika kipindi hicho hali ya kifedha kwenye Sekretarieti ya OACPS imeimarika.

**94. Mheshimiwa Spika**, mwezi Desemba 2020, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 111 wa Baraza la Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya OACPS uliofanyika kwa njia ya mtandao chini ya uenyekiti wa Tanzania. Kupitia Mkutano huo, Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi 10 za Jumuiya hiyo zitakazonufaika na utekelezaji wa mradi wa kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao ya samaki ujulikanao kama FISH4ACP unaogharimu shilingi bilioni 110. Katika mradi huo Tanzania imetengewa kiasi cha shilingi bilioni 8 kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao ya samaki aina ya migebuga na dagaa kutoka mkoa wa Kigoma. Mradi huo utatekelezwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania.

**95. Mheshimiwa Spika**, mwezi Oktoba 2020, Wizara iliratibu na kufanikisha kusainiwa kwa Mkataba kati ya Tanzania na Uswisi wa msaada wa shilingi bilioni 39.15 kugharamia utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini nchini na Mkataba wa shilingi bilioni 4.95 ikiwa ni msaada wa kuchangia Mfuko wa Pamoja wa Afya. Pia, Wizara iliratibu kusainiwa kwa Mkataba kati ya Tanzania na Uswisi wa shilingi bilioni 15.8 ikiwa ni msaada kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kitaifa ya Kutokomeza Malaria Awamu ya Kwanza; na Mkataba wa shilingi bilioni 24.76 ikiwa ni msaada kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kuimarisha Mfumo wa Kutoa Huduma za Afya Awamu ya Tatu. Misaada hiyo imeendelea kuchangia jitihada za Serikali katika kupunguza umaskini na kuboresha huduma za afya nchini.

**96. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu la kuvutia utalii, biashara na uwekezaji, Wizara iliratibu ziara zifuatazo za wafanyabiashara na wawekezaji hapa nchini:



i. Ziara za wawekezaji kutoka Austria na Uturuki zilizofanyika nchini mwezi Desemba 2020 na Februari 2021 mtawalia, ambao wamevutiwa kuwekeza katika sekta za miundombinu, madini, elimu, sayansi na teknolojia na utalii;

ii. Ujio wa kampuni ya Green Iceland Trading Company ya nchini Qatar ambayo imeonesha utayari wa kuanza kununua nyama ya ng'ombe na mbuzi; matunda na mbogamboga (maembe, maparachichi, mananasi na pilipili); na

iii. Ujio wa kampuni ya uandaaji wa matamasha na makongamano makubwa ya utalii na uwekezaji ya nchini Qatar KON Group ambayo imekubali kuandaa makongamano ya biashara na utalii wa Tanzania nchini humo.

**97. Mheshimiwa Spika**, aidha, pamoja na changamoto zilizosababishwa na UVIKO-19, Wizara iliendelea kutekeleza Diplomasia ya Uchumi kwa kutumia njia ya mtandao kuendesha makongamano na mikutano kama ifuatavyo:

i. Kongamano la 15 la biashara na uwekezaji kati ya India na Afrika lililofanyika mwezi Septemba 2020, ambapo Tanzania ilitangaza fursa zilizopo katika sekta za nishati, maji, kilimo, miundombinu, afya na TEHAMA;

ii. Kongamano la usalama wa chakula lililoandaliwa na taasisi ya *Improvate Teck Talk* ya Israel mwezi Septemba na Novemba 2020, ambapo Tanzania ilitangaza mazao ya kilimo yanayozalishwa nchini kwa wingi kwa ajili ya kupata soko katika Ukanda wa Mediterania;

iii. Mkutano baina ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania, Chama cha Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo Tanzania, Jumuiya ya Wafanyabiashara na Wawekezaji wa Afrika Mashariki nchini Sweden na mataifa ya Nordic uliofanyika mwezi Novemba 2020; na

iv. Mkutano kati ya wadau wa utalii wa hapa nchini na Chama cha Mawakala wa Usafiri wa Anga cha Uturuki

(TURSAB) uliofanyika mwezi Septemba 2020, ambapo pande hizo mbili zilikubaliana kuweka msingi wa ushirikiano katika kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania nchini Uturuki na kuongeza ushiriki wa Tanzania katika maonesho ya utalii yanayoandaliwa nchini humo.

## **4.2 Kuratibu Masuala ya Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa**

### **4.2.1 Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)**

**98. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kunufaika na fursa za mtangamano kama ifuatavyo:

#### **Mkutano wa 21 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**99. Mheshimiwa Spika**, mwezi Februari 2021, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 21 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika kwa njia ya mtandao. Katika Mkutano huo, Wakuu wa Nchi waliidhinisha lugha za Kiswahili na Kifaransa kutumika rasmi kwenye shughuli za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hatua ya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya Jumuiya ni muhimu kwa nchi yetu kwa sababu itachochea kuongezeka kwa matumizi ya lugha hiyo katika Nchi Wanachama na kutoa fursa za ajira kwa wataalamu wa Kiswahili hapa nchini kufundisha, kutoa huduma ya ukalimani na kutafsiri. Aidha, kurasimishwa kwa lugha ya Kiswahili kutarahisisha mawasiliano ya kibiashara miongoni mwa wananchi wa Jumuiya.

**100. Mheshimiwa Spika**, Mkutano huo pia uliazimia kwamba Nchi Wanachama zilizo tayari kuendelea na Mkataba wa Ubia wa Uchumi (EPA) ziruhusiwe kuanza mashauriano na Umoja wa Ulaya kwa kutumia kanuni ya *Variable Geometry*. Hii ni kutokana na kuwa baadhi ya Nchi Wanachama hazikubaliani na baadhi ya vipengele vilivyopo katika Mkataba huo.

**101. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Mkataba wa EPA kwa kutumia kanuni ya *Variable Geometry* unakabiliwa na changamoto. Kulingana na tafsiri ya Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki katika Shauri Na. 1 la mwaka 2010, Kanuni hii ni nyenzo ya utekelezaji wa makubaliano ya pamoja (consensus).

Kwa mujibu wa Mkataba wa EPA Nchi zote Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinatakiwa kusaini, kuridhia na kutekeleza Mkataba huo kwa pamoja na endapo baadhi ya nchi zitasaini na nyingine kutosaini, Mkataba hautakuwa wa Jumuiya na hivyo, kanuni ya *Variable Geometry* haiwezi kutumika. Kwa muktadha huo, uamuzi uliofikiwa wa kutumia kanuni hiyo kutekeleza Mkataba hautaathiri msimamo wa Tanzania wa kutaka kufanyika kwa maboresho katika baadhi ya vipengele vya Mkataba kabla ya kusainiwa.

**102. Mheshimiwa Spika**, Mkutano wa 21 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya pia ulimteua Dkt. Peter Mathuki kutoka Kenya kuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuchukua nafasi ya Balozi Liberat Mfumukeko kutoka Burundi ambaye amemaliza muda wake. Vilevile, Mkutano huo ulimchagua Mheshimiwa Uhuru Muigai Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Februari 2021 na Jamhuri ya Burundi kushika nafasi ya Mnukuu wa Vikao vya Jumuiya.

**103. Mheshimiwa Spika**, mwezi Februari 2021, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 40 wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mkutano huo ulijadili na kupitisha Sera ya Uwekezaji ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inayolenga kuboresha mazingira ya uwekezaji, kuvutia uwekezaji pamoja na kuitangaza Jumuiya ya Afrika Mashariki kama eneo moja la uwekezaji. Utekelezaji wa Sera hii utawezesha kukuza uwekezaji, kurazinisha vivutio vya uwekezaji pamoja na kutangaza Jumuiya ya Afrika Mashariki kama eneo moja la uwekezaji.

**104. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Mkutano wa 40 wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki ulipitisha azimio la kuanzisha Taasisi ya Fedha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ifikapo mwezi Julai, 2021.

### **Utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki**

**105. Mheshimiwa Spika**, mwezi Desemba 2020, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Dharura wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji la Afrika Mashariki uliofanyika kwa njia ya mtandao. Mkutano ulipokea na kuridhia Taarifa ya Biashara na Uwekezaji ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2019.

**106. Mheshimiwa Spika**, taarifa hiyo imebainisha kuwa thamani ya manunuzi baina ya Nchi Wanachama iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 2,835.9 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani milioni 3,175.8 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 12. Thamani ya mauzo ya bidhaa baina ya Nchi Wanachama iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 3,145.2 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani milioni 3,162.8 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 0.6.

**107. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Tanzania, thamani ya bidhaa zilizouzwa kwenda Nchi Wanachama iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 444.3 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani milioni 674.4 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 51.8. Thamani ya manunuzi ya bidhaa kutoka Nchi Wanachama iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 302.7 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani milioni 329.2 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 8.7. Aidha, takwimu za awali za mwaka 2020 zinaonesha mauzo ya Tanzania kwenda Nchi Wanachama ni Dola za Marekani milioni 812.55 wakati manunuzi kutoka Nchi Wanachama yalikuwa Dola za Marekani milioni 324.31. Baadhi ya bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni mahindi, mchele, bidhaa za chuma, marumaru, karatasi na saruji.

**108. Mheshimiwa Spika**, Tanzania imeendelea kuwawezesha wafanyabiashara wadogo kunufaika na fursa zilizopo katika Mtangamano wa Afrika Mashariki. Katika kipindi cha mwezi Julai 2020 hadi Aprili, 2021 Tanzania ilitoa vyeti 37,111 vya uasili wa bidhaa kwa wafanyabiashara wadogo wa Tanzania wanaofanya biashara katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vyeti hivyo, vimewasaidia wafanyabiashara kupata unafuu wa kodi kwa kutolipa ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazozalishwa nchini na zinazokidhi vigezo vya uasili wa bidhaa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### **Utekelezaji wa Miradi na Programu za Miundombinu ya Kiuchumi na Huduma za Kijamii**

**109. Mheshimiwa Spika**, mwezi Aprili 2021, Wizara iliratibu na kushiriki ziara ya ukaguzi wa mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira ya Ziwa Victoria Awamu ya Pili unaotekelezwa katika Wilaya za Geita na Sengerema; mradi wa Kimataifa wa Mawasiliano na Uchukuzi katika Ziwa Victoria; na mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Bonde la Ziwa Victoria unaotekelezwa wilayani Magu. Miradi hiyo inayotekelezwa kwa uratibu wa Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria itawezesha wananchi waishio katika Bonde la Ziwa Victoria kupata maji safi na salama, kuimarisha utunzaji wa mazingira na kunufaika na matumizi endelevu ya rasilimali za bonde hilo.

**110. Mheshimiwa Spika**, mwezi Aprili 2021, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 20 wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Afya la Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika jijini Arusha. Katika mkutano huo, Nchi Wanachama zilikubaliana kuunda Kamati ya Uratibu ya Kikanda ya UVIKO – 19 na Kamati ya Ushauri ya Chanjo ya UVIKO – 19. Kamati hizo zitashauri namna ya kukabiliana na maambukizi ya UVIKO - 19 na utaratibu wa chanjo ya ugonjwa huo katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**111. Mheshimiwa Spika**, mwezi Februari 2021, Wizara iliratibu na kushiriki katika ziara ya kikanda ya ukaguzi wa mradi wa ujenzi wa kituo cha kufua umeme cha Murongo/Kikagati (MW 14) unaotekelezwa kati ya Tanzania na Uganda katika bonde

la Mto Kagera. Mradi unatekelezwa na mwekezaji binafsi, kampuni ya *Kikagati Power Company Limited (KPCL)* iliyosajiliwa nchini Uganda na Tanzania.

**112. *Mheshimiwa Spika***, mradi huo unahusisha pia ujenzi wa njia za kusafirisha umeme wa msongo wa kV 33 kutoka Murongo (Tanzania) hadi Kikagati (Uganda). Mradi utakapokamilika utahudumia maeneo ya wilaya za Kyerwa na Karagwe ambayo kwa sasa yanapata umeme kutoka Uganda kwa gharama kubwa.

**113. *Mheshimiwa Spika***, mwezi Novemba 2020, Wizara iliratibu uwasilishaji wa miradi ya miundombinu ya Tanzania katika awamu ya pili ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Miundombinu ya Afrika kupitia Kamisheni ya Umoja wa Afrika. Hatua hii ni utekelezaji wa programu ya miradi ya miundombinu ya Bara la Afrika. Miradi mitano ya Tanzania imejumuishwa katika programu hiyo miongoni mwa miradi 71 ya Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika itakayotekelezwa kwa kipindi cha mwaka 2021 – 2030.

**114. *Mheshimiwa Spika***, miradi ya Tanzania iliyojumuishwa ni: ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa ya Dar es Salaam – Tabora - Isaka – Mwanza, Tabora – Uvinza - Kigoma kwenda Kigali (Rwanda) na Musongati/Gitega (Burundi); ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa ya Mtwara – Mbamba Bay yenye matawi kwenda Liganga na Mchuchuma; ujenzi wa njia za kusafirisha umeme kutoka Masaka (Uganda) – Mwanza (kV 400); ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenda DRC kupitia Ziwa Tanganyika; na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenda Msumbiji.

**115. *Mheshimiwa Spika***, mwezi Septemba 2020, Wizara ilikagua utekelezaji wa miradi ya kikanda ya miundombinu katika mikoa ya Kigoma na Kagera inayotekelezwa na Serikali kupitia Programu ya Kuendeleza Mtandao wa Barabara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Miradi iliyokaguliwa ni ujenzi wa barabara ya Kabingo – Kasulu – Manyovu (km 260.6) unaohusisha pia ujenzi wa Kituo cha Huduma kwa Pamoja Mpakani (OSBP) Manyovu/Mugina

(Tanzania/Burundi); ujenzi wa barabara ya Bugene – Kasulo – Kumunazi (km 133); na ujenzi wa barabara ya Kyaka – Mutukula (km 30).

**116. *Mheshimiwa Spika***, Wizara pia ilikagua hali ya miundombinu na uendeshaji wa Vituo vya OSBP vya Kabanga/Kobero(Tanzania/Burundi),Mutukula/Mutuku la (Tanzania/Uganda) na Rusumo/Rusumo (Tanzania/Rwanda). Ukaguzi ulibaini changamoto zinazoathiri uendeshaji wa vituo vya OSBP na kupendekeza kuandaliwa mkakati wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa utatuzi wa changamoto zilizobainika ili kuandaa modeli moja ya OSBP. Mapendekezo hayo yamewasilishwa kwenye Sekretarieti ya Jumuiya kwa ajili ya hatua zaidi.

**117. *Mheshimiwa Spika***, kufuatia ziara hiyo ya ukaguzi, mwezi Novemba 2020, Wizara iliratibu uwekaji saini Hati ya Makubaliano baina ya Tanzania, Burundi, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Taasisi ya Uwezeshaji Usafiri katika Ushoroba wa Kati. Hati hiyo inahusu kusimamia utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Kabingo – Kasulu – Manyovu (km 260.6) /Rumonge – Gitaza (km 45). Uwekaji saini ulifuatiwa na makabidhiano ya eneo la ujenzi wa Kituo cha Huduma kwa Pamoja Mpakani (OSBP) Manyovu/Mugina (Tanzania/Burundi). Mradi huo unatekelezwa kwa mkopo wa Dola za Marekani milioni 256.2 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika.

**118. *Mheshimiwa Spika***, barabara hiyo ni kiungo muhimu cha mtandao wa barabara kwa upande wa mikoa ya magharibi mwa Tanzania inayounganisha bandari ya Dar es Salaam na nchi za Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Aidha, utekelezaji wake unahusisha uboreshaji wa miundombinu ya huduma za kijamii katika wilaya za Buhigwe, Kasulu na Kibondo ikiwemo ujenzi wa stendi mpya za mabasi; ukarabati wa masoko; ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji na usafi wa mazingira; ujenzi wa vituo vya afya na ukarabati wa hospitali za wilaya za Kasulu na Kibondo pamoja na ununuzi wa magari manne (4) ya kubebea wagonjwa katika miji ya Makere na Busunzu.

**119. Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kuratibu Miradi ya Miundombinu ya Vipaumbele ya Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kufuatilia utekelezaji wake. Katika kipindi hiki mradi wa ujenzi wa Jengo la Abiria la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (Terminal III) umekamilika na ulizinduliwa mwezi Septemba 2020 na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Awamu ya Saba wa Zanzibar.

**120. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki iliratibu kupatikana kwa fedha kiasi cha shilingi bilioni 371.36 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kipande cha Pangani – Mkange (km 124.5) na daraja la Pangani katika barabara ya kikanda ya Bagamoyo – Tanga Horohoro/Lungalunga - Malindi (km 425); Dola za Marekani milioni 256.2 kutoka AfDB kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami ya Kasulu – Kabingo - Manyovu (km 260.6)/ Rumonge – Gitaza (km 45); na Dola za Marekani milioni 12 kutoka AfDB kwa ajili ya ujenzi wa jengo la OSBP Manyovu/Mugina. Aidha, Wizara iliratibu upatikanaji wa fedha kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Rusumo – Lusahunga kwa kiwango cha lami, ambapo taratibu za kumpata mkandarasi zinaendelea.

**121. Mheshimiwa Spika**, mwezi Septemba 2020, Wizara iliratibu na kushiriki katika Maadhimisho ya Siku ya Mara yaliyofanyika Butiama mkoani Mara, kwa lengo la kuhamasisha utunzaji wa mazingira katika Bonde la Mto Mara. Maadhimisho hayo yalikusisha upandaji miti na majadiliano ya mikakati ya utunzaji wa mazingira ya bonde la mto huo. Kufanyika kwa maadhimisho hayo hapa nchini kumetoa fursa kwa wananchi wa maeneo ya wilaya ya Butiama na maeneo mengine ya jirani kunufaika na fursa za biashara.

**122. Mheshimiwa Spika**, mwezi Agosti 2020, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye uzinduzi wa Kitaifa wa mradi wa kuwawezesha wanawake kiuchumi ujulikanao kama “ *50 Million African Women Speak Networking Platform*”. Uzinduzi huo ulifanywa na Mawaziri wanaohusika na Maendeleo ya



Jamii katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Mradi huu unatekelezwa katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Soko la Pamoja la Mashariki na Kusini mwa Afrika (COMESA) na Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS). Kwa mwaka 2020, mradi uliwezesha wanawake wapatao 5000 kutoka pande zote mbili za Muungano kupata taarifa muhimu za ujasiriamali kwa njia ya mtandao.

**123. Mheshimiwa Spika**, katika kufanikisha utekelezaji wa mradi huo nchini, Wizara iliratibu mafunzo ya kuwawezesha wanawake kiuchumi yaliyofanyika mwezi Desemba 2020 jijini Dar es Salaam. Mafunzo hayo yalishirikisha takribani wanawake 200 kutoka Taasisi za Serikali na Asasi za Kiraia zinazoratibu masuala ya maendeleo ya wanawake kutoka pande zote mbili za Muungano. Mafunzo hayo yaliwajengea uwezo wa kutumia mtandao wa kuwaunganisha wanawake milioni 50 Barani Afrika; kuwahamasisha kuwa mabalozi na waelimishaji kwa wanawake wengine katika kutatua changamoto zinazowakabili kibiashara; na kutoa elimu ya fursa za kibiashara.

**124. Mheshimiwa Spika**, mwezi Julai 2020, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Pamoja wa Mawaziri wa Mambo ya Nje, Afya na Miundombinu wa Nchi za Tanzania na Rwanda kujadili zuio la malori ya mizigo kutoka Tanzania kuvuka mpaka wa Rusumo kuingia Rwanda kwa lengo la kudhibiti kuenea kwa UVIKO-19. Mkutano huo uliwezesha kupatikana kwa ufumbuzi wa mgogoro uliokuwepo kwa pande mbili kukubaliana kuendelea kutekeleza mwongozo uliotolewa na Mawaziri wa Afya wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mkutano wa Dharura uliofanyika mwezi Machi 2020.

**125. Mheshimiwa Spika**, Wizara imefanikisha kupatikana kwa wajumbe saba watakaoiwakilisha Tanzania katika Bodi ya Wakurugenzi wa Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2020 hadi 2025. Kati ya hao, wajumbe wanne wanatoka Tanzania Bara na watatu Zanzibar.

**126. Mheshimiwa Spika**, wajumbe hao ni Prof. James E. Mdoe, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Dkt. Amos Nungu, Mkurugenzi Mkuu wa Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia; Dkt. Ali Ahmed Uki, Mkufunzi Mwandamizi kutoka Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU); Dkt. Rose Rita Kingamkono, Mwenyekiti Mtendaji wa Taasisi ya Maendeleo ya Wanawake kwenye Masuala ya Kilimo (CAWAT); Dkt. Asifu Petro Nanyaro, Katibu Mtendaji wa *Tanzania Academy of Science - TAAS*; Dkt. Haji Mwevura Haji, Mkufunzi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA); na Dkt. Zidi Mussa Makame, Mkufunzi Mwandamizi wa Chuo cha Sayansi cha Karume (Zanzibar).

### **Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki**

**127. Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika maandalizi ya Rasimu ya Katiba ya Fungamano la Kisiasa la Afrika Mashariki kama hatua ya mpito kuelekea Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki. Hadi kufikia mwezi Aprili 2021, zoezi la kukusanya maoni na kutoa elimu kwa umma limefanyika katika nchi za Burundi na Uganda. Kulingana na ratiba ya zoezi hilo, timu ya wataalam ya Jumuiya inayokusanya maoni kuhusiana na rasimu ya katiba hio itatembelea Tanzania mwezi Agosti 2021.

### **Demokrasia na Utawala Bora**

**128. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki, nchi mbili wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda zilifanya Uchaguzi Mkuu. Jumuiya ya Afrika Mashariki ilituma timu ya waangalizi wa uchaguzi hapa nchini mwezi Oktoba 2020. Timu hiyo iliongozwa na Mheshimiwa Sylvester Ntibantunganya, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Burundi. Katika uchaguzi huo Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyekuwa mgombea kutoka Chama Cha Mapinduzi alishinda nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kwa upande wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi mgombea kutoka Chama Cha Mapinduzi alishinda nafasi ya Rais wa Zanzibar.

**129. Mheshimiwa Spika**, taarifa ya timu ya waangalizi wa uchaguzi kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki ilieleza kuwa uchaguzi huo ulifanyika katika mazingira ya amani na utulivu, na ulikidhi vigezo vya kuwa huru na haki kama ilivyoainishwa katika mwongozo wa uangalizi wa uchaguzi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**130. Mheshimiwa Spika**, mwezi Januari 2021, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika timu ya waangalizi wa uchaguzi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye Uchaguzi Mkuu nchini Uganda. Zoezi la uangalizi lililenga kuhakikisha kuwa misingi ya demokrasia inatekelezwa kama ilivyoainishwa katika Kanuni za msingi za Jumuiya. Katika uchaguzi huo, Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni mgombea kupitia Chama cha *National Resistance Movement* alishinda nafasi ya Rais. Taarifa ya awali ya waangalizi wa uchaguzi kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki inaonesha uchaguzi huo ulifikia vigezo vya msingi vilivyoainishwa katika mwongozo wa uangalizi wa uchaguzi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### **Ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya Nyingine a) Utatu wa COMESA-EAC-SADC**

**131. Mheshimiwa Spika**, mwezi Machi 2021, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Kwanza wa Kamati ya Mawaziri wa Utatu wa COMESA – EAC – SADC wanaohusika na Biashara, Fedha, Uchumi, Mambo ya Ndani na Afya uliofanyika kwa njia ya mtandao. Mkutano huo uliridhia na kupitisha Mwongozo wa Kusimamia Uvukaji Salama wa Watu na Mizigo kwa kipindi cha mlipuko wa UVIKO-19 kwa kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa na Nchi Wanachama; na kuhimiza kuendelea kubadilishana uzoefu wa njia bora za kukabiliana na kudhibiti ugonjwa huo.

**132. Mheshimiwa Spika**, mwezi Februari 2021, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Pili wa Dharura wa Baraza la Mawaziri wa Eneo Huru la Biashara la Utatu wa COMESA-EAC-SADC uliofanyika kwa njia ya mtandao. Mkutano ulipokea taarifa ya kusainiwa na kuridhiwa kwa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Utatu wa COMESA-EACSADC.

**133. *Mheshimiwa Spika***, nchi 10 kati ya 22 zilizosaini Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Utatu wa COMESA-EAC-SADC zimeridhia na kuwasilisha hati za kuridhia mkataba huo kwa Mwenyekiti wa Sekretarieti ya Utatu. Mkataba utapata nguvu ya kisheria na kuanza kutekelezwa baada ya nchi 14 kuridhia na kuwasilisha hati za kuridhia. Tanzania inaendelea na taratibu za kuridhia Mkataba huo.

**b) Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika**

**134. *Mheshimiwa Spika***, mwezi Desemba 2020, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 13 wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika kwa njia ya mtandao. Mkutano huo pamoja na maamuzi mengine, ulielekeza Nchi Wanachama kukamilisha majadiliano ya Viambatisho vya Ufunguaji wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Vigezo vya Uasilia wa Bidhaa ili biashara katika Eneo Huru la Biashara la Afrika iweze kuanza ifikapo tarehe 01 Januari, 2021. Hata hivyo, kutokana na kuendelea kuenea kwa UVIKO-19, Nchi Wanachama hazikufanikiwa kukamilisha majadiliano ya Viambatisho husika na hivyo kuathiri mtiririko wa biashara baina ya Nchi Wanachama. Majadiliano ya Viambatisho hivyo yanatarajiwa kukamilika Juni, 2021 na biashara kuanza Julai, 2021.

**c) Majadiliano ya Mkataba wa Biashara Baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Uingereza**

**135. *Mheshimiwa Spika***, mwezi Septemba 2020, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji la Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika kwa njia ya mtandao. Mkutano huo ulijadili maombi ya Uingereza ya kufanya majadiliano ya Mkataba rasmi wa Biashara na Jumuiya ya Afrika Mashariki, kufuatia Uingereza kujitoa katika Umoja wa Ulaya.

**136. *Mheshimiwa Spika***, Baraza la Mawaziri la Kisekta, lilikubaliana na pendekezo la majadiliano hayo na kuagiza Nchi Wanachama kushiriki majadiliano kwa pamoja kama Jumuiya. Aidha, ilipendekezwa Serikali ya Uingereza isogeze mbele muda wa kukamilisha majadiliano kutoka tarehe 31

Desemba, 2020 hadi tarehe 31 Desemba, 2021 ili kutoa muda kwa Nchi Wanachama kufanya mashauriano ya ndani.

**137. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Uingereza haikuafiki mapendekezo hayo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kusisitiza azma yake ya kuendelea na majadiliano na nchi zitakazokuwa tayari. Kufuatia msimamo huo, Kenya iliendelea na majadiliano na kusaini Mkataba huo mwezi Desemba, 2020. Hata hivyo, Ibara ya 37(4) ya Itifaki ya Umoja wa Forodha inazitaka Nchi Wanachama kutoa taarifa ya kusudio la kuingia Mkataba wa Biashara na Nchi nyingine nje ya Umoja wa Forodha, kwa lengo la kuwezesha nchi nyingine kutoa maoni kama Mkataba huo una athari kwenye Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki. Hivyo, Katibu Mkuu wa Jumuiya ameikumbusha Jamhuri ya Kenya kuzingatia matakwa ya Ibara hiyo.

#### **Bunge la Afrika Mashariki**

**138. Mheshimiwa Spika**, mwezi Januari hadi Februari 2021, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Pili, Kikao cha Nne cha Bunge la Nne la Afrika Mashariki uliofanyika kwa njia ya mtandao. Mkutano huo ulijadili muswada binafsi wa sheria kuhusu mifugo. Lengo la muswada huo ni kuweka mfumo wa kisheria wa kuratibu masuala ya mifugo katika Jumuiya ikiwa ni pamoja na kudhibiti magonjwa yanayoathiri mifugo. Vilevile, Bunge lilijadili na kupitisha muswada binafsi wa sheria kuhusu masuala ya uadilifu na mapambano dhidi ya rushwa. Muswada huo unalenga kukuza uadilifu na kuimarisha mfumo wa kisheria katika kuzuia na kupambana na masuala ya rushwa katika Asasi na Taasisi za Jumuiya.

#### **4.2.2 Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)**

**139. Mheshimiwa Spika**, mwezi Mei 2021, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Mawaziri wanaohusika na Masuala ya Kazi na Ajira katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Kupitia Mkutano huo Nchi Wanachama wa SADC ziliweka msimamo wa pamoja kuhusu maboresho ya Katiba ya Shirika la Kazi Duniani. Marekebisho hayo yanalenga kuongeza wigo wa demokrasia katika maamuzi ndani ya

Shirika hilo. Msimamo huo wa nchi za SADC unatarajiwa kuwasilishwa katika vikao vya Umoja wa Afrika kwa majadiliano na kuweka msimamo wa pamoja wa nchi za Afrika kuhusu maboresho ya Katiba ya Shirika la Kazi Duniani.

**140. Mheshimiwa Spika**, mwezi Aprili 2021, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Troika Mbili wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika uliofanyika jijini Maputo, Msumbiji. Troika Mbili inajumuisha Jamhuri ya Msumbiji (Mwenyekiti wa sasa wa SADC), Jamhuri ya Malawi (Mwenyekiti ajaye), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mwenyekiti aliyemaliza muda wake), Jamhuri ya Botswana (Mwenyekiti wa sasa wa Asasi ya SADC ya Ushirikiano wa Siasa, Ulinzi na Usalama), Jamhuri ya Afrika Kusini (Mwenyekiti ajaye wa Asasi) na Jamhuri ya Zimbabwe (Mwenyekiti wa Asasi aliyemaliza muda wake). Katika Mkutano huo Nchi Wanachama zilizimia kuendelea kushirikiana kuimarisha hali ya ulinzi na usalama kaskazini mwa nchi ya Msumbiji hususan kwenye Jimbo la Cabo Delgado. Mkutano uliazimia kuiwezesha na kuitumia *Standby Force* ya SADC kutatua tatizo la ugaidi katika Jamhuri ya Msumbiji.

**141. Mheshimiwa Spika**, mwezi Machi 2021, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika uliofanyika kwa njia ya mtandao. Mkutano huo uliridhia kuongeza wigo wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mikutano ya kisékta ya SADC. Aidha, Mkutano ulielekeza Sekretarieti ya SADC kukamilisha ujenzi wa sanamu ya Mwalimu Nyerere inayojengwa katika Jengo la Amani na Usalama kwenye Makao Makuu ya Umoja wa Afrika jijini Addis Ababa, Ethiopia ifikapo mwezi Aprili 2022. Vilevile, Mkutano huo uliridhia kufanyika kwa maadhimisho ya kumbukumbu ya miaka 40 ya SADC na kuhimiza Nchi Wanachama kutangaza mafanikio ya SADC na kuelimisha umma juu ya programu zinazofanywa na Jumuiya hiyo.

**142. Mheshimiwa Spika**, mwezi Desemba 2020, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Dharura wa Ngazi

ya Juu wa Mashauriano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa nchi za Afrika Kusini, Botswana, Msumbiji, Tanzania na Zimbabwe uliofanyika jijini Maputo, Msumbiji. Mkutano huo uliweka mikakati ya pamoja ya kuimarisha amani katika Jumuiya ya SADC.

**143. Mheshimiwa Spika**, mwezi Novemba 2020, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Troika Mbili wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Washirika wa Maendeleo uliofanyika kwa njia ya mtandao. Kupitia mkutano huo, Nchi Wanachama wa SADC na Washirika wa Maendeleo zilikubaliana kujikita katika kujenga uwezo wa kitaasisi na kitaalam, uhaulishaji wa teknolojia na misaada ya kifedha katika kutekeleza miradi ya kuhifadhi mazingira.

**144. Mheshimiwa Spika**, mwezi Novemba 2020, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wanaounda Utatu wa Asasi ya SADC ya Ushirikiano katika Siasa, Ulinzi na Usalama uliofanyika jijini Gaborone, Botswana. Mkutano huo pia ulishirikisha nchi za Msumbiji, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) pamoja na nchi za Tanzania, Malawi na Afrika Kusini ambazo zinachangia vikosi vya kijeshi katika Kikosi Maalum cha Ulinzi wa Amani (Force Intervention Brigade - FIB) kilichopo DRC. Mkutano huo uliweka mikakati ya pamoja ya kukabiliana na ongezeko la matukio ya ugaidi na uvunjifu wa amani katika nchi za Msumbiji na DRC. Aidha, Mkutano huo uliridhia kuanzishwa kwa Kituo cha SADC cha Kupambana na Ugaidi.

#### **4.2.3 Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Mwambao wa Bahari ya Hindi (IORA)**

**145. Mheshimiwa Spika**, mwezi Desemba 2020, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 20 wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Nchi zilizopo kwenye Mwambao wa Bahari ya Hindi (IORA) uliofanyika kwa njia ya mtandao. Vilevile, mwezi Februari 2021, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mjadala wa Saba wa IORA uliofanyika kwa njia ya mtandao. Katika mikutano hiyo, Nchi Wanachama zilikubaliana kuendelea kuimarisha ushirikiano katika kukuza

uchumi kupitia uchumi wa bluu; kuimarisha ajira, biashara na uwekezaji; kuimarisha ulinzi na usalama wa bahari na kupunguza athari za maafa na majanga; kuimarisha usafiri na usafirishaji wa baharini; na kuendelea kuwawezesha wanawake na vijana kiuchumi.

#### 4.2.4 Umoja wa Afrika

**146. Mheshimiwa Spika**, mwezi Mei 2021, Wizara iliratibu ushiriki wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Mkutano wa Mtandao wa Viongozi Wanawake Barani Afrika (AWLN) uliofanyika kwa njia ya mtandao. Wakati wa Mkutano huo, Mheshimiwa Rais alipongezwa kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuahidiwa kupewa ushirikiano katika masuala mbalimbali yakiwemo maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii, haki za wanawake, amani na usalama wa kikanda na kukabiliana na janga la UVIKO-19.

**147. Mheshimiwa Spika**, pamoja na masuala mengine, Mheshimiwa Rais ameahidi kuendelea kushirikiana na Taasisi na Mashirika ya Kimataifa katika kukuza maendeleo nchini na kuendelea kuwapa kipaumbele wanawake katika nafasi mbalimbali za Uongozi Serikalini.

**148. Mheshimiwa Spika**, mwezi Februari 2021, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 34 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika kwa njia ya mtandao. Baadhi ya agenda zilizojadiliwa katika Mkutano huo ni: programu ya kutekeleza kaulimbiu ya mwaka 2021 inayosema **“Sanaa, Tamaduni na Urithi katika kufikia Azma ya Afrika Tuitakayo”**; mapambano dhidi ya UVIKO-19; uchaguzi wa uongozi mpya wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi 2024; na uchaguzi wa majaji wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu.

**149. Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano huo, Umoja wa Afrika pia uliridhia ombi la Tanzania la kujumuisha lugha ya Kiswahili na uanzishaji wa Kituo cha Urithi wa Afrika jijini Dar es Salaam katika programu ya kutekeleza kaulimbiu ya mwaka 2021 inayosema **“Sanaa, Tamaduni na Urithi katika kufikia Azma**



**ya Afrika Tuitakayo".** Maamuzi hayo yamejumuishwa kwenye shughuli za programu hiyo zinazotekelezwa na Umoja wa Afrika katika mwaka 2021.

**150. Mheshimiwa Spika,** vilevile, katika Mkutano huo Tanzania ilisitiza umuhimu wa Afrika kuwajengea uwezo wataalam wake katika eneo la tafiti kwenye sekta ya afya. Msisitizo uliwekwa katika kutengeneza dawa za kujikinga na kutibu maradhi ikiwemo chanjo dhidi ya UVIKO-19 na magonjwa mengine ili Afrika iweze kujitegemea katika sekta ya afya kwa kuongeza urahisi na unafuu wa upatikanaji wa dawa.

**151. Mheshimiwa Spika,** aidha, Nchi Wanachama zilimchagua Mhe. Moussa Faki Mahamat kutoka Chad kuwa Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika kwa muhula wa pili. Mkutano pia ulimchagua Mhe. Dkt. Monique Nsanzabaganwa kutoka Rwanda kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamisheni hiyo. Viongozi hao watahudumu kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2021 hadi 2024.

**152. Mheshimiwa Spika,** Mkutano huo pia ulifanya uchaguzi wa majaji wanne wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Mhe. Jaji Imani Aboud, Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania alichaguliwa kwa kura 51 kati ya kura 52 zilizopigwa kuhudumu katika Mahakama hiyo kwa muhula wa pili wa miaka sita kuanzia mwezi Februari 2021. Wingi wa kura alizozipata Mhe. Jaji Imani Aboud ni ushahidi wa kutosha wa ukomavu wa diplomasia yetu na kuungwa mkono kwa nchi yetu na nchi nyingine za Afrika.

**153. Mheshimiwa Spika,** vilevile, Tanzania ilitumia nafasi ya Mkutano huo kuzitaarifu nchi za Umoja wa Afrika kuhusu hali ya kisiasa nchini na namna ambavyo nchi yetu inaendelea kuheshimu utawala wa sheria na haki za binadamu tofauti na habari potofu zilizokuwa zikisambazwa baada ya kukamilika kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Tanzania ilihakikishia Umoja huo kwamba uchaguzi ulikuwa wa haki, huru na wazi, uliozingatia misingi ya demokrasia na utawala bora, na ulifanyika katika mazingira ya amani na utulivu.

**154. Mheshimiwa Spika**, mwezi Januari 2021, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Kamati Maalum ya Umoja wa Afrika ya Mawaziri wa Ulinzi uliofanyika kwa njia ya mtandao. Mkutano huo ulipitisha mwongozo wa Umoja wa Afrika kuhusu upangaji, uendeshaji na usimamizi wa shughuli za ulinzi wa amani Barani Afrika.

**155. Mheshimiwa Spika**, mwezi Desemba 2020, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika kwa njia ya mtandao. Mkutano huo ulijadili taarifa ya utekelezaji wa Mkakati wa Kumaliza Vita Barani Afrika ifikapo mwaka 2020. Mkutano uliongeza muda wa utekelezaji wa Mkakati huo kwa miaka 10 kuanzia mwaka 2021 hadi 2030 ikiwa ni pamoja na kuendelea kuadhimisha mwezi wa usalimishaji wa silaha haramu kwa hiari mwezi Septemba kila mwaka.

**156. Mheshimiwa Spika**, Mkutano huo pia uliamua kuwa ni vyema Nchi Mwanachama wa Umoja huo kabla ya kuingia makubaliano ya kuwa wenyeji wa kambi za kijeshi za mataifa ya nje kushauriana na Baraza la Amani na Usalama la Afrika, Jumuiya za kikanda pamoja na nchi jirani ili kuhakikisha zinakidhi malengo ya Umoja wa Afrika.

**157. Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano huo, Tanzania ilitoa wito kwa Jumuiya ya Kimataifa kutoingilia mambo ya ndani ya Afrika. Tanzania pia ilisisitiza umuhimu wa Umoja wa Afrika kuendelea kuzungumza kwa kauli moja na kuhakikisha Afrika inapata nafasi mbili za kudumu na tano zisizo za kudumu za uwakilishi katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

#### **4.2.5 Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu (ICGLR)**

**158. Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Misheni ya Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu ya uangalizi wa Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Kongo uliofanyika tarehe 21 Machi, 2021. Katika uchaguzi huo Mheshimiwa Denis Sassou-Nguesso alishinda nafasi ya Rais kupitia Chama cha *Congolese Labour Party* kwa kupata asilimia 88 ya kura zilizopigwa.

**159. Mheshimiwa Spika**, mwezi Novemba 2020, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa Nane wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu uliofanyika kwa njia ya mtandao. Mkutano huo ulipokea na kujadili taarifa ya hali ya amani na usalama katika Ukanda wa Maziwa Makuu. Taarifa hiyo, ilieleza kuimarika kwa hali ya amani na usalama kwenye maeneo mengi ya ukanda huo isipokuwa Jamhuri ya Afrika ya Kati na eneo la Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambayo yanaendelea kukabiliwa na changamoto za kiusalama. Vilevile, Mkutano uliridhia wito uliotolewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Nchi Wanachama kuendelea kushirikiana katika kupambana na vikundi vyenye silaha ili kuimarisha hali ya utulivu katika Ukanda huo.

#### **4.2.6 Ushirikiano wa Kimataifa**

**160. Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Kikao cha 46 cha Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa kilichofanyika kuanzia mwezi Februari hadi Machi 2021 Geneva, Uswisi. Katika Kikao hicho, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipata fursa ya kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa haki za binadamu nchini ikiwa ni pamoja na hatua zilizofikiwa katika kutoa haki ya elimu, huduma za afya, maji safi na salama pamoja na nishati.

**161. Mheshimiwa Spika**, Tanzania pia ilitumia Kikao hicho kuielezea jumuiya ya kimataifa kuhusu Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba 2020 ambao kwa mara ya kwanza katika historia ya Taifa letu uligharamiwa kwa fedha za ndani; na kuwa uchaguzi huo ulikuwa wa haki, huru na wazi, uliozingatia misingi ya demokrasia na utawala bora, na ulifanyika katika mazingira ya amani na utulivu. Hatua hizi, zimesaidia kujenga mtazamo chanya kwa jumuiya ya kimataifa kuhusu Taifa letu ambao ni muhimu katika kuimarisha mahusiano na ushirikiano kati ya nchi yetu na jumuiya ya kimataifa.

**162. Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Kikao cha 75 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kilichofanyika kuanzia mwezi Septemba hadi Desemba 2020.

Tanzania ilitumia fursa hiyo kueleza jumuiya ya kimataifa kuhusu hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha huduma za kijamii na kutengeneza fursa za kiuchumi kwa kuimarisha miundombinu ya reli, barabara, maji, nishati, afya na elimu. Vilevile, Tanzania ilieleza kuhusu hatua zinazochukuliwa katika kupambana na rushwa na ubadhirifu wa mali za umma; kusimamia nidhamu kwenye utumishi wa umma; na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**163. *Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Umoja wa Mataifa, mashirika, taasisi na majukwaa ya kimataifa.

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kutokana na ushiriki huo ni pamoja na:

i. Kujumuishwa kwa Tanzania katika Programu Shirikishi baina ya Nchi na Washirika wa Maendeleo kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO) mwezi Novemba 2020. Programu hii inalenga kuzisaidia Nchi Wanachama kujiletea maendeleo jumuishi na endelevu ya viwanda. Majadiliano yanaendelea kati ya Serikali na UNIDO ya kuandaa andiko la utekelezaji wa programu hiyo litakaloainisha vipaumbele vya nchi;

ii. Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) umeridhia kutoa mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Marekani milioni 58.8. Fedha hizo zitatumika kuendeleza sekta ya uvuvi kwa kununua meli nane za uvuvi katika bahari kuu ambapo meli nne zitatumika Tanzania Bara na nne Zanzibar. Vilevile, fedha hizo zitategeneza miundombinu ya ufugaji wa samaki na kuimarisha vikundi shirikishi vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika maeneo ya bahari kuu. Kadhalika, fedha hizo zitatumika kuimarisha uwezo wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania na kuboresha uzalishaji wa mbegu bora katika mashamba ya Wakala wa Mbegu Tanzania; na

iii. Tanzania kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Hati za Utambulisho ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kwa mwaka 2020/2021. Kamati hiyo ina jukumu la kupitia hati zote

za utambulisho zinazowasilishwa na Wakuu wa Nchi na Serikali au Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa na kujiridhisha iwapo zimekidhi vigezo na masharti kwa mujibu wa sheria za kimataifa na Mkataba wa Umoja huo.

**164. Mheshimiwa Spika**, mafanikio haya ni ishara ya kuaminika na kukubalika kwa misimamo na sera za nchi yetu kimataifa.

#### **4.3 Kufuatilia na Kusimamia Utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa na Hati za Makubaliano**

**165. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara iliratibu na kushiriki katika majadiliano na kusimamia uwekaji saini Mikataba na Hati za Makubaliano ya Kimataifa zifuatazo:

i. Mkataba wa Uenyeji kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kampuni ya Mafuta Ghafi ya Afrika Mashariki (EACOP) kuhusu Ujenzi wa Mradi wa Bomba la kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima, Uganda mpaka Tanga, Tanzania mwezi Mei, 2021;

ii. Hati ya Makubaliano ya Kusafirisha Gesi Asilia kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kenya mwezi Mei 2021;

iii. Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano katika Masuala ya Utamaduni, Sanaa, Mahusiano ya Jamii na Urithi wa Taifa kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Kenya mwezi Mei 2021;

iv. Hati ya Makubaliano kuhusu Mradi wa Kufua Umeme kwa Kutumia Nishati ya Gesi kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kampuni ya *Monitor Power System* ya Norway mwezi Februari 2021;

v. Hati ya Makubaliano Kuanzisha Ushirikiano wa Kijeshi kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu mwezi Februari 2021;

vi. Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano katika Mapambano dhidi ya Rushwa kati ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Taifa la Palestina mwezi Februari 2021;

vii. Mkataba kati ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Ulinzi ya Shirikisho la Ujerumani kuhusu Msaada wa Vifaa kwa kipindi cha tarehe 1 Januari 2021 hadi tarehe 31 Desemba 2024;

viii. Hati ya Makubaliano Kuanzisha Tume ya Pamoja ya Ushirikiano wa Kiuchumi kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kiislam ya Pakistan mwezi Desemba 2020;

ix. Hati ya Makubaliano kuhusu Mashauriano ya Kisiasa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kiislam ya Pakistan mwezi Desemba 2020;

x. Hati ya Makubaliano Kuanzisha Ushirikiano kati ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Mambo ya Nje na Biashara ya Serikali ya Hungary kuhusu Mpango wa Mafunzo kwa mwaka 2021 – 2023 mwezi Desemba 2020;

xi. Mkataba wa Uwakilishi wa Heshima kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bw. Jhody Prabawa, Mwakilishi wa Heshima wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Jamhuri ya Indonesia mwezi Novemba 2020; na

xii. Hati ya Makubaliano ya Kusimamia Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kabingo – Kasulu – Manyovu (Kilometa 260)/ Rumonge Gitaza (Kilometa 45) baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Jamhuri ya Burundi, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Taasisi ya Ushoroba wa Kati mwezi Novemba 2020.

**166. Mheshimiwa Spika**, Mikataba na Hati za Makubaliano zilizosainiwa zinalenga kuimarisha ushirikiano uliopo kati ya Tanzania na nchi marafiki, Jumuiya za Kikanda na Kimataifa. Tanzania itanufaika na fursa zilizopo katika maeneo yaliyolengwa katika mikataba pamoja na makubaliano hayo.

#### **4.4 Kuratibu Masuala ya Itifaki, Uwakilishi na Huduma za Kikonseli**

**167. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara imeendelea kuratibu masuala ya itifaki na huduma za kikonseli kama ifuatavyo:

##### **4.4.1 Ziara za Viongozi wa Kitaifa na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa Kutoka Nje ya Nchi**

**168. Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto za kusafiri kimataifa zinazosababishwa na janga la UVIKO-19, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara imeendelea kuratibu ziara za viongozi wa kitaifa na mashirika ya kikanda na kimataifa waliotembelea nchini kama ifuatavyo:

i. Ziara ya Mheshimiwa Ezechiel Nibigira, Waziri wa Masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Vijana, Michezo na Utamaduni na Mjumbe Maalum wa Rais wa Jamhuri ya Burundi tarehe 21 Mei, 2021;

ii. Ziara za Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda tarehe 20 Mei, 2021 na 13 Septemba, 2020;

iii. Ziara ya Mheshimiwa Mikhail Bogdano, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Mjumbe Maalum wa Rais wa Shirikisho la Urusi tarehe 14 Mei, 2021;

iv. Ziara ya Mheshimiwa James Duddrige, Waziri wa Uingereza anayeshughulikia masuala ya Afrika tarehe 11 Mei, 2021;

v. Ziara ya Mheshimiwa Balozi Dkt. Amina Mohamed, Waziri wa Michezo, Utamaduni na Urithi wa Jamhuri ya Kenya,

Mjumbe Maalum wa Mheshimiwa Uhuru Muigai Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya tarehe 10 Aprili, 2021;

vi. Ziara ya Mheshimiwa Sahle – Work Zewde, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia tarehe 25 Januari 2021;

vii. Ziara ya Mheshimiwa Filipe Jacinto Nyusi, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji tarehe 11 Januari 2021;

viii. Ziara ya Mheshimiwa Wang Yi, Mjumbe wa Baraza la Taifa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Watu wa China tarehe 7 hadi 8 Januari 2021;

ix. Ziara ya Mheshimiwa Dkt. Netumbo NandiNdaitwah, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Jamhuri ya Namibia tarehe 8 Desemba, 2020;

x. Ziara ya Mheshimiwa Dkt. Lazarus McCarthy Chakwera, Rais wa Jamhuri ya Malawi tarehe 7 hadi 8 Oktoba, 2020; na

xi. Ziara ya Mheshimiwa Meja Jenerali Évariste Ndayishimiye, Rais wa Jamhuri ya Burundi tarehe 19 Septemba, 2020.

**169. Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu ziara za viongozi mbalimbali waliokuja nchini kushiriki hafla ya uapisho wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyofanyika tarehe 5 Novemba, 2020 jijini Dodoma. Viongozi hao ni:

i. Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda;

ii. Mheshimiwa Emmerson Dambuzo Mnangagwa, Rais wa Jamhuri ya Zimbabwe;

iii. Mheshimiwa Azali Assoumani, Rais wa Muungano wa Visiwa vya Comoro;



iv. Mheshimiwa Slumber Tsogwane, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Botswana;

v. Mheshimiwa Alain Guillaume Bunyoni, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Burundi;

vi. Mheshimiwa Carlos Agostinho Do Rosário, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Msumbiji;

vii. Mheshimiwa Adan Mohamed, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Maendeleo ya Kikanda na Mjumbe Maalum wa Mheshimiwa Uhuru Muigai Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya;

viii. Mheshimiwa Sultan Bin Saad Al – Muraikhi, Waziri wa Mambo ya Nje wa Taifa la Qatar na Mjumbe Maalum wa Mtukufu Sheikh Tamim bin Hamad Al-Thani, Emir wa Taifa la Qatar; na

ix. Mheshimiwa Sylvestre Ntibantunganya, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Burundi na aliyekuwa Mwenyekiti wa Timu ya Uangalizi wa Uchaguzi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**170. Mheshimiwa Spika**, hafla hiyo ilihudhuriwa pia na Mawaziri kutoka nchi mbalimbali kama ifuatavyo:

i. Mheshimiwa Dkt. Naled Pandor, Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Afrika Kusini;

ii. Mheshimiwa Andre Kabanda Kana, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo;

iii. Mheshimiwa Mohamed Sidik Mia, Waziri wa Uchukuzi na Ujenzi wa Jamhuri ya Malawi;

iv. Mheshimiwa Gospel Kazako, Waziri wa Habari wa Jamhuri ya Malawi;

v. Mheshimiwa Mhandisi Dkt. Asim Abdelhamid ElGazar, Waziri wa Makazi wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri; na

vi. Mheshimiwa Joseph Malanji, Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Zambia.

**171. Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu ziara za viongozi mbalimbali waliokuja nchini kushiriki katika mazishi ya kitaifa ya Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yaliyofanyika tarehe 22 Machi, 2021 jijini Dodoma. Viongozi hao ni kama ifuatavyo:

i. Mheshimiwa Felix Antoine Tshisekedi Tshilombo, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika;

ii. Mheshimiwa Uhuru Muigai Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

iii. Mheshimiwa Filipe Jacinto Nyusi, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika;

iv. Mheshimiwa Cyril Matamela Ramaphosa, Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini;

v. Mheshimiwa Mokgweetsi Eric Keabetswe Masisi, Rais wa Jamhuri ya Botswana;

vi. Mheshimiwa Azali Assoumani, Rais wa Muungano wa Visiwa vya Comoro;

vii. Mheshimiwa Dkt. Lazarus McCarthy Chakwera, Rais wa Jamhuri ya Malawi;

viii. Mheshimiwa Edgar Chagwa Lungu, Rais wa Jamhuri ya Zambia; na

ix. Mheshimiwa Emmerson Dambuzo Mnangagwa, Rais wa Jamhuri ya Zimbabwe.

**172. Mheshimiwa Spika**, viongozi wengine walioshiriki ni:

- i. Mheshimiwa Prosper Bazombana, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Burundi;
- ii. Mheshimiwa Sylvestre Ntibantunganya, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Burundi;
- iii. Mheshimiwa Dkt. Nangolo Mbumba, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Namibia;
- iv. Mheshimiwa Alain Guillaume Bunyoni, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Burundi;
- v. Mheshimiwa Dkt. Edouard Ngirente, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Rwanda;
- vi. Mheshimiwa Carlos Agostinho Do Rosário, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Msumbiji;
- vii. Mheshimiwa Tété Antonio, Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Angola;
- viii. Mheshimiwa Lamin Yahyaoui, Mjumbe Maalum wa Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kiarabu ya Saharawi;
- ix. Mheshimiwa Gotabaya Rajapaksa, Mjumbe Maalum wa Mheshimiwa Dkt. Kana Kananathan, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kisoshalisti ya Sri Lanka; na
- x. Mheshimiwa Richard Kabonero, Balozi wa Jamhuri ya Uganda nchini na Mjumbe Maalum wa Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda.

**173. Mheshimiwa Spika**, Wakuu wa Mashirika na Taasisi za Kikanda na Kimataifa walioshiriki katika msiba huo wa kitaifa ni pamoja na Wakuu wa Jumuiya za Kikanda:

- i. *Balozi* Libérat Mfumukeko, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- ii. Dkt. Stergomena Tax, Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika;

- iii. Mhe. Martin Ngonga, Spika wa Bunge la Afrika Mashariki;
- iv. Mhe. Jaji Sylvain Oré, Rais wa Mahakama ya Watu na Haki ya Afrika;
- v. Mhe. Jaji Nestor Kayobela, Rais wa Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki; na
- vi. Bw. Younouss Djibrine, Katibu Mkuu wa Umoja wa Posta Afrika

**174. Mheshimiwa Spika**, Wizara pia inatoa shukrani za dhati kwa Waheshimiwa Mabalazi na Wakuu wa Mashirika na Taasisi za Kimataifa wanaoziwakilisha nchi na Mashirika yao hapa nchini kwa kushiriki katika mazishi ya kitaifa ya Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

#### **4.4.2 Ziara za Viongozi wa Kitaifa Nje ya Nchi**

**175. Mheshimiwa Spika**, Wizara iliratibu ziara za Viongozi wa Kitaifa waliokwenda katika nchi mbalimbali kama ifuatavyo:

- i. Ziara za Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nchini Msumbiji kushiriki Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Troika Mbili wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika uliofanyika mwezi Aprili na Mei 2021, akimwakilisha Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- ii. Ziara Rasmi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Uganda kuhudhuria sherehe za uapisho wa Mhe. Yoweri Kaguta Museveni mwezi Mei 2021;
- iii. Ziara ya Kitaifa ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Kenya kufuatia mwaliko wa Mhe. Rais Uhuru Muigai Kenyatta mwezi Mei 2021;
- iv. Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Uganda

kushuhudia uwekaji saini wa makubaliano ya kuanza ujenzi wa Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Tanga mwezi Aprili 2021;

v. Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Msumbiji kushiriki Mkutano wa Dharura wa Utatu wa Asasi ya Ushirikiano wa Siasa, Ulinzi na Usalama ya Wakuu wa Nchi na Serikali mwezi Desemba 2020;

vi. Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Botswana kushiriki Mkutano wa Utatu wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Asasi ya Ushirikiano wa Siasa, Ulinzi na Usalama mwezi Novemba 2020;

vii. Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Malawi kushiriki katika sherehe za maadhimisho ya miaka 56 ya Uhuru wa Jamhuri ya Malawi zilizofanyika mwezi Julai 2020; na

viii. Ziara za Waheshimiwa Marais Wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye mikutano mbalimbali nje ya nchi.

#### **4.4.3 Kuanzisha na Kusimamia Huduma za Kikonseli**

**176. *Mheshimiwa Spika***, nchi yetu imeendelea kuongeza uwakilishi katika nchi mbalimbali ambapo Serikali imekamilisha taratibu za kufungua Konseli Kuu mpya katika Jiji la Lubumbashi nchini DRC na Jiji la Guangzhou nchini China. Ufunguzi wa Konseli Kuu hizo unafanya Tanzania kuwa na jumla ya Balozi 43 na Konseli Kuu tano (5) na hivyo kuiwezesha nchi yetu kunufaika zaidi na fursa za kiuchumi na kibiashara.

**177. *Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutoa huduma za kikonseli kama ifuatavyo:

- i. Kurahisisha upatikanaji wa viza kwa maafisa na watendaji wa Serikali, viongozi wa vyama vya siasa, waheshimiwa wabunge na taasisi nyingine zinazostahili huduma hiyo;
- ii. Balozi zetu zimeendelea kuratibu utoaji wa viza kwa raia wa nje wanaoitembelea Tanzania;
- iii. Kuratibu uwasilishaji wa Hati za Utambulisho za mabalozi wapya kutoka nchi za Ireland, Italia, Marekani, Msumbiji, Namibia, Pakistan, Uingereza, Uswisi, Uturuki na Viet Nam;
- iv. Kushirikiana na mamlaka nyingine kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zinazowakabili Watanzania wanaoishi nje ya nchi;
- v. Kutatua changamoto na kulinda maslahi ya Watanzania wanaofanya kazi kwenye Balozi mbalimbali na Mashirika ya Kimataifa hapa nchini; na
- vi. Kutoa huduma za kikonseli kwa Balozi zote za nje na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa yaliyopo hapa nchini.

**178. Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara iliratibu na kufanikisha kuwarejesha nyumbani Watanzania wapatao 5,360 waliokuwa wamekwama katika nchi mbalimbali duniani kutokana na vizuizi vya safari vilivyowekwa na nchi hizo kama njia ya kudhibiti kuenea kwa ugonjwa wa UVIKO-19. Hatua hii imesaidia kuokoa maisha ya nguvu kazi ya Taifa hususan wale waliokuwa katika nchi ambazo ugonjwa huo umeenea kwa kiasi kikubwa.

#### **4.5 Uratibu wa Watanzania Wanaoishi Nje ya Nchi (Diaspora)**

**179. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuratibu masuala yanayohusu jamii za Diaspora ili kuongeza mchango wao katika maendeleo ya Taifa. Kupitia jukumu hili, Tanzania imeendelea kunufaika na Diaspora ambapo kwa mujibu wa Benki Kuu ya Tanzania fedha zilizotumwa na Diaspora nchini kwa mwaka 2020 zilikuwa ni Dola za Marekani milioni 189.13.

Vilevile, katika kipindi hiki Diaspora wamenunua nyumba kupitia Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) zenye thamani ya shilingi milioni 423.8.

**180. *Mheshimiwa Spika***, mwezi Agosti 2020, Wizara iliratibu kufanyika kwa mkutano wa Diaspora wanaoishi Uingereza na Jamhuri ya Ireland uliokuwa na kaulimbiu isemayo “*Mtu Kwao Umoja Wetu Ndiyo Ngao Yetu*”, uliofanyika kwa njia ya mtandao. Mkutano uliwezesha Diaspora na wadau kutoka sekta ya umma na binafsi nchini kubadilishana taarifa za biashara za huduma na bidhaa zinazozalishwa nchini kwa ajili ya kutafuta masoko nje ya nchi na kuwahamasisha Diaspora kuwekeza nchini.

#### **4.6 Elimu kwa Umma**

**181. *Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa za ajira, elimu, biashara, uwekezaji na utalii zitokanazo na uanachama wa Tanzania katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa pamoja na mahusiano na nchi nyingine. Fursa hizo hutangazwa kupitia makongamano, mikutano, maonesho ya biashara, maadhimisho ya sherehe za kitaifa na vyombo vya habari kama vile vituo vya runinga na redio, magazeti, majarida, machapisho, tovuti na mitandao ya kijamii.

**182. *Mheshimiwa Spika***, Wizara ilishiriki katika maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba) yaliyofanyika mwezi Julai 2020; maadhimisho ya siku ya wakulima (Nanenane) yaliyofanyika kitaifa mwezi Agosti 2020 Pemba, Zanzibar; na maonesho ya biashara wakati wa Maadhimisho ya miaka 57 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yaliyofanyika mwezi Januari 2021. Wakati wa maonesho hayo, Wizara ilitoa elimu kuhusu majukumu yake pamoja na kusambaza machapisho kwa wananchi kuhusu Sera ya Mambo ya Nje, 2001 na fursa zinazotokana na Mtangamano wa Afrika Mashariki.

**183. *Mheshimiwa Spika***, mwezi Oktoba 2020, Wizara iliendesha semina kuhusu masuala ya Mtangamano wa Afrika Mashariki na fursa zake kwa wanafunzi 200 wa Shule za Sekondari za

Dodoma na Viwandani zilizopo jijini Dodoma. Wanafunzi hao walielimishwa kuhusu majukumu ya Wizara na nafasi ya Tanzania katika Mtangamano wa Afrika Mashariki na nafasi yao kama vijana na viongozi wa baadaye wa Taifa. Vilevile, Wizara iliandaa makala ya video yenye kuonesha namna ilivyotekeleza Diplomasia ya Uchumi na kurushwa na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) mwezi Novemba 2020.

**184. Mheshimiwa Spika**, mwezi Desemba 2020, Wizara ilishiriki kwenye kongamano la wafanyabiashara wanawake wa Tanzania lililoandaliwa na Chama cha Wafanyabiashara Wanawake lililofanyika jijini Dar es Salaam. Kupitia kongamano hilo, Wizara ilitoa elimu kwa wanawake 120 walioshiriki, kuhusu fursa zilizopo katika Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na taratibu zinazopaswa kufuatwa ili kunufaika na soko la Afrika Mashariki na Soko Huru la Biashara la Bara la Afrika.

#### 4.7 Utawala na Maendeleo ya Watumishi

**185. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kusimamia masuala ya utawala na maendeleo ya watumishi kwa lengo la kuboresha na kuimarisha utendaji wa kazi. Wizara ina jumla ya watumishi 455 wa kada mbalimbali. Kati yao watumishi 228 wapo Makao Makuu ya Wizara na watumishi 227 wapo kwenye Balozi za Tanzania. Katika kuimarisha utendaji kazi wa Wizara, masuala mbalimbali yanayohusu utawala na maendeleo ya watumishi yameendelea kusimamiwa kama ifuatavyo:

##### 4.7.1 Uteuzi wa Viongozi

**186. Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliniteua kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na viongozi wengine walioteuliwa ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa *Balozi* Mbarouk Nassor Mbarouk (Mb) kuwa Naibu Waziri; Mheshimiwa *Balozi* Joseph Edward Sokoine kuwa Katibu Mkuu; Mheshimiwa *Balozi* Fatma Mohammed Rajab kuwa Naibu Katibu Mkuu; na Mheshimiwa Yusuph Tindi



Mndolwa kuwa Balozi na Mkuu wa Itifaki. Aidha, Mheshimiwa Rais ameteua Mabalazi 23 watakaoiwakilisha nchi yetu katika mataifa mbalimbali na wengine kupangiwa majukumu hapa nchini. Naomba kutumia fursa hii kuwapongeza viongozi wenzangu kwa uteuzi huo na kuwasahi tuendeleo kuchapa kazi kwa bidii, uzalendo na weledi ili kuleta maendeleo kwa Taifa letu.

#### 4.7.2 Mafunzo

**187. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake ambapo jumla ya watumishi 219 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani mbalimbali ndani na nje ya nchi. Watumishi wanane walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 211 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi.

#### 4.7.3 Upandishaji Vyeo

**188. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021, jumla ya watumishi 194 wa kada mbalimbali wamepandishwa vyeo.

#### 4.7.4 Kubadilisha Kada Watumishi

**189. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021, watumishi 12 walibadilishwa kada ndani ya Wizara. Kati ya watumishi hao, mmoja alibadilishwa kuwa Afisa Mambo ya Nje Mwandamizi; sita kuwa Maafisa Mambo ya Nje Daraja la II; watatu kuwa Maafisa Utumishi Daraja la II; na mtumishi mmoja kuwa Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II.

#### 4.7.5 Uhamisho

**190. Mheshimiwa Spika**, ili kuboresha utendaji kazi katika Utumishi wa Umma, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021 watumishi 17 walihamishwa kwenda Wizara na Taasisi nyingine za Serikali na watumishi 37 walihamia Wizarani kutoka Wizara na Taasisi nyingine za Serikali.

#### 4.8 Kuratibu na Kusimamia Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara na Taasisi Zilizochini ya Wizara

##### 4.8.1 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara

**191. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ilitengewa bajeti ya maendeleo ya **shilingi 20,000,000,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo iliyoopo ndani na nje ya nchi.

**192. Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kufuatilia Wizara ya Fedha na Mipango fedha za bajeti ya maendeleo zilizotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 baada ya kukamilisha nyaraka za miradi hiyo kama taratibu zinavyoelekeza.

##### 4.8.2 Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi Zilizochini ya Wizara

**193. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki, Wizara imeendelea kuzisimamia taasisi zilizochini yake ambazo ni: Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC); Chuo cha Diplomasia (CFR); na Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora (APRM) katika kutekeleza majukumu yao kama ifuatavyo:

##### **Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC)**

**194. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki, Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) kimeendelea kuendesha biashara ya mikutano; upangishaji wa nyumba na ofisi; na kutoa huduma ya afya kupitia hospitali inayomilikiwa na kituo hicho.

**195. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021 Kituo kilipanga kukusanya mapato ya **shilingi 16,001,559,000**. Hadi mwezi Aprili 2021, Kituo kilikusanya mapato ya **shilingi 7,970,640,495** sawa na asilimia **48** ya malengo. Mapato hayo yalitokana na:

i. Huduma za kumbi za mikutano (AICC na JNICC) - **shilingi 2,608,160,544** kati ya lengo la **shilingi 6,339,350,000**;

ii. Upangishaji wa ofisi na nyumba za kuishi **shilingi 2,995,497,441** kati ya lengo la **shilingi 4,956,540,000**; na

iii. Huduma za hospitali - **shilingi 2,366,982,510** kati ya lengo la **shilingi 4,705,669,000**.

Sababu za kushuka kwa mapato ya Kituo ni kupungua kwa idadi ya mikutano hali iliyochangiwa kwa kiasi kikubwa na changamoto ya UVIKO-19.

**196. Mheshimiwa Spika**, vilevile katika kipindi hicho, Kituo kilifanikiwa kutekeleza yafuatayo:

i. Kuhudumia mikutano 143 ya kitaifa na minne ya kimataifa ambayo ilileta washiriki 46,811 wa kitaifa na 3,621 wa kimataifa;

ii. Kufanya matangazo kwa njia ya kielektroniki, magazeti na "screen" kwenye makutano ya barabara za jiji la Arusha, pamoja na kwenye mitandao ya kimataifa kwa ajili ya kuvutia wateja wa ofisi na nyumba za kupangisha pamoja na kumbi na huduma za mikutano;

iii. Kutoa huduma za afya kwa wagonjwa wapatao 55,452;

iv. Kuhuisha mifumo ya kielektroniki na usimamizi wa taarifa katika nyanja za uhasibu, miliki na uendeshaji wa hospitali;

v. Kukamilisha taratibu za umiliki wa kiwanja chenye ukubwa wa ekari 15 katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba, jijini Dodoma kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha kisasa cha mikutano; na

vi. Kukarabati majengo ya Kituo yaliyopo Arusha na Dar es Saalam.

**197. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Kituo kilitoa **shilingi 150,000,000** kama gawio la awali kwa Serikali.

## Chuo cha Diplomasia (CFR)

**198. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hiki, Chuo cha Diplomasia kimeendelea kutoa mafunzo na kufanya tafiti katika masuala ya diplomasia, uhusiano wa kimataifa, stratejia, usuluhishi wa migogoro na ujenzi wa amani.

**199. *Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Chuo kilitengewa kiasi cha **shilingi 5,805,064,000**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 2,427,064,000** ni Mishahara, **shilingi 1,000,000,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **shilingi 2,378,000,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, Chuo kilipanga kukusanya **shilingi 2,988,195,000**.

**200. *Mheshimiwa Spika***, hadi mwezi Aprili 2021, Chuo kilipokea **shilingi 2,662,052,633.30** kutoka Hazina. Kati ya fedha hizo, **shilingi 1,828,719,300** ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi 833,333,333.30** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Pia, Chuo kilikusanya jumla ya **shilingi 2,041,033,718** sawa na **asilimia 68.3** ya lengo la mwaka.

**201. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwezi Julai 2020 hadi Mei 2021, Chuo kilitoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa Wizara/Taasisi na Mashirika ya Serikali, mashirika na kampuni binafsi, balozi na watu binafsi; na kutoa mafunzo ya lugha saba za kigeni ambazo ni Kiarabu, Kifaransa, Kihispania, Kiingereza, Kichina, Kikorea na Kireno. Aidha, Chuo kimekamilisha mtaala wa mafunzo ya lugha ya Kiswahili kwa wageni. Vilevile, katika mwaka wa masomo 2020/2021 Chuo kimedahili wanafunzi 1,514 kutoka wanafunzi 1,280 kwa mwaka wa masomo 2019/2020, sawa na ongezeko la asilimia 18.3. Chuo pia kilitoa mchango serikalini kiasi cha **shilingi 32,000,000**.

## Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora (APRM)

**202. *Mheshimiwa Spika***, APRM Tanzania ilifanya tathmini kuhusu utawala bora nchini na kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa APRM nchini Tanzania. Taarifa hiyo

imeangazia maeneo makuu manne ambayo ni: Demokrasia na Siasa; Usimamizi wa Uchumi; Utendaji wa Mashirika ya Biashara; na Maendeleo ya Jamii. Taarifa imeainisha mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha 2015 hadi 2019 kama ifuatavyo:

i. Kuongezeka kwa ufanisi wa utendaji kazi katika sekta ya utumishi wa umma na hivyo kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi;

ii. Kuongezeka kwa makusanyo ya Serikali kutokana na hatua zilizochukuliwa kuziba mianya ya ukwepaji kodi na kuimarisha elimu kwa walipa kodi;

iii. Kuimarika kwa Taasisi za Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU na ZAECA) pamoja na mapambano dhidi ya rushwa;

iv. Kuimarika kwa usimamizi wa rasilimali za madini na kuanzisha masoko ya madini ili kukuza ushiriki wa wachimbaji wadogo wadogo katika mnyororo wa thamani, kuzuia utoroshwaji na usafirishaji wa madini ghafi nje ya nchi; na

v. Kuimarika kwa miundombinu ya uchumi kama reli, barabara na nishati; na huduma za jamii hususan elimu na afya.

**203. *Mheshimiwa Spika***, mwezi Desemba 2020, APRM Tanzania iliendesha warsha ya kitaifa ya uhakiki wa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa APRM nchini kwa lengo la kupata maoni. Warsha hiyo ilishirikisha wadau wa sekta ya umma na binafsi kutoka pande zote mbili za Muungano.

**204. *Mheshimiwa Spika***, kikao cha 30 cha Wakuu wa Nchi na Serikali zinazoshiriki Mpango wa APRM, kilichofanyika mwezi Machi 2021 kwa njia ya mtandao kilimteua Mheshimiwa *Balozi* Ombeni Yohana Sefue, Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu kuwa Mwenyekiti wa Jopo la Watu Mashuhuri wa APRM, Barani Afrika (The Panel of Eminent Persons). Napenda kutumia fursa hii kumpongeza kwa uteuzi huo. Tuna imani kuwa uzoefu

wake wa muda mrefu na umahiri katika masuala ya diplomasia, utaendelea kuwa hazina na rasilimali ya kipekee kwa maslahi ya nchi yetu na Bara zima la Afrika.

**205. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, APRM Tanzania ilitengewa **shilingi 800,000,000**. Hadi kufikia mwezi Aprili 2021, APRM Tanzania ilipokea na kutumia **shilingi 666,666,666.70** sawa na asilimia **83.3** ya bajeti yake.

## 5.0 CHANGAMOTO ZILIZOPO NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA

**206. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021, pamoja na kuwepo mafanikio ya kiutendaji, Wizara ilikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo:

- i. Upungufu wa watumishi ukilinganisha na wingi wa majukumu; na
- ii. Sekta binafsi kutotumia ipasavyo fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na mtangamano wa kikanda na masoko ya kikanda na kimataifa.

**207. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imechukua hatua zifuatazo:

- i. Kuendelea kuwasiliana na Mamlaka ya Ajira kwa ajili ya kupata vibali vya ajira mpya na ajira mbadala vya kujaza nafasi zilizo wazi; na
- ii. Kuendelea kushirikiana na sekta binafsi, asasi za kiraia na vyombo vya habari katika kutoa elimu kwa umma juu ya fursa mbalimbali zitokanazo na ushiriki wetu katika mtangamano wa kikanda na masoko ya kikanda na kimataifa.

## 6.0 SHUKRANI

**208. Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Mabalizi na Wawakilishi wa Taasisi za Umoja wa Mataifa pamoja na Mashirika ya Kimataifa hapa nchini kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa kufanikisha mipango mbalimbali ya

maendeleo inayotekelezwa na Serikali yetu chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**209. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kupata mafanikio kutokana na ushirikiano kutoka kwa wadau mbalimbali na Washirika wa Maendeleo kutoka nchi na asasi za kikanda na kimataifa. Naomba nitumie fursa hii kuzishukuru nchi za Algeria, Australia, Austria, Brazil, Canada, China, Cuba, Denmark, Ethiopia, Finland, Hispania, Hungary, Italia, Iran, Ireland, Indonesia, India, Israel, Jamhuri ya Korea, Japan, Kuwait, Malaysia, Malta, Marekani, Mexico, Misri, Morocco, New Zealand, Nigeria, Norway, Oman, Pakistan, Poland, Qatar, Romania, Saudi Arabia, Singapore, Sri Lanka, Sweden, Sudan, Thailand, Tunisia, Ubelgiji, Uganda, Ufaransa, Uingereza, Uholanzi, Ujerumani, Urusi, Uswisi, Uturuki, Ureno, Umoja wa Falme za Kiarabu, Venezuela na Viet Nam kwa kuchangia mafanikio hayo muhimu kwa Taifa.

**210. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa shukrani pia kwa *African Capacity Building Foundation (ACBF)*; Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); Benki ya Dunia; *Investment Climate Facility for Africa*; Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD); Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DfID); Mfuko wa Maendeleo wa Abu Dhabi (ADFD); Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF); Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait (Kuwait Fund); Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA); Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden (SIDA); Shirika la Kimataifa la Kuzuia Matumizi ya Silaha za Kemikali (OPCW); Ofisi ya Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN RCO); Mfuko wa Kukuza Mtaji wa Umoja wa Mataifa (UNCDF); Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP); Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na UKIMWI (UNAIDS); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (FAO); Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO); Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wakimbizi (UNHCR); Shirika la Kazi Duniani (ILO); Shirika la Umoja wa Mataifa la Uhamaji (IOM); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF); Shirika la

Maendeleo la Kimataifa la Israel (MASHAV); Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA); Shirika la Misaada la Marekani (USAID); Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Korea (KOICA); Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO); Shirika la Umoja Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Wanawake (UNWOMEN); Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP); Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD); Shirika la Umoja wa Mataifa Kuhusu Madawa ya Kulevya na Uhalifu (UNODC); Umoja wa Ulaya (EU); Shirika la Afya Duniani (WHO); na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP). Vilevile, napenda kuwashukuru Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi ya Afrika (BADEA); Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB); Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GiZ); *Global Fund*; *International Committee of the Red Cross*; *International Federation of the Red Cross and Red Crescent Societies*; Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola; *Khalifa Fund for Enterprise Development* (Khalifa Fund); *Medecins Sans Frontieres*; Mfuko wa Dunia wa Wanyama Pori (WWF); *The Association of European Parliamentarians with Africa*; *The Bill and Melinda Gates Foundation*; *TradeMark East Africa (TMEA)*; Umoja wa Posta Duniani (UPU); Umoja wa Posta Afrika (PAPU) pamoja na Mifuko na Mashirika mbalimbali ya Misaada. Ni dhahiri kuwa ushirikiano wao umekuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha malengo ya Serikali.

**211. Mheshimiwa Spika**, kwa moyo mkunjufu, napenda kuwashukuru watendaji na watumishi wa Wizara na Taasisi zake kwa kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ipasavyo. Kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Mheshimiwa *Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk (Mb)*, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; *Balozi Joseph Edward Sokoine*, Katibu Mkuu; *Balozi Fatma Mohammed Rajab*, Naibu Katibu Mkuu; Waheshimiwa Mabalazi wa Tanzania; Wakuu wa Idara na Vitengo; Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara; na watumishi wote kwa kufanya kazi kwa umahiri, weledi na ufanisi katika kunisaidia kutekeleza majukumu yangu ya kulinda na kutetea maslahi ya Taifa letu ndani na nje ya nchi.



**212. Mheshimiwa Spika**, kipekee napenda kuwashukuru Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb), aliyekuwa Waziri; Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb) na Mhe. William Tate Ole Nasha (Mb) waliokuwa Naibu Mawaziri; Mhe. *Balozi* Brig. Gen. Wilbert A. Ibuge aliyekuwa Katibu Mkuu na Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu kwa mchango wao mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Wizara katika Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**213. Mheshimiwa Spika**, kwa nafasi ya pekee kabisa, napenda kumshukuru mume wangu mpendwa Mhandisi Dkt. George Steven Mulamula; watoto wangu pamoja na familia yangu kwa ujumla kwa uvumilivu wao na kuwa karibu nami wakati wote wa kutekeleza majukumu yangu ambayo wakati mwingine yanatilazimu kuwa mbali nao kwa muda mrefu.

## **7.0 MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**214. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara imeweka kipaumbele katika kutekeleza majukumu yafuatayo:

- i. Kuendelea kutekeleza diplomasia ya uchumi ikiwa ni pamoja na kuwezesha balozi zetu kuwa kiungo muhimu cha kukuza uwekezaji, upatikanaji wa masoko ya bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini na kuvutia watalii;
- ii. Kuendelea kuboresha na kuimarisha uhusiano na nchi nyingine, jumuiya za kikanda na mashirika ya kimataifa;
- iii. Kuendelea kuweka mazingira wezeshi, kuratibu na kuhamasisha ushiriki wa Watanzania wanaoishi nje ili kushiriki kikamilifu katika kuchangia maendeleo ya nchi;
- iv. Kuendelea kulinda na kutetea misingi ya Taifa letu ndani na nje ya nchi;
- v. Kuendelea kushawishi na kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa nchi moja moja, jumuiya za kikanda na kimataifa;

- vi. Kuendelea kushiriki katika juhudi za kulinda na kuimarisha amani duniani na maendeleo kupitia Umoja wa Mataifa;
- vii. Kuendelea kujenga na kukarabati majengo kwa ajili ya balozi zetu ili kupunguza gharama na kuleta mapato kwa Serikali;
- viii. Kuendelea kufungua ofisi za Balozi na Konseli Kuu mpya katika nchi za kimkakati;
- ix. Kuendelea kushiriki kikamilifu katika kuimarisha utangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC);
- x. Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara, masuala ya uhusiano wa kimataifa na utangamano wa kikanda;
- xi. Kuendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zilizopo chini ya Wizara; na
- xii. Kuendelea kusimamia rasilimali watu na fedha Makao Makuu ya Wizara na Balozini.

## **8.0 MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

### **Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC)**

**215. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kituo kimepanga kukusanya mapato ya **shilingi 17,763,743,153**. Kati ya mapato hayo, **shilingi 16,202,606,216** ni kutoka vyanzo vya ndani vya mapato na **shilingi 1,561,136,937** zitatokana na mkopo. Fedha za mkopo ni kwa ajili ya kugharamia nyongeza ya mradi wa jengo la wagonjwa wa nje la Hospitali ya AICC, ununuzi wa vifaa tiba pamoja na gharama za awali za kujenga jengo la biashara jijini Arusha.

**216. Mheshimiwa Spika**, Kituo kinaendelea kufanya taratibu za kuanza ujenzi wa Kituo cha mikutano kitakachoitwa *Mount Kilimanjaro International Convention Centre (MK-ICC)* jijini

Arusha. Kituo hicho kitaimarisha na kuongeza kasi ya utekelezaji wa diplomasia ya mikutano na maonesho hapa nchini.

### **Chuo cha Diplomasia (CFR)**

**217. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Chuo kimepanga kukusanya **shilingi 3,511,965,000** kutoka katika vyanzo vya ndani. Aidha, Chuo kinatarajia kutekeleza majukumu yafuatayo:

- i. Kuendelea kutoa mafunzo ya mahusiano ya kimataifa; lugha ya Kiswahili kwa wageni; na mbinu za kidiplomasia;
- ii. Kuendelea kufanya tafiti katika maeneo ya mahusiano ya kimataifa na mbinu za kidiplomasia;
- iii. Kutathmini matokeo ya mafunzo yaliyotolewa na mipango ya mafunzo kwa ujumla;
- iv. Kuendelea na ujenzi wa vyumba vya mihadhara kwa lengo la kuongeza udahili na mapato ya Chuo; na
- v. Kuendelea kutoa ushauri na huduma za kitaalamu kwa Serikali na Taasisi zake.

### **Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora (APRM)**

**218. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022, APRM inatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

- i. Kuendelea kufanya tathmini za utawala bora za mpango wa APRM ikiwa ni pamoja na kuhuisha mbinu za utafiti kwa kupitia upya hojaji ya APRM;
- ii. Kuboresha viashiria vya utafiti, kuzingatia matumizi ya teknolojia katika utekelezaji wa Mpango na kupanua wigo wa zana zinazotumika katika utafiti;

iii. Kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa APRM kwa kushirikiana na Wizara, Idara na Wakala za Serikali katika kuandaa taarifa ya mwaka na kuweka mfumo madhubuti wa ufuatiliaji; na

iv. Kuimarisha mawasiliano na utoaji taarifa kuhusu Mpango wa APRM kwa kuendelea kutekeleza Mpango wa Mawasiliano wa Miaka Mitano 2021/2022–2025/2026.

## 9.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**219. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha **shilingi 2,550,879,000** ikiwa ni mapato ya Serikali yatakayopatikana kutokana na vyanzo vilivyopo Makao Makuu ya Wizara na Balozi za Tanzania ambavyo ni pango la nyumba za Serikali zilizopo nje ya nchi na kuthibitisha nyaraka.

**220. Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara imetengewa bajeti ya kiasi cha **shilingi 192,265,438,000**. Kati ya fedha hizo **shilingi 178,765,438,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida zinazojumuisha **shilingi 167,937,219,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; **shilingi 10,828,219,000** kwa ajili ya Mishahara; na **shilingi 13,500,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**221. Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha za bajeti ya Matumizi Mengineyo ya Wizara, **shilingi 800,000,000** ni kwa ajili ya Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Masuala ya Demokrasia na Utawala Bora (APRM), **shilingi 1,000,000,000** ni kwa ajili ya Chuo cha Diplomasia (CFR), **shilingi 1,280,000,000** ni kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (ACHPR) na **shilingi 170,000,000** ni kwa ajili ya Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika (AUABC). Aidha, kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mishahara, **shilingi 2,202,193,800** ni kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Diplomasia.

**222. Mheshimiwa Spika**, kati ya **shilingi 13,500,000,000** zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, **shilingi 6,500,000,000** ni kwa ajili ya awamu ya kwanza ya ujenzi wa ofisi ya ubalozi na kitega uchumi ubalozi wa Tanzania Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo; **shilingi 5,000,000,000** ni kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na makazi ya Balozi, ubalozi wa Tanzania Muscat, Oman; **shilingi 1,000,000,000** ni kwa ajili ya ujenzi wa makazi ya Balozi wa Tanzania Addis Ababa, Ethiopia; na **shilingi 1,000,000,000** ni kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa vyumba vya mihadhara katika Chuo cha Diplomasia.

#### 10.0 HITIMISHO

**223. Mheshimiwa Spika**, ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **shilingi 192,265,438,000**. Kati ya fedha hizo **shilingi 178,765,438,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 13,500,000,000** ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

**224. Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia nafasi hii adhimu kukushukuru tena wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

**225. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

#### WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja imetolewa lamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; karibu sana. Tunashukuru kwa hotuba yako nzuri na kuainisha mambo mengi yanayohusu Afrika Mashariki na mambo ya nje kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Sasa moja kwa moja nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kwa niaba yake, karibu sana Mheshimiwa na kwa vile ni kazi

ya siku moja tu, nakushauri uweke *preamble* kidogo, lakini zaidi tupeleke kwenye maoni na ushauri wa Kamati ili utubakizie dakika za uchangiaji. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI – K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kuwasilisha mbele yako hotuba fupi kwa niaba ya Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Fungu 34 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa hii iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa mezani mapema asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Spika, utangulizi; awali ya yote Kamati inampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mwanadiplomasia namba nchini kwa uteuzi wa mabalozi 23 ambao kati yao mabalozi saba na asilimia 30 ni wanawake, kazi iendelee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2020/2021; pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na kuliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 6(3)(c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni miongoni mwa Wizara zinazosimamiwa na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Aidha, Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane na Kanuni za Bunge kimezipa jukumu Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu katika kutekeleza jukumu hilo, tarehe 28 Machi, 2021 Kamati ilipokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama inavyoelekeza Kanuni ya 114(2) ya Kanuni za Bunge kwa lengo la kulinganisha na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, ili kulisaidia Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha unaoishia, pamoja na kuishauri vyema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi, Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022, taarifa ninayoiwasilisha itatoa maelezo kuhusu mambo yafuatayo:-

(i) Mapitio ya Taarifa ya Wizara kuhusu uzingatiaji wa maoni yaliyotolewa na Kamati ya Bunge wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ukurasa wa 5 hadi 9;

(ii) Uchambuzi wa ukusanyaji wa maduhuli ikilinganishwa na lengo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021; ukurasa wa 9 hadi 12;

(iii) Mapitio ya Taarifa ya Wizara kuhusu upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge, utekelezaji wa majukumu na changamoto katika mwaka wa fedha 2020/2021, ukurasa wa 12 hadi 15;

(iv) Uchambuzi wa majukumu na malengo yanayowekwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022, ukurasa wa 12 hadi 18;

(v) Mapitio ya Malengo ya Bajeti na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022, ukurasa wa 19 hadi 21;

(vi) Uchumi wa Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2021/2022, ukurasa wa 21 hadi 28; na

(vii) Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, ukurasa wa 29 hadi 33.

Mheshimiwa Spika, lengo la maelezo haya ni kuliwezesha Bunge kupata taswira ya hali ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na kulinganisha na makadirio ya fedha za matumizi ya mwaka wa fedha 2021 ili Bunge liweze kuamua kuhusu maombi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021; taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020 ilihusu maeneo makuu matatu. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati;
- (ii) Mapitio ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge; na
- (iii) Utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ilipitia na kuchambua kwa kina maeneo yote matatu kama inavyoonekana katika ukurasa wa 5 hadi wa 18 wa taarifa hii. Hata hivyo, naomba kuwasilisha masuala muhimu yaliyobainika na Kamati kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati; Bunge lilipokuwa likijadili hoja ya Serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka



wa fedha 2020/2021, kamati ilitoa ushauri katika masuala kumi na tatu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba miongoni mwa ushauri uliotolewa, upo ushauri uliotekelezwa kikamilifu, upo unaoendelea kutekelezwa na upo ushauri unaohitaji kuzingatiwa zaidi katika kutekeleza wajibu wake hususan ushauri uliohusu masuala ya kibajeti.

Mheshimiwa Spika, kati ya ushauri ambao ulizingatiwa ulikuwa na changamoto za kibajeti ulihusu Serikali kutoa fedha zote za maendeleo zilizo tengwa katika mwaka wa fedha 2019/2020 kiasi cha shilingi bilioni nne. Hata hivyo, maelezo yaliyotolewa yalionesha kuwa hadi kufikia Juni 2020, Wizara ilipokea shilingi 603,473,965.60 sawa na asilimia 15.09 tu.

Mheshimiwa Spika, aidha, sambamba na ushauri huo, kamati ilishauri kuwa fedha za maendeleo zilizotengwa katika mwaka 2020/2021 zitolewe kwa ukamilifu na kwa mtiririko uliopangwa. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Februari, 2021, Wizara haikuwa imepokea fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusesitiza kuwa, ushauri wa Kamati kuhusu wizara hii kupelekewa fedha za maendeleo kwa kadri zinavyo idhinishwa na Bunge unapaswa kupewa uzito stahiki. Kwa kufanya hivyo Serikali itaokoa fedha nyingi zinazotumika kulipia kodi ya pango kwa majengo yaliyo kodiwa kwa ajili ya makazi na ofisi za watumishi wa balozi zetu nje ya nchi, vilevile itaongeza pato lake kwa kukodisha majengo ya balozi yatakayojengwa na sehemu yake kutumika kama kitega uchumi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa bajeti uliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2020/2021; Kamati ilipitia taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara katika kipindi cha 2020 hadi Februari, 2021 kwa kuchambua hali ya ukusanyaji wa mapato pamoja na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara hii ilikuwa na lengo la kukusanya maduhuli ya kiasi cha shilingi 2,550,879,000. Kati ya fedha hizo shilingi 47,170,000 ni makusanyo ya makao makuu ya Wizara na shilingi 2,503,709,000 ni makusanyo kutoka Balozi za Tanzania nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2021 Wizara ilikuwa imekusanya asilimia 18.9 tu ya lengo lililowekwa. Aidha, kati ya fedha zilizokusanywa, shilingi 29,535,000 zilikuwa ni makusanyo ya makao makuu ya Wizara ambayo ni asilimia 56.3 ya lengo lililowekwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ulinganisho wa makusanyo ya Wizara kwa kipindi cha kufikia Februari, 2020 na kubaini kuwa makusanyo ya kipindi hiki ni pungufu kwa asilimia 90.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa upungufu huu wa makusanyo umechangiwa na kukosekana kwa wapanganji katika baadhi ya majengo ya Serikali kwenye Balozi za Tanzania nje ya nchi. Kamati ilielezwa kuwa hali hii imesababishwa na uwepo wa janga la ugonjwa wa homa kali ya mafua unaosababishwa na virusi vya *Covid- 19*.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; Kamati ilitoa taarifa ya upatikanaji wa fedha kwa Mwaka Wa Fedha 2020/2021 ilibaini kuwa hadi kufikia Mwezi Machi, 2020 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 107,834,686,039.66 sawa na asilimia 53.9 ya fedha zote za bajeti zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya matumizi.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha fedha kilichotolewa ni pungufu ya asilimia 5.19 ikilinganishwa na fedha zilizotolewa hadi kufikia mwezi Machi, 2020 ambazo zilikuwa ni asilimia 68 ya fedha zote za bajeti zilizoidhinishwa kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa hadi kufikia Machi, 2021 hakukuwa na fedha

zozote za maendeleo zilizokuwa zimepelekwa kati ya shilingi bilioni 20 zilizokuwa zimeidhinishwa. Fedha hizi zililenga kutekeleza miradi nane iliyojumuisha ujenzi wa uzio viwanja vya balozi, pamoja na ujenzi na ukarabati wa majengo ya Balozi za Tanzania nje ya nchi, na upanuzi na uboreshaji wa miundombinu ya Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kama zilivyo idhinishwa na Bunge lako Tukufu, kunaathiri ratiba za utekelezaji wa miradi hiyo ambayo ingeokoa fedha zilizotumika kama pango, vilevile ingeingiza mapato Serikalini kutokana na kukodisha sehemu ya majengo yanayo kusudiwa kuwa vitega uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, ukarabati wa jengo la zamani la ubalozi wa zamani Washington DC utawezesha ubalozi kuhamia katika jengo hilo na jengo linalotumika sasa kupangishwa kama kitega uchumi ambapo linakadiriwa kuwa litakuwa na uwezo wa kuiingizia Serikali mapato ya shilingi bilioni 2.4 kwa ukarabati wake kwa mwaka wa fedha 2020 umekadiriwa kugharimu bilioni 3,868,440,000.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara; taarifa iliyotolewa na Wizara ilibainisha kuwa katika kipindi cha Julai, 2020 hadi tarehe 10 Machi, 2021, Wizara iliendelea kutekeleza majukumu yake tisa kama inavyoonekana katika ukurasa wa 16 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza majukumu yake kama ilivyopangwa licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali kama ilivyofafanuliwa katika ukurasa wa 17 wa taarifa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mpango na bajeti ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022; uchambuzi wa malengo ya bajeti; kabla ya kueleza uchambuzi wa makadirio ya matumizi ya Wizara hii,

napenda kutoa taarifa kuwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wizara imepanga kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele kumi tofauti na ilivyokuwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo Wizara ...

**SPIKA:** Nakushauri Mheshimiwa Zahor sasa uende kwenye maoni na ushauri.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI – K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati; baada ya maelezo hayo, sasa naomba niwasilishe maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

(i) Serikali itoe fedha za maendeleo shilingi bilioni 20 zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kulingana na muda uliobaki wa kukamilisha mwaka wa fedha 2020/2021 Kamati inashauri kipaumbele kitolewe kwa ajili ya mradi wa kukarabati jengo la zamani la Ubalizi wa Tanzania Washington DC ulioidhinishwa shilingi 3,868,440,000. Ukarabati huu utakapo kamilika utawezesha jengo hili kuwa na uwezo wa kuliingizia Serikali mapato zaidi ya shilingi bilioni 2.4 kwa mwaka.

(ii) Serikali itekeleze mpango wake wa miaka kumi na tano 2018/2019-2031/2032 wa ujenzi, ununuzi na ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi katika balozi zetu kwa kuendelea kutoa fedha kadri zinavyoidhinishwa na Bunge lako. Kamati inaamini kuwa Serikali itaokoa fedha nyingi zinazotumika kulipia pango endapo mpango huo utafanikiwa. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali inatarajia kutumia takribani shilingi 24,769,113,038 kwa ajili ya pango katika balozi za Tanzania nje.

(iii) Serikali ikamilishe mchakato wa kuandaa Sera ya Mambo ya Nje katika mwaka wa fedha 2020/2021 kama

ilivyoahidi, kulingana na umuhimu wake kisiasa, kiuchumi na kijamii.

(iv) Serikali iweke mpango mkakati wa kushughulikia changamoto ya muda mrefu ya uchakavu na uhaba wa magari hususan katika Balozi za Tanzania nje. Kutokushughulikiwa kwa changamoto hii kunaweza kuharibu taswira ya nchi yetu nje ya nchi.

(v) Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora ione umuhimu wa kutoa vibali vya ajira mpya na mbadala za kujaza nafasi zilizo wazi katika balozi zetu ambazo zimekuwa zikikabiliwa na uchache wa watumishi licha ya kuwa na majukumu mengi. Changamoto hii imekuwa ya muda mrefu jambo ambalo linaweza kuathiri utendaji katika balozi zetu nje. Aidha, watumishi hao wawe ni pamoja na wataalam wa diplomasia ya uchumi;

(vi) Serikali iendelee kuhamasisha Watanzania waishio nje kujiandikisha katika balozi zetu na kuwawekea mazingira wezeshi ya kufanya uwekezaji nchini;

(vii) Serikali iziwezeshe na kuzifuatilia baadhi ya Wizara za Kisekta ambazo zikifanya kazi kwa juhudi na ufanisi zitaongeza pato la Taifa kwa kusimamia uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo ambayo yana soko kubwa nje ya nchi kama vile nyama ya mbuzi katika masoko ya nchi za Kiarabu;

(viii) Serikali izidishie juhudi za kuzisimamia balozi zetu nje ya nchi kutangaza fursa za kitalii na vivutio mbalimbali zilizopo nchini kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii;

(ix) Serikali iendelee kuhamasisha sekta binafsi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na matangazo ya Afrika Mashariki na Masoko ya kimataifa;

(x) Serikali iendelee kutafuta wawekezaji ambao wana maslahi na nchi yetu ili kuongeza pato la nchi na ajira; na

(xi) Wizara iendelee kutekeleza maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambavyo hayaja tekelezwa hususan katika bajeti za miaka mitatu iliyopita 2018/2019; 2019/2020 na 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi, Mbunge, Naibu Waziri, Mheshimiwa William Ole Nasha, Mbunge na aliyekuwa Katibu Mkuu Balozi Kanali Wilbert Ibuge, pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kuwezesha uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2021/2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inawapa pongezi Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, Mbunge, kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu, kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Aidha, tunaomba kumpongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk kwa kueuliwa kuwa Mbunge na Naibu wa Wizara hii. Aidha, tunampongeza Balozi Joseph Sokoine kwa kueuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru aliyekuwa Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake kwa ufanisi na Ndugu Nenelewa Mwiambi kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Katibu wa Bunge na hatimaye

kuiwezesha Kamati kuandaa na kukamilisha kazi yake kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Gerald Magili Mkurugenzi Msaidizi, Makatibu wa Kamati hii Ndugu Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii, liikubali na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama yalivyo wasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (FUNGU 34) KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote, Kamati inampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwanadiplomasia namba moja nchini kwa uteuzi wa Mabalazi 23 ambao kati yao, Mabalazi 7 sawa na asilimia 30 ni wanawake, kazi iendelee.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020 [Kanuni za Bunge], naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) (c) cha Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Bunge, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni miongoni mwa Wizara zinazosimamiwa na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Aidha, Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kimezipa jukumu Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki tarehe 28 Machi, 2021.

**Mheshimiwa Spika**, katika kikao hicho, Kamati ilipokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama inavyoelekeza Kanuni ya 114 (2) ya Kanuni za Bunge kwa lengo la kulinganisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, ili kulisaidia Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, pamoja na kuishauri vyema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Taarifa ninayowasilisha inatoa maelezo kuhusu: -



- i) Mapitio ya Taarifa ya Wizara kuhusu uzingatiaji wa Maoni yaliyotolewa na Kamati Bungeni wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;
- ii) Uchambuzi wa ukusanyaji wa maduhuli ikilinganishwa na lengo lililowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;
- iii) Mapitio ya Taarifa ya Wizara kuhusu upatikanaji wa Fedha zilizo dhinishwa na Bunge, utekelezaji wa majukumu na changamoto katika Mwaka wa Fedha 2020/2021;
- iv) Uchambuzi wa majukumu na malengo yanayowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;
- v) Mapitio ya Malengo ya Bajeti na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;
- vi) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; na
- vii) Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la maelezo hayo ni kuliwezesha Bunge kupata taswira ya hali ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na kulinganisha na Makadirio ya Fedha za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ili Bunge liweze kuamua kuhusu Maombi ya Wizara hii.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 MAPITIO YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ilihusu maeneo Makuu matatu. Maeneo hayo ni: -

- i) Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati;
- ii) Mapitio ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge; na

iii) Utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilipitia na kuchambua kwa kina maeneo yote matatu kama ifuatavyo: -

## 2.1 Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Bunge lilipokuwa likijadili hoja ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Kamati ilitoa ushauri katika masuala kumi na tatu (13). Katika kufuatilia namna ambavyo Wizara imezingatia Ushauri huo, tarehe 28 Machi, 2020, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki alijulisha Kamati kuhusu utekelezaji wa masuala hayo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, upo ushauri uliotekelzwa kikamilifu, upo unaoendelea kutekelezwa na upo ushauri unaohitaji kuzingatiwa zaidi katika utekelezaji wake hususan ushauri uliohusu masuala ya Kibajeti.

**Mheshimiwa Spika**, miongoni mwa ushauri uliotekelzwa kikamilifu ni kuhusu Serikali kupeleka watumishi wa kutosha katika Balozi zetu ikiwemo wataalam wa masuala ya Diplomasia ya uchumi.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yaliyotolewa yalionesha kuwa Serikali ilizingatia ushauri huo ambapo zoezi la kuwapata Maafisa wenye sifa kwenda Ubalozini limekamilika na taratibu za mwisho za kuwapleka vituoni zilikuwa zikiendelea.

**Mheshimiwa Spika**, moja ya ushauri unaoendelea kufanyiwa kazi unahusu kuipatia APRM – Tanzania fungu lake la Bajeti (Vote) ili kuiwezesha kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi zaidi. Maelezo yaliyotolewa na Serikali yalionesha kuwa, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaendelea na majadiliano yatakayowezesha kuipatia APRM - Tanzania fungu lake la bajeti. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa maelezo hayo hayo

yalitolewa kwa Ushauri kama huo ulitolewa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Ni rai ya Kamati kuwa suala hili lipewe uzito unaostahili kwani limekuwa likishauriwa na Kamati tangu Bunge la 10 bila kukamilika.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya ushauri ambao uzingatiaji wake ulikuwa na changamoto za Kibajeti ulihusu Serikali kutoa fedha zote za maendeleo zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 kiasi cha shilingi Bilioni Nne. Hata hivyo, maelezo yaliyotolewa yalionesha kuwa hadi kufikia Juni 2020, Wizara ilipokea Shilingi 603,473,965.60 sawa na asilimia 15.09 tu.

Aidha, sambamba na ushauri huo, Kamati ilishauri kuwa fedha za maendeleo zilizotengwa katika Mwaka 2020/2021 zitolewe kwa ukamilifu na kwa mtiririko uliopangwa. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Februari, 2021, Wizara haikuwa imepokea fedha hizo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla ushauri wa Kamati umefanyiwa kazi na utekelezaji upo katika hatua mbalimbali. Hata hivyo, Kamati inaendelea kusesitiza kuwa, ushauri wa Kamati kuhusu Wizara hii kupelekewa fedha za maendeleo kwa kadri zinavyoidhinishwa na Bunge unapaswa kupewa uzito stahiki. Kwa kufanya hivyo Serikali itaokoa fedha nyingi zinazotumika kulipia Kodi ya Pango kwa majengo yaliyokodiwa kwa ajili ya makazi na Ofisi za Watumishi wa Balozi zetu nje ya nchi na vilevile itaongeza pato lake kwa kukodisha majengo ya Balozi yatakayojengwa na sehemu yake kutumika kama kitega uchumi.

## **2.2 Uchambuzi wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipitia Taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara katika Kipindi cha Julai 2020 hadi Februari, 2021 kwa kuchambua hali ya Ukusanyaji wa Mapato

pamoja na upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina kwa kipindi hicho.

### 2.2.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara hii ilikuwa na lengo la kukusanya Maduhuli ya kiasi cha Shilingi 2,550,879,000.00 ikiwa ni tofauti ya Shilingi 72 tu ikilinganishwa na lengo la Mwaka 2019/2020. Kati ya fedha hizo Shilingi 47,170,000.00 ni makusanyo ya Makao Makuu ya Wizara na Shilingi 2,503,709,000.00 ni makusanyo kutoka Balozi za Tanzania Nje ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia Mwezi Februari, 2021 Wizara ilikuwa imekusanya Shilingi 482,134,630 tu sawa na asilimia 18.9 tu ya lengo lililowekwa. Aidha, kati ya fedha zilizokusanywa, Shilingi milioni 26,535,000 zilikuwa ni makusanyo ya Makao Makuu ya Wizara ambayo ni asilimia 56.3 ya lengo la Shilingi 47,170,000 lililowekwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ulinganisho wa makusanyo ya Wizara kwa kipindi cha kufikia Februari, 2020 na kubaini kuwa makusanyo ya kipindi hiki ni pungufu kwa asilimia 90. Katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini yafuatayo:-

i) Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ilipanga kukusanya Shilingi **2,550,879,072.00**. Hata hivyo, hadi kufikia Mwezi Februari, 2021 Wizara ilikuwa imekusanya Shilingi Billioni **5,010,149,591.26** sawa na asilimia 196.4 ya lengo la ukusanyaji lililokusudiwa. Makusanyo hayo yalichangiwa na baadhi ya Balozi kuendelea kukusanya maduhuli ya VISA ambayo yanapaswa kukusanywa na Idara ya Uhamiaji. Hata hivyo, tangu Mwezi Novemba, 2019 hakuna Ubalози wowote ulioendelea kukusanya maduhuli hayo.

ii) Wizara kukusanya asilimia 18.9 ya lengo lililopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kumetokana na kukosekana kwa Wapanganji katika baadhi ya majengo ya Serikali kwenye Balozi za Tanzania nje ya nchi. Kwa mfano, Ubalози wa Tanzania Maputo ulikusanya asilimia 14.3 tu ya lengo

lililowekwa la Shilingi 180,789,102.00 na Ubalizi wa Tanzania New York ulikusanya asilimia 14.3 ya lengo lililowekwa la Shilingi 108,953,294.83. Kamati ilielezwa kuwa hali hii imesababishwa na uwepo wa janga la ugonjwa wa homa kali ya Mapafu unaosababishwa na Virusi vya Corona (COVID- 19).

iii) Fedha zilizokusanywa, Shilingi 482,134,630 ni ongezeko la asilimia 25 ikilinganishwa na Shilingi 385,627,026.30 zilizokusanywa na Wizara nje ya fedha za VISA hadi kufikia Februari, 2020.

**Mheshimiwa Spika**, kulingana na uchambuzi uliofanyika, Kamati ina maoni kuwa Mwenendo wa makusanyo ya Wizara kwa makao makuu ni wa kuridhisha na inaamini lengo lililowekwa litafikiwa hadi kufikia Mwezi Juni, 2021. Hata hivyo, kwa upande wa Makusanyo katika Balozi za Tanzania nje, ni dhahiri kuwa ugonjwa wa homa kali ya mapafu umechangia makusanyo hayo kutofikia nusu ya lengo lililowekwa hasa kwa kuzingatia kuwa asilimia 98.15 ya lengo hilo la makusanyo lilikuwa ni makadirio kutoka Balozi za Tanzania nje.

## 2.2.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipochambua Taarifa ya upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ilibaini kuwa hadi kufikia Mwezi Machi, 2021, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 107,834,686,039.66 sawa na asilimia 53.9 ya fedha zote za Bajeti zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya Matumizi ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, kiwango cha fedha kilichotolewa ni pungufu ya asilimia 5.19 ikilinganishwa na Shilingi 113,743,812,858.06 zilizotolewa hadi kufikia Mwezi Machi, 2020 ambazo zilikuwa ni asilimia 68 ya fedha zote za Bajeti zilizoidhinishwa kwa Mwaka 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa upungufu huo umechangiwa na fedha za matumizi mengineyo zilizotolewa kwa upungufu wa asilimia 5.59. Aidha, katika fedha

zilizotolewa hadi kufikia Mwezi Machi, 2020 asilimia 0.42 ilikuwa ya fedha za maendeleo tofauti na Mwaka 2020/2021 ambapo kati ya fedha zilizopokelewa hakukuwa na fedha zozote kwa ajili ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini pia, kati ya Fedha zilizopokelewa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Shilingi 100,459,141,116.98 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Fedha hizo ni sawa na asilimia 58.9 ya Shilingi 167,717,723,000 zilizotengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, Shilingi 7,375,544,922.68 zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara ikiwa ni sawa na asilimia 61.29 ya Shilingi 12,032,961,000 zilizotengwa kwa ajili hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa shilingi Bilioni 20 zilizokuwa zimeidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hazikuwa zimetolewa hadi kufikia Mwezi Machi, 2021. Fedha hizi zililenga kutekeleza miradi nane (8) inayojumuisha ujenzi wa uzio wa viwanja vya Balozi<sup>1</sup> pamoja na ujenzi<sup>2</sup> na ukarabati<sup>3</sup> wa majengo ya Balozi za Tanzania nje ya nchi; na upanuzi na uboreshaji wa miundombinu ya Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina maoni kuwa kutokutolewa fedha za maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu, kunaathiri ratiba ya utekelezaji wa miradi hiyo ambayo ingeokoa fedha zinazotumika kama pango vilevile ingeingiza mapato Serikalini kutokana na kukodisha sehemu ya majengo yanayokusudiwa kuwa na vitega uchumi.

Kwa mfano, ukarabati wa jengo la zamani la Ubalozi wa Tanzania Washington D.C. utawezesha Ofisi za Ubalozi Ofisi za Balozi kuhamia katika jengo hilo na jengo linalotumika sasa kupangishwa kama kitega uchumi ambapo linakadiriwa kuwa litakuwa na uwezo wa kuiingizia Serikali mapato ya shilingi Bilioni 2.4 kwa Mwaka na ukarabati wake kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 umekadiriwa kugharimu Shilingi Bilioni 3,864,440,000.

### **2.3 Utekelezaji wa majukumu ya Wizara**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa iliyotolewa na Wizara ilibainisha kuwa katika kipindi cha Julai 2020 hadi 10 Machi, 2021, Wizara iliendelea kutekeleza majukumu yake tisa ikiwemo kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje, Kuratibu na kusimamia masuala ya Watanzania waishio ughaibuni, kuratibu masuala ya mahusiano baina ya Tanzania na nchi mbalimbali; Kusimamia na kuratibu masuala ya Itifaki na Uwakilishi na kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Taasisi zilizo chini ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilichambua Taarifa za Taasisi zilizo chini ya Wizara hii ikiwa ni pamoja na Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC); Chuo cha Diplomasia na Mpango wa Afrika wa Kujitathmini (APRM). Kamati iliridhika na utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza majukumu yake kama ilivyopangwa licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali zikiwemo za ukosefu wa fedha kwa ajili ya utelezaji wa miradi ya maendeleo; uchache wa watumishi ikilinganishwa na wingi wa majukumu; uchakavu na uhaba wa magari katika Ofisi za Makao makuu, Ofisi ya Zanzibar na Balozini; na mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu ambao uliathiri pamoja na mambo mengine, lengo la makusanyo ya mapato.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, katika Uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa changamoto nne (4) kati ya tano (5) zilizotolewa Taarifa kuwa ziliathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2020/2021, ni zile ambazo Kamati imekuwa ikiishauri Serikali mara kwa mara kuhusu umuhimu wa kuzitatua. Ushauri huo ni pamoja na Serikali kupitia Ofisi ya Rais- Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kutoa vibali vya ajira mpya na mbadala za kujaza nafasi zilizo wazi hususan katika Balizi za Tanzania nje.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, ushauri kuhusu Wizara kutoa fedha zinazo idhinishwa na Bunge hususan fedha za maendeleo

umekuwa ukitolewa mara kwa mara kwa Wizara hii. Kamati ina maoni kuwa, endapo fedha hizi zingetolewa kwa kufuata ratiba ya utekelezaji wa miradi hiyo, Serikali ingekuwa na majengo mengi ya vitega uchumi katika Balozi zetu nje ambayo yangesaidia kukuza pato la Taifa na vilevile kuokoa fedha zinazotumika kulipia pango kwa ajili ya kukodisha makazi na Ofisi katika Balozi zetu.

## SURA YA TATU

### 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA BAJETI YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

#### *3.1 Uchambuzi wa Malengo ya Bajeti*

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya kueleza uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii, namenda kutoa Taarifa kuwa, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara imepanga kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele Kumi (10) tofauti na ilivyokuwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambapo Wizara ilijiwekea vipaumbele kumi na moja (11).

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, kamati imebaini kuwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara haijaweka kipaumbele cha Kukamilisha Sera ya Mambo ya Nje na Kanzidata ya Diaspora. Hata hivyo, kamati imebaini kuwa kipaumbele hicho kinatarajiwa kutekelezwa na kukamilika ndani ya Mwaka huu wa Fedha (2020/2021).

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Kamati imekuwa ikishauri mara kwa mara kuhusu suala la kukamilisha Sera ya Mambo ya Nje itakayojumuisha masuala muhimu ya Diaspora na mtangamano wa Afrika Mashariki, ni imani ya Kamati kuwa sasa Sera hii itakamilika kabla ya kumalizika kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, Kamati imebaini kuwepo kwa vipaumbele vipya vitatu (3) ikilinganishwa na vipaumbele vya Mwaka 2020/2021. Vipaumbele hivyo ni: -

i) Kuimarisha na kudumisha mahusiano ya kidiplomasia na nchi nyingine duniani;



ii) Kuweka mazingira wezeshi na kuendelea kuratibu na kuhamasisha ushiriki wa Watanzania waishio nje ili waweze kuzitangaza fursa zinazopatikana nchini na kushiriki kikamilifu katika kuchangia maendeleo ya nchi; na

iii) Kulinda na kutetea misingi ya Taifa letu ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa vipaumbele hivyo na ina amini kuwa vitaleta tija inayokusudiwa katika kuimarisha na kukuza mahusiano ya kimataifa.

### ***3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipitia Makadirio ya ukusanyaji wa Mapato yanayopendekezwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini kuwa kiasi cha Shilingi 2,550,879,000. 00 kinachokadiriwa kukusanywa ni sawasawa na Makadirio ya makusanyo yaliyowekwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yaliyowasilishwa mbele ya Kamati yalibainisha kuwa, Shilingi 47,240,000 sawa na asilimia 1.85 ni fedha zinazotarajiwa kukusanywa na Makao Makuu ya Wizara. Aidha kiasi kinachobaki cha Jumla ya Shilingi 2,503,639,000 sawa na asilimia 98.15 kinatarajiwa kukusanywa kutoka katika Balozi za Tanzania Nje.

Aidha, katika Uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa ni Balozi tano (5) tu za Tanzania nje ya Nchi katika Majiji ya Lusaka, Maputo, New York, Paris, na Harare ndizo zinatarajiwa kukusanya mapato ya Serikali kupitia pango la Nyumba za Serikali. Balozi hizo ndizo pia zilitegemewa kukusanya katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 hivyo hakuna Balozi mpya ambazo zinatarajiwa kuingizia Serikali mapato kutokana na kodi ya pango.


**Mheshimiwa Spika**, baada ya kufanya uchambuzi wa kina Kamati imejiridhisha kuwa lengo lililowekwa limeendana na hali halisi.

### 3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara iliileza Kamati kuwa inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Shilingi 192, 265,438,000/= Kati ya fedha hizo, Shilingi 167,937,219,000/= ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), Shilingi 10,828,219,000/= ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi 13,500,000,000/= ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua maombi hayo na kubaini kuwa asilimia 87.34 ya fedha zinazoombwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), asilimia 5.6 ni kwa ajili ya Mishahara na asilimia 7 ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo kama inavyoonekana katika Chati Na. 1 ya Taarifa hii.

#### Chati Na. 1: Uwiano wa Fedha zinazoombwa kwa Matumizi ya Wizara



#### Chanzo: Randama ya Wizara 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi Kamati imebaini kuwa, Bajeti inayoombwa kwa ajili ya Mwaka 2021/2022 imepungua kwa asilimia 3.74 ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa fedha 2020/2021. Upungufu huo umechangiwa na kupungua kwa Bajeti ya Maendeleo kwa asilimia 32.5 na Bajeti ya Mishahara kwa asilimia 10 ikilinganishwa na fedha zilizoidhinishwa kwa matumizi hayo katika mwaka wa fedha 2020/2021. Hata hivyo, fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo zinazoombwa ni ongezeko la asilimia 0.13.


**Mheshimiwa Spika**, sura ya uwiano wa Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, Mishahara na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na ulinganisho wake kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 inaonekana katika Jedwali Na. 1 na grafu Na. 1

**Jedwali Na. 01: Uwiano wa aina za Bajeti ya Matumizi na ulinganisho wake kwa Mwaka 2020/2021 na 2021/2022**

| MWAKA                   | 2020/2021          |          | 2021/2022          |          | % +/- |
|-------------------------|--------------------|----------|--------------------|----------|-------|
|                         | KIASI              | ASILIMIA | KIASI              | ASILIMIA |       |
| MISHAHARA (PE)          | 12,032,961,000.00  | 6        | 10,828,219,000.00  | 5.6      | -10   |
| MATUMIZI MENGINEYO (OC) | 167,717,723,000.00 | 84       | 167,937,219,000.00 | 87.34    | 0.13  |
| MIRADI YA MAENDELEO     | 20,000,000,000.00  | 10       | 13,500,000.00      | 7        | -32.5 |
| JUMLA                   | 199,750,684,000.00 | 100      | 192,265,438,000    | 100      |       |

**Chanzo:** Randama ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano 2021/2022

**Grafu Na. 1: Ulinganisho wa Uwiano wa Bajeti ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na 2021/2022**



**Chanzo:** Randama ya Wizara 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, katika uchambuzi wake, Kamati ilirejea mapendekezo ya Bajeti Kuu ya Serikali na kubaini kuwa wakati Bajeti ya Maendeleo kwa Wizara ni asilimia 7 tu ya Bajeti yote, asilimia 37 ya bajeti kuu imeelekezwa kwenye matumizi ya maendeleo. Aidha, Kamati ilibaini kuwa, wakati Bajeti ya Maendeleo ya Bajeti kuu ya Serikali imeongezeka kwa asilimia nne (4) ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Bajeti ya Wizara iliyotengwa kwa ajili ya Maendeleo imepungua kwa asilimia 32.5 ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, pamoja na kuwa mapendekezo ya Bajeti ya maendeleo imepungua ikilinganishwa na Shilingi Bilioni ishirini (20) zilizoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, uhalisia ni kwamba fedha hizo bado hazijatolewa. Kiasi hicho kilipangwa kutekeleza miradi nane (8) ambapo katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Bajeti inayoombwa ni kwa ajili ya kutekeleza miradi minne (4) ya maendeleo. Hivyo, ni maoni ya Kamati kuwa upangaji wa miradi michache ambayo inaweza kutekelezeka ni suala linalotakiwa kupewa umuhimu wa kipekee. Ni rai ya Kamati kuwa katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali itoe fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa ukamilifu na kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kati ya miradi minne (4) iliyopangwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, ipo miradi mitatu (3) kati ya miradi nane (8) iliyokuwa imepangwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021. Miradi hiyo inayojumuisha Ujenzi wa majengo ya Ofisi na Makazi katika Balizi za Tanzania Kinshasa na Muscat, pamoja na upanuzi wa miundombinu ya Chuo cha Diplomasia. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kuendelea kutekeleza miradi ya Mwanzo kabla ya kuibua miradi mingine mipya.

## SURA YA NNE

### 4.0 MAONI NA USHAURI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuwasilisha uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, naomba sasa niwasilishe Maoni na Ushauri wa Kamati, kama ifuatavyo: -

i) Serikali itoe fedha za maendeleo shilingi Bilioni ishirini (20) zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Kulingana na muda uliobaki wa kukamilisha mwaka wa fedha 2020/2021, Kamati inashauri kipaumbele kitolewa kwa ajili ya mradi wa kukarabati jengo la zamani la Ubalizi wa Tanzania Washington D.C. ulioidhinishwa Shilingi 3,864,440,000/. Ukarabati huu utakapokamilika utawezesha jengo hili kuwa na uwezo wa kuiingizia Serikali mapato zaidi ya Shilingi Bilioni 2.4 kwa Mwaka.

ii) Serikali itekeleze Mpango wake wa Miaka Kumi na Tano (2018/2019-2031/2032) wa Ujenzi, Ununuzi na Ukarabati wa Majengo ya Ofisi na Makazi katika balozi zetu kwa kuendelea kutoa fedha kadri zinavyoidhinishwa na Bunge. Kamati inaamini kuwa Serikali itaokoa fedha nyingi zinazotumika kulipia pango endapo mpango huo utafanikiwa. Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Serikali inatarajia kutumia takribani Shilingi bilioni 24,769,113,034 kwa ajili ya pango katika Balozi za Tanzania Nje.

iii) Serikali ikamilishe Mchakato wa kuandaa Sera ya Mambo ya Nje katika Mwaka wa fedha 2020/2021 kama ilivyoahidi, kulingana na umuhimu wake kisiasa, kiuchumi na kijamii.

iv) Serikali iweke mpango mkakati wa kushughulikia changamoto ya muda mrefu ya uchakavu na uhaba wa magari hususan katika Balozi za Tanzania nje. Kutokushughulikiwa kwa changamoto hii kunaweza kuharibu Taswira ya Nchi yetu nje ya Nchi.

v) Serikali kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora ione umuhimu wa kutoa vibali vya ajira mpya na mbadala za kujaza nafasi zilizo wazi katika Balozi zetu ambazo zimekuwa zikikabiliwa na uchache wa watumishi licha ya kuwa na majukumu mengi. Changamoto hii imekuwa ya muda mrefu jambo ambalo linaweza kuathiri utendaji katika Balozi zetu nje. Aidha watumishi hao wawe ni pamoja na wataalam wa diplomasia ya uchumi;

vi) Serikali iendelee kuhamasisha watanzania waishio nje (diaspora) kujiandikisha katika Balozi zetu na kuwawekea mazingira wezeshi ya kufanya uwekezaji nchini;

vii) Serikali iziwezeshe na kuzifuatilia baadhi ya Wizara za Kisekta ambazo zikifanya kazi kwa juhudi na ufanisi zitaongeza pato la Taifa kwa kusimamia uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo ambayo yana soko kubwa nje ya nchi kama vile nyama ya mbuzi katika masoko ya nchi za kiarabu.

viii) Serikali izidishie juhudi za kuzisimamia Balozi zetu nje ya nchi kutangaza fursa za kitalii na vivutio mbalimbali zilizopo nchini kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii.

ix) Serikali iendelee kuhamasisha sekta binafsi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na mtangamano wa Afrika Mashariki na Masoko ya kimataifa;

x) Serikali iendelee kutafuta wawekezaji ambao wanamaslahi na nchi yetu ili kuongeza pato la nchi na ajira.

xi) Wizara iendelee kutekeleza Maoni na Mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambayo hayajatekelezwa hususan katika Bajeti za miaka mitatu iliyopita ya 2018/2019, 2019/2020 na 2020/2021.

## SURA YA TANO

### 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe

wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard): -

1. Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Vicent Paul Mbogo, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Bonnah Ladislaus Kamoli, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani - Mjumbe
8. Mhe. Janeth Maurice Masaburi - Mjumbe
9. Mhe. Cosato David Chumi, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Alexander Pastory Mnyeti, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Muharami Shabani Mkenge - Mjumbe
17. Mhe. Mwinikondo Rajab Mustafa - Mjumbe
18. Mhe. Ali Juma Mohammed, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Godwin Emmanuel Kunambi, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi, (Mb), Naibu Waziri, Mhe. William Ole Nasha, Mb na aliyekuwa Katibu Mkuu Balozi Kanali Wilbert Ibuge, pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Aidha, kipekee, Kamati inawapongeza Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, Mb kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Aidha, tunampongeza Balozi Joseph Sokoine kwa kueuliwa kuwa Katibu mKuu wa Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru aliyekuwa Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi yake kwa ufanisi na Ndg. Nenelwa Mwihambi kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Katibu wa Bunge na hatimaye kuiwezesha Kamati kuandaa na kukamilisha kazi yake kwa wakati. Aidha, nawashukuru Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Gerald Magili Mkurugenzi Msaidizi, Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Mussa Azzan Zungu, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO  
YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

Juni, 2021

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zahor Haji kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, tunakushukuru sana, ahsante sana.

Sasa tunaingia katika eneo la uchangiaji ambalo ningeliomba tuanze na Mwenyekiti wa Kamati, atuanzishie



Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu na atafuatiwa na Mheshimiwa Cosato David Chumi.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Kamati yetu hii, na kunipa nafasi ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, mimi nipo kwenye Kamati hii toka mwaka 2005 nilikuwa Makamu Mwenyekiti wakati wa Mama Anna Abdallah, Makamu Mwenyekiti kipindi cha Masilingi, Makamu Mwenyekiti kipindi cha Lowassa na Mungu amenijalia sasa kwa rehema zake na mapenzi yake nimekuwa Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni pesa za maendeleo ambazo zinatakiwa zije kwenye Wizara hii haziji. Tunatatizo kubwa sana za kutumia pesa kulipa pango katika mabalozi nje ya nchi, takribani kwa miaka kumi Serikali inatumia siyo chini ya shilingi bilioni 220 kulipa pango tu, pesa hizi zingeweza kuwa *re-invested* na tukawa tuna majengo yetu na ikawa ni heshima kwa Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiwa na majengo yetu tuna nafasi ya kupata kodi na tuna nafasi ya kutokulipa kodi kwa nchi zingine, sijui kwa nini hii hoja Serikali wanaiona ni nzito kwao. Mwaka 2021 na tumeitoa kwenye taarifa pesa za maendeleo shilingi bilioni 20 hata senti tano mpaka leo hajjatoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeahidiwa kwenye kikao cha pamoja kwa mujibu wa kanuni zetu, Kamati ya Uongozi na Kamati ya Bajeti kwamba fedha zitalipwa *by May* na sina taarifa mpaka sasa hivi kama hizo fedha zimelipwa. Ni jambo ambalo linaturudisha nyuma. Kuishi katika nyumba za kupanga Balozi wa Tanzania ni *kutoku-secure information* za nchi huko tuliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, usalama wa taarifa za Balozi na makao makuu ya nchi unakuwa na mashaka makubwa. Tulipangiwa mwaka 2019/2020 bilioni nne; fedha zilizotoka ni

takribani milioni 300 tu. Sasa bila kuwa na fedha zetu au bila kuwa na majengo yetu hatuwezi kuwa na diplomasia nzuri ya uchumi. (Makofi)

Hoja yangu kubwa na Waziri wa Fedha yuko hapa, niombe waweke uzito mkubwa sana wa namna gani kuisaidia Wizara hii iweze kupata fedha za maendeleo. Tumeweza kununua nyumba *New York* naipongeza Serikali, nyumba ile sasa nayo tunakaa wenyewe bila kulipa kodi, lakini vilevile sasa tunatoza watu kodi kwa kuwapangisha katika eneo lile. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tuna kiwanja Uingereza *primed area*, huu zaidi ya mwaka wa 15 mpaka kiwanja kile sasa kinaota magugu. Kuna gharama kubwa ya kutoa ile mizizi na inakuwa ni aibu na mpaka sasa mwisho, majirani kwenye kiwanja kile wanalalamikia kwenye Serikali yao, kiwanja kile tunyang'anywe na kiwe mali ya Serikali ya Uingereza na sisi tukose. Yote hatupeleki fedha za kujenga majengo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mengi tunayasema kwenye ripoti yetu sitaki kuingia kwenye mambo mengi sana niwaachie wajumbe wengine, lakini mimi nilitaka kujenga hoja kwenye nyumba tu, tuweze kununua nyumba zetu, tumiliki nyumba zetu na tuzikarabati ziwe mali ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunashindwa sasa hivi mpaka na mataifa mengine madogo namna wanavyokuwa na majengo. Kuna nchi hapa Afrika Mashariki ukienda pale Mtaa wa *UN*, unaona jina lake inapendeza kuona pale *House of Uganda*.

Kwa hiyo, mimi niombe sana Serikali, Waziri wa Fedha uko hapa, *Chief Whip* yuko hapa, tunaomba Wizara hii muipe fedha iweze kukarabati na muwape fedha ili tuweze kununua tumiliki nyumba katika nchi za mabalozi yetu nje ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, nilishakutaja Mheshimiwa Cosato Chumi, utafuatiwa na Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na ningependa kuanza kwa pongezi kwa Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan, nampongeza Mheshimiwa Rais hasa kwa ile ziara yake ya majirani zetu Kenya. Ziara ile Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mashahidi imeendelea kufungua fursa za kibiashara sio tu kwa sisi ambao tunatoka tunakolima mahindi kama mikoja ya Nyanda za Juu Kusini na hususani Mafinga, lakini kwa maeneo mengi mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napongeza jitihada hizi kwa sababu katika maisha huwezi kuchagua jirani, lakini jirani ndio ndugu yako. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais na hii kama yeye *diplomat* namba moja, hii ndio maana halisi ya diplomasia ya uchumi. Lakini pia naendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uteuzi wa Mabalazi ambao miongoni mwao watakuwa ni Wakurugenzi katika Wizara ya Mambo ya Nje kwa sababu kwa muda mrefu Wizara ilikuwa ukiacha Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na Mkurugenzi wa Utawala na Fedha na *Chief Accountant* na mtu wa *PMU, the rest* walikuwa wanakaimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kitendo hiki cha kuteua kwa kweli ni jambo la kupongeza sana na linawapa watumishi wale *confidence* katika kufanya kazi. Lakini pia nitumie nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri kwa uteuzi na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa kweli, yaani ninyi ni wanadiplomasia wabobevu na nikuambie tu Mheshimiwa Waziri, matumaini aliyonayo Mheshimiwa Rais kwenu ninyi na sisi Wabunge na Watanzania kwa ujumla, ni makubwa sana na sisi tunawaombea mfanye kazi kwa bidii na Mungu atawaongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha sasa diplomasia ya uchumi yapo mambo ni muhimu katika kuwezesha jambo

hili lifanikiwe kama alivyosema Mheshimiwa Zungu Mwenyekiti wetu wa Kamati. Baadhi ya mambo muhimu ni pamoja na watumishi katika Balozi zetu, lakini pamoja na vitendea kazi kama magari pamoja na nyumba kama ofisi, lakini pia nyumba kama makazi. Sasa katika suala la makazi na ofisi kama alivyosema Mheshimiwa Mwenyekiti pale. Nianze kwanza na yale maeneo ambayo ni muhimu kwa Serikali kutenga fedha, ili kuendana na mpango wa Serikali wa mwaka 2018/2019 mpaka 2030/2031; mpango kama wa miaka 10 hivi. Mpango huu lengo lake ni ujenzi, ununuzi na ukarabati wa majengo na makazi na ofisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema mjumbe aliyetangulia, tunatumia fedha nyingi sana kwa ajili ya ofisi na makazi na haikwepeki kwa sababu lazima tuwe na ofisi na lazima tuwe na makazi. Lakini hili pia ni eneo moja ambalo Serikali inaweza ikawekeza ikapata fedha. Nitatoa mfano, kwa mfano, Nairobi tuna kiwanja pale ambacho pakijengwa kitega uchumi, *projection* yake kwa mwaka tunaweza tukapata *2.3 billion* na hivyo tutakuwa tumeokoa pango ambalo tunalipa kwa sasa *1.4 billion*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kujenga kwanza tuta-*generate income*, lakini pili, tutapunguza gharama ambazo sasa tunaziingia katika kukodi majengo ya ofisi na makazi. Tukienda Congo DRC tuna kiwanja pale ambapo tunaweza tukajenga jengo la ofisi na kitega uchumi ambapo tunaweza tukapata karibu bilioni 13 kwa mwaka na tukaokoa gharama ambazo ni milioni 540 tunazotumia kwa sasa. Lakini vivyo hivyo tukijenga Comoro tunaweza tukapata mapato milioni 520, lakini tukawa tumeokoa milioni 420. Kwa hiyo, kiujumla kama unapata 520 na umeokoa milioni 420 umepata kama bilioni moja. Kwa hiyo, niombe kwa Serikali na hasa hususani Wizara ya Fedha kujenga majengo nje ya nchi sio *luxurious*, ndio uchumi wenyewe kwa sababu tutaokoa fedha lakini pia, tutakuwa tumeingiza fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika taarifa yetu ya Kamati, unaweza ukaona yako maeneo ambako mpaka sasa hivi yanatuingizia fedha nyingi sana mojawapo ni hiyo New York.

Lakini katika mwaka huu wa fedha huu ambao tunaumaliza, tunatumia karibu shilingi bilioni 22 kwa makazi na ofisi. Bajeti hii tunayoenda nayo tutatumia bilioni 24 kwa makazi na ofisi, masuala ambayo kama tutajielekeza katika ule mkakati wetu wa miaka 10 kwamba tujenge na tukarabati baadhi ya maeneo na bahati nzuri viwanja vyetu viko maeneo ambayo ni *prime*, kwa hiyo, tutaokoa hizi gharama lakini pia tuta-*generate income*, lakini *diplomatically* unapokuwa na jengo lako mwenyewe nayo inaongeza hadhi ya heshima katika Taifa lako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni suala la watendaji na maafisa katika Balozi zetu, ni muhimu sana Balozi hizi ili kuleta tija katika diplomasia ya uchumi zikawezeshwa kwa kupeleka maafisa wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumezungumza hapa ndani nadhani ni miaka minne na kuna mwaka mimi nilishika mpaka shilingi, lakini mara zote Serikali ilisema watapeleka, watapeleka na mbaya zaidi maafisa wengi wamerudi. Nchi kama Marekani ina tofauti ya masaa baina ya *West* na *East* masaa matatu, sasa unakuwa na afisa pale mmoja au unakuwa na Balozi tu. Nchi kuna vituo nitatoa mfano hapa. Vituo ambavyo ni *multilateral* kwa mfano, Kituo kama Geneva pale kuna Mashirika makubwa ya Umoja wa Mataifa, Shirika la Kazi, Shirika la Afya, *WTO* wako pale, lakini sasa unapokuwa tu na Balozi bila maafisa wa kumsaidia tija ya diplomasia ya kiuchumi haiwezi kupatikana. (*Makofi*)

Maeneo kama Rome kuna mashirika pale ya Kimataifa, lakini hata pale New York kwenye makao makuu ya Umoja wa Mataifa. Umoja wa Mataifa unafanya kazi kwa kutumia Kamati zake zile sita ni kama hili Bunge Waheshimiwa Wabunge, tunakutana kwenye Kamati tunakubaliana tunakuja hapa tunayahitimisha, vivyo hivyo Umoja wa Mataifa ndivyo unavyofanya kazi, kwa hiyo, kama huna *staffing* ya kutosha ina maana kuna Kamati itakaa, itajadili mambo, itayapitisha, wewe utakuwa umekosa mchango wako ama kwa namna nyingine utakosa kitu ambacho kingeweza kukunufaisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano, masuala ya *peace keeping*, Umoja wa Mataifa umeendelea kupunguza *budget* ya *peace keeping*, lakini sisi ni moja ya nchi ambayo inashiriki sana katika masuala ya *peace keeping*.

Sasa kama hukuwepo kwenye ile Kamati ina maana ile bajeti itapita, lakini kama ungekuwepo au masuala kama ya wakimbizi kama ungekuwepo ungejenga hoja kwamba jamani jambo hili ni la muhimu lisipite, tulirekebisha kwa mtindo moja, mbili, tatu. Kwa hiyo, huu ni umuhimu mkubwa sana wa kuhakikisha kwamba tunapeleka maafisa ili kusudi hiyo diplomasia ya uchumi iweze kutimilika na iweze kuwa na tija. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nchi kama China unakuta Balozi yuko peke yake na wale waambata tu, hana maafisa wale ambao ni *foreign service officer* wa kumsaidia na ni nchi kubwa, lakini ni rafiki na ina uchumi mkubwa. Kwa hiyo, niombe sana Serikali kama ni Wizara ya Fedha kama ni Wizara yenyewe ilione hilo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, baada ya kuwa nimepongeza uteuzi wa Wakurugenzi niombe pia Wizara, tuweze kushirikiana na Utumishi wapatikane Wakurugenzi Wasaidizi ambao ndio wanakuwa *head of section* ili kusudi kuwe na *succession plan* isiwe kama sasa hivi ambapo watu wamekaimu karibu miaka minne. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe na hii Mheshimiwa Waziri ni jukumu ambalo liko ndani yenu ninyi kama Wizara, kisha mnashirikiana na Utumishi mnawapandisha watu na Mheshimiwa Balozi Mulamula wewe watu wengi pale ni matunda yako.

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe ni sehemu ya matunda yako, kwa hiyo, unawajua nani ana weledi, wana uwezo kiasi gani, wapatieni watu hizo fursa wawe Wakurugenzi Wasaidizi, diplomasia ya uchumi iweze kuthibitika kwa vitendo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno haya Mungu atubariki sote, Mungu aibariki Tanzania, kazi iendelee, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimwia Cosato David Chumi. Sasa tunaenda kwa Mheshimiwa Balozi Pindi Hazara Chana na atafuatiwa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa PAC, Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka.

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza nimpungeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, lakini ili kutimiza itifaki nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan. Kwa kweli Tanzania inang'ara, amefanya ziara katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki tunamshukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanja na majengo mengi yamezungumzwa; mimi nitazungumza kidogo ili ku-avoid kurudia.

Mheshimiwa Spika, umefika Nairobi kwenye ule Ubalozi tuna kiwanja kile, muda mrefu sana. Sasa hivi majengo haya ambayo Waheshimiwa wengine wamezungumza, sio lazima tujenge kwa kutumia mtaji wa Serikali, tunaweza tukajenga kwa kutumia *public private partnership*, unaweza ukaingia mashirikiano na taasisi mbalimbali. Nachukulia mfano, labda CRDB Bank wanataka kufungua *branch* pale, kwa hiyo, CRDB Bank mnakubaliana *public private partnership* sisi uwekezaji wetu unakuwa ni ile ardhi. Kwa hiyo, ningepomba eneo hilo la majengo na viwanja tuweke kipaumbele sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tujitahidi kuendelea kuwapa viwanja Mabalazi hapa Dodoma sasa hivi ndio makao makuu, tutafurahi makao makuu tuanze kuona bendera za Mabalazi zinapepea. Ubalozi wa nchi hii uko hapa Dodoma, Ubalozi wa nchi hii na tukiwapa viwanja Balozi hizi, kimsingi huwa tunabadilishana, ile *good gesture* ambayo sisi tumewaonesha na wao hivyo hivyo wanatupa viwanja kule katika makao makuu ya nchi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nipongeze sana Mheshimiwa Waziri hapa mtusaidie na Naibu tuna imani kubwa sana na ninyi. Hata zile Balozi ambazo hazina ofisi hapa Tanzania, ziko Balozi ambazo zina-*serve* Tanzania, lakini wameweka ofisi zao katika nchi zingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki na hapa mimi nakuja na swali. Tunatambua kwamba tunazo Balozi takribani 30 hazina ofisi Tanzania; tujjulize kwa nini? Balozi hizi ambazo wanakuja kufanya kazi na sisi wana-*present credential* hawana ofisi tuwashawishi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, unakuta hizi Balozi nyingi zimekaa katika nchi fulani na zingine nchi fulani, sisi tujjulize tatizo ni nini hawaweki ofisi hapa? Tuwape *incentive* kama ni masuala ya VAT huwa wanadai tuwarudishie kwa wakati, mawasiliano, tuimarisha. Ubalozi mmoja ukiwepo hapa Tanzania wanatumia mafuta, wataajiri vijana wetu hadi wa kule Njombe, huko Ludewa wataajiriwa, kutakuwa kuna *local best staff*, wahudumu *gardener*, wale watu wa *security*, uchumi unaongezeka. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya nchi yaani wao uchumi wao unaongezeka kwa kuamua tu kuweka taasisi za Kimataifa, dola zinapita mishahara kwenye *account*, you see. Hizi Balozi 30 naomba tu-*pay attention*, hatujachelewa na Balozi zingine mpya ambazo zinaendelea kuweka mashirikiano na Tanzania, tuombe wanavyokuja kuomba kuanza Ubalozi na sisi tuombe waweke ofisi. Mzunguko wa fedha ukiwa na Ubalozi mmoja tu, matumizi ya Balozi moja kwa hizi nchi za nje zikiwa hapa kwetu, unakuta sio chini ya dola 60,000 kwa mwezi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, bado hapo mishahara inapita kwenye Mabenki kwa hiyo, uchumi huu utaongezeka. Kwa hiyo, niombe sana *Madame* Waziri tuna imani utusaidie Naibu Waziri, Katibu Mkuu wote hawa ni wataalam ma-*guru* wa *foreign*. Balozi hizi zije na watoke Tanzania kwenda nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kutoa huduma, ku-*serve* au waende nchi za *SADC* kutokea Tanzania. Wanapoenda wanatumia *ATC* ni mfano tu, kwa hiyo, uchumi utabadilika



kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, naendelea kuunga mkono hii hoja na hizi changamoto ndio naziweka mezani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la watumishi limezungumzwa; kuna baadhi ya Vituo hatuna Maafisa wa Uhamiaji na kuna kada zingine nyingi kwa kweli ambazo ni muhimu sana. Kada hizi za afisa wa uhamiaji pale unahitaji utoe *Visa, tourist visa*, unahitaji utoe *business visa*, unahitaji utoe *multiple entry visa*, sasa kada hizi wakati umefika tuone namna gani wataalam hawa wanaenda.

Katika hilo hilo eneo la *visa*, kuna *visa* inaitwa *referred visa* sasa hivi *visa* zinatolewa kwenye mtandao. Lakini hiyo *referred visa* mara nchi hiyo inapoomba kupata *visa* watu wake, lazima taarifa ziende makao makuu ya nchi na wafanyie upekuzi. Wakati mwingine suala hili mchakato wake unachukua muda mrefu, tuko kwenye uchumi shindani, tuangalie *list* yetu ya *Referred Visa*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, unakuta sisi tumewekea nchi kadhaa *referred visa*, lakini ile nchi ambayo sisi tumeiwekea *referred visa* yamkini yenyewe haijaweka *referred visa* kwa Tanzania. Kwa hiyo, naomba tu-*review list* ya nchi ambazo tunazitambua kama nchi za *referred visa*. Leo hii mtalii anakuja anasema, nataka kuja Tanzania tunasema nchi yako iko kwenye *referred visa*, subiri wiki tatu, ataangalia Mlima Kilimanjaro kutokea nchi jirani, ataenda nchi jirani atasema *beach* ya Zanzibar inafanana na *beach* fulani ya nchi jirani, ata-*opt* kwa sababu ile nchi jirani inampa *Visa on arrival*, lakini sisi tunamuambia *you know Sir referred visa you have to wait two weeks*. Anakuambia *vacation* yangu imeisha, *my holidays are gone I can't wait*, ataenda nchi nyingine. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, twende na *reforms*, Waziri mtusaidie tunaomba sana. Wenzetu nchi jirani wameshabadilika hamna ma-*referred visa* inategemeana. Huko nyuma wakati tunapigania uhuru na nini changamoto zilikuwepo, sasa hivi kuna mitandao watu wa usalama wanajua kujua kama huyu ni *criminal* ama vipi?

Mheshimiwa Spika, eneo lingine kwa haraka haraka diplomasia ya uchumi, Balozi zetu nawapongeza sana Mabaloz wote, wanafanya kazi kubwa nzuri sana, diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa tuendeleo kuimarisha tunahitaji masoko ya mbao za kutoka Njombe, Mufindi. Mimi nashukuru sasa hivi mbao za Mufindi, Njombe tumejitahidi zinakwenda mpaka Somalia. Lakini ili jambo hili lifanikiwe mazao kama mahindi, viazi, korosho, pamba lazima tupeleke taarifa za kutosha katika Balozi zetu kiasi kwamba mwekezaji anapokwenda pale Ubalozini anapouliza kwamba una tani ngapi za pamba, una tani ngapi za korosho isiwe tena, ngoja kwanza niwasiliane na Wizara wanilettee, inachukua muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini taarifa hizi zikiwa kwenye website za Balozi zetu *e-government* yaani ni haraka sana wawekezaji watakuja, tutapata masoko na watatanga fursa mbalimbali kwa hiyo nawapongeza sana Mabaloz wamekuwa wakifanya kazi kubwa na nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine, ambalo ni muhimu, tufungue Balozi mpya, tusiogope kufungua Balozi mpya. Hivi karibuni tumefungua Balozi Mpya takriban saba/nane ni pongezi nyingi lakini dunia ni kubwa *we need to connect*. tuendeleo kufungua Balozi. Unaweza ukachagua nchi ukafungua Ubaloz pale unaamua kupelekea chai, unasema nchi fulani ni soko langu la uhakika la chai. Sasa hivi tunauza chai takriban dola 7 kwenye mnada wa Mombasa, lakini chai inaweza kutujengea Bandari ya Tanga. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda nimekusikia.

## T A A R I F A

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimpe Taarifa mzungumzaji anayezungumza sasa kwamba anachokisema ni sahihi, Guangzhou ni mji ambao ni mji wa kibiashara lakini pale hatuna Balozi mdogo ambaye angeweze kusaidia wafanyabiashara wetu wakienda wakasaidiwa kwa haraka. Ninamuunga mkono na ninampa taarifa hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Taarifa hiyo unaipokea Mheshimiwa Hazara.

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa hiyo naipokea na nimekumbuka kuweka msisitizo chini ya Balozi kuna *Honorary Consul, you see* kwa hiyo tunaweza tukaweka *Consular* Mkuu, pia tunaweza tukaweka enhee *Honorary Consul*, kwa hiyo haya yote yanawezekana utakuta nchi hatuna uwakilishi, hatuna *Honorary Consul*, hatuna *Consular* Mkuu, *Consular General, we need to connect*, huu ni wakati Mheshimiwa Waziri tusaidie, tusaidie, tuna Balozi chache sana tukilinganisha na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi za *SADC*. Wenzetu wanafunguka, wanafunguka wakati umefika vijana wetu hawa wakasome nje, wapate fursa mbalimbali za masomo, utaalum wa aina mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sijasikia kengele nadhani, naendelea, ahsante.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni *diaspora; diaspora* Watanzania waliopo nje wanarudisha fedha nyingi sana nyumbani. Wanasaidia kuongeza uchumi, duniani kote *diaspora* wamekuwa ni *tool* muhimu sana. Kwa hiyo, *diaspora* wetu ambao wako nje ni pongeze sana Mabalazi wamekuwa wakiwasajili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Dkt. Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Balozi. Nilishakutaja Mheshimiwa Naghenjwa

Kaboyoka na atafuatiwa na Mheshimiwa Jelly Silaa na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis wajiandae.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, suala la pango limeongelewa sana labda sitalirudia rudia sana, lakini niseme tu kwamba hata ripoti ya CAG tangu nimekuwa Mwenyekiti wa Kamati hii mwaka wa sita sasa imezungumzia sana fedha nyingi inayopotea kwenye kulipia fedha za pango kwenye Balozi zetu mbalimbali. Ni wazi kwamba fedha zile zingekuwa tumejenga ofisi zetu, kwanza mpaka sasa hivi tungekuwe tumeshamaliza na ofisi zile zingepangishwa.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme pia kwamba pamoja na hayo, ukiangalia kwa mfano Ubalozi wetu wa Washington, Mheshimiwa Liberata Mulamula - Waziri wewe nakufahamu sana na cv yako ni nzito hebu tembelea Ubalozi wetu tena uangalie. Inasikitisha na ni aibu, yaani jengo limechakaa, ni aibu *furniture* ni za zamani, labda ziwe zimewekwa mwaka jana ambapo sijakwenda. Lakini hata ukifika pale *layout* yake inatisha, yaani unatoka Ubalozi wa Kenya, uone wenzetu walivyopanga ofisi zao za kibalozu, ingia yetu ya Tanzania, utafikiri tupo ofisi ya Kariakoo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nakuomba sana tukaangalie hizi balozi zetu jinsi ambavyo zipo katika hali mbaya na ya aibu. Hiyo itatuwezesha kuona umuhimu wa kujenga majengo ya kisasa ambayo ni mazuri na kuweka *furniture* ambayo inayoendana na nchi yetu ambayo tumesema tunaingia katika uchumi wa kati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo maadili ya *staff*, nimekwenda kwenye balozi nyingi nyingi kitu ambacho nime-*observe* bado sisi sio *staff* wote, lakini pale unapokutana nao kwenye mambo ya *visa* kuna rafiki zangu wanasema hebu tukusindikize kwenye ubalozi wenu tukapate *visa*, utapata

aibu. Sitawataja hapa maana si vizuri, lakini unakuta watu wameweka maandazi, wameweka vitumbua, wamekaa wanakula, ukifika wanakuchekea, karibuni karibuni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mtu amekuja yupo *serious* katoka labda *state* ya mbali, anataka ahudumiwe haraka haraka, lakini anakutana na watu wanacheka cheka, wameweka maandazi yao hapo, wanakula, hawana hata aibu. Sasa unasema hivi kweli ile shule yetu ya Diplomasia si inafundisha watu *ethics*, enheee kwamba mnajiwekaje, mkiwa kwenye ubalizi mna-*behave* vipi, lakini hilo kwa Watanzania sisemi ni wote, wala sisemi ni Balizi zote, lakini sijui kama Europe na Marekani kuna Balizi za wenzetu ambazo sijaingia. Kwa hiyo tuna tatizo hilo kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nizungumzie watanzania wengine tunaokwenda kwenye *delegation* za nje. Hili halipo kwenye ripoti sijaliangalia, lakini zamani tulikuwa *delegation* ikitakiwa kwenda nje, Chuo chetu cha Diplomasia wanakaa nao wanawaeleza, sasa hivi ni wengi, lakini tuwe na mikakati ya kueleza watu wetu. Unakuta mmekwenda na *delegation* kikazi karibu *three quoters* wamekwenda *shopping*, mmekaa watu wawili/watatu pale. Tunaibisha kwamba kweli tumekwenda kufanya *shopping* hatukwenda kwa ajili ya yale yaliyotupeleka kama mikutano, ni aibu kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini pia *table manners* ni kitu muhimu sana, ni kitu hatukiongelei lakini nataka tukiongelee. Unakuta mmepangiwa *buffet*, mtu anajaza lisahani mpaka chakula kinamwagika, enhee! Yaani wakati tungefundishwa huku kwetu tumezoea kujaza maana utakula mara moja basi, lakini kule wenzetu *buffet* urudi hata mara tatu/mara nne. (Makofi/Kicheko)

Nimgeomba sana tuwe na njia ya kutengeneza semina ambazo zinahamasisha au zinaeleza *ethics* za kwenda kula kule nje. Niliona moja niliibika sana, mtu kaenda kachukua supu na mkate kaweka, kaenda kajaza chakula, alivyomaliza alisema sasa nishushie na supu sasa, yaani ile supu ya *starter* yeye ndio kafanya ndio ya kushushia.

Sasa wanatuangalia kwamba hawa watu gani hawa, wametoka wapi! (*Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa hao ni Wanyamwezi, Wasukuma. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, unaogopa kusema tumetoka Tanzania.

Kwa hiyo naomba sana yaani tuangalie hivi vitu vya kidiplomasia, *it matters a lot* kwamba tuna-*portray* picha gani tunapokenda nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuangalie hii Sera ya Diplomasia ya Uchumi. Nimefurahi mlivyoonesha kwamba mnaifanyia kazi na mnaikamilisha. Mimi ningeomba tu, kwenye sera ile sijaisoma, kwa hiyo, sijui. Lakini nadhani tuwe na *priority* ya kuonesha kwamba mabalozi wetu tuna-*identify*, kwa mfano, Balozi aliyepo Uchina au Japan au New York au wapi tunakupa kwamba ututafutie wawekezaji kwenye maeneo hayo, tuwe *specific* ili mtu asiamue tu yeye huyu anakuja kutengeneza tu *wine* hapa na nini, kumbe tuna vitu vingi ambavyo vingi-*create employment*, viwanda kama vya pamba, tuchakate pamba, tutengeneze nguo, tu-*add value* kwenye *products* zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *which means* Wizara ya Mambo ya Nje wakikaa na Wizara ya Viwanda na Kilimo wanaweza ku-*prioritize* zile *areas* ili wawape mabalozi kwamba hizi ndio *areas* ambazo tunaona mzipe kipaumbele wafanya mikakati ya ziada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wenzetu utakuta Wachina walikuwa nyuma sana, ni miaka kumi tu walitutangulia, lakini sasa hivi wanasaidia karibu Afrika nzima. Kwa nini, wao walilenga mwekezaji anayekuja wanampa *conditions* sisi tunataka uwekeze hapa, kama huwekezi hapa basi kwaheri. Halafu sasa sisi wewe unampa mtu, anaweka kakitu kadogo amechukua ardhi kubwa halafu *returns* zake hatuzioni.

Mheshimiwa Spika, *area* nyingine nakata kuzungumzia, sasa hivi tunataka ku-*promote* Kiswahili kuwa lugha ya Taifa na nchi nyingi za nje zimekubali zitumie lugha ya Kiswahili, lakini nakumbuka kuna chuo kimoja tu nafikiri ni Michigan, Mnigeria ndio anafundisha Kiswahili kule, wakati nafikiri tungekuwa na mipango mikakati kwamba ni sehemu zipi au vyuo vipi vinahitaji vya huko nje kufundishwa Kiswahili, tukaomba jinsi nchi yetu inavyoweza kutupia wale walimu wakapelekwa kule. Lakini hapo hapo na sisi kwa vile tunakwenda kwenye Kiswahili, unakuta lugha ya kingereza itatutupa nje. Sasa hivi lugha ya Kiingereza bado ni tata, je, tutakapoingia moja kwa moja Kiswahili itakuwaje.

Mheshimiwa Spika, zamani kulikuwa na wale *volunteers from* nchi kama za Marekeni, Uingereza na nakumbuka...

*(Hapa kengele illia)*

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Nafikiri kengele ya kwanza hiyo.

Nakumbuka Waingereza walikuwa na *retired officers* ambao ni walimu na walikuwa tayari wapelekwe nchi za nje kama Tanzania waje wasaidie kufundisha Kiingereza ambacho mahitaji yao wao walitakiwa nyumba tu wala sio malipo. Hebu tuwape mabalozi wetu kazi za kuweza ku-*identify* hizi *areas* kuona kwamba je, hatuwezi kupata walimu wa kutufundisha Kiingereza *properly*. Maana ukiangalia sasa hivi hata mtu akitoa *speech* hakuna wale wenzetu makabila watanisamehe ambao "r" anasema "*lailway*" hasa nitasema "*lailway*" ni kitu gani ni "*railway*" hiyo. Sasa unakuta mtoto wa kwanza anafundishwa kingereza na mtu ambaye kwao hakuna "r" au Kiingereza chenyewe huyo anayekifundisha naye ni mbabaishaji, watoto wetu watajifunza lugha gani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo unakuta kwamba tunakuwa tuna-*specialization* kwamba sasa Kiingereza iwe tuna-*specialize* kwa hiyo tunakijengea mikakati au Kifaransa

au Kichina tupate walimu wazuri wa kufundisha vizuri ambao watafundisha ile lugha kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, sisi nchi yetu bado tuna nafasi sana ya ku-*liaise* na mabalozi wetu tukapata *volunteers* kama hatutaweza kuajiri walimu hao ambao wakatusaidia na pia hata kupeleka walimu wetu nje wapate *exposure*. Unakuta mwalimu anafundisha Kiingereza hajawahi kumsikia muingereza mwenyewe akiongea, kwa hiyo unakuta hata anavyofundisha inakuwa ni aibu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Nje ni kioo chetu kwa nchi za nje, kwa hiyo ningeiomba Wizara mtusaidie sana kuonesha kwamba Tanzania ni nchi yenye utajiri mkubwa sana, lakini tumekwenda zaidi katika ombaomba, tuna-*feel proud* tukiona nchi fulani inatusaidia, inatukopesha. Tutoke huko, tuangalie kwamba namna gani tuangalie kanchi kadogo kama Indonesia. Indonesia hawana *resources* kabisa, *natural resources* lakini wamewekeza kwenye *skills* za watu wao kiasi kwamba wameweza kukuza uchumi wao kwa hali ya juu sana kuliko kutegemea mikopo au misaada. Misaada inatudumaza, misaada inatufanya kwamba kila tukikaa unasema wawekezaji au wahisani hawajatupa fedha, sasa matokeo yake nchi ambayo tuna utajiri mkubwa kama sisi Tanzania kwa nini tu-*rely* kwa *donors* kila wakati tunakuwa ombaomba. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka. Nilishamtaja Mheshimiwa Jerry Silaa na atafuatiwa na Mheshimiwa Kamishna Fakharia Shomar.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Balozi Libelata Rutageruka Mulamula kwa uteuzi wake wa kuwa Waziri wa Wizara hii, lakini na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nasser Mbarouk.



Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii vilevile kuwapongeza Watendaji Wakuu wa wizara, kaka yangu na rafiki yangu Balozi Joseph Edward Sokoine na Mheshimiwa Balozi Fatma Mohammed Rajabu kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Mambo ya Nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuteua wanadiplomasia wabobezi kwenye Wizara hii, lakini kwa kuzingatia si tu mgawanyiko wa Muungano wa nchi yetu lakini vilevile na jinsia kwenye teuzi zake. *(Makofi)*

Mimi naamini kama wachangiaji wengine kwamba ubobezi wa wana diplomasia hawa kwenye Wizara hii utaleta matokeo chanya kwenye utendaji wa kazi wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na kazi yetu sisi ni kuwaunga mkono, kuwatia moyo na kuendelea kuwasadia kuhimiza Serikali kutenga fedha za kutosha kama walivyoomba kwenye bajeti yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeisikiliza kwa makini hotuba ya Mheshimiwa Waziri na mimi niungane na wenzangu kupongeza kazi kubwa Wizara hii inayofanya kwenye eneo la *economic diplomacy*, wamefanya kazi kubwa, miradi mingi inatekelezwa na Wizara hii inaratibu na yapo mambo mengi baadhi ya Wabunge walioanza kuchangia wametoa wito, namie nitoe wito kwa Wizara hii kuongeza nguvu kwa kuisemea na kuitangaza nchi yetu. Na mimi naamini kama Serikali itachukua ushauri wa Mheshimiwa Mbunge Balozi Pindi Hazara Chana na kufungua Balozi nyingi zaidi, lakini si tu kufungua Balozi na kuziweka *strategic*, umetolewa mfano mzuri sana hapa, leo watanzania wengi wanakwenda China kufanya biashara, lakini ukimuuliza mtanzania wa kawaida kama amewahi kufika ubalozini Beijing hata hafahamu ni eneo gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania wangi wanafanya biashara kweye Miji ya Guangzhou, Shenzhen, Yuan na hata kama tutashindwa kupata Balozi mdogo basi hata ukipata

*Honorary Consular* maslahi ya Watanzania kibiashara yatalindwa kwenye maeneo yale. *(makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba Wizara imefanya kazi kubwa kwenye utalii, lakini iongeze kazi kubwa ya kutangaza utalii kwenye balozi zetu kwa sababu utalii ni moja ya kati ya sekta ambazo inategemewa sana kwenye uchumi wetu kutuingizia pato la kigeni.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu ningeomba kuchangia kwenye eneo la itifaki, ukurasa wa 87 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Na ningemuomba Waziri pamoja na ubobezi wao wa diplomasia nimrudishe kwenye sheria, kwenye Katiba ambayo ndio sheria mama ya nchi yetu. Nimuombe Waziri nimrejeshe kwenye Ibara ya 4(2) ya Katiba yetu ambayo inaeleza utawala wa nchi yetu ulivyogawanyika katika mihimili yake mitatu; kwa maana ya Serikali, Bunge na Mahakama. *(Makofi)*

Lakini nimrudishe kwenye Ibara ya 62 ya Katiba yetu ambayo inalitaja Bunge na kuelezea kazi na mamlaka ya Bunge letu. Lakini Ibara ya 66 inayowaeleza Waheshimiwa Wabunge, Ibara ya 84 inayomwelezea Spika wa Bunge letu hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini na Ibara ya 85 inayomwelezea Naibu Spika na Ibara ya 105 inayoelezea Baraza la Wawakilishi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini naeleza ibara hizi? Kumekuwa na dhana na wenzetu wanaosimama itifaki ya shughuli zetu za kitaifa. Unakwenda kwenye shughuli ambayo Mheshimiwa Spika amehudhuria, unafanyika utambulisho Mheshimiwa Spika hatambulishwi. Si tu kutokumtambulisha ni fedheha kwake yeye binafsi, maana inawezekana Spika wetu Job Ndugai wote mnafahamu ni mtu rahim na mtu ambaye hana makuu. Lakini usipomtambulisha Spika maana yake umeamua wewe mwenyewe kuandika Katiba yako mpya na kuondoa Bunge ambalo linawakiwalisha wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini haiishii kwa Spika, zipo shughuli nyingi wanakwenda Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Wabunge wakienda vilevile tusingalie wao kwa majina yao, wanakwenda kuwawakilisha wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye shughuli zile. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ziko shughuli anakwenda Mheshimiwa Naibu Spika, ziko shughuli wanakwenda Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge. Ziko baadhi ya shughuli ambazo uratibu wa itifaki una-*fail* na Waheshimiwa Wabunge wanakuwa kama ma-*gate crasher* kwenye shughuli zile. Kuingia tabu mpaka watu waulizane wee mtu asimame pale mlangoni kila anayepita anakushangaa, bwana vipi! Tupo tumekuja kwenye shughuli. Kila anayepita anakuonea imani, wamekuona? Enhee wameniona wanashughulikia. Mpaka itokee hisani ama kiongozi wa itifaki afike aseme basi andika jina lako uingie. Lakini ndani ya shughuli ile utambulisho utatambulishwa sisemi kwa sababu Babu Tale hapa hayupo mpaka wasanii watatambulishwa, Mheshimiwa Mbunge hajatambulishwa.

Sasa hatusemi haya kwa maana tu ya kusema labda Wabunge wanataka makuu, hapana. Nayasema haya kwa kuwa Katiba inatambua nafasi hizi. Shughuli inapoandaliwa, viongozi wanapoalikwa, wanapofika wapate heshima na stahiki inayostahili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nikiri Mheshimiwa Waziri ameliona, Mheshimiwa Naibu Waziri ameliona na Mheshimiwa katibu Mkuu ameanza kulifanyia kazi, ni Mabalazi wazuri wanafanya kazi vizuri sana. Nalisema kuweka kumbukumbu sahihi kwa kuwa nawaamini sana viongozi hawa niliowapongeza mwanzo wa mchango wangu. Kulikuwa na dhana kwamba shughuli hii inaandaliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, shughuli hii inaandaliwa na *TPDC*, shughuli hii inaandaliwa na *TANESCO*, ukisoma vizuri utaratibu wa shughuli za Kitaifa na za Kimataifa huwezo ukaondoa majukumu ya Idara ya Itifaki ya Wizara ya Mambo ya Nje katika kusimamia itifaki ya shughuli zile. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimuombe Waziri bahati nzuri umekuja na mzee na nilidhani atatoka baada ya kutambulishwa, lakini amebaki. Kwa heshima yake, twende kwa utaratibu wa kushauri, naamini ukija kuhitimisha hotuba yako utahitimisha vizuri na kunyoosha itifaki ya shughuli zetu.

Mheshimiwa Spika, na nikuambie kwa dhati ya moyo wangu, ikitokea tena Spika wangu wa Bunge hili aidha kwa makusudi ama kwa bahati mbaya kwenye shughuli yoyote hakutambulishwa au hakupewa itifaki inayostahili Mheshimiwa Waziri utakutana na jambo linaitwa Azimio la Bunge na wala usitafute mchawi, mimi nimeamua kununua hiyo kesi. Lakini sina shaka na wewe, sina shaka na Naibu Waziri wako na watendaji wako, naamini mtajipanga vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yako hayo na mengine madogo madogo tu, hata Rais wetu anaenda kwenye shughuli haijulikani gari linasimama wapi, anashuka watu wamejipanga upande huu anashukia upande mwingine. Ni majukumu yenu, chukueni *role* yenu ya itifaki na msikubali mtu yeyote akachukua majukumu ambayo sio ya kwake kwa kuwa majukumu ya itifaki ni majukumu yenu chini ya Wizara yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naamini haya yakifanyiwa kazi na yale ambayo wachangiaji wenzangu wamechangia, Wizara hii ikawezeshwa kwa fedha sit u kutengewa fedha lakini kuhakikisha fedha zinapelekwa hasa katika uwekezaji wa majengo ya ubalozi kwenye nchi ambazo tuna uwakilishi na kufungua Balozi nyingine za ziada. Wizara hii ikija hapa mwakani itakuja na mafanikio makubwa kuliko ilivyofanya hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jerry Silaa. Mheshimiwa Fakharia Shomar, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohammed Soud Jumah.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza sina budi kukushuru wewe kwa kunipatia hii nafasi, pia na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wao wote wa Bara na Zanzibar kwa kazi nzuri wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nataka kuzungumzia hii diplomasia ya uchumi. Diplomasia ya uchumi ni wazo zuri wallilotoa Wizara ya Mambo ya Nje ili kuisaidia nchi kukua kiuchumi. Lakini lengo walilolifanya bado halijafikia. Kwa sabababu lengo lilikuwa kutafuta masoko, masoko bado kitendawili, hamna masoko na hayo masoko, ilikuwa sisi kama Watanzania, tuweze kusarifu bidhaa zetu ziweze kwenda kuuzwa nje, ina maana bidhaa ziwe *value added* na hayo hatujayaweza kwa sababu hatuna viwanda. Sasa utakuta bado sera ya diplomasia haijakamata kasi.

Vilevile hii sera ilikuwa ihamasishe watalii ambao wana uwezo wa kuja Tanzania. Tanzania ni nchi nzuri, Tanzania Bara kuna Mlima Kilimanjaro, mbuga za wanyama nzuri. Ukija Zanzibar kuna fukwe mwanana, kuna bustani ndani ya bahari ambavyo hivyo ni vitu vya maajabu. Lakini kwa sababu hii sera bado haijafanya kazi kikamilifu haya yote hayajaweza kufanyiwa au kutendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ukiangalia ilikuwa Wizara itoe sera mpya ya mambo ya nchi za nje na ilikuwa hii Juni, 2021 wawe nayo mkononi. Haijapatikana hadi leo na hatukui itapatikana lini. Sasa hii sera mpya ya mambo ya nje ingeshirikiana na diplomasia ya uchumi ina maana tayari tungekuwa tumejua nini tunachokifanya kwa sababu sera ilikuwa idhibiti *diasporas* wafanyiwe kanzidata ili tujue kila nchi tuna nani na nani wako vipi, lakini tumeshindwa. Balozi zetu kuwadhibiti wanashindwa na ilikuwa hawa *diasporas* ambao ilikuwa wao washirikiane na Mabalozzi wetu, wawe muda mwingi kwa mazingira ya raha na shida wanakua nazo, lakini halitendeki.

Mheshimiwa Spika, utakuta tunawafanyakazi raia wa Tanzania nchi za nje wanapata manyanyaso,

wanaharibikiwa, lakini wanashindwa kwenda ubalozi kutokana na sera hakuna inayowafanya wafike ofisi zetu za ubalozi. Sasa hili itabidi wazidi kuliangalia kwa mapana ili waweze kujua kwamba hawa vijana wetu wa Tanzania waliokuwepo nje ya Tanzania nao pia wanataka kusaidiwa. Tazama vijana wetu wale wanaofanya kazi majumbani nchi za nje wanavyonyanyaswa. Mtu anafika ananyang'anywa *passport* yake, mtu anafika halipwi, aende wapi? Hana pa kwenda, lakini kama hiyo sera mtakapokuwa mmeifanya na mkampa nguvu, atakuwa anakwenda kifua mbele hana matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakuja uhaba wa wafanyakazi; Wizara ina uhaba wa wafanyakazi kutoka Makao Makuu, Kurugenzi ya Zanzibar na Balozi zetu. Hata wewe mwenyewe umelizungumza hilo ingawa unalifanyia kazi. Lakini kwa nini mkawa na uhaba wa wafanyakazi ndiyo unaosababisha majukumu yenu yote mshindwe kuyatekeleza kwa sababu mna *desk* zina majukumu, lakini hazina wafanyakazi. Makaimu ndiyo mmekuwa nao wengi, sasa ina maana hayo mnayoyapanga yatakuwa? Hayawezi kuwa, tatizo lenu ni uhaba wa wafanyakazi, uhaba wa vitendeakazi, hivi sasa hivi magari hakuna ya kutosha na kazi zenu zinahitaji gari, maana mnafuatilia.

Mheshimiwa Spika, ukija Zanzibar hawana gari, ukija Bara Makao Makuu hakuna gari, Balozi zetu hazina gari, sasa hilo pia tatizo. Najua kwa bajeti hii ndiyo mmeshachelewa, hakuna kitakacho. Lakini bajeti ya mwakani mkija haya angalau mawili/matatu mtuletee tuyapitishie angalau tuone yanafanya kazi na hayo ndiyo yatakayowasaidia na ninyi wakati mkishakuwa na sera mpya, ita-*guide* mambo yenu yote na mtajua ninyi mnafanya na mtafanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakuja na suala dogo la mwisho; najua mimi nikizungumzia Zanzibar na Muungano tu, tuna miaka 57, lazima nilizungumze na nyumbani. Zanzibar mnayo ofisi, lakini ile sio ofisi ni nyumba, ile imekaa kama *rest house*. Lakini pale kwenye ofisi yenu mliyosema ofisi, nafasi mnayo ya kutosha. Pale mngejenga kiofisi chenu ambapo mtaa

mliokuweko mzuri Maisara, nyumba kuna ofisi za SMZ nzuri, ubavuni nzuri, pembeni nzuri na ninyi mngeteremsha kiofisi chenu pale na nafasi mnayo. Mkawa na *rest house* ambayo mmeifanya ofisi.

Siku moja mimi nilialikwa kwenye mkutano pale Mambo ya Nje, nimeenda sijui hata niingilie mlango gani. Nimeingia pale nimejikuta niko juu. Mkutano kumbe, daah naambiwa jamani mkutano naambiwa uko chini. Nipenye wapi nitoke huko chini kwenye mkutano kwa sababu ile nyumba mtu alijenga mwenyewe anavyotaka, haikujengwa kiofisi. Sasa inabidi hata utakapokuwa unakwenda kwa shughuli za Kiserikali, inabidi uhangaikwe. Nafasi tunayo na tutaweza. Ninajua Waziri akiwa mwanamke anakuwa msikivu na ninajua hili japo ofisi ndogo pale kaweke, unaweka alama alikaa Waziri mwanamke kafanya kitu fulani, hiki hapa kinaonekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nafikiri kwa hayo machache naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Ruksa.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kwa sababu hotuba inayosomwa hapa randama haijaonekana kwenye hiki kitabu. Randama ya Wizara ya Mambo ya Nje. Taarifa iliyoko hapa inasomeka Taarifa ya Utekelezaji ya Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021 na Makadirio na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa 2021/2022 iliyowasilishwa mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

**SPIKA:** Tutafafanua muda si mrefu. Mheshimiwa Mohammed Soud Jumah atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Fiyao.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataalah* kwa kutujaalia na kutupa afya njema na kuendelea na Bunge sasa hivi karibu mwezi wa pili.

Lakini pia nikushukuru wewe kwa kuweza kunipa hii nafasi kuweza kutoa mchango wangu muhimu katika Wizara hii muhimu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Hali kadhalika niwashukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri Sheikh Mbarouk pamoja na watendaji wa Wizara hii kwa kweli wamekuwa wakifanya kazi nzuri na tumeanza kuona mabadiliko chanya katika maeneo mengi. Kwa mfano, kule Zanzibar hivi sasa hivi tayari tuna mchoro wa bandari na nafikiria kwamba Wizara yetu hii itafanya hima kuweza kuhakikisha kwamba utekelezaji wa ujengaji wa bandari unafanyika haraka ili yale matokeo chanya yanayokusudiwa kutokana na bandari zile basi yaweze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia mchango wangu katika maeneo mawili makubwa; la kwanza ambalo Mheshimiwa Fakharia amelianza ni kuhusu ofisi yetu ya Zanzibar. Kwa kweli Ofisi ya Zanzibar kama alivyosema Mheshimiwa Fakharia, sio ofisi kwa kweli na ni nyumba ambayo ni ya muda mrefu sijui kama tulijenga au tuliamia tu lakini haina hadhi ya kuwa ni Ofisi ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Ofisi ile imechoka na hivi sasa tuna taarifa kwamba inafanyiwa marekebisho. Sio kujengwa mpya, inafanyiwa marekebisho.

Kwa hiyo, ningewaomba tu wenzetu wa Wizara kwa kweli aidha, sahihi kama tunafanya marekebisho au matengenezo haya ya dharura basi tuendeleo na matengenezo ili tuweze angalau kupata pa kuanzia, lakini tuwe na utaratibu wa muda mrefu wa kuangalia uwezekano wa kujenga ofisi mpya aidha pale kwa sababu pale sasa hivi pameshakuwa kama ni *museum*, ni eneo la mji lile sasa hivi. Kwa hiyo, sio mbaya tukatafuta eneo nje ya mji, kiwanja kizuri tukaenda tukajenga ofisi kubwa ambayo itakuwa na hadhi ya Ofisi ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje.



Mheshimiwa Spika, kama tunavyojua kwamba ile ofisi ndiyo sehemu kubwa ambayo mabalozi wakienda Zanzibar ile ndiyo sehemu yao kubwa ya kufikia. Lakini pia hata viongozi mbalimbali wenye hadhi ya Kimataifa ile ndiyo ndiyo *center* yao ya kuweza kufikia, lakini sasa hivi viongozi hawa wengi wanafikia hotelini. Kwa hiyo, ningepomba Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri Sheikh Mbarouk tukajitahidi katika kipindi chenu hiki *Inshallah* tukaweza kushuhudia kwamba angalau katika kipindi hiki cha miaka mitano tunapata eneo na miaka mitano inayokuja tunajiandaa kwa kujenga ofisi yenye hadhi ya kimataifa ambayo itakuwa ina-*represent* Umoja wa Mataifa kule kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala zima la uratibu na taratibu za ofisi zetu za kikanda na za kimataifa. Kama tunavyojua kwamba kwamba Zanzibar ni kisiwa na inategemea sana ndugu zao wa upande wa pili wa Muungano kuweza kuwawakilisha katika mambo ya kikanda na ya kimataifa. Lakini kidogo kuna changamoto mbili kubwa ambazo zinakabili katika maeneo haya; changamoto ya kwanza ni uwezo wa taasisi za Zanzibar kuweza ku-*access* fursa za mbalimbali zinazopatikana katika maeneo ya kikanda na maeneo ya kimataifa.

**SPIKA:** Hebu rudia hapo hujaeleweka.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, uwezo au *capacity* ya Taasisi...

**SPIKA:** Tangu ulipoanzia kwamba Zanzibar...

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, naam!

**SPIKA:** Rudia kidogo hapo ulipoanzia hoja yako.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, nasema kwamba changamoto mbili ambazo zinakabili ya kwanza ni uwezo wa taasisi za Zanzibar kuweza ku-*access* fursa zinazopatikana katika maeneo ya kikanda na maeneo

ya kimataifa. Nitatoa mfano, ya kwanza kama tunavyojua kwamba kuna mifuko ya fedha mbalimbali, lakini hali kadhalika kuna balozi zetu hizi kama mfano ukienda Ubalozi wa Japan kuna Shirika la Maendeleo la *JICA*, ukienda Shirika kama *USAID*, kuna mashirika mbalimbali ya kikanda, kuna *ADB* lakini ningependa kuwashauri wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje wakatusaidia kutujengea uwezo zile taasisi za Zanzibar kuweza kutafuta hizi fursa kwa sababu sasa hivi kuna malalamiko mengi, lakini ukiangalia wakati mwingine changamoto vilevile sio kama iko katika upande wa Wizara peke yenu, lakini pia wale wenzetu wa Zanzibar bado uwezo wao sio mzuri sana kuweza ku-*access* hizi fursa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ni urasimu au wenzetu wa upande wa pili kwa sababu kama tunavyojua kwamba Zanzibar hata kama ni jambo sio la Muungano kwa mfano jana mwenzangu Mheshimiwa Ravia alizungumzia hapa suala la michezo. Suala la michezo sio suala la Muungano lakini tukitoka nje ya nchi ni lazima tuweze kuungana. (*Makofi*)

Sasa tukienda kwenye masuala ya *CAF*, *FIFA* lazima tuwe tuko pamoja. Sasa wenzetu wa upande wa pili wa Muungano kama ni Wizara hizi zote lazima washike mkono wenzetu wa Zanzibar vizuri, kwa sababu mimi mwenyewe nimeshawaji kupata changamoto kipindi fulani. Kulikuwa kuna mradi ambao nilikuwa nauratibu Zanzibar kule na nikaomba mradi mimi mwenyewe ambapo ilitangazwa *call for proposal*, nikaomba na ile *call* ilikuwa *call* ambayo ni *competitive* ya kupambana mwenyewe. Tukaomba ile pesa na tukawa tumeshapata, lakini wakati tunatafuta zile fedha ilikuwa lazima kwa sababu pesa tumezipata *through ADB* lazima Waziri wa Fedha wa Muungano ndiyo asaini ule mkataba. Ilichukua miezi sita nahangaika kutafuta *signature* ya Waziri wa Fedha, mpaka tulipomtumia Waziri wa Fedha wa Zanzibar pia naye alishindwa kuweza ku-*fast track* kuweza kupata *signature* ya Waziri wa Fedha haraka. (*Makofi*)

Sasa wakati mwingine changamoto zinakuja kwa sekta za Bara, Wizara za Bara hizi zinakuwa zinashindwa

kuzishika mkono zile taasisi za upande wa Zanzibar. Kwa hiyo, ningependa tujitahidi fursa kuweza kusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kumaliza kwa upande wa mikutano ya kikanda hasa ya Afrika Mashariki. Kuna mikutano ambayo tunashiriki sisi kwa upande wa Tanzania, lakini kuna wenzetu wa Tanzania Visiwani inabidi tuwaalike tuwe nao pamoja lakini taarifa hizi zinakwenda Zanzibar *late*, inawezekana mkutano uko kesho taarifa zinakwenda leo.

Pia inawezekana mkutano ule unafanyika *either* Arusha, Kigali, Entebbe na kadhalika katika Afrika Mashariki au *SADC*. Lakini taarifa zinakuja *late*, Wazanzibari wanashindwa kujitandaa mapema na ukienda kwenye mikutano wanakuwa ni wasikilizaji tu hawana mchango wowote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kuna tatizo la kwamba kwa sababu hakuna maandalizi inawezekana taarifa zile zikienda hata bajeti kule hakuna ya kuweza kumpeleka mwakilishi. Pia kuna mikutano ya maandalizi ambayo aidha inafanyika Dodoma au Dar es Salaam, mikutano ile mara nyingi Wazanzibari hawahudhuria kwa sababu hawapati taarifa mapema na hata wakija kwa sababu inaonekana ni gharama matokeo yake inakuwa ni *Tanzania Mainland* peke yao ndiyo wanahudhuria kwenye vile vikao na inakuwa havina tija kwa upande wa Zanzibar. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ningependa tu Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na Wizara kwa ujumla wakajitahidi kuondoa urasimu vile vile kusaidia kujenga uwezo Zanzibar na kuwashika mkono ili waweze kuweza kupata hizi fursa au kuzi-*access* fursa za kikanda na za kimataifa. Ahsante nashukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mohammed Soud Jumah. Nilikutaja Mheshimiwa Stella Fiyao utafuatiwa na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa na Mheshimiwa Grace Tendega ajiandae.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi na mimi niopate kuchangia katika Wizara ya Mambo ya Nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitaanza kuzungumzia suala la ajira; wako wafanyakazi wengi ambao wanatoka nje ya nchi na wanakuja kuajiriwa katika nchi yetu ya Tanzania, lakini pamoja na kwamba wanaajiriwa, wanaajiriwa kwa kigezo cha kwamba ni wataalam, lakini pamoja na kuajiriwa wamekuwa wakilipwa fedha nyingi sana ambazo fedha hizo wakati mwingine wamelipwa fedha dola za Kimarekani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo lakini bado katika nchi yetu tumekuwa na wataalamu ambao wakati mwingine wanazidi vigezo vya hao wageni ambao wamekuja kupata ajira katika nchi yetu, lakini wafanyakazi hao wengi wamekuja kwa namna ya kupitia makampuni mbalimbali ambayo yamekuwa yakipata *tender* katika nchi yetu, hususan katika masuala ya barabara, uchimbaji wa madini, katika masuala ya minara, na kadhalika. Wamekuwa wakipata *tender* hizo kupitia hao wataalam ambao wamekuwa wakija kupitia hizo kampuni ambazo zimekuwa zikija kupata *tender* katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote kumekuwa na changamoto kubwa na kumekuwa na utofauti mkubwa wa Watanzania wanapokwenda kuomba ajira ama kupata fursa nje ya nchi. Watanzania wengi wanapokuwa wakienda kupata fursa nje ya nchi za kupata ajira wamekuwa wakiambulia kupata mambo yasiyoridhisha kama vile kufanya usafi, kulinda, kufanya kazi za ndani, changamoto nyingi pia wamekuwa wakikumbana nazo ikiwa ni pamoja na kuteswa na kudhalilishwa wakati mwingine utu wao kwa sababu tu ni Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hiyo changamoto, naomba niiombe Serikali, ni wakati muafaka sasa Serikali kupitia balozi zetu kwenye nchi mbalimbali duniani kuhakikisha wanafanya njia mbalimbali kuhakikisha Watanzania wetu wanapata fursa stahiki wanapokuwa

wamekwenda kuomba kazi huko nje ya nchi. Kinyume na hapo balozi zetu zisipofanya hivyo zitakuwa hazijatutendea haki kwa sababu sisi sote tunashuhudia namna ambavyo Watanzania wamekuwa wakati mwingine wakipitia mazingira magumu sana wanapokuwa huko nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tuombe Serikali sasa itumie fursa hii kupitia mabalozi wetu walioko nje ya nchi kuhakikisha wanazitafuta fursa maana yake pia ni sehemu ya wajibu wao, watafute fursa za ajira kwa ajili ya Watanzania wetu kwa sababu tumeona wakati mwingine hao wageni wanapokuja kupata ajira katika nchi zetu wamekuwa wakipewa ushirikiano wa kutosha na Serikali zao huko nje, jambo ambalo limesababisha wamefanya kazi kwa ufasaha na wamefanya kazi kwa kuhakikisha wanatimiza wajibu wao kisawasawa. Ni wakati sasa na sisi tuombe balozi zetu zitusaide huko nje kuhakikisha zinatafuta fursa stahiki kwa Watanzania ili waweze kupata ajira za kutosha huko nje na mwisho wa siku pia warudi kufanya maendeleo katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote naomba nizungumzie suala la uwajibikaji wa mabalozi wanapokuwa huko nje. Ni wazi kabisa kwamba uwajibikaji wa mabalozi haujawa wazi. Uwajibikaji wa mabalozi wetu huko nje haujawa zai kabisa na tuseme wazi ili kuhakikisha kuwa mabalozi wetu wanakwenda kusimamia na kukuza diplomasia ya uchumi tunatakiwa tuweke mikakati, lakini pia tunatakiwa tufanye mabadiliko ya mfumo wa uwajibikaji wao, lakini mwisho wa siku mabalozi hawa waweze kuwajibika kwa hili Bunge. Wakiwajibika kwa hili Bunge ninaamini watafanya kazi kiufasaha na uwajibikaji wao utakuwa wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunahitaji hawa mabalozi wawe wanawasilisha mpango wao wa kazi kila mwaka. Wawasilishe mpango wao wa kazi kila mwaka katika Bunge hili kupitia Kamati ya Mambo ya Nje, wakifanya hivyo inaweza kusaidia wao kuwajibika ipasavyo wanapokuwa huko nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninaamini kwamba ikiwa taarifa zao za uwajibikaji zitaletwa katika hili Bunge, pia Bunge tupewe nafasi ya kutoa mapendekezo kwa nafasi zao za teuzi. Tunapoonna wamepwaya katika suala zima la uwajibikaji Bunge tuna uwezo wa kutoa mapendekezo ni nini wafanye. Ninaamini tukifanya hivyo tunaweza tukasaidia uwajibikaji wa mabalozi wetu wanapokuwa huko nje.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Kuna Taarifa Mheshimiwa Stella Fiyao.

### T A A R I F A

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kumpa Taarifa Mheshimiwa Stella kwamba kwa mujibu wa utaratibu wa miongozo, taratibu, kanuni, sheria na miongozo mbalimbali zipo taratibu za kila makundi kuwa na sehemu ya uwajibikaji wake. Serikali itawajibika kwa utaratibu wake kwa maana ya watumishi wanajua jinsi ya kuwajibika, lakini vilevile tunayo Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Kamati hii imekuwa ikipata taarifa mbalimbali za uwajibikaji wa mabalozi, ikipata taarifa mbalimbali za masuala yote ambayo yanahusu Wizara ya Mambo ya Nje. Kwa hiyo, haipo na wala haitakuja kutokea Bunge kuja kuanza kuwahoji mabalozi kuhusu uwajibikaji wao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao unapewa hiyo Taarifa.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza huo nilikuwa natoa ushauri wangu. Kwa ushauri una uwezo wa kupokelewa ama kutokupokelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini tukifanya hivyo hii itaondoa uzembe katika utendaji, pia itasababisha mabalozi kuwajibika ipasavyo katika majukumu yao wanapokuwa nje ya nchi na itaondoa dhana iliyojengeka muda mrefu kwamba cheo cha ubalozi ni cheo cha starehe.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Stella Fiyao. Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Tendega na Mheshimiwa Yahya Mhata ajiandae.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa fursa hii niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara yetu hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Naomba nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kufanya teuzi nzuri za mabalozi hawa wawili, Mheshimiwa Liberata Mulamula kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk kuwa Naibu wake.

Mheshimiwa Spika, mimi naimani sana na mabalozi hawa, kubwa, kwani nawafahamu. Na ninamfahamu Mama Mulamula kuwa yeye ni mbobezi katika eneo hili la diplomasia. Na kwa muda mfupi tu ametuonesha kwa ku-*stimulate* diplomasia ya uchumi kati yetu na nchi zetu za Afrika Mashariki kwa kumshauri vyema Mheshimiwa Rais na kutembelea nchi hizi na kufanya mikutano ya kibiashara na hasa Kenya na kufanya kufungua biashara ya mazao baina ya nchi yetu ya Tanzania na Kenya.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kuishauri Serikali tuendeleze na kukazania sana diplomasia hii ya uchumi kwani wote tunafahamu nchi ikiwa na mahusiano mema ya kiuchumi naamini kabisa tutaweza kuuza biashara na bidhaa zetu nje kwa wingi na tukiuzi nje kwa wingi tutapata fedha za kigeni, lakini pia tuta-*stabilize* uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hivyo nilikuwa napenda sana kuishauri Wizara ya Fedha iangalie diplomasia ya uchumi nayo ina gharama yake, mahusiano yana gharama yake kwa hiyo, tuangalie sana kupeleka fedha kwa wakati; kama ni *OC* tusipeleke *OC* za mishahara tu, tupeleke *OC* pia za kugharamia mahusiano haya ya diplomasia ya uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwani tunaweza tukalaumu wakati mwingine tunaweza tukafika mahali tukalaumu ma-*diplomat* wetu waliokuwepo nje kwamba, wanachelewa kutekeleza

majukumu yao ya diplomasia ya uchumi, sababu tu wanaweza wakawa wanakosa hata gharama ya kugharamia ile *round coffee table* ya kuweza kuwaita na kuwashawishi *potential investors* kwa kukaa nao na kunywa nao kahawa na kuwaelezea hali halisi ya kwetu na kushawishi waweze kufika huku. Kwa hiyo, ni muhimu sana Wizara ya Fedha kutenga na kusambaza fedha zile zinazotakiwa kwa ajili ya mabalozi wetu nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini lingine napenda sana kuishukuru Wizara kwa kutekeleza ushauri wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ya kuona kuna umuhimu wa kuongeza watumishi katika balozi zetu hasa wanaohusiana na wenye utaalum wa kufanya kazi hii ya diplomasia ya uchumi. Tunawapongeza sana kwanza wameshatekeleza jukumu hilo na sasa wako katika uratibu nadhani wa kupeleka hawa ma-*diplomat* wetu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naipongeza Wizara kwa kutambua na kushirikiana nao mabalozi wetu wastaafu, tumewaona leo wamekuja hapa. Mabalozi wastaafu hawa ni *encyclopedia* ya Wizara hii ya Mambo ya Nje na Waziri umedhihirisha mahusiano mema ya diplomasia kuwakumbuka na kuwatambua mabalozi hawa na leo kuwaleta hapa na kushirikiana nao. Mabalozi hawa ndio walifanya kazi kubwa sana katika nchi hii kipindi cha nyuma wakati wakiwa kazini kwa hiyo, ni vema wana uzoefu mkubwa sana. Wizara iendeele kuwatumia mabalozi hawa ili kutoa ushauri wao na *experience* yao katika Wizara hii na mahusiano ya kimataifa, lakini pia katika dilpomasia ya uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa na hayo tu machache, naomba nikushukuru na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa. Mheshimiwa Grace Tendega utafuatiwa na



Mheshimiwa Yahya Mhata na Mheshimiwa Neema Lugangira ajiandae.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nianze kwa kuchangia katika Sera ya Mambo ya Nje na Diplomasia ya Kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kuna mwanadiplomasia mahiri sana na alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa 38 wa Australia, Julie Bishop ambaye katika moja ya hotuba zake alizungumzia masuala haya; naomba niyanukuu kidogo na alisema; wakati diplomasia ya kizamani ililenga amani diplomasia ya uchumi inalenga ustawi kwa kukuza ustawi wa maisha ya watu, diplomasia ya kiuchumi inakuwa ndio msingi wa kudumisha amani, ikitekelezwa vizuri diplomasia ya kiuchumi ni lazima ilete matokeo ya kukua kwa uchumi, kuongezeka kwa ajira na kufunguka kwa vyanzo vipya vya uwekezaji wa ndani na wa kimataifa kuchochea ubora wa maisha ya watu na nchi husika. Kinyume cha matokeo hayo diplomasia ya kiuchumi itakuwa ni neno tu ambalo tunaweza tukaiga yaani *copy and paste*.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nazungumza hivi; diplomasia ya uchumi itasaidia sana nchi yetu kuweza kutoka hapa tulipo. Itasaidia sana kuwa na mafanikio makubwa katika nchi yetu kwa sababu tunaposema diplomasia tunahitaji kuwa na wataalamu wazuri, tunahitaji mahitaji ya viongozi wenye maono, tunahitaji watu wenye ushawishi, tunahitaji mikakati madhubuti. Bila kuwa na hivi vitu tutapata changamoto kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kupata hii nafasi, najua wewe ni mbobezi na ni mzoefu. Tunakuomba uweze kuifanyia kazi tuweze kuipata hii sera na tuweze kufanyia yale ambayo Watanzania wanahitaji kuyaona katika kutafuta masuala

mengi ambayo wameyasema wengine, napenda nisiyarudie. Ajira inatakiwa ipatikane kwa wenzetu ambao ni mabalozi wako kule waangalie fursa zilizopo ni zipi ili waweze kuzileta. Kwa hiyo, tunataka *visionary leadership, strong negotiators*, tunataka *lobbyists* na tunataka *smart strategies* ambazo zitasaidia nchi yetu iweze kutambulika na kupata yale ambayo mengi ambayo tunaweza kuyafanyia kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa twende kwenye hadhi za balozi zetu, wamezungumza kuanzia Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje. Hadhi za balozi zetu zinasikitisha, balozi zetu ziko hohehahe, hatupeleki pesa za maendeleo, ndio mwanzo wa haya yote ambayo unayaona. (Makofi)

Kwa hiyo, tunaishauri Serikali, tunamuona Waziri wa Fedha yupo apeleke pesa ili balozi zetu ziendane basi angalau hata na balozi za nchi za Afrika ambazo zipo maeneo hayo, tunatia aibu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, yaani balozi zetu unaangalia zina majengo yanavuja, balozi zetu zimechoka huko, majengo ya balozi zetu yanatia uchungu. Kwa hiyo, naomba nisiyaelezee sana haya, kuna maeneo mengi viongozi wetu wakuu walikwenda wakaahidi, lakini bado mpaka leo hatujajenga. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la uraia pacha; mimi nazungumza kwamba uraia pacha ni fursa kimkakati. Tunaangalia nchi za wenzetu wameweza kufanya hivyo, watu wanapata uraia pacha. Tuchukulie mfano tuna wachezaji wanacheza nchi za wenzetu, kuna mchezaji anaitwa Rashford yuko kule anacheza *Manchester United*, yule inasemekana wazazi wake ni Wazanzibari, sasa angekuwa na uraia pacha angeweza kurudi akachezea nchi yetu na wengine wengi ambao wako huko wakipata hii fursa kwetu inasaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wenzetu Wakenya *diaspora* yao imechangia dola za Kimarekani bilioni 2.7 kwa mwaka 2018

na ambayo ni asilimia tatu ya pato la Taifa ambayo imetokana na uraia huo pacha. Kwa hiyo, sisi tukiweza tusikae kama kisiwa, tuwaangalie wenzetu wanafanya nini na sisi tuangalie pale ambapo italeta tija na sisi tuifanyie kazi hivyo kwa sababu hii tunajikosesha wenyewe mapato kwa nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kuna nchi moja inaitwa Estonia. Hii nchi wana uraia wa kidijitali, kwa hiyo, hapo ulipo unaweza ukapata uraia, unaweza kuomba una kampuni uweze kuwekeza kule na wanaendesha nchi inakwenda, wanakwenda kidijitali, lakini sisi kuna vitu ambavyo tunavifinya. Kwa hiyo, kama kuna mambo ambayo tunataka tuyaweke sawa basi Mheshimiwa Waziri aangalie ni mambo gani ambayo tuyaweke sawa, lakini tuweze kuwafikia wenzetu ili na sisi tuweze kusonga mbele tunyanyue uchumi wa nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hatutumii vizuri *diaspora* zetu. Kwa nini nasema hivi; balozi zetu zikiangalia Watanzania walioko katika nchi ile, tuwe na kanzidata, tujue kabisa kuna wanafunzi wangapi na wanasoma masomo gani na yatasaidiaje kwa nchi yetu? Wapi wanafanya kazi gani? Kama ni watu wa kufanya kazi za majumbani tufahamu, itambulike kabisa na hizi ni fursa wafanyabiashara wangapi? Wanafanya biashara zipi?

Mheshimiwa Spika, sasa tukitambua hivyo mabalozi hawa watatusaidia kuona fursa ziko wapi. Tuna watu wako kule wanasoma nini? Wanafanya nini? Kwa hiyo, sisi kama nchi itatusaidia kutambua kwamba tuwekeze wapi kwa zaidi kwa sababu tunakuwa tuna *data* kamili ya watu ambao wako nje ya nchi ambao tunaweza kuwa-*supervise* na kuona nini ambacho wanaweza wakakifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nije kwa mabalozi; mabalozi wana wajibu mkubwa sana wa kutafuta fursa za ajira kwa nchi yetu. Fursa za ajira watatutafutia mabalozi wetu, kama kweli tutawachukua wale ambao wamefuzu, wamesoma diplomasia, wanaelewa ni kitu gani wafanye katika nchi hizo.

Kwa hiyo, wanapokuwa pale wanaweza wakazona fursa, amesema Mheshimiwa Balozi Pindi Chana hapa. Watu tuna mazao mengi yako kule tunakosa masoko, lakini balozi ambayo itaona kwamba hapa pana fursa hii ndio kazi yao kubwa ya kuhakikisha inashirikiana na nchi hii kujua kwamba mkoa fulani wazalishe hiki ni fursa huku na tunaweza tukaipelekaje hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia sisi tunakuwa hatuungali, wenzetu wa Kenya wana-*market strategies* ambazo wanatangaza utalii. Unakuta wanatangaza kabisa kwamba pengine Mlima Kilimanjaro uko kule kwa sababu sisi tuna vitu ambavyo ni vikwazo.

Mimi kuna jamaa yangu alikuwa yuko huko Sweden, lakini ametaka kuja, kwenda kwenye ubalozi wetu wanasema hawatoi *visa* ya *East Africa*. Sasa anakwenda kwenye ubalozi wa Kenya na nchi nyingine anapata *visa*, anakuja kupitia Kenya, kule anatoa pesa inabaki kule, sisi tumezuwia, lakini atafika Tanzania kapitia Kenya. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kuna fursa kama hizo zipo sisi tunazizua kwa vikwazo ambavyo kwa kweli kama kuna msingi mkubwa ambao tunauona hauna manufaa basi turekebishe ili na sisi tuweze kupata pesa kutoka kwa watalii wengi wanaotaka kuja kwetu. Kwa hiyo, hayo ndio mambo ambayo ninaya-*insist*.

Mheshimiwa Spika, wenzetu kule kuna lugha ya Kiswahili, lugha ya Kiswahili nje wanaofundisha wengi ni Wakenya wanafundisha Kiswahili, sisi tupo na ndio waanzilishi na wenye Kiswahili hapa, hatufanyi hivyo. Ukiangalia kwenye mtandao unakuta kuna *translation* za Kiswahili wamefanya Wakenya, wameingia mkataba na *google*, wanapata fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi tuzione hizo kama ni fursa na sisi tuweze kutumia mabalozi wetu na wengine kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaitendea haki Wizara hii, tunaitendea haki nchi yetu ili tuweze kusonga mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini cha mwisho sio kwa umuhimu, basi angalau hawa mabalozi wabakiziwe maduhuli yale ambayo badala ya kupeleka Serikalini wabaki nayo mabalozi yawasaidie kwa ajili ya ujenzi wa balozi zao, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, ahsante Mheshimiwa Grace Tendega tunakushukuru kwa mchango wako. Mheshimiwa Yahya Mhata na Mheshimiwa Neema atatuhitimishia mchana wa leo.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, na mimi naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Balozi Mulamula kwa kuwasilisha vizuri sana na kwa umahiri mkubwa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Lakini pia naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru watumishi wote wa Wizara hii kwa ushirikiano walioutoa katika uandaaji wa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa maono mazuri aliyonayo juu ya Wizara hii. Kwa mara ya kwanza Wizara hii inaongozwa na wabobezi wa diplomasia, hakuna atakayebisha Waziri wetu ni mbobezi hakuna atakayebisha, Naibu Waziri ni mbobezi hata Katibu Mkuu wa Wizara hii ni mbobezi katika masuala ya diplomasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi sina mashaka na watu hawa na namshukuru sana, sana, sana Mheshimiwa Rais kwa kuliona hilo. Wakati Rais wetu analihutubia Bunge baadhi ya maneno ambayo aliyazungumza katika Wizara hii ni kama ifuatavyo na naomba ninukuu alisema; "tunafanya uchambuzi utakaobaini nafasi ya kila ofisi ya Ubalozi katika kukuza biashara, uwekezaji na utalii, uchambuzi huo ndio utakaotumika kupanga Maafisa kulingana na uwezo wa kila Balozi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nakuja kwenye mchango, tunazo changamoto nyingi sana katika balozi zetu,

Mheshimiwa Rais ameeleza hapa. Bahati nzuri mimi nimewahi kufanya kazi katika balozi zetu, nilikuwa Ubalozi wa Tanzania New Delhi, India ni jambo la kushangaza Ubalozi ule una watumishi watatu ambao wanawakilisha ukiondoa India kuna nchi zingine za uwakilishi. Hapa unajuliza diplomasia ya kiuchumi utaitekeleza vipi kwa idadi hii ya watumishi. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri maelezo yale ya Mheshimiwa Rais ayafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na nimuombe Mheshimiwa Waziri aangalie umuhimu wa India kimkakati katika kukuza biashara, kimkakati katika masuala mazima ya utalii. India ndio makao makuu au ndio soko letu kuu la korosho zote zinazotoka Tanzania. Kuna Jimbo linaitwa Kerera, korosho zote za dunia hii zinakwenda pale, kwa hiyo, lazima tuwe na watumishi wa kuhakikisha wanalikamata soko lile. India ndio makao makuu ya *textile industry*ukienda Jimbo la Gujarat, ndio pamba yote inayozalishwa duniani inakwenda kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, India ndio makao makuu ya matibabu, ukiwa na tatizo la kiafya usipoona India wewe ujue huponi tena. Kwa hiyo, kuna kila sababu kuhakikisha tunapeleka watumishi wa kutosha wa kuweza kuhakikisha kwamba tunaweza kupata wawekezaji wa kutosha ambao watakuja kuisaidia nchi yetu. Lakini hali ilivyo sasa inatia huzuni sana haiwezekani nchi kama India *sub-continent* unakuwa na watumishi watatu, ambao unatakiwa utoe huduma Srilanka, utoe huduma Bangladesh na utoe huduma na Nepal jambo hili haliwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namuomba sana Mheshimiwa Waziri aangalie maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuna kila sababu ya kujipanga kimkakati katika kuhakikisha kwamba tunawapanga watumishi wetu kwa lengo zima la kukuza biashara zetu, kukuza utalii wetu na kukuza uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna suala la rasilimali watu, nimelizungumza upungufu wa watumishi na jambo hili kwa kila mahali ukienda China, kuna watumishi watatu Balozi na

watumishi wawili, mwambata wa jeshi na mwambata wa fedha hauwezi ukafanya kazi kwa kuleta tija katika nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini suala la maslahi ya watumishi; unaweza ukawaona watumishi wa Ubalozini wanapata maslahi makubwa kweli jambo hili si sahihi. Bara la Asia watumishi hawa wamegawanywa kimatabaka, mtumishi aliopo New Delhi, India analipwa tofauti na mtumishi aliyopo China. Mtumishi aliyopo China analipwa tofauti na mtumishi aliyopo Malaysia, kwa nini watumishi hawa tunawapa *allowance* tofauti? Ningeshuri Mheshimiwa Waziri ili kulinda maslahi ya watumishi tuhakikishe watumishi wetu tunawapa maslahi yaliyosahihi na yanayolingana. Haiwezekani Balozi wa India analipwa tofauti na Balozi wa China, analipwa tofauti na Balozi wa Malaysia wakati hawa wote ni Mabalozzi, hawa wote ni watumishi walioko katika nchi zetu kwa hiyo, naomba maslahi ya watumishi yaangaliwe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini kingine watumishi waliopo Ubalozini hawalipwi stahili zao, takribani miaka kumi hakuna mtumishi wa Ubalozini anayelipwa fedha ya likizo, watumishi hawa inabidi wajitegemee wao wenyewe jambo hili kwa kweli linakwamisha sana ustawi wa kazi zao.

Mheshimiwa Spika, lakini imeelezwa hapa changamoto ya makazi ya watumishi, naomba niishauri Wizara naomba tutumie mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii tuliyonayo ikajenge nyumba katika Balozi zetu, kwa kufanya hivi tutakuwa tumefanya mambo mawili, kwanza tutaisaidia Serikali kutoa fedha kwa kujenga nyumba lakini pili, tutarejesha fedha zetu hapa hapa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama utawaambia *National Housing* waende Nairobi wakajenge nyumba, nyumba ambazo watumishi wa Ubalozzi watakaa, maana yake Wizara ya Fedha itailipa *National Housing*. Kama utawaambia *National Housing* wakajenge nyumba India maana yake watumishi wa Ubalozini watakaa katika nyumba za *National*

*Housing* na Wizara ya Fedha itailipa *National Housing*, kwa hiyo, tutaacha fedha zetu ndani ya nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, na kwa kufanya hivi tutajenga nyumba nyingi sana, lakini kama tutaendelea na utaratibu wa kumbana ndugu yangu Mwigulu atoe fedha Hazina, tutakesha hatutamaliza tatizo la nyumba.

Mheshimiwa Spika, kuna mjumbe hapa amezungumzia masuala ya raia pacha, niliwahi kuzungumza ndani ya Bunge hili kwamba tatizo hili liliwakuta wenzetu wa India, lakini walilimaliza kwa utaratibu mzuri sana. Badala ya kutoa uraia pacha, wao waliwatambua raia wao waliopo nje ya nchi kwa kuwapa kadi, wanaitwa *Non-residence of India (NRI)* na sisi tuwatambue Watanzania waliopo nje ya nchi tuwaachie na uraia wao lakini tuwape kadi *Non-residence of Tanzania*. (Makofi)

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo...

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Mbunge wa Longido.

## TAARIFA

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nimpe mzungumzaji taarifa kwamba katika Taifa la Marekani pia wanawapa wageni *green card* kuwatambua kwamba wanaweza kuishi na kufanya kazi huko.

**SPIKA:** Unapokea jambo hilo?

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru naipokea taarifa hiyo. Kwa hiyo, ninachojaribu kueleza hapa...



(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

**SPIKA:** Ahsante sana bahati mbaya na muda wako umeishia hapo hapo.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahya Mhata, Mheshimiwa Neema Lugangira atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho mchana wa leo.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii. Kwanza kabisa ningependa kwa kuanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa ziara yake ya kwanza aliyofanya nchini Kenya ambayo imeleta matokeo makubwa sana katika *economic diplomacy* ambayo tunaihitaji na kama tutakuwa tunafuatilia *weekend* hii Serikali ya Tanzania na Kenya wamekubaliana kuondoa tozo za biashara 30 na pia kuna mchakato wa kuondoa tozo 34. Kwa hiyo, hii ni matokeo ya jitihada kubwa za Mheshimiwa Rais na hapa pia nimpongeze Waziri wa Viwanda na Biashara kwa kufanikisha jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile ningependa kusesitiza kwamba, mtazamo wa Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan kuhusu Kenya kwamba, Kenya sio adui yetu uungwe mkono, Kenya ni mshindani mwenzetu, Kenya wanatupa changamoto. Hivyo tusiwaogope, tunawaweza na tunaweza kuwakabili na ninasema hivi kwa sababu hata nchini Tanzania tupo Watanzania wengi ambao tumesoma nchini Kenya, kwa hiyo, tunawafahamu na tunaweza kushindana nao ipasavyo tusiwaogope. (*Makofi*)

Aidha, napenda niungane na Wabunge wenzangu ambao wametoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kuhusiana na kutengeneza safu mpya kwenye Wizara ya Mambo ya Nje iliyojaa wabobezi kwenye fani hii

ya diplomasia chini ya uongozi makini wa Balozi Mwanamama Liberata Mulamula, Naibu Waziri Balozi Mbarouk, Katibu Mkuu Balozi Sokoine, Naibu Katibu Mkuu Balozi Fatma Rajabu lakini pia na *Chief of Protocol* Balozi Mndolwa ambao kwa ujumla wao wote tuna imani nao kubwa sana na sasa tunaendelea kuona diplomasia ya nchi yetu ikipaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa kugusia suala la *diaspora*; hili jambo lilishajadiliwa sana na tulishapiga hatua ambapo *diaspora* hawa mikutano mbalimbali ilifanyika nje ya nchi kukusanya maoni ya *diaspora* lakini hata na *diaspora* walishirikishwa katika kutoa maoni kwenye Katiba mpya ambayo inapendekezwa. Sasa nimefurahi katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amegusia suala la *diaspora* lakini na hata katika mapendekezo ya Kamati nao pia wamegusia suala la *diaspora*.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2010 hadi 2015 zilifanyika ziara nyingi sana nje ya nchi kama ambavyo nimesema kukusanya maoni na hawa *diaspora* pia walishiriki kwenye huu mchakato wa Katiba mpya na yote haya yalipelekea kuanzishwa kwa Idara ya *Diaspora* ndani ya Wizara ya Mambo ya Nje ambapo kulikuwa na Mkurugenzi mwenye jukumu la kufanya *co-ordination* na ufuatiliaji. Hivi sasa jambo hili ni kama tumerudi nyuma kwenye hii ajenda nzima ya *diaspora*, kwa sababu hivi sasa kuna sheria ambazo zinamzuia Mtanzania anayeishi nje kumiliki ardhi, lakini zipo pia sheria ambazo zinamnyima Mtanzania anayeishi nje ya nchi haki ya msingi kwa mfano hata kurithi mali za wazazi wake, Mtanzania anayeishi nje ya nchi hawezi kurithi mali ya baba yake au mama yake kwa sababu sheria zimeweka hicho kizuizi.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo mimi ambacho ningependa kupendekeza ni kwamba Waziri au Wizara ya Mambo ya Nje ije na sera ya *diaspora* kwa sababu kama tunavyofahamu nchi za wenzetu wanatumia *diaspora* katika kuendeleza na kukuza uchumi pamoja na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, ninaendelea kuisistiza kwamba Serikali itunge sera ya *diaspora* na sera hii ni muhimu kwa sababu jambo hili haliwezi kuendeshwa na Wizara ya Mambo ya Nje peke yake, suala hili linahusu Uhamiaji, linahusu Ardhi na mambo kadha wa kadha.

Mheshimiwa Spika, Mbunge mwenzangu aliyetoka kuzungumza ametolea mfano wa India, lakini ningependa kufafanua kidogo India walichofanya wamewapa watu wa India wanaoishi nchi za nje kitu kinachoitwa *Peoples of India Origin (PIO)* na hii *PIO* inamruhusu yule mwenye *passport* ya *PIO* kuingia India na kutoka muda wowote bila *visa*, inamruhusu kuwekeza kwenye hiyo nchi, inamruhusu kufanya kazi kwenye sekta zote kasoro sekta ya ulinzi na usalama na jambo lingine ambalo hawaruhusiwi kufanya ni kujishughulisha na masuala ya kisiasa na kupiga kura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa mantiki hiyo, na mimi ningependa kupendekeza na sisi kama Tanzania tufike huko, hatuwezi kwenda huko bila kuwa na sera ya *diaspora* na sheria ambayo itatuelekeza ni namna gani tutatoa fursa kwa hawa *diaspora*, na tusichanganye mambo mawili *diaspora* na uraia pacha, hili la uraia pacha tumeshalijadili na limeonekana lina ugumu, hivyo lisituchukulie muda, lakini hili la *diaspora* ninaamini lipo ndani ya uwezo wetu na hata sasa hivi *diaspora* wananunua viwanja, wanawekeza lakini wanafanya hivyo kwa kutumia njia ambazo sio rasmi kwa kutumia ndugu, jamaa na marafiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunachotakiwa tufanye ni tuwe tu na sera ya kuweka hili suala rasmi na kupitia hiyo tutaweza kujua tuna *diaspora* wangapi tutaweza kujua mchango wa *diaspora* kwenye ukuaji wa uchumi wetu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kwa kumalizia ningeomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atuambie na atupe *commitment* ya Serikali ya kuja na sera ya diaspora ambayo itawezesha Watanzania wanaoishi nje kuchangia

kwenye maendeleo ya nchi yetu na kutupa rasilimali fedha ambayo tunaihitaji kwenye uwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema Lugangira kwa mchango wako na wale wote ambao mmechangia asubuhi ya leo; jioni tutamalizia wale ambao majina yenu tunayo hapa tuweze kuitendea haki Wizara hii ya Mambo ya Nje moja ya Wizara muhimu kabisa katika nchi yetu, ambayo inatuunganisha na mataifa jirani ya Afrika Mashariki, lakini pia na dunia nzima kwa ujumla. Miaka kama mitatu/ minne iliyopita niliwahi kwenda safari moja kule Sweden tukakutana na Watanzania wengi sana hao wanaoitwa *diaspora* kwenye meli, Balozi wetu Dkt. Silaa aliandaa hiyo shughuli, walikuwa wengi *almost* sawa sawa na idadi ya Wabunge wote hawa.

Kwa hiyo, tulisafiri nao tukaenda nchi moja hivi nchi ya *Eastern Europe* ilikuwa *part of Russia*, tukasafiri kwenye meli mle tukiwa tumejaa sisi Watanzania na usiku kucha na kesho yake halafu tukarudi tena Stockholm kwa meli hiyo hiyo. Tulizungumza mambo mengi sana nashukuru kwamba baadhi yake sasa mnayachangia sasa kama sehemu ya jinsi gani ambavyo tunashughulika na *diaspora*.

Baadhi yao mliokuwa nao mle walikuwa na mawazo tofauti sana kuhusu nchi yetu ila tulitumie muda ule kuwaeleza nyumbani kukoje, namna gani, hali ikoje, fursa zikoje, baadhi yao walikuwa wakitoa machozi mbele yangu, wakijutia jinsi gani ambavyo walilazimishwa na mazingira kuchukua uraia wa kule waliko kwa sababu za kiuchumi, lakini sasa wakirudi nyumbani hapa wanakuja kama wageni kama ulivyoeleza hawawezi kuwekeza, hawawezi kurithi, watoto wao hawatambuliki huku, itabidi wao wenyewe wazikwe ugenini na watoto wao wazikwe ugenini yaani mtu anaeleza mpaka anatoa machozi analia kabisa, anakumbuka nyumbani na hasa wanapoanza kuwa watu wazima. (*Makofi*)

Wanapokuwa bado vijana wanakimbilia mimi nina *storeaway*, lakini wanapoanza kuwa watu wazima sasa ile busara na hekima inanza kuja ya nyumbani lakini fursa ya nyumbani haipo kwa hiyo ningependa na mimi kupigia tu mstari wa kuwaomba wenzetu wa mambo ya nje na Serikali kwa ujuma kuliangalia hili jambo, hawa watu ni wenzetu, hawa watu ni watoto wetu ni ndugu zetu kwa hiyo tuangalie hakuna anayesema tufungue milango yote, hayupo, tuangalie maeneo ya ulinzi, maeneo ya siasa hizi na mengine ambayo tunaona ni kwa sababu ya kusita kidogo, lakini hakuna shinda, lakini maeneo ya uchumi wa watu wetu tufungue. (*Makofi*)

Tulizungumza nao mambo mengi sana, of course moja wapo ilikuwa na tulienda na watu wa Benki ya CRDB sijui na nani tulikuwa nao mle kwenye meli ile. (*Makofi*)

Ilikuwa ikirushwa *live* huku Tanzania wakati tukiwa kule wakati huo *of course* maswali mengine yalikuwa magumu kuna baadhi ya diaspora mabinti wakatuuliza hizi fomu ukitaka kupeleka fedha nyumbani kwenye Akaunti ya CRDB fomu zake hizi lazima unapotuma fedha ueleze umezipataje pataje, sasa wengine tupo huku tuna shughuli maalum sasa tunaandikaje yaani hoja ikawa swali. (*Kicheko*)

Tupunguze maswali maswali kama mtu anarudisha fedha nyumbani maswali ya nini si fedha inarudi tu nyumbani hata uwe a kijana wako anarudisha fedha nyumbani umezipateje pataje una binti yako umezipataje pataje hizi fedha. (*Makofi*)

Sasa mwisho wake akikujibu kweli usianze kutafuta mahali pa kujificha ilo la mwisho lilikuwa mazungumzo baada ya habari. (*Kicheko*)

*Otherwise* tunawatakia kila la kheri Mambo ya Nje mnafanya kazi nzuri, ila sasa na nyie mhamie Dodoma mambo yenu fanyieni Dodoma, Dodoma ndio makao makuu ili mabalozi hawa wawe wanawafuata Dodoma, mkifanyia sana Dar es Salaam mnawaaminisha mabalozi kwamba

Dodoma bado, wakati Dodoma tayari imeshakamilika.  
(Makofi)

Kwa hiyo hilo tunalitilia umuhimu wa aina yake kabisa mwakani hilo litakuwa swali kubwa kwenu mmehamia Dodoma au imewekwa tu kuegesha Dodoma, hapana. Mambo ya Nje fanyieni mambo yenu Dodoma, nyinyi ndio wakwanza kuonyesha uzendo kwa mabalozi wetu na uzalendo mmojawapo ni kufanyia kazi zetu Dodoma. (Makofi)

Basi baada ya maelezo hayo tunawashukuru tena, tunaomba Waheshimiwa mrudi jioni ili tuweze kukamilisha suala hili la Mambo ya Nje leo leo, hili zege la leo halilali.  
(Makofi)

Basi naomba nitishe sasa shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni ya leo.

*(Saa 7:05 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi saa 11:00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

### HOJA ZA SERIKALI

#### **MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Mheshimiwa Zahor Mohammed atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mheshimiwa Tecla Ungele ajiandae.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nianze kwa kuwapongeza wataalam wetu wa Wizara ya Mambo ya Nje wakiongozwa na mama yetu, hakika ndani ya nafsi yangu nafarijika kwamba Wizara imepata mtaalam ambaye kwa kweli amelelewa na kukulia ndani ya chombo hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda mfupi nimewahi kufanya kazi naye lakini ndani ya nafsi yangu sina mashaka na uwezo wa Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake lakini Pamoja na hayo Wizara ikiongozwa na Waziri pamoja na wataalam wake ombi langu kwao warudishe heshima ya Taifa letu, warudishe umoja wa nchi yetu mbele ya jumuiya za kimataifa, tulitetereka kidogo hasa kwa sababu ya kutokuendana na wenzetu na mawazo ya wenzetu pamoja na kwamba sisi tunamini, lakini ni wajibu wetu kama walimwengu ambao tunaishi na wenzetu maana yake lazima tuishi na wenzetu ili tuweze kwenda nao pamoja na yale yote ambayo yanatupa changamoto kama walimwengu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mdogo ni suala la *covid* ambalo kwasasa nashukuru sana tumeanza kulivalia njuga na ninaamini sasa taaluma itatolewa na hatua za tahadhari zitaendelea ili tuendeleo kuishi kama walimwengu, Tanzania siyo sehemu ya pekee Tanzania inaishi kama wanavyoishi wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Waziri Wizara ya Mambo ya Nje ni taaluma pekee, ni taaluma *unique*, siyo kila mmoja anaweza aka-*practice* mambo ya uhusiano wa kimataifa, ni taaluma iliyotukuka. Siyo kila mmoja anaweza kupangwa kwenda kufanyakazi Wizara ya Mambo ya Nje. Tumejifunza muda mfupi au miaka mchache iliyopita Pamoja na kwamba ni mamlaka ya Wizara yetu ya Utumishi kuweza kumtumia mfanyakazi yeyote kumpeleka popote ombi langu kwa Wizara yetu ya Utumishi lakini vilevile kwa wenzetu wa Wizara ya *Foreign Affairs* ikae ifanyakazi na wenzetu wakubaliane kwamba siyo kila mmoja anaweza akapangwa kwenda kufanyakazi hasa za kidiplomasia ndani ya Wizara hii. Tunaweza tukapeleka mwandishi wa habari,

mhasibu, mpiga picha lakini kazi zinazohusu diplomasia tuwaache wanadiplomasia wafanyakazi za diplomasia ili nchi yetu iweze kufanyakazi zake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa maana hiyo hiyo ningepomba sana sasa tumezungumza wenzetu wengi hapa wamezungumza kuhusu *economic diplomacy* mana yake tunalazimika sasa kuondoka tulipokuwa tupo huko miaka ya nyuma, sasa hivi tunatakiwa kuangalia ni Nyanja gani na nani ambaye tunaweza kushirikiana naye hasa inapokuja maslahi ya Taifa letu. Marafiki wako wengi, lakini waswahili wanasema nionyeshe Rafiki yako nitakwambia wewe ni mtu wa aina gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani tulikuwa na mirengo ya siasa; kuna wenye siasa kali za kijamaa, kuna mabepari kuna na wasiofungamana, naamini kidogo tumeanza kutoka hapo sasa hivi tunaangalia *economic diplomacy*.

Ombi langu kwa Wizara tuchague marafiki zetu na tusione haya kuchagua ili mradi Taifa letu litafaidika pamoja na wananchi wake kuhakikisha kwamba tunatengeneza ajira, lakini na biashara zinafanyika ndani na nje ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imejaaliwa kuwa na bidhaa nyingi sana hasa zinazotokana na kilimo. Ombi langu sana kwa Wizara hii ifanye kazi ya makusudi wala isiogope kufungua balozi kwenye maeneo mengine eti kwa sababu tunaogopea gharama. Gharama ni pesa, lakini pesa zinatafutwa, lakini hakuna kazi kubwa duniani kama kutunza marafiki, ni kazi ya gharama, ni kazi ngumu, lakini lazima sisi kama Tanzania tuhakikishe kwamba tunaishi kama wanavyoishi wenzetu tuweze kuwatunza marafiki zetu. *(Makofi)*

Ombi langu sana tutafute mataifa ambayo balozi zetu zitafunguliwa, lakini kubwa liwe ni kuhakikisha kwamba Taifa letu linatafaidika ili tuweze kufanyabiashara za ndani na nje. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati huo huo naomba nizungumzie hoja moja kuhusu wataalam wetu, ni kweli kwamba tunafundisha, ni kweli kwamba watoto wetu vijana wetu wanasoma kwenye maeneo mbalimbali, ombi langu kwa Serikali wenzetu hawa kama mtakumbuka hotuba aliyoisoma Mheshimiwa Waziri ukiipitia kwa ndani utagundua kwamba mambo mengi waliyoyapanga walishindwa kuyatekeleza kwa sababu tumeshindwa kuwapatia uwezo. Sasa tutaendelea kuwalaumu, tutawashambulia, lakini ukweli ni kwamba sisi kama Bunge tumepitisha bajeti, tumeidhinisha walichokitaka, bahati mbaya sana tulishindwa au Serikali haikuwapatia fedha kama ambazo walizomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali ili wenzetu waweze kufanya kazi zao na ili kesho na kesho kutwa tuje tufanye tathmini walichokiomba na walichokifanya, naiomba sana Serikali tuwapatie uwezo wenzetu ili waende wakafanye majukumu waliyojipangia ili Taifa letu lifaidike. Kama unajipangia kazi za Serikali halafu Serikali yenyewe haikuwezeshi maana yake ni kama vile tunatwanga maji kwenye kitu. Ombi langu kwa Serikali tuhakikishe kwamba tunawapatia wenzetu hawa ili waweze kufanyakazi zao kama walivyojipangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo linaweza likaungana na hili niliwahi kusema kule nyumba kwamba tutawalaumu Wizara zote tutazilaumu tutalaumu Mambo ya Nje, Polisi, Jeshi tutawalaumu Wizara ya Maji, Miundombinu tatizo siyo Mawizara, tatizo ni sisi wenyewe kama Wabunge tumeshindwa kuchukua nafasi yetu ya kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wetu basi kuisimamia na kuishauri ili waweze kupatiwa fedha wenzetu hawa wahakikishe wanatekeleza majukumu yao, *then* ndiyo tuje tuwahukumu hapa kwamba kuna kitu hawakutekeleza tuanze kulalamika. Vinginevyo kila mwaka tutapitisha bajeti haiendi, kila mwaka tutapitisha bajeti kwa sababu tumeiachia Wizara ya Fedha kwa mujibu wa makubaliano yetu kwamba ndiyo iamue nani impe, nani isimpe, impe lini, impe kiasi gani, hili halijakaa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nawaomba sana naiomba sana Serikali naliomba sana Bunge hili tuone namna gani tunaweza kusimamia au kufanyakazi yetu kama Wabunge kusimamia Serikali lakini kuhakikisha yale tunayoamua humu ndani basi yanatekelezwa kwa mujibu ambavyo tumeamua, vinginevyo sisi hatufanyi wajibu wetu na Serikali hatuisaidii ili iweze kuwahudumia wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo atafatiwa na Mheshimiwa Tecla Ungele, Mheshimiwa Joseph Thadayo ajiandae.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mulamula - Waziri wa Mambo ya Nje kwa taarifa yake nzuri aliyoiwasilisha hapa Bungeni nawapongeza watendaji wote, lakini pia nawapongeza mabalozi wote pamoja na *UN agencies* zilizokuja leo hapa asubuhi kuungana nasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuzungumzia suala la Jumuiya ya Afrika Mashariki na muda ukiruhusu nitazungumza mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ilianza toka mwaka 1967 lakini ika-*collapse* mwaka 1977, ikaanza tena rasmi mwaka 2000. Watanzania wengi ukiwauliza hata kule vijijini hawajui hii Jumuiya ya *East Africa* inafanyaje kazi, hawajui tumeungana nini na hawajui hata ile *treaty*/ule mkataba ambao Tanzania imesainiana na nchi nyingine ambazo ni Rwanda, Burundi, *South Sudan*, Kenya na Uganda hawajui kimeandikwa nini. Hivyo basi niombe ofisi ya Mheshimiwa Waziri iweze kueleza ni kitu gani ambacho tumeungana kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilikuwa ningependa pia hizi nchi ambazo tumeungana ziweze kwenda kwenye *treaty*. Tuliona hapa juzi juzi kulipotokea na ugonjwa wa *Covid* kila nchi ilikuwa na mwelekeo wake, tuliona madereva wengi walikuwa wakikwama mpakani, lakini tuliona pia mahindi yakikwamba pale mipakani, tunamshukuru Mheshimiwa Rais alivyoenda haya mambo yalinyooka, lakini wananchi walikuwa tayari wameshapata hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni nini; hoja yangu ni kwamba kama nchi nyingine ina mahindi mengi basi ile nchi inunue yale mahindi. Haiwezekani Tanzania tukawa tunaagiza sukari toka nje wakati labda Kenya kuna sukari na Uganda kuna sukari. Kwa hiyo, hoja yangu ni kwamba hizi nchi zilizoko kwenye Jumuiya zishirikiane kiuchumi, lakini pia ili kuleta nafuu kwa wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilikuwa naomba wale wawakilishi wetu ambao wanatuwakilisha huko tunao Wabunge wa *East Africa* ambao kwa kweli sielewi uwajibikaji wao huwa ukoje, yale wanayoyapitisha kule wangekuwa wanajaribu kutuletea hapa tukaona kumepitishwa nini. Nalisema hilo kwa sababu tunawachagua hapa, lakini tungepata mrejesho kule wamefanya kazi gani kwenye Bunge lile la Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuzungumza suala ambalo limezungumzwa na wachangiaji wengi waliopita hapa. Napenda kuzungumzia suala la uraia pacha. Kama walivyozungumza wachangiaji waliopita ipo haja sasa ya kuangalia sheria yetu hasa ile *Citizen Act* kuangalia jinsi gani tutaweza kuwa-*accommodate* hawa Watanzania wanaoishi nje ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengi walioenda nje ya nchi walikwenda kutafuta kazi, lakini wengine walikwenda kusoma, baada ya kusoma walipoona wamekosa kazi huku wakaajiriwa kule. Hivyo basi zile sababu ambazo zilikuwepo zamani labda za kusema kwamba

hatuwezi tukawa na uraia pacha wakati ule dunia ndiyo ilikuwa bado haijawa kijiji, kwa sasa hivi dunia ilivyo kijiji ipo haja ya kuwa na uraia pacha. Lakini tunapokuwa na uraia pacha maana yake nini; tunapokuwa na uraia pacha kwanza tunamwezesha yule Mtanzania aliyeko kule nje ya nchi ambaye alikwenda kwa ajili ya kutafuta maslahi na pia kusaidia ndugu zake aweze pia kuwa na ule moyo mkunjufu wa kujiona kwamba na mimi bado ni Mtanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wale watu wako kule wameoa na wamezaa na wengine mpaka wana wajukuu kuwaacha kukaa kule moja kwa moja kwa sababu wamechukua uraia wa nchi nyingine ni kama vile tunakipoteza kizazi cha Watanzania ugenini. (Makofi)

Hoja yangu nilikuwa nataka niishauri Serikali inaweza ikawa-*accommodate* huu uraia pacha, lakini ikawawekea masharti ya wale Watanzania na huu uraia pacha hauji kwa wageni kwa maana kwamba ya *foreigners*, uraia pacha uwe kwa Watanzania ambao wamezaliwa humu nchini Tanzania, lakini wameenda kule nje kwa ajili ya masomo na hii katika nchi nyingi za Afrika zinaendelea ku-*accommodate* hili suala kuna nchi karibu 24 zimesharuhusu uraia pacha. Kwa hiyo, na sisi tujaribu kuangalia sheria zetu na tuwawekee sheria ambazo zitaweza ku-*accommodate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo faida ya kuwa na uraia pacha kuliko kutokuwa na uraia pacha kwa sababu ya uwekezaji kiuchumi pamoja na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia leo ni suala la mabalozi walioko...

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taska Mbogo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Boniphace Getere.

## T A A R I F A

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba jambo analolizungumzia la uraia pacha yaani yako mambo ya kufikiria sana, kwa mfano Mtanzania anakwenda kusoma MarekaniM ameenda kwa ajili ya masomo atazaa huko huko Marekani na kwa sheria za Marekani ukizalia Marekani anakuwa na uraia wa Marekani. Sasa kama huyu mtoto naye hatapata uraia wa Kitanzania tutakuwa tunapoteza watoto wanaenda Ulaya na mama anarudi nyumbani au baba anarudi nyumbani au baba anarudi nyumbani. Kwa kweli hili jambo ni la kufikiria sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taska Mbogo unapokea taarifa hiyo?

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea hiyo taarifa, ni taarifa ambayo ni sahihi ni kweli kizazi cha Watanzania kinapotea kule ughaibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nazungumzia suala la mabalozi, hawa mabalozi ambao wapo kwenye nchi zile zilizopo ambazo sisi tuna ofisi zetu za balozi kule nilikuwa naomba waitangaze nchi yetu, wanaitangaza vipi. Nilikuwa naomba iwasiliane na Wizara ya Maliasili na Utalii wachukue zile *brochures* ambazo zinatangaza vivutio ambavyo viko nchini kwetu Tanzania ili waweke kwenye zile ofisi za mabalozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia waweze kuchukua bidhaa ambazo tunazo huku nchini kwetu Tanzania waziweke kwenye ofisi za mabalozi. Nimeona kwenye ofisi nyingine za balozi nchini kule nje ya nchi unakuta kuna bidhaa, kuna kahawa, kuna majani ya chai, kuna nini, kila kitu wame-*advertise*/wanatangaza zile bidhaa ambazo zinatoka kwenye nchi zao.

Kwa hiyo. nilikuwa naomba hawa mabalozi waweze kufanya hiyo kazi. Lakini zaidi ya hapo wawe na mikutano

ya kuangalia kwa mfano mtu yuko Ethiopia ajaribu kuita wale matajiri wa pale Ethiopia labda wenye viwanda vya ngozi au viwanda vya nguo aongee nao jinsi gani wanaweza wakaja nchini kwetu kununua ngozi zilizopo hapa. Ngozi za Tanzania zinatupwa tu, lakini kule Ethiopia wana viwanda wanatengeneza majaketi, wanatengeneza vitu vizuri sana vya ngozi mpaka viatu, lakini sisi ngozi zetu zinatupwa hata ukienda hapa Dodoma zinatupwa, ukienda Dar es Salaam zimetupwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe wale walioko kwenye hizo nchi waweze kuwasiliana na wale wafanyabiashara na wale wenye viwanda ili waweze kuja kuchukua malighafi zinazotokana huku nchini kwetu Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kuongelea ni suala la Sera ya Mambo ya Nje, haiwezekani tunakaa tunazungumza kumbe Wizara ya Mambo ya Nje haina sera, niombe kwanza Serikali ilete Sera ya Mambo ya Nje ili pia wale Watanzania waliopo nje waelewe kwamba sera ya mambo ya nje ni ipi nah ii itawasaidia sana wale Watanzania wanaoishi nje ya nchi. Nilimsikia Mheshimiwa Waziri alisema kwamba ameagiza Balozi ziwaorodheshe, kuwaorodhesha sawa waorodheshwe, lakini je, baada ya kuwaorodhesha Sera ya Mambo ya Nje inasema nini kuhusu watu wanaoishi nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hii Watanzania wako kama nilivyosema mwanzo wako zaidi ya milioni moja, lakini hawana fursa pia ya kupiga kura, hatujaweka *system* kwenye balozi zetu za kuwaruhusu hawa Watanzania kupiga kura. Sasa inapofika wakati wa uchaguzi wale Watanzania walioko nje ya nchi hawapigi kura. Lakini kama mzungumzaji aliyepita alisema kunapokuwa na maoni ya kitu chochote cha Serikali huwa wanaulizwa yale maoni kwa sababu bado ni Watanzania na bado ni kizazi chetu tuweze kuwa-*accommodate* ili sera hiyo ikitoka nafikiri itajumuisha na hayo mambo mengine wataweza kupata haki zao za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipenda pia kuzungumzia suala lingine ambalo litakuwa ni...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tecla Ungele atafatiwa na Mheshimiwa Joseph Thadayo, Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei ajiandae.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na awali ya yote naipongeza Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia kuhusu jinsi Tanzania tulivyoshiriki ukombozi wa Bara la Afrika hasa nchi za Kusini mwa Bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waasisi wetu Mwalimu Nyerere na wenzake waliamini kabisa kwamba uhuru wetu Tanzania hautakuwa na maana kama nchi za Kusini mwa Bara la Afrika hazitakuwa huru na ndiyo maana ilikuwa ni ajenda kubwa ya wakati ule. Hivyo basi, kwa nchi hii ya Tanzania tulivyoshiriki kwa kiasi kikubwa na wakati ule hasa kwenye Mikoa ya Kusini ya Lindi, Mtwara na Ruvuma ikawa ndiyo *base* kubwa ya wapigania uhuru wa nchi ya Msumbiji, Angola, Namibia, Afrika Kusini na Zimbabwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi imekuwa kama historia, lakini nakumbusha kwamba maeneo ya Lindi ikiwepo Nachingwea kulikuwa na maeneo ya Matekwe, Kwamsevumtini na kule Mtwara maeneo ya Samora na Lindi Vijijini, Lutamba, Ruvuma maeneo ya Namtumbo yale sehemu ya Seka Maganga na kwingineko ili kuwa ndiyo *base* na ma-*camp* ya wapigania uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yale pamoja na kuwa *base* tu lakini bado jamii husika ilikuwa nayo iko katika harakati zile, wanaotoka maeneo yale wanafahamu sana. Hivyo basi, wakati ule sasa, wakati wote wa harakati wa kupigania uhuru mikoale ya Lindi, Mtwara na Ruvuma ilikuwa ni vigumu kwa wawekezaji kwenda kuwekeza kule kwa sababu wakati wowote Mreno anaweza akaja akaleta vurugu kule na wengine, kwa hiyo, hakukuwa salama. Hivyo tukaja kujikuta kwamba maeneo yale kwa namna fulani yakawa nyuma kimaendeleo, huo ni ukweli usiopingika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya harakati zile kwisha maeneo yale sasa Halmashauri husika zikaendeleza maeneo yale, wakaanzisha Sekondari zile za Matekwe na kwingineko, lakini ni juhudi za Halmashauri husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya kufanya hivyo nini ushauri wangu. Nashauri hivi tunaomba kwa Wizara hii ninaomba kwa unyenyekevu mkubwa wizara hii naamini kabisa inaongozwa na Mheshimiwa Mama Mulamula na Naibu Waziri na timu yote ya Wizara ya Mambo ya Nje naamini kabisa wanavyofika wakuu wa nchi hizi za Kusini mwa Bara la Afrika tulizopambana kwa kiasi kikubwa kuwakomboa tunaomba muwaambie na muwalete maeneo ya Nachingwea na kule Ruvuma ili waje waone yale makambi, waje waone jitihada zile tulizozifanya sisi wenyewe ndani ya halmashauri husika bado hazitoshi tunaomba mchango wao, tunaomba waje waweke wafanye jambo fulani kama ni la maendeleo ili tuone kumbukumbu kubwa ifanyike kama inavyofanyika sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia hii kwa uchungu kweli, tumeachwa hivyo na ndiyo hiyo naona kama vile historia inajijendeleza vile kwamba kila kitu tuko hivyo tuko nyuma tu...

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.



**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tecla Ungele kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

## T A A R I F A

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe Taarifa mama yangu anachokizungumza ni kweli kabisa na ndiyo maana Mikoa ya Lindi na Mtwara miaka ya nyuma ilikuwa mikoa ya adhabu kwamba mtu akifanya makosa anapelekwa mikoa hiyo na mikoa hiyo haikuendelezwa ni kwa sababu tu ya hayo makambi ya hiyo vita za ukombozi wa Kusini mwa Afrika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tecla Ungele, malizia mchango wako.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napokea hiyo taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili siyo jambo geni kwa watu uliowafanyia hisani wakashukuru na kama mtu hashukuru basi kama kunauwezekano wa kumkumbusha. *(Makofi)*

M imi naamini kabisa watakapoletwa wale viongozi kule wakaona wakasema hapa ndiyo ilipokuwa *camp* fulani, hapa ndiyo *ANC* walikuwa hapa, watakuwa na uchungu fulani wa kuweka jambo fulani vinginevyo wala hawafahamu kwa sababu wako kwenye neema sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ndiyo ombi langu na hii imeshatokea na kwingine na kwingine, siyo ajabu hili ninalolizungumza, wakipelekwa kule wakaja kuona hali halisi ninaomba, ninaomba, ninaamini kabisa Mheshimiwa Mulamula ninakuaminia, ni mama, una uchungu wa nchi hii, ninaomba hilo uliweke katika priority naomba utuungalie kwa kila hali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Joseph Tadayo, atafuatiwa na Mheshimiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, Mheshimiwa Ali Hassan King, ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii, awali ya yote nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Dada yetu Balazi Liberata Mulamula, Naibu Waziri, Balazi Mbarouk Nassor pamoja na wajina wangu, Katibu Mkuu Balazi Joseph Sokoine na timu nzima ya Wizara kwa kazi nzuri ambayo kwa muda mfupi toka wameaminiwa wameifanya na tumeiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pongezi hizi lazima zitanguliwe na pongezi na shukrani kubwa kwa Mheshimiwa Rais Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo wameonesha uwezo mkubwa sana na nia ya kushungulikia masuala ya kidiplomasia na kukuza diplomasia ya nchi yetu. Hata uteuzi wa mabalazi uliofanyika hivi karibuni ni ishara tosha kwa sababu uteuzi huu umefurahisha watu wengi kutokana na jinsi ambavyo umefanyika kwa umakini na kwa wigo mpana wa kuwagusa watu wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu kwa miaka mingi imekuwa na sauti kubwa sana kwenye mambo ya kimataifa hasa upande huu wa Kusini mwa Afrika kutokana na mambo mawili; kwanza, historia yetu na pili msimamo wetu ambao tumekuwa nao katika mambo yanayohusiana na haki na mambo mengine ya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni waasisi wa *SADC* ambayo ilianza kwenye Umoja wa Nchi Tano za Mstari wa Mbele, sisi ni waasisi wa *African Union* ulioanzia kwenye *OAU* pamoja na *East Africa* na hata katika masuala ya *Pan Africanism* umajumui Afrika nchi yetu ilikuwa mstari wa mbele na tumeaminika na kuheshimika kwa hilo. Tunaiomba Wizara iendelee kuratibu ushiriki wetu katika jumuiya hizi ili sauti yetu iendelee kuwa pale pale na sasa hivi tuna nguvu kubwa zaidi kwa sababu tuko katika uchumi wa kati, kundi ambalo najumuisha karibu asilimia 75 ya *population* ya dunia

tunapokuwa pale na sauti yetu tunakuwa na nguvu zaidi kuliko hata ambayo tulikuwa nayo mwanzoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi na uteuzi mzuri wa mabalozi ambao unafanyika ingawa bado hawajapelekwa kwenye nchi mbalimbali, lakini tuendeleo tu kusisitiza vigezo na masharti kwamba mabalozi wetu wanakokwenda huko ni muhimu wakazingatia kwamba *either* huko waliko watuletee wawekezaji au watuletee masoko au fursa za elimu au ajira zote za chini na za kibigwa pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu si kila balozi ataleta wawekezaji kwa sababu pengine nchi halioko haina wawekezaji wengi ambao tunawahitaji, lakini kutakuwa na masoko, kutakuwa kuna ajira au kutakuwa na fursa za elimu nina amini kabisa nchi yetu haiwezi ikafungua ubalozi mahali ambapo hakuna fursa, tunachohitaji ni kwamba mabalozi wetu watutangulie katika kuhakikisha kwamba fursa hizo tunazipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tusiwe watu tunasisitiza tu kwamba tutowe *permit* haraka haraka kwa watu wafanye kazi kwetu, lakini je, sisi kwenda kufanya kazi kwenye maeneo mengine. Uniruhusu nitaje tu kwamba mimi binafsi nafurahishwa sana na utendaji wa balozi wetu alioko China, tunaona jinsi ambavyo anashughulika na matokeo tunayaona, naamini kabisa mfumo huo ukienda namna hiyo tutaendelea kufaidi Zaidi katika diplomasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni mfupi ninzungumze moja tu la mwisho juu ya Chuo chetu cha Diplomasia. Tunafahamu kwamba chuo kile kilikuwa hakidahili sana wanafunzi kutoka nje kilikuwa ni zaidi ya kukuza uwezo wa ndani, lakini hivi karibuni kimekuwa kikidahili wanafunzi wengi hata vijana wanaotoka Jimbo langu la Mwanga wengi wanasoma pale na wengine wameshasoma pale tayari. Kwa hiyo, ipo haya ya kukiongezea nguvu ya miundombinu pamoja na walimu na rasilimali zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo Lingine ambalo linasumbua kidogo kwenye chuo kile ni kwamba vijana wanapokwenda *field* kuna tatizo kubwa sana ya kupata nafasi sehemu ambazo ni *relevant*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu taratibu za *ki-protocol* ambazo zinafanya vijana hawa wasipokelewe kwenye balozi kufanya *field*, lakini mimi ningeshauri Wizara au Serikali i-*negotiate* na hizi balozi ili vijana wetu waweze kwenda kufanya *field* katika hizi balozi ili waweze kupata hasa uzoefu wa kile ambacho wanakisomea, si lazima tuanze na balozi zote tunaweza tukaanza na balozi chache kama za *East Africa Community* au za *SADC* ili vijana wetu wanaposoma waweze kutoka vizuri zaidi kwa kufanya mazoe katika mambo ambayo wanayasomea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naunga mkono sana hoja ya Wizara hii na nasisitiza kama walivyosema wenzangu kwamba Serikali itoe fedha kama ambavyo zimeombwa na zitakavyopitishwa kwenye bajeti ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake, ahsante sana na naunga mkono hoja (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan King, Mheshimiwa Kenneth Nollo, ajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nashukuru sana kupata fursa ya kuchangia kwenye Wizara hii ambayo inamajukumu makubwa sana hususani katika kipindi hiki.

Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwapata watu makini wanadiplomasia makini kuongoza Wizara hii. Namfahamu sana Mheshimiwa Mama yetu mpendwa Balozi Mulamula, kazi aliyofanya kujenga *diaspora* pale Washington na Marekani kwa ujumla na ninaamini sasa tutaona tofauti kubwa kwenye suala hili la *diaspora* kwa sababu ni mtu anayelifahamu, anafahamu uwezo wa *diaspora* kuchangia kwenye maendeleo ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na ninaamini kwamba suala linalozungumzwa la *dual passport* (*passport pacha*) litashughulikiwa, lakini pia tukijua kwamba hawa watu hawawezi kuja kuwekeza kwenye nchi ambayo siyo raia, hata kuweka akiba tu wakitaka kufungua *account* kwenye mabanki yetu inakuwa shida. Kwa sababu wanaambiwa onesheni *passport* ya Tanzania, kwa hiyo, inakuwa kwamba akiba nyingi ambazo tunaweza tukazileta *remittances* kutoka nje huko, kutoka kwa *diaspora*, ambako kwa nchi nyingine zinachangia sehemu kubwa ya pato la Taifa, mpaka asilimia tano kwa watu wa Ethiopia inachangiwa na watu wa *diaspora*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwetu hata ukisema unahesabu haifikii hata 0.1 *percent of GDP*. Kwa hiyo, ina maana tunapoteza uwezo, lakini pia tunapoteza nguvu kazi ambayo ina uzoefu tofauti na wana-*skill* tofauti, ambayo wakija hapa wakiwa na uhuru wa kuja na kuondoka wataiacha hapa nchini. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba mimi ninamuamini sana kwamba sasa kwenye Wizara hii tumepata watu Mheshimiwa Mbarouk na Mama Mulamula naamini hawa watatufanyia kazi nzuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye suala zima la diplomasia ya kiuchumi ambalo limezungumzwa na wengi. Mimi ningesema hivi, hauwezi kuwa na Balozi ambazo hazina wafanyakazi wa kutosha, tunataka Balozi ziwe na wanamasoko, zamani ilikuwa ni *trade attachees*, wanakaa kwenye Balozi kazi yao ni kuzunguka na kuangalia ni nani anawekeza, nani mwenye *interest*, nani anauza nini kwenye masoko yale na kuunganisha watu wetu na wale watu kule pamoja na wawekezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nataka niombe kwamba tuiseme tu kwamba tunapeleka mabalozzi wazuri tupeleke pia wafanyakazi wa kutosha kwenye Balozi hizi na tusifungue tu Balozi nchi kama China jamani unakuwa na Balozi moja kwa nini usifungue *consul* nyingi miji mingi kule Thailand, miji hata mitano tukawa na *consulars*. Tukiwa na hizo ofisi ndogo ndogo za Balozi, zitakuwa na watu ambao

sasa sio tu wanadiplomasia, sasa hivi tutawapeleka watu ambao watasaidia kwenye mambo ya masoko, kwa sababu masoko yako Guangzhou yako na sehemu nyingine. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba nimeona mmefungua Ofisi ndogo kule Mumbai, tufanye zaidi China jamani ni Taifa la kimkakati, lakini yako mataifa mengine kama Marekani, Uingereza pengine Ujerumani na wapi pia ni ya kimkakati basi tufanye mbinu ya kuongeza *presence* yetu kwenye hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kingine ambacho ningeomba kuzungumzia ni *issue* ya ushirikishwaji wa wafanyabiashara kwenye safari za viongozi wetu. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwamba alivyoenda Kenya juzi hapo alianza kutuonesha mfano mzuri kwamba anachukua watu waliochujwa, wafanyabiashara waliochunjwa kutoka *TPSF* pamoja na *maybe CTI* pamoja na Mawaziri. Lakini ukweli ni kwamba, wakienda wenyewe hawa wafanyabiashara wanakuwa wanajua na watakuwa wamelenga na wanaunganishwa na watu ambao wataleta uwekezaji haraka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kila mtu atataka mbia, wewe ukiwa hapa ndani ukitaka kuanzisha biashara kubwa ni lazima uwe na wabia kutoka sehemu hizo na mimi ninaamini hili linakuwa na tija na ninaomba kwamba liendelezwe sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni kwamba tumeona pia kwamba mmejaribu na ninawapongeza sana Wizara, kusema ukweli nawapongeza Wizara kwa sababu wamejaribu kuunganisha wajasiriamali kwenye maonesho ya viwanda nimeona kuhusu China na NMB wameweza ku-*sponsor*, wameweza kutoa ufadhili kwenye jambo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri hili ni jambo la kuomba sana kwamba liendelezwe, lakini na mabenki mengine au na wafadhili wengine hata wabia wenyewe

watu wa maendeleo tuwaombe waweze kuchukua vijana wetu kwenda kuona, kwa sababu kuona ndiyo kuelewa na ndiyo kuamini. Kule China viwanda vidogo vidogo vimejaa na bei zake ni bei chee kabisa, unaweza kununua kiwanda kidogo cha shilingi hata laki tano ukaja nacho hapa ukachakata vitu, ukatengeneza fedha, ukawa tajiri, tena tuna umeme. Kwa hiyo naamini kwamba, tukiwapeleka wale vijana kule wakiona hata wale wanaofanya kama mashamba wataunda vitu ambavyo ni demonstration tukiwapeleka wale wachache, lakini watakuja kuwaonesha wenzao kwamba ni *possible* kufanya vitu vikubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine ni ujenzi wa maofisi ya Balozi ambapo ni vizuri tujenge, nimeona kwamba wanamkakati wa kujenga hizo ofisi, nilikuwa nasema kwanini tusitumie *mortgage financing* kule? Bei ya mkopo kule Marekani au Uingereza nchi nyingi bei ya mkopo riba ni asilimia mbili na hususan ya *mortgage*. Tunaweza tukachukua *mortgage* zile na kwa sababu hatuna mtaji wa kutosha wakati huu kwa sababu tunawekeza kwenye miradi ya kimkakati basi tunaomba mkopo kwenye benki ya kule, tunachukua *mortgage* ile fedha tunaipeleka Balozi kwa pango ikatumika kama ni fedha ya kulipa *mortgage* na baada ya miaka siyo zaidi ya 10, 20 mnakuwa mmeshalipa *mortgage*, nyumba ni yenu na hamjatoa fedha yoyote. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati mimi nafurahi kwamba *NSSF* walitaka kufanya vile, lakini ilikuwa pia siyo nadharia nzuri, kule *mortgage* ni kitu *straight forward*. Kwa hiyo, tunaweza tukafanya, tukakopa kwenye benki kule balozi ikajengwa wakakaa lakini wanajipa ile *mortgage* kwa fedha ya pango. Hata wafanyakizi wa balozi wanaweza wakafanya vile. Naomba sana hilo lizingitiwe kwa sababu naamini litaweza kuleta tija. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ninataka niseme kwamba, nimefurahishwa sana na nilivyosoma kwamba kwenye taarifa ya utekelezaji ya mwaka uliopita, wameweza kufanya vitu vingi, miradi mingi ambayo wemeweza

kuhamasisha kutoka kule na nikasema kwamba kweli Wizara hii imechangia vizuri na ninawapongeza kwa sababu huu ulikuwa ni mwaka mgumu sana ni mwaka wa ku-*survive*, lakini bado tunaweza kupata miradi, tunaweza kupata ufadhili wa kutosha kutoka kwenye nchi mbalimbali na tunaweza kupata wawekezaji.

Mimi nawapongezeni na ninaamini kwamba kweli tukitia nguvu kwenye Wizara hii basi uchumi wa kati wa kipato cha juu unaweza ukafikika kwa kipindi ambacho tunataraji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ali Hassan King atafuatiwa na Mheshimiwa Keneth Nollo, Mheshimiwa Ngw'asi Damas Kamani ajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante awali ya yote kwanza nishukuru kwa kupata hii nafasi nimshukuru mwenyezi mungu na pia niishukuru Serikali hii inavyokwenda vizuri hasa katika mambo ya nje kwa hiyo ni jambo la kupongezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kuzungumzia mambo matatu katika *East Africa* na nitaanza kwa msemu unaosema ndege wenye bwawa za rangi moja na mlio mmoja siku zote huwa wanaruka pamoja. Na katika nchi zetu hizi za Afrika Mashariki ni sawa na kusema ni ndege wenye bwana za rangi moja na mlio mmoja basi pia kuna stahiki tuwe tunaruka pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inapotokea kwamba mruko wa pamoja hatuupati, basi ujue hapo kuna ndege ameshabadilika mbawa, mlio na ndege huyo wakati mwingine anaweza tukasema anaweza anastahili kutengwa. Sasa jambo la kwanza ambalo linalozungumza kwanza nipongeze Serikali kwa mahusiano haya mazuri tunayoyaendeleza maana sisi Tanzania ni kinara katika kuendeleza masuala haya. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru Serikali ya kuendeleza masuala haya tunaishukuru Serikali pale Rais alipotoka kwenda Kenya, tukakubaliana masuala ya biashara, tunaishukuru tena Serikali Rais alipokwenda Uganda, tukakubaliana mambo ya biashara, tunaishukuru tena Serikali Rais aliyepita naye pia alipatana sana na Burundi na tukapanga mipango yetu ya maendeleo katika nchi zetu hizi za *East Africa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawaziri nao wa sekta nao tumewaona kwamba nao wamekwenda wameshirikiana na wenzao na hili ndilo jambo linalotakiwa. Sasa kuna kitu ambacho kinaweza kikaondosha mazingira haya ya biashara. Katika *protocol* yetu ya *East Africa* kuna ibara ya 24 ambayo katika *article* hiyo ya 24 inahitaji kuwa na Kamati ya Biashara; kamati hii ya biashara hata panapotokea matatizo inatakiwa watu wakae na waweze ku-*solve disputes* zote zinazotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mpaka hivi sasa mwaka wa 16 hii Ibara haijatekelezwa hakuna kamati iliyoundwa ya biashara na ndio maana leo Tanzania utasema fungia mahindi yasiende Kenya, kesho mahindi yanapelekwa Kenya, Kenya wanasema rudisha, leo tumekaa hatuna mapatano mengine ambayo yaliyokuwa sio ya kikodi kwa sababu hii *article* haijatekelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe Serikali ili hii *article* iweze kutekelezwa na kwa mujibu wa ile sheria tokea imetungwa wakati nchi hizi za *East Africa* zipo tatu peke yake. Ilikuwa kuna Uganda Kenya na Tanzania na ndio maana katika hiyo *article* kilichozungumzwa humo ni wajumbe tisa, watatu kutoka kila nchi. Sasa hilo ndipo tunaiomba Serikali ikae Waziri wetu wa Mambo ya Nje, Mama yetu unayependeza sana na unapendwa na watu pamoja na kijana wako hapo mwende mkaunde hii kamati, hayo matatizo yote ya biashara kwa sababu hii kamati haipo na huku haya yaliyopangwa mengine ya biashara yakija kuvurugika tunakaa kikao gani cha kuyapanga, maana

wameenda kukua Marais, hawa wajumbe wengine walikuwa awaendi na walikuwa hawapo kwa hiyo hilo ni moja..

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili ambalo nataka nizungumzie kuhusiana na hao ndege wenye mbawa moja; katika ukurasa 51 *paragraph* ya 100 ya hotuba ya Waziri ameongea hapa kuhusiana na kwamba nchi hizi wananchama zilikutana na wakasema kwamba mwanachama anaweza kuendelea na mkataba wa ubia wa uchumi wa *EPA*. Kwa hiyo nchi zinazotaka ziruhusiwe lakini hilo jambo limefanyika Februari, 2021 Kenya alikwisha jiunga mapema, huyu sijui kama ndege ambaye ana rangi za kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa sababu nchi zote tulikuwa tunaogopa kuja kuondoa *protocol* yetu hii ya *customs union*, yeye atakapokuwa anapata bidhaa na anafanya biashara na nchi za Jumuiya ya Ulaya ina maana kwamba tayari kuna mambo yetu ambayo tumekubaliana humu ndani yatakuwa hayaendi sambamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa mujibu wa Ibara ya 37.4 ya Itifaki ya Umoja wa Forodha hapa tunatakiwa wote tuwe kitu kimoja na yeyote anayetaka kujiunga huku basi kwanza atizame yale makubaliano yetu kwamba hayawezi kuharibika. Lakini hapa kuna wenzetu wameshajiunga sisi tunasema kwamba tumekubaliana waruhusiwe kumbe tayari wameshajiunga na ndio maana nilianza na msemu ule msemu wa ndege wenye rangi moja huruka pamoja, lakini sasa inaelekea tuna rangi tofauti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja suala lingine ambalo alilizungumza Mheshimiwa Taska kwamba tunawatuma Wabunge wa Afrika Mashariki, lakini hawawajui wanaenda kufanya kitu gani. Mimi ninachoshauri tuwe na sera sisi Tanzania yakuiendea Afrika Mashariki kama hatuna sera ni kweli wale hatukuwa *instrument* tutakuja kuwauliza nini, tuliwaambia wakafanye nini, sasa inawezekana wakaja wakaunga kipaumbele cha nchi nyingine kwa sababu sisi wenyewe hatuna sera. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibi Spika, sera tungekuwa na mkakati, mkakati tungekuwa na malengo ambayo tumejiwekea na vipaumbele vyetu. Kwa hiyo, mimi nashauri tuwe na sera yetu ambao vipaumbele vyetu, vitakuwemo kwenye hii sera na hapa ndipo tutakapokwenda vizuri na tutawajua hawa Wabunge kwa sababu watakuwa tayari wana *instrument*, watakapokuja kuomba kura aliyekuwa ameenda kinyume na sera na lile ambalo tunalolitaka sisi kama Tanzania basi tuna uwezo wa kumlaumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapa hatuwezi kuwalaumu kwa sababu hakuna hiyo sera ya Tanzania kuendea *East Africa* kwa hiyo, naliomba hili nimeomba mambo matatu tukafuate kanuni ya 37(4) haidhuru tunasema kwamba mtu anaweza akaruhusiwa, lakini tuangalie athari zitakazokuja kutokezea kiuchumi na kibiashara, kwa sababu tuna makubaliano ya kibiashara na nchi za *East Africa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naliomba hili nimeomba mambo matatu tukafuate kanuni ya 37(4) haidhuru tunasema kwamba mtu anaweza akaruhusiwa lakini tuangalie athari zitakazokuja kutokezea kiuchumii na kibiashara kwa sababu tunamakubaliano na biashara na nchi za *East Africa*. Na lingine nimeomba kuwepo na sera Waziri atakaposimama hapa kwa nini kwanza hii sera haipo, lakini atuambie lini hii sera itakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na lingine tunazungumzia kamati ya biashara ya *East Africa* iwepo, haya yote tunayoenda kukubaliana ikatokezea mizozo hatuna mahali pakwenda tukakaa tuka-*solve* huo mzozo. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri niombe jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine wamenituma wananchi tena hawa ni wa Jang'ombe, wameondoka wameenda Uganda juzi, wamepimwa vipimo vya corona vingi sana, kwa hiyo, mimi kama Mbunge wao nilisikitika sana na kwa sababu hatuaminiani katika Jumuiya hii ya Afrika Mashariki...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Nashukuru kupata nafasi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Keneth Nollo atafuatiwa na Mheshimiwa Ngw'asi Damas Kamani Mheshimiwa Khalifa Mohamedi Issa ajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Mambo ya Nje. Nchi yetu imekuwa inaheshimika katika sura ya kimataifa kwa muda mrefu sana. Lakini heshima ambayo tumekuwa nayo tangu enzi ya awamu ya kwanza ni kutokana na nchi yetu kuwa na misimamo thabiti katika kutetea haki na unyanyasaji wa aina yoyote katika nchi mbalimbali hapa duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatukujipambanua tu kwa kutetea haki kwa kutetea waafrika wenzetu wanavyosanyanyaswa au kuonewa lakini tumeenda nje kabisa ya Afrika na kutetea kokote duniani ambako tunaona haki inabinywa. Nataka niseme hili kwa kuangalia kwamba nchi yetu sawa inaingia kwenye uchumi wa dipomasia, lakini tunafika mahali sasa tunaanza kwenda kama watu wanaotaka kujiuza, tunapoteza heshima yetu, tunapoteza sisi tusema maskini ambaye sasa hana aibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana sasa unaweza ukawa maskini, lakini aibu unayo, una heshima yako unalinda heshima yako. Nalisema hili kwa sababu moja, wiki mbili zilizopita dunia nzima imeona namna Palestina ilivyoshambuliwa kwa kiasi kikubwa ambacho binadamu yeyote hawezi akasema hiki ni kitu gani kinatokea. Nchi yetu hatujatoa hata tamko la kulaani, hata kusikitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na mwingine anaweza aka-*justify* akasema mbona nao Hamas walikuwa wanarusharusha mawe upande ule, lakini ukiangalia

kulichofanyika pale nchi yetu tulitakiwa tuweze kufanya *condemnation* kwa namna gani Palestina walivyofanyiwa. Hata Mwalimu alikuwa na msimamo thabiti kuhusu Palestina na msimamo wa nchi yetu ilikuwa ni kwamba pale inatakiwa mataifa mawili na juzi Rais wa Amerika huyu mpya amesema pale panatakiwa mataifa mawili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nisema ni kwa nini tunaanza kupoteana, Waziri atuambie msimamo wetu kuhusu Palestina ni nini? Anachofanyiwa Palestina sisi msimamo wetu Tanzania ni nini? Hili Waziri atuambie na ikiwezekana basi leo alaumu kilichotokea juzi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na msimamo mkali kuhusu Morocco, alijitangazia kwa *west sahara* anaitawala na sisi Tanzania tukawa wakali hata tukatoa *influence* yetu kwenye Umoja wa Afrika na Morocco akajaribu kuingia pale akazuiwa, lakini hili nalo tumepoteana kwanza tumefungua ubalozi wetu Algeria ambao ulikuwepo, lakini tume-*extend* na Morocco sasa tuna ubalozi ambao tunautumia ule wa Algeria. Lakini na hili nalo Waziri atuambie msimamo wetu kuhusu *West Sahara* ni nini? Tumekubali kwamba tunakuja kujengewa kiwanja basi imekuwa *give and take* tunawaacha *West Sahara* ambako ulikuwa msimamo wetu tangu awali. Hili nalo Mheshimiwa Waziri atuambie msimamo wetu kuhusu *West Sahara* ni nini sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kuhusu *economic diplomacy* ambayo wengi wameisema kwamba sisi tuangalie nchi yetu tunapata nini, ndio maana nikasema sasa ile ni maskini anayejirahisisha na nchi yetu imekuwa na heshima kubwa na watangulizi wetu walitumia damu na nguvu zote kutetea hili, lakini hatuwezi tukatumia kitendo cha uchumi wa diplomasia tuweze sasa kusema hili sisi walau kwa vile tunapata pesa basi hili tuliruhusu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, balozi zetu tunazifungua, lakini ni lazima tuangalie kwamba tunapata nini pale. *Economic diplomacy* isichukuliwe kwamba sasa tumekubali ubeberu ututawale tunavyotaka na vyovyote itakavyoenda

lakini lazima tuseme hapana kwa *imperialism*, ni nchi yetu lazima iseme bado kuna shida ya ubeberu na ubeberu wa namna yoyote ile nchi yetu lazima isema hapana, tusipoangalia tutakuwa ma-*purpet* wa mabeberu na tutasema kila kitu tutakabiliiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme hili kwa sababu moja wakati corona inaingia nchi yetu watu waliishangaa na tulionekana hatufai kwa nini atufungii watu wetu ndani, na hili tulisimama kidete, lakini majirani zetu na Afrika wakaanza kuwaambia sasa chukueni *package* ya kujinusuru na ya kunusuru uchumi wenu na majirani zetu wamekopa *IFM, World Bank*, nani hela nyingi sana, lakini sisi msimamo wetu tulisema kwamba kwenye hili hapana kama wanataka kutusaidia basi watupunguzie riba ya madeni haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na ninataka niseme na wizara waelewe tunakoelekea tunajipeleka kwenye chanjo, sawa, lakini kwenye jambo hili tuangalie tuwe na msimamo thabiti kwamba chanjo ile bado inazungumzwa kwa tofauti. Mheshimiwa Rais ameunda Kamati na imeshauri lakini ni lazima ndugu zangu wa Tanzania tuendelee kuliangalia hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado twendeni kwa kushtukastuka, tusingize miguu yote, kama tulivyostuka hatua za awali za kufungia watu wetu bado na hili lazima twende kwa kustukastuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu balozi zetu kama nilivyogusia tusipekele tu watu ambao wamesoma *international relations*, tupeleke watu mbalimbali wenye ujuzi, wataalam wa masoko, biashara, wa uwekezaji, lakini kwamba balozi anakuwa na afisa mmoja tu pale halafu mnategemea mpate chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unateuwa balozi kwenda Lubumbashi unamchukulia kwa minajili kwenda kusuluhisha tu migogoro, lakini bado tunanaangalia kwamba balozi wetu

huyu atuletee nini Tanzania. Kinachotushinda ni kwamba tunashindwa sasa kuangalia *potential* zilizopo za kibiashara tuweze kuzileta hapa kwetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nilitaka nishauri, nchi yetu inavutia wawekezaji lakini tutaweza kupata wawekezaji wengi, lakini baadae tunaweza tukasema hawa watu wamekuja kutuibia kwa sababu moja tu, ukienda Malaysia kwamba mwekezaji lazima awe na mzawa, hapa kwetu tunasema lakini hatulifanyi, hata mzawa akiwepo anakuwa na ka-*minor share* na anakuwa *diluted*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili tuliwekee mkazo kwamba ni lazima Mtanzania awepo kwenye kampuni ile na ashiriki kikamilifu, lakini kingine tuzalishe na sisi matajiri wa kwenda kuwekeza nje, Dangote yupo kwetu hapa ametengenezwa, lakini mkakati wa kumpeleka Bakhresa nje upo wapi, matajiri wetu mkakati wao huko wapi? Nataka nishauri kwamba Wizara ya Fedha na ninachukulia mfano wa nchi ya Ufaransa ina *department* ya *Private Sector for Overseas Investment* na sisi tuwe na hicho na kitengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zetu wa China wakija hapa wawekezaji wao wanakopa hela kwenye Exim Bank ya China ndio maana inakuwa rahisi kuwekeza hapa kwetu. Sasa na sisi ni lazima tuwe na *Overseas Department* kwa ajili ya *private sector* ambayo itaweza kuwatafutia masoko, *opportunities* na hata kuangalia namna gani Serikali iweze kufanya *business negotiations* badala kuwaacha waende namna hiyo walivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya hivi tutasaidia nchi yet una kwa maana hiyo tutakuwa washindani katika biashara, katika shughuli za uwekezaji zinazofanyika na namna hiyo tutaweza kweli kusema tunatekeleza *economic diplomacy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana na naunga mkono hoja, ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Keneth Nollo.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu tena kwa matakwa ya Katiba yetu ni muhimu sisi kama Wabunge tukatafuta taarifa zinazotusaidia kutoa michango yetu humu Bungeni kwa namna ambayo, moja; tutakuwa hatuendi kinyume na misimamo ya nchi; lakini la pili, tutakuwa hatuendi kinyume na misimamo kwa sababu humu ndani ukiacha Mwanasheria Mkuu wa Serikali watu wote tumekuja kupitia vyama vyetu. Kwa hiyo, misimamo ya vyama vinaamini nini katika yale yanayoendelea.

Ni muhimu sana kuyafahamu wewe mwenyewe uwe umeyafuatilia kabla, kwa nini? Kwa sababu nimeona niwakumbushe hili maana tunaelekea kwenye chaguzi za hizi uwakilishi wa Bunge hili kwenye vyama mbalimbali huko nje. Sasa kuna wakati mtu anakuwa na wazo fulani hajafahamu msimamo wa nchi ni upi anaenda kule anachangia cha kwake yeye anachokifikiri.

Sasa wakati huo tunakuwa tunafanya makosa makubwa sana kama hufahamu msimamo wan chi uliza kwanza kabla hujatoa mawazo yako, kama hujafahamu msimamo wa chama chako cha siasa pia uliza kwanza kwa sababu hivyo vyote vinakuongoza vizuri katika namna yako ya kuelewa mambo, lakini pia namna ya kuyazungumza, inakusaidia sana wewe kama kiongozi, lakini pia unaliweka Bunge letu katika mazingira mazuri.

Nilishawahi kusema huko nyuma wakati mwingine watu uwa hawatofautishi msimamo wa Bunge ni upi au ukisema Bunge limesema ni nani akiwa amesema. Wakati mwingine Mbunge mmoja tu akizungumza wao wanasema Bunge limesema.

Kwa hiyo, ni vizuri Waheshimiwa Wabunge kujielimisha kuhusu haya mambo ili wote tuwe tumekaa kwa namna ambayo Katiba yetu inaturajia.



Mheshimiwa Ng'wasi Kamani atafuatiwa na Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda ajandae.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii. Lakini pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wanafanya kuendelea kuimarisha mahusiano yetu na nchi jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tu kwa kutoa takwimu ndogo iliyotolewa na Benki ya Dunia ambayo inaonesha kwamba kati ya mwaka 2018 mpaka mwaka 2030 idadi ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi kwenye nchi zenye uchumi wa chini na uchumi wa kati itaongezeka kwa idadi ya milioni 552. Lakini idadi ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi kwenye nchi zenye uchumi wa juu kwa kipindi hiki hiki, itashuka kwa idadi ya watu milioni 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba nadhani ni wakati Serikali yetu, hasa Wizara hii tunayoichangia leo, ikaanza kuangalia ni namna gani tuta-*tackle* ongezeko hili la watu kwenye nchi yetu ambayo itakuwa ni *general* kwa Bara letu, lakini pia tutatumia vipi fursa ya upungufu wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi kwenye nchi za wenzetu ili kuweza ku-*facillitate* Watanzania kwenda kuziba pengo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu kuishauri Wizara hii iangalie namna gani inaweza kushirikiana na Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba ifikapo muda ambao *gap* hili tunaanza kuliona kwa ukubwa basi watu wetu wa Tanzania wawe na *skills* za kutosha kuweza kukidhi nafasi hiyo, hasa vijana wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia takwimu hizi hizi zinaonesha kwamba kufikia mwaka 2050 mazingira ya Kiafrika yatakuwa *uninhabitable* kwa maana ya mabadiliko ya tabia nchi kama tusipochukua hatua za kutosha kurekebisha shida

zilizopo katika mazingira. Maana yake hii pia inaiamsha Wizara hii kuangalia kwamba ni namna gani sasa tunatumia mahusiano yetu ya kimataifa kuhakikisha kwamba watu wetu wanaweza kufaidika na mahusiano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kutaka kujua kutoka kwa Wizara hii ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba ina-*scout* vya kutosha kupitia Balozi zetu zilizopo katika nchi mbalimbali, fursa mbalimbali, mikopo na *grants* ambazo zinaweza zikatumiwa na vijana wetu wa Kitanzania kujinufaisha na mahusiano ambayo tumeendelea kuyajenga kwa gharama kubwa na kwa muda mrefu kati ya nchi yetu na nchi jirani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni namna gani Wizara hii inajenga hamasa kwa Watanzania hata fursa hizi zinapopatikana wazichangamkie. Lakini si kuwahamasisha tu, bali kuendelea kuwajengea uwezo ili hata wanapopata fursa hizi wazitumikie ipasavyo na kuweza kuifaidisha nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea kwamba mahusiano tuliyonayo kati ya nchi yetu na nchi zingine itufaidishe sawasawa na inavyowafaidisha wale tulio na mahusiano nao. Lakini pia sisi vijana wa Tanzania tunategemea sana kupata taarifa ya fursa zote zilizopo katika nchi nyingine kupitia Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni jambo la kusikitisha kwamba hata ukiingia kwenye *website* ya Wizara hii, fursa wanazoelezea ni zile ambazo zinapatikana ndani ya nchi yetu. Hakuna sehemu ambayo mimi kijana wa Kitanzania nitakwenda kwenye *website* ya Wizara hii nipate kujua fursa zilizopo nchi nyingine ili mimi niweze kuzifanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si tu kuona hizo fursa, hata nione kwamba kuna nini nchi gani, lakini hata niende kwa nani, niende wapi, niwasiliane na nani, ili niweze kupata fursa hizi. Kwa hiyo, sisi kama vijana wa Kitanzania tunaomba Wizara hii iboreshe mifumo yake ya taarifa ili tuweze kupata

taarifa ya fursa zote zinazopatikana kule na tuzichangamkie. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia Wizara hii iangalie namna gani tunakuza wingi wa watu wetu wanaokwenda kufanya kazi katika nchi za wenzetu ili tuongeze mapato na si mapato tu, tuongeze pia *skills*, *knowledge* na *technological transfer* kutoka kwenye nchi za wenzetu kuja kwetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama vijana tunasema sawa, pesa tunapata kama mapato, japo hata ukilinganisha *remittances* tunazopata Tanzania ni tofauti sana na zile ambazo nchi nyingine zinapata. Mfano mdogo mwaka 2018 Nchi ya Egypt imepata kipato cha *USD* bilioni 28.9 kama *remittance* kutoka nje. Nigeria mwaka huohuo wamepata dola bilioni 24.3. Wakati nchi yetu ya Tanzania kwa mwaka huo ime-*register* kipato cha dola milioni 365.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wanaongelea dola bilioni ishirini na kitu, sisi hata bilioni moja hatujafika. Maana yake ni kwamba hatutumii vizuri mahusiano tuliyonayo na nchi nyingine, tunayoendelea kuyajenga kwa kutumia kodi za Watanzania kujinufaisha kama nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ni wakati sasa Wizara hii iangalie, mahusiano haya tunayoyajenga, je, yana manufaa kwetu? Je, ni mahusiano ya kimkakati? Na kama ni hivyo, basi kuanzia sasa tuanze kutengeneza mahusiano ya kimkakati ambayo tunajua *as much as* tunawafaidisha wengine na sisi Watanzania tunafaidika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, na faida zinazopatikana zimguse Mtanzania, ikiwa ni pamoja basi na kuangalia namna gani tuna-*bridge gap* ya ajira kwetu kwa kuwachukua watu wetu waende ili wazidi kuturudishia mapato zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuongelei tu suala la mapato, tunaongelea pia suala la *technology*, suala la *knowledge* na *skills*. Nchi za wenzetu wanakwenda mbali

kuanza kuchukua watu kuanzia ngazi ya chini wakiwa na umri mdogo kwenda kuwafundisha kwenye nchi za wenzetu ili wapate *knowledge* na *technology* waturudishie kwenye nchi zetu. Tanzania bado mpango huo uko chini kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani mahusiano tunayoyajenga tunayajenga na nchi husika lakini siyo na Watanzania walioko kwenye nchi husika. Inasikitisha sana kwa mfano nchi ya Finland kwenye Kampuni ya Nokia, zaidi ya asilimia 80 ya ma-*engineer* walioko pale ni Watanzania, lakini kitu kinachoonessa kwamba hatuna mahusiano nao mazuri ni kwamba mpaka leo hatuna hata kampuni ya simu kwenye nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, na tungekuwa na mahusiano nao mazuri maana yake wangeweza ku-*transfer technology* hiyo, wakaja hapa na kutupa hiyo teknolojia basi tukazidi kutengeneza ajira na kukuza uchumi wa nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri na Wabunge wenzangu wengi wameshauri tuwe na *database* ya kuonesha idadi ya Watanzania wetu waliko nje, na si kuwa na *database* ya ujumla, *database* hii tui-*cluster* kwa maana ya kutenga watu wenye *profession* fulani, watu wenye kazi zingine kulingana na umuhimu wao ili tujue tunawa-*support* vipi watu hao na watatuletea nini kwenye nchi yetu, hivyo ndivyo tunavyoweza kunufaika na mahusiano yetu na nchi zinazotuzunguka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze, tumefungua *Consulate General*/Lubumbashi, lakini utajjuliza taasisi zipi za Kitanzania au makampuni yapi ya Kitanzania yanasaidiwa na Wizara hii kwenda na yenyewe kufungua au kuanza kufanya kazi zake katika nchi za wenzetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunajua kwamba tuna taasisi nyingi za kifedha, kwa mfano tuna *CRDB*, *NMB*, *NBC*, taasisi ambazo zina nguvu na uzoefu, hata nguvu ya kifedha pia inajitosheleza. Lakini taasisi za kifedha ambazo zinafanya

kazi kwenye nchi zingine zote ni taasisi za Kikenya, tuna *Equity Bank, KCB* na hata Mtanzania akitaka kufanya kazi, japokuwa tuna Ubalozi Kenya, akifika mpakani anaachana na benki za Kitanzania anaanza kutafuta namna ya kufanya kazi na benki za kigeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tusiwape nguvu hata taasisi zetu na zenyewe zisambae kwenda kwenye sehemu mbalimbali ambao tuna mahusiano nayo ili kukuza uchumi wa nchi. Kwa hiyo, bado rai yangu ni kwamba mahusiano tunayoyatengeneza yasiwe mahusiano tu ya *diplomacy* bali tuwe na faida kwenye mahusiano hayo. Na faida hizi basi tuzitengeneze kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze pia Wizara hii na Mama yetu Samia Suluhu Hassan, juzi tumempokea mfanyabiashara mkubwa Dangote, hilo ni jambo zuri sana kwa sababu anasaidia kuwekeza na kujenga ajira. Lakini hii iwe ni kama *wake up call*. Tuna wafanyabiashara wakubwa sana kwenye nchi yetu, namna gani na sisi tunaweza kuwa-*promote* kwenda kuwekeza na kutambulika kwa ukubwa kwenye nchi zingine kama sisi tunavyowatambua wafanyabiashara wa nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, basi kama wamekwenda kuwekeza, je, Serikali ina mkono kwenye uwekezaji wao au wamekwenda kuwekeza kwa nguvu zao wenyewe, na hata baada ya wao kwenda kuwekeza kule, Serikali inawashika vipi mkono. Kwa hiyo haya yote ni mambo ambayo lazima tuyaangalie na tusiwe tu tunakaribisha wawekezaji wa nje kuja ndani bila sisi kutoa wawekezaji wetu wa Kitanzania waende wakawekeze nje, hiyo ndiyo namna ambayo tutakuza uchumi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, ajiandae Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda,

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ajiandae.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kutujalia jioni hii ya leo uzima na afya kuweza kuzungumza machache kuhusu Wizara yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mama Samia, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchagua safu makini katika Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kwa kweli Mheshimiwa Balozi Mulamula na Mheshimiwa Balozi Mbarouk, hawa ni watu wabobezi ambao wanajua diplomasia ya kidunia. Kwa hiyo, ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hayo, mimi mchango wangu utakuwa mfupi tu ambao sanasana utakumbusha ziara ambayo imewahi kuandaliwa kama sikosei, mwaka 2019. Ubalози wetu ulioko kule Abu Dhabi ukishirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje uliandaa ziara ambayo aliyekuwa Rais wa Zanzibar wa Awamu ya Saba, Dkt. Ali Mohamed Shein, alifanya ziara katika nchi zile za Falme za Kiarabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na miongoni mwa matunda ambayo yamepatikana katika ziara ile ni kupatikana kwa ahadi ya msaada kwa Zanzibar, msaada wa dola za Kimarekani zisizopungua milioni kumi ambazo zingesaidia wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo wadogo wa Zanzibar kwa ujumla. Dola Kimarekani milioni kumi si pesa ndogo kwa nchi kama ya Zanzibar, ni pesa ambazo zingeweza kuzunguka na zikasaidia pato la nchi na uchumi wa nchi kwa ujumla; kwa hiyo hili lilikuwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, katika Mfuko wa Abu Dhabi *(Abu Dhabi Fund)* nao uliahidi kutoa dola

milioni kumi hivyo hivyo kwa ajili ya Hospitali ya Wete iliyoko katika Mkoa wa Kaskazini Pemba. Yaani kuifanyia ukarabati mkubwa hospitali ile, lakini pia kuifanyia mambo makubwa, pamoja na kuleta vifaa tiba pamoja na dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo ninachokumbusha ni kwamba msaada ule kila kitu mwaka 2019 walishakuweka saini ule mkataba, kilichobakia ilikuwa maafisa wale wajumbe wa mifuko ile wa *Khalifa Fund* pamoja na Abu Dhabi, waje Tanzania Zanzibar ili kukagua miundombinu na namna gani zile pesa watakazozileta zitatumika vipi, lakini kwa sababu ya mlipuko wa *Covid* duniani, basi mpaka leo hawakuweza kuja katika nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokumbusha ni kwamba Ubalozi wetu wa Abu Dhabi ukitiwa hima na Wizara yetu hii basi waweze kuhimiza, kukumbusha na kuwaambia Tanzania sasa iko salama kwa *Covid-19*. Kwa hiyo, waje wakague ili baadaye watupatie pesa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba katika Bunge lililopita tulikuwa na mvutano kidogo hapa wa nani anahusika kuweka saini katika msaada fulani wa kujenga barabara iliyoko Pemba vilevile; kutoka Wete – Piki – Melitano – Chakechake. Tuliambiwa watu wa *ADB* pamoja na *Saudi Fund* walikuwa tayari watoe msaada wa kujenga barabara ile ambayo ni muhimu sana katika maendeleo ya uchumi wa Pemba kwa mazao ya biashara pamoja na mazao ya chakula. Lakini mpaka leo tunasikia danadana, hatujui msaada ule umekwama wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninamuomba Mheshimiwa Waziri akija hapa aki-*summarize* basi atueleze nini *position* ya msaada ule wa kujenga barabara hii ya Wete, wanaita barabara ya Njia Kongwe kufika Melitano mpaka Chakechake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika pia tumeona katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri akizungumza kwamba China wako tayari kusaidia ujenzi wa barabara kuu za

Zanzibar, kilometa 148. Lakini hakukuwa na ufafanuzi. Kwa hiyo, tunamuomba Waziri pia akija hapa atueleze ni barabara zipi hizo ambazo China watatusaidia na lini tunategemea kuanza kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia kwa kuwateua majembe mawili makubwa haya. Tunasema kama Wizara hii ni upele basi upele umepata mkunaji. Kwa hiyo tunawatia moyo, waendeleo kuchapa kazi ili maendeleo ya nchi hii kupitia Wizara hii yapatikane. Ahsante sana *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, Mheshimiwa mtoa hoja ajiandae.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na kwa kuanza tu ninataka nikushukuru kwa kutukumbusha kuzingatia misimamo ya nchi yetu na sera za chama chetu ambazo zimeainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nilipokuwa nimejipanga kuchangia nikaenda kuangalia sera zetu za mambo ya nje, nisije nikasema jambo ambalo liko kinyume na sera za chama kuhusu mambo ya nje, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa imani yangu mimi nchi yetu imepata hifadhi kubwa sana ambayo haitoki kwa mtu mwingine yeyote wala Taifa lingine lolote, inatoka kwa Mungu mwenyewe kutokana na namna ambavyo sisi kama Taifa tumeji-*address* siku zote kwamba ni Taifa linalosimamia haki na linaloheshimu utu na haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hilo ni toka Taifa letu lilipoasisiwa na Mzee wetu, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Mzee Abeid Aman Karume. Tumeji-*address* hivyo, duniani kote wanatufahamu kwamba Tanzania ni nchi



ambayo inaheshimu haki za binadamu na inatetea haki.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzangu ametoka kusema muda mfupi uliopita juu ya msimamo wetu kama Taifa kuhusu hali inayoendelea Mashariki ya Kati, na ukisoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hakuligusia. Amegusia diplomasia ya uchumi, Mashariki ya Kati tunauza nyama Qatar, Oman, Kuwait; ni jambo jema, lakini ninachotaka kusema ni kwamba tusirudi nyuma, wala tusione woga, wala tusione aibu kusema sisi kama Taifa jambo hili hatulioni sawa, tunawaomba wakubwa kaeni muone jinsi ya kutatua matatizo haya. Si jambo baya wala si dhambi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na hapa ninakumbuka maneno ya Askofu Desmond Tutu wakati wa harakati za ukombozi Kusini mwa Afrika; alisema hivi; *If you are neutral in situations of injustice, you have chosen the side of the oppressor.* Kama unakaa kimya katika jambo ambalo wengine wanakandamizwa, maana yake wewe umechagua upande wa wale wakandamizaji ndiyo upande wako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi hatuwezi kuwa upande wa wakandamizaji, tunataka Mungu aendeleo kutoa baraka kwenye Taifa hili. Msimamo wetu toka wakati wa Mwalimu na mpaka leo haujabadilika, ni kwamba Wapalestina wamefika mahali wamekaliwa katika ardhi yao na kwamba ni lazima waachiwe ardhi yao. Huo ni msimamo ambao tumekuwa nao na hatujawahi kurudi nyuma katika msimamo huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawaomba hao wakubwa huko watafute namna ya kufanya mambo huko Mashariki ya Kati yaende vizuri badala ya kushuhudia dunia watu wanakufa kwa maelfu halafu sisi tunasema tunakaa kimya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu, tulikuwa na msimamo mkali hata juu ya Morocco ambayo ilikuwa

inaikalia Sahara ya Magharibi, na huo msimamo wetu hatujawahi mahali popote kuuondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninachotaka kusema ni kwamba katika jambo hili lazima tupaze sauti na tusione vibaya kama Taifa kusema kwamba hili hatuoni vizuri. Hatumshutumu yeyote, hatukai upande wowote, lakini hatuoni vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze sasa kuzungumzia hasa masuala yanayohusu diplomasia ya uchumi. Katika ukurasa wa 23 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia ushirikiano wa Tanzania na nchi za Afrika, na akaeleza kwa mtiririko; Kenya, Burundi, Msumbiji na nchi nyingine amezitaja nyingi. Lakini kwa bahati mbaya sikuona DRC Kongo ikiwa imetajwa, inawezekana zipo sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilichotaka kusema mimi natoka Kigoma Mjini, sisi jirani zetu pale ni watu wa DRC na hawa watu wa DRC wamechangia sana mzunguko wa fedha katika Mkoa wa Kigomana hii inatokana na nani, inatokana na ukweli kwamba watu wa DRC hasa Mkoa wa Kivu ambao tunapakana nao, huduma nyingi wanazipata kutoka nchini kwetu. Na hili ni eneo na fursa kubwa sana kwa sababu Mkoa wa Kivu una *population* ya watu karibu milioni sita, lakini umbali kutoka Mkoa wa Kivu kwenda Kinshasa ni zaidi ya kilometa 1,900 maana yake unatokana Kigoma, unapita Mtwara unaingia mpaka Msumbiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ya nchi ile bado hajawa mizuri sana, kwa hiyo huduma nyingi bado wanazitegemea katika nchi yetu, fursa hii tumeipoteza kwa sababu ya kutokutengeneza mazingira mazuri ya kibiashara ya sisi na DRC. Na hapa ningependa Mheshimiwa Waziri unisikilize vizuri, moja ya jambo ambalo limekuwa likilalamikiwa ni pamoja na *visa* kubwa kwa wafanyabiashara wadogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna *visa* ya dola 50 ambazo ni hela nyingi kwa mfanyabiashara mdogo anayetoka DRC Kongo kuja kufuata bidhaa ambazo anajua atazipata kutoka Kigoma, lakini sasa hivi kimeongezeka tena kitu kingine mbali na hiyo *visa* kila Mkongo anayeingia anatakiwa apimwe *covid* na kupimwa *covid* dola 25 sisi ndiyo tuna kiwango kikubwa cha kupima *covid* kuliko Kenya, kuliko Uganda, kuliko DRC yenyewe. Wenzetu wengine ni dola tano sisi dola 25 halafu tunasema tunataka tuvutie uhusiano wa kibiashara, haiwezekani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninachotaka Mheshimiwa Waziri utakapofika mahala unafanya majumuisho unisaidie, nini mkakati wenu katika soko kubwa hili la watu karibu milioni sita ambalo tunalitegemea, nini, mkakati wenu wa kupunguza gharama ya *visa* ili tuweze kufanya nao biashara vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hilo nilitaka kuzungumzia tumekuwa sisi ni mafundi wa kuanzisha uhusiano, nilitaka kuuliza hivi uhusiano wa sisi na Msumbiji tukaanzisha mpaka ile TAMOFA imekwenda wapi? imekufa au ipo na hawa Msumbiji ni ndugu zetu naweza nikasema ni ndugu zetu wa damu, tukishirikiana nao tunakuwa tuna uhakika tupo katika mikono salama, uhusiano huu umekwenda wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuzungumzia *diaspora* na uraia pacha; ibara ya 132 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi imezungumza namna ambavyo tutawashirikisha *diaspora* katika kusaidia suala la diplomasia ya uchumi na kusaidia uwekezaji katika nchi yetu, tumeeleza, siwezi kunukuu hapa nitachukua muda mrefu, lakini ipo kwenye ibara ya 132.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati tunazungumza kuwashirikisha sijui tunapata kigugumizi wapi cha uraia pacha na katika hili nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri utakapokuja kufanya majumuisho unisaidie nini kigugumizi cha uraia pacha? Tuna ndugu zetu, tena hawa mbali na

kuwa na wana mitaji kama alivyosema dada yangu hapa Mheshimiwa Ng'wasi muda mfupi, wengine wana-*technology*, wana maarifa, wakiyaleta hapa nchini tutanufaika, kigugumizi kinatoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilikuwa naomba sana, sana wakati tunazungumza diplomasia ya uchumi tuone jinsi ya kuwatumia *diaspora* kutusaidia katika suala la uwekezaji na maarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, narudia kukushukuru, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk atafuatiwa na mtoa hoja.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia na kutoa ufafanuzi wa hoja ambazo zimetolewa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniruzuku uhai na afya njema na kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Aidha, nichukue fursa hii kwa kipekee kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniadini na kwa kunitewa kwanza kuwa Mbunge na pili kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaahidi kuwa nitaitumikia nafasi hii kwa weledi na juhudi kubwa nikiongozwa na falsafa ya kutanguliza mbele maslahi ya Taifa na nitatumia uzoefu wangu wa muda mrefu katika diplomasia na uhusiano wa kimataifa kwa maslahi mapana ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kukushukuru wewe binafsi na Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza Bunge hili kwa umahiri, hekima, busara na umahiri mkubwa. Aidha, ninaomba kuishukuru Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa maoni na ushauri wao walioutoa kupitia taarifa iliyowasilishwa asubuhi hii. Hii ni Kamati makini kwani wajumbe wake wana uelewa mkubwa wa masuala ya kidiplomasia na hivyo wamekuwa wakitoa mchango mkubwa ambao umeendelea kusaidia kuboresha utendaji kazi wa Wizara na diplomasia ya nchi yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, Mbunge na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki kwa uongozi wake mahiri ndani ya wizara na ushirikiano mkubwa anao nipatia. *(Makofi)*

Pia ninamshukuru Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara na taasisi zote zilizochini yake kwa ushirikiano mkubwa ninaoupata katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuishukuru familia yangu kwa upendo na uvumilivu wao na kuendelea kuniunga mkono wakati wote nikitekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri nijielekeze katika kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Kwanza nitoe shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia na kutoa maoni na ushauri katika kikao hiki ambacho kimejadili hotuba ya bajeti ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, michango ya Waheshimiwa Wabunge wote tumeipokea, na ninaahidi kujumuisha katika utekelezaji wa mipango ya Wizara, naomba nitolee ufafanuzi wa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nichangie *issue* au hoja ya itifaki; hoja hii imeongelewa asubuhi hii kwa hisia kubwa, hapa bora nimtaje ni Mheshimiwa Jerry Silaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Wizara inasikitika sana na mapungufu yaliyojitokeza na ili kuepusha changamoto hiyo nakuhakikishia kwamba itifaki inazingatiwa katika shughuli zote za kitaifa ambazo zinawahusisha viongozi wetu wakuu, hususan viongozi na mhimili wa Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaandaa mkutano ambao utajumuisha *stakeholders* wote wanaohusiana na mambo ya itifaki na tutawajumuisha pia na Ofisi ya Bunge, Ofisi ya Waziri Mkuu, tutazungumza kwa pamoja ili kuboresha utendaji wa Serikali na kuimarisha uhusiano uliopo katika mihimili yote ya dola katika kuratibu shughuli za kitaifa. Na hiki kikao kitafanyika tarehe 14 mpaka 18 hapa Jijini Dodoma kwa ajili ya kujadili masuala haya ya kiitifaki ya viongozi na tunaahidi kwamba suala hili tutajitahidi lisitokee tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kukamilisha Sera ya Mambo Nje na kujumuisha masuala ya *diaspora*; Wizara ipo katika hatua za mwisho kukamilisha Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2021 pamoja na mambo mengine sera hiyo pia itatoa mwongozo wa utekelezaji wa masuala ya *diaspora* kiseru na kimkakati kwa manufaa mapana ya *diaspora*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umuhimu wa kujenga Ofisi ya Idara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Zanzibar ambayo ina hadhi, kwa sasa Wizara inamiliki jengo la Ofisi ambalo sasa hivi lipo katika ukarabati na ukarabati wake unaendelea kwa nguvu. Naona muda unakwenda sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa ufafanuzi hapa kidogo kuhusiana na *issue* ya Palestina ambayo imeongelewa na Wabunge hapa. Ni kweli kwamba hivi karibuni mgogoro kati ya Israel na Palestina umeongezeka na kusababisha madhara makubwa kwa pande zote mbili

ikiwemo vifo na uharibu wa miundombinu katika miji ya Gaza, Tel Aviv, Jerusalem na Ukingo wa Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania muda wote imekuwa ikilaani mapigano hayo, dhamira ya Tanzania ni kuona mgogoro huo unatatuliwa kwa njia ya amani na utulivu na usalama unashamiri. Tanzania haijakaa kimya kwenye suala hili, tumeendelea kushiriki na kushawishi Jumuiya za Kikanda na za Kimataifa kuchukua hatua zaidi na za pamoja ili kuona mgogoro huo unatatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa mantiki hiyo Tanzania inaendelea kuunga mkono maazimio ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika kuhusu mgogoro huo ambao unazitaka pande husika kuheshimu makubaliano ya kuwepo kwa nchi mbili ikiwa ni Palestina huru na Israel salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Tanzania haijabadili msimamo wake kutoka hapo awali na kuhusu msimamo wa Tanzania kuhusu Sahara Magharibi haujabadilika pia. Serikali yetu imeendelea kutambua haki ya msingi ya watu wa Jamhuri ya Kiarabu wa Demokrasia ya Sahrawi kujiamulia mambo yake wenyewe kupitia kura ya maoni na tunaendelea kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Umoja wa Mataifa kwa kushirikiana na Umoja wa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha ufunguzi wa ubalozi wa Morocco hapa nchini si ishara ya kubadili msimamo wetu, bali ni hatua ya kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia na kutoa fursa kujadili masuala mbalimbali ya ushirikiano ikiwemo suala la utatuzi wa mgogoro wa Sahara Magharibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze kidogo kuhusu ahadi ya msaada wa Falme za Kiarabu. Ni Wizara yetu kupitia ubalozi wake wa Abudhab imekuwa ikifanya juhudi kuhakikisha kwamba msaada wa fedha uliotolewa na mifuko hiyo miwili inapatikana mapema inavyowezekana. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba taratibu zote zimekamiliika kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na

kinachosubiriwa sasa ni *Khalifa Fund* kutoa fedha hizo ambazo ni dola za Kimarekani milioni mbili kila mwaka kwa muda wa miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kuhusu hospitali ya Wete mchakato unaendelea, ulikwama kutokana na *Covid*, lakini hii ni ahadi iliyotolewa na viongozi wa *UAE* na ahadi hii tunahakikisha kwamba inatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kuhusu barabara ya Chakechake hadi Wete tayari Serikali imeshasaini mkataba na *Saudi Fund* tarehe 19 Aprili, 2020 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Chakechake hadi Wete - Njia Kongwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine yaliyobakia tutayajibu na kuyawasilisha kwa Wabunge wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Balozi Mbarouk, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite mtoa hoja Mheshimiwa Liberata Mulamula, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru tena kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kutoa na kufanya majumuisho ya mjadala uliokuwa unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na kupitia kwako kumshukuru Mheshimiwa Spika kwa kuongoza na kusimamia mjadala wa bajeti yetu kwa umahiri sana. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kushiriki mjadala huu, maoni, michango na ushauri uliotolewa yataiwezesha na kuisaidia Wizara yangu kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba kuishukuru tena Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge na Wajumbe wote wa Kamati kwa kuipatia wizara yetu ushirikiano mkubwa na kwa michango yao ambayo mizuri sana, ambayo wameitoa katika mjadala huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba muda nilionao ni mfupi, lakini niwatambue sio kwa majina, lakini niwatambue na kuwashukuru kwa njia ya pekee Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja niliyoitoa leo asubuhi, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 25 wamechangia kwa kuzungumza na pia Waheshimiwa Wabunge wengine wamewasilisha michango yao kwa maandishi, naomba niwashukuru sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa zimejibiwa kwa ufasaha muda mfupi uliopita na Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, Mbunge, nichukue tu fursa hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa hoja zote na maoni ya Waheshimiwa Wabunge zilizotolewa zitazingatiwa na zimepokelewa kwa moyo mkunjufu na zitazingatiwa na Wizara katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ambazo hazitapata majibu ya kutosheleza katika hitimisho langu tutazijibu na tutaziwakilisha katika Ofisi ya Bunge kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze katika kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa; kwanza kabisa nitambue mchango wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nje, Ulinzi na Usalama. Maeneo waliyoyagusia ambayo mengi yao pia yamegusiwa na Wabunge, kubwa zaidi niseme ni suala la kuhusu majengo; kuhusu kuwekeza katika vitenga uchumi katika kujenga ofisi za balozi zetu na makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika mwaka wa fedha 2021Wizara imetenga shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kuendeleza viwanja na ukarabati wa majengo balozini. Hadi kufikia sasa Wizara ilitoa kazi ya usanifu na uandaaji wa mahitaji ya ukarabati wa majengo ya balozi mbalimbali kupitia kwa Mshauri Elekezi Chuo Kikuu cha Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari mshauri elekezi ameshawasilisha mchoro na makisio ya gharama kwa ajili na ukarabati wa majengo wa Balozi zifuatazo; moja ambayo imekuwa inasemeka muda mrefu sana ni Ubalozi wetu Mascut - Oman. Ujenzi wa jengo la Ubalozi na makazi ya Balozi Mascut ambao utagharimu shilingi trilioni 3.6 zimeshatengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Ubalozi wetu wa Nairobi ujenzi wa jengo la ubalozi shilingi trilioni 3.9 na pia Kinshasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi hii Wabunge waliongelea kuhusu ujenzi wa jengo la ubalozi na kitega uchumi Kinshasa DRC; fedha tayari imeshatengwa na pia, Moroni - Comoro kuhusu ujenzi wa jengo la ubalozi tayari pia fedha imetengwa karibu shilingi trilioni 1.8.

Vilevile Wizara inafanya ukarabati wa jengo la ofisi ya Mambo ya Nje ya Zanzibar kama ilivyoelezwa, shilingi bilioni tatu badala ya trilioni tatu samahani nilikuwa namaanisha bilioni sio trilioni, shilingi bilioni tatu. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, iliongelewa kuhusu jengo la ofisi yetu Zanzibar ambayo Naibu wangu ameieleza, lakini napenda nilihakikishie Bunge kwamba, ukarabati wa jengo hilo umeanza. Pamoja na ukarabati wa jengo la Ubalozi wetu Washington DC ambalo ukarabati wa jengo hilo unategemea utagharimu kiasi cha shilingi bilioni 5.8 na unatarajiwa kukamilika hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nieleze tena pia, kuna Mpango wa mwaka 2018/2032 wa ujenzi, ununuzi na ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi balozini ambapo Wizara inatenga fedha za maendeleo kwenye bajeti ya Wizara kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imeongelewa sana kwamba tumekuwa tunatenga hizi fedha kwenye bajeti, lakini hatupati, lakini napenda kushukuru Wizara ya Fedha imetuona. Wametenga karibu shilingi bilioni 20 ambazo zitasaidia kuweza kukarabati hayo majengo na kujenga mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba, Serikali ikamilishe mchakato wa kuandaa sera ya mambo ya nje; kama alivyoeleza Naibu Waziri wangu, hii rasimu imekamilika, kinachosubiriwa sasa ni kuweza kuridhiwa na mamlaka katika mwaka huu tutakuwa tumeikamilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, sera hii ina sehemu kubwa ya *diaspora* kwa hiyo, sera ya *diaspora* itakuwa sehemu ya Sera ya Mambo ya Nje. Nataka kuihakikishia Bunge Tukufu kwamba sera hii kwa kweli haitamaliza mwaka huu tutakuwa tumeimaliza. Hii ni kwa kutambua umuhimu wa *diaspora* katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu, masuala ya *diaspora* kwa kweli yanapewa kipaumbele na kama alivyosema Mheshimiwa Kimei, mimi nilikuwa mdau sana, nimekuwa mdau sana wa masuala ya *diaspora* na nitahakikisha kwa kweli kama sikutunguliwa suala la *diaspora* kwa kweli nitaipa umuhimu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na niseme pia kuhusu uraia pacha, hili ni suala lilishafanyiwa kazi kweli, iliyopo tu ni maamuzi ya kisera liweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya kwamba, Serikali iweke mpango mkakati wa kushughulikia changamoto ya muda mrefu ya uchakavu wa uhaba wa magari, hususani katika balozi zetu; naomba kukuhakikishia

kwamba changamoto hii tayari tumeishughulikia Wizara imepata kibali kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kununua magari 67 katika mwaka huu wa fedha. Tayari fedha zimeshatumwa kwenye balozi zetu 18nje, kuweza kununua magari na bado tunaendelea kufuatilia magari mengine ambayo tumeagiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeanza pia, kupeleka vituoni watumishi 137 katika kipindi hiki. Tumesikia kilio cha Waheshimiwa Wabunge kuhusu balozi zetu kwamba hazina watumishi.

Sasa mimi nitumie pia nafasi hii kuweza kuishukuru Wizara ya Fedha. Wizara ya Fedha imetuwezesha, tutapeleka watumishi 137 katika mabalozi zetu na tumezingatia weledi, tumezingatia uzoefu na tumezingatia ujuzi, kwa hiyo, sio kupeleka tu. Lakini kwa kweli tutakuwa tumeziimarisha balozi zetu na kila tunapopata rasilimali zaidi ya fedha, tutakuwa tunawaongezea uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, iliongelewa asubuhi hapa pia kwamba Wizara yetu iweze kufuatilia baadhi ya Wizara za kisekta, ambazo zikifanya kazi kwa juhudi na ufanisi zitaongeza pato la Taifa, kwa kusimamia uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo ambayo yana soko kubwa nje ya nchi kama vile, nyama ya mbuzi katika masoko ya nchi za Kiarabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaambie Wabunge kwamba, ushauri umepokelewa na unazingatiwa, lakini pia ulishaanza kufanyiwa kazi. Niwashukuru pia Mawaziri wenzangu kutoka hizi Wizara za kisekta, tumekuwa na ushirikiano wa karibu, tukiwa na ugeni tunakaa pamoja kimkakati na kuweza kuweka yale maslahi, ambayo kila sekta inaona inaupa kipaumbele, kwa hiyo, tunafanya kazi kwa karibu sana na sekta zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pia katika ushirikiano huu Wizara ilifanikisha upatikanaji wa vibali kwa kampuni nane za Tanzania kuuza minofu ya samaki aina ya sangara katika nchi ya Saudi Arabia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Serikali kuzidisha juhudi kusimamia balozi zetu za nje, kutangaza fursa za kitalii na vivutio mbalimbali zilizopo nchini kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, tumepokea ushauri huu na kwamba utazingatiwa, lakini niwahakikishie kwamba tayari Balozi zetu kwa kweli zinafanya mambo mengi makubwa sana katika kuvutia utalii na kama mtakumbuka tulieleza hapa asubuhi kwamba mathalani balozi zetu zimepeleka sampuli za zao za korosho, lakini pia ubalozi wetu wa Malaysia umeweza kufanikisha kwamba ndege ya Malaysia inaweka matangazo ya utalii wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja mbalimbali kuhusu Wizara iendelee kuwapa viwanja mabalozzi wa nje hapa Dodoma, kwa ajili ya kujenga ofisi na makazi ili balozi zihamie hapa. Napenda kukufahamisha kwamba Serikali tayari ilishatoa viwanja Jijini Dodoma kwa balozi zote na tayari ilishatoa hati kwa balozi zote zinazowakilishwa nchi zao hapa nchini. Kwa hiyo, sisi ni kuhamasisha kwamba wajenge ili waweze kuhamia makao makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, iliulizwa pia kwamba Wizara ihakikishe inapeleka taarifa za kutosha ubalozini kuhusu mazao na fursa za biashara ili kufanikisha utekelezaji wa diplomasia wa uchumi. Kama nilivyoeleza hapo awali kwamba Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara za kisekta na taasisi za biashara za sekta binafsi nchini kutafuta masoko ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia imeshiriki pamoja na *TANTRADE* katika maonesho mbalimbali ya kibiashara. Kwa hiyo, balozi zetu zimepeleka sampuli za zao la korosho kwa ajili ya kuwasilisha katika nchi mbalimbali ikiwemo Vietnam, India na China. Aidha, balozi zetu zote zimeendelea kutangaza bidhaa za kimkakati zinazopatikana Tanzania. Vilevile Wizara imeendelea kuhamasisha taasisi za Serikali zinazohusika na biashara, kushirikiana na sekta binafsi kushiriki katika maonesho mbalimbali ya Kimataifa, ambayo yanatoa fursa kwa nchi kutangaza bidhaa zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia, imeendelea kufungua *of course* Balozi mpya kama ilivyoelezwa na mwenzangu. Lakini nisisitize pia kwamba kwa kipindi hiki Wizara ipo katika hatua za mwisho kufungua *consul*/kuu huko Guangzhou nchini China, niwahakikishie kwamba tuko katika hatua za mwisho. Pia Lubumbashi Jamhuri ya Demokrasia ya Congo baada ya kupata vibali kutoka katika nchi husika, maana yake katika kufungua hizi *consul* au balozi, lazima mpate pia kibali kutoka kwenye nchi zinazohusika. Hamuwezi kwenda mnaingia tu mnasema tumefika tunaanzisha na wenyewe inabidi watukubalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama sisi kwa upande wetu tumeshamaliza mchakato huo, lakini tunasubiria hizo nchi husika na wenyewe waweze kuturuhusu wamalize mchakato wao, kusudi tuweze kufungua hizi balozi. Nina imani haitapita mwaka huu kabla hatujazifungua hasa Guangzhou na Lubumbashi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine *of course* yameongelewa kuhusu kutangaza Kiswahili na kupeleka walimu na kufundisha lugha hiyo nje ya nchi, tayari mikakati hii imefanyika. Balozi zetu zimejipanga, tayari vyyo vikuu vya nchi za *SADC* karibu nyingi sana zimeanza mtaala/ *curriculum* ya Kiswahili. Kwa hiyo, sasa iliyopo ni sisi huku wenyewe kujipanga na walimu wakaweza kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana nilikuwa juzi Afrika Kusini wameniambia Afrika Kusini tayari vyyo vyao vimeshaanzisha tayari *curriculum* ya Kiswahili. Botswana imeanza, Lesotho inaanza, lakini shida ni kwamba walimu wako wapi. Kwa hiyo, sisi tunaomba tushirikiane na sekta zote zinazohusika tuweze kuwapata walimu waende kufundisha Kiswahili kwenye hizo nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kuhusu hili suala la Wizara kwamba iweke mkakati *of course* niliyosema ya kutangaza utalii nimeshaiongelea. Lakini niseme pia kwamba juhudi zinaendelea kwa mfano, Ubalozi Tanzania nchini Malaysia kama nilivyosema imeshawishi Kampuni ya Ndege

ya *Lion Group Air* ya nchini Indonesia inayomiliki zaidi ya ndege 350 kuweka video kwenye ndege zao zinazoonesha utalii wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimsikia Mbunge hapa nakumbuka mimi nilikuwa mmoja wa mwanachama wa Mozambique na Tanzania, kile chama kitafufuliwa Mheshimiwa Mbunge, maana mimi nilikuwa mjumbe, nilikuwa kwenye bodi lakini kwa uhusiano wetu wa Mozambique tena uko karibu sana na kutokea na yale yanayotokea Mozambique nadhani hiko chama kinahitajika sana, kutoa msukumo na kuweza kusimamia yanayoendelea katika nchi ya rafiki yetu hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nikuhakikishie hayo ya DRC hatuna tatizo kabisa kama ninavyosema tunamalizia mchakato wa kufungua hiyo *consul* kuu nchini Lubumbashi kwa ajili ya kuendeleza mahusiano ya biashara, lakini najua tena kuna mambo mengi kati ya DRC na Kigoma. Kwa hiyo, tunayatambia na tuna *consul*/kule ya DRC, kwa hiyo, wanataka nao kuanzisha mahusiano hayo. Kwa hiyo, kwa kweli tutaendeleza na kwa mchango wenu kwa kweli mimi naona kwamba kuna fursa nyingi sana ambazo saa nyingine wengi hawazifahamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui nina muda gani, lakini naomba kwa hitimisho niruhusu kwamba baada ya maelezo hayo, ninaliomba Bunge lako Tukufu lipitishie na kuunga mkono bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2021/2022 ili niweze kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, tunapende kutekeleza ipasavyo masuala yote yaliyoainishwa katika Sura ya Saba ya Ilani ya CCM yam waka 2020/2025 inayohusu mambo ya nje na ushirikiano wa kimataifa.

Pili, tuko tayari kutekeleza majukumu ya msingi ya Wizara kama ambavyo Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mkazo aliouweka katika hotuba yake hapa Bungeni tarehe 22 Aprili,

2021 ambapo ndio msingi wa mpango wa bajeti niliowasilisha. Vipaumbele hivyo ni pamoja na kuimarisha na kukuza uhusiano na mataifa mengine pamoja na jumuiya za kikanda na taasisi za kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tumejipanga kuimarisha utendaji kazi wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na balozi zetu zote zilizoko nchi mbalimbali. Yale yote ambayo tumepata hapa leo kwa kweli itasaidia sana katika kujipanga na kuweza kuimarisha utendaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, tutaendelea kushirikiana na Wizara za kisekta na sekta binafsi katika kutangaza vivutio vyetu vya utalii, kuvutia uwekezaji na kutafuta masoko ya bidhaa zetu nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, tutaendelea kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za Kimataifa ikiwemo ushiriki wa Tanzania kwenye kulinda amani duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba yale yote ambayo wameyasema tumeyachukua hasa yale ambayo wametaka kwa mfano, Zanzibar kwamba tuwe tunawapa taarifa mapema kuhusu ushiriki wao katika hii mikutano ya kikanda, lakini pia kuweza kuangalia nafasi za ajira watu wetu waweze kufanya na wenyewe kazi nje, lakini pia kuweza kuwapeleka watu wetu waweze kupata ujuzi na uzoefu kutoka katika nchi za nje hasa katika mahusiano yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Wizara yangu imeongeza kasi ya kutekeleza majukumu yake kwa kufanya maboresho makubwa ili kufikia malengo yake pamoja na matarajio ya Watanzania. Hivyo kwa timu niliyonayo na kikosi nilichoongezewa na Mheshimiwa Rais, naomba Bunge lako lituunge mkono na kutupitishia bajeti niliyoiomba ili tukachape kazi, kazi iendelee. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa lamuliwe*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa na mkono na kwa mujibu wa taratibu zetu tutaendelea. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**NAIBU SPIKA:** Kamati ya Matumizi.

#### **KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti tunaanza na kitabu cha pili, matumizi ya kawaida, Fungu 34 ukurasa 184 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

#### **KAMATI YA MATUMIZI**

#### **KITABU CHA PILI**

#### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **FUNGU 34 – WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI**

Kifungu 1001 – *Administration and Human  
Resource Management*.....Sh. 12,522,132,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, fungu hili ndilo lenye mshahara wa Waziri na nina majina ya Waheshimiwa Wabunge wawili hapa wanaotaka ufafanuzi. Nataka kupata

hisia kwamba pengine ufafanuzi uliombwa kabla hoja haijahitimishwa, lakini wacha tuwasikie Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nilitaka nipate ufafanuzi na kama nisipopata majibu mazuri basi nitaondoka na shilingi ya Mheshimiwa Waziri.

Katika kutekeleza sera ya diplomasia ya uchumi ni vizuri sana watanzania ambao tuko ndani na watanzania ambao wako nje, wakaweza kushirikishwa pamoja ili tuweze kutekeleza hii sera ya uchumi. Sasa katika watanzania ambao wako nje hawawezi kushiriki kwenye huu uchumi wa diplomasia ya uchumi kwa sababu ya vikwazo ambavyo vimewekwa na Serikali kutokana na kwamba hawana uraia pacha.

Sasa nilitaka majibu ya Serikali ili niweze kujua imejipangaje kutokana na hili suala kwa sababu kwa kipindi cha miaka mitano 2015 hadi 2020 tumekuwa tukilizungumzia hili jambo lakini mpaka sasa hivi halijaweza kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.  
(Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kuhusu hili suala kama nilivyoelezea kwa kweli tumelifanyia kazi sana na wakati umefika Serikali itachukulia uamuzi ya kiseru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba ni suala ambalo pamoja na kwamba sisi tunaliratibu lakini linagusa Wizara mbalimbali. Ni suala la Uhamiaji, ni suala la Usalama, linazingatia mambo mengi. Lakini nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hili suala sasa kwa kweli tutalifanyia mkakati na *Inshallah* mambo yakienda vizuri litaletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuhakikisie kwamba iko mikono mizuri na imefanyiwa kazi sana, sana, sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bonnah naona ameridhika amekaa. Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda. Aaah, Mheshimiwa Bonnah Kamoli naona umesimama.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema wanalifanyia mkakati na ndio majibu ambayo tumekuwa tukiyapata muda wote. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu waniunge mkono ili tuweze kulijadili.

**MWENYEKITI:** Hawajafika Wabunge kumbi.

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wametimia.

**MWENYEKITI:** Kwa sababu akishatoa hoja na yeye anakuwa amesimama, kwa hiyo naangalia mara moja waliosimama ni kina nani siwezi kuwa nasubiria watu waanze kusimama Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mmesimama baada ya muda kwa sababu nikiwa naangalia huwa natazama. Hapa alisimama mmoja tu Mheshimiwa, hapa alisimama mmoja tu, Mheshimiwa Taska Mbogo na hapa walikuwa wamesimama Wabunge sita kwa hiyo nipo vizuri. Niko vizuri hawajafika sita Mheshimiwa Bonnah Kamoli. Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda. (*Makofi*)

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mjadala wa bajeti hii nilizungumzia suala la *visa* ya Congo Dola 50 na ambayo sasa hivi zaidi ya hiyo dola 50 na sasa hivi kumekuwa na dola 25 ambazo zinatozwa kama kipimo cha *Covid* kwa wageni wanaoingia.

Sasa nilikuwa nimetoa hoja ya kuona Wizara ya uwezekano *either* ya kupunguza au kuifuta hii ili kujenga mazingia mazuri ya kibiashara katika diplomasia hii ya uchumi

tunayokweda nayo. Kwa bahati mbaya Mheshimiwa Waziri wakati anajibu hakulielezea jambo hili. Mimi sikuridhika kwa hiyo nina kusudio kutoa shilingi iwapo sitaridhika. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri naona hapo yametajwa mambo mawili moja ni dola 50 ya *visa* halafu dola 25 ya kupima *Covid*.

Sasa Mheshimiwa Waziri wewe subiri ya kwako ya *visa*, ngoja aanze Waziri wa Afya atoe ufafanuzi kuhusu hii dola 25 inayolipwa kwa ajili ya kupimwa *Covid*.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

**MBUNGE FULANI:** Simbachawene.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli dola 25 inalipwa kwa ajili ya kupima *Covid* na hii tuliitoa kwenye *travelers Advisory Note* yetu Na. 7 ambayo ilitoka hivi karibuni na hii ilitokana kwamba kile kipimo ambacho unakuwa umepimwa huko cha *RTPCR* unapewa, unaambiwa sasa safari, kule unalipa labda dola 100 kama matakwa ya mashirika ya ndege unayokwenda kusafiria. Ukifika huku nchini haina maana kwamba ikichukuliwa damu unaweza ukawa salama na hadi sasa kati ya hao waliopimwa kuna watu wamekutwa na maambukizi ikabidi wawekwe kwenye sehemu salama ya uangalizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo katika *spirit* ya kuilinda hii nchi yetu na huenda ndio maana Mungu ametuwezesha mpaka sasa hivi tupo salama. Na hii fedha ndiyo inayosaidia kuwa na uendeleo wa zile huduma za kununua *supplies* ili tuzidi kuwapima wengine. Lakini tunapokea maoni kama tunavyoyapokea hapa na hivi karibuni kutakuwa na kikao cha *East African Community* kujadili masuala haya, tuone tunaboresha vipi. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Kilumbe huenda nikasahau nitakupa nafasi nyingine kama utakuwa hujaridhika na huo ufafanuzi Mheshimiwa Waziri hoja ya *visa*. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu hoja ya Mheshimiwa Ng'enda, juu ya *visa* za kutokea Congo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma udhibiti huu na bei hii ya dola 50 ilikuwa imewekwa kwasababu mbalimbali ikiwemo sababu za kiusalama. Lakini kwa sasa linaweza kuzungumzika na kwa hii ya dola 25 ni wale ambao wanapita *on transit* ndio imewekwa dola 25. Kwa hiyo, nikubaliane tu kwamba kwa kweli kwa kuiangalia ni kubwa, lakini kwa mazingira tuliyopita nayo huko nyuma na Congo mnavyofahamu ilibidi tufanye hivyo ili kudhibiti, lakini kwa sasa inaweze kuzungumzika na nataka nikuhakikishe kwamba tunaweza tukafanya marekebisho. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri yeye amesema 50 nakusikia unasema 25, 25 inahusu kupima *Covid*. Lakini *visa* ni dola 50 sio dola 25. Ama mimi ndio sijaelewa.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, upo sahihi, isipokuwa yeye ameongeza kitu kingine *visa* ya *transit*. Hiyo ya dola 50 ni ya wale wamaokuja nchini na kukaa hapa wale wanaopita ndio dola 25 ambayo mimi haikuwa *issue* yangu.

**MWENYEKITI:** Sawa sasa rudi kwenye ile dola 50 ambayo ni hoja yake yeye ya wale wanaokuwa hapa nchini.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio nilivyosema kwamba tutajaribu kuiangalia. Lakini ilikuwa hivyo na ni kweli ipo hivyo na sababu ni hizo nilizosisema.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilumbe naona umeridhika na maelezo.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa lugha yenyewe haijitoshelezi, lakini naomba nikubaliane na Serikali kwamba tutaliangalia na haina muda, haina wakati, lakini niseme kwamba wacha nikubaliane na Serikali kwa sababu bado tu wote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afya nadhani yeye amesema watakakuwa na kikao hivi karibuni na Mheshimiwa Waziri amesema watalingalia kwa maana ya sasa wamelisia kwamba ni hoja nzito na sasa wapate muda wakalitazame. Lakini nadhani kwa michango yote iliyotolewa na Wabunge siku ya leo ni vizuri kuangalia majirani zetu, sisi tumewazidi nini na wao wanadai kiasi gani, ili tusije vile vitu ambavyo wote tuko navyo wao wakidai kidogo basi mtu anakwenda huko badala ya sisi tukiwa tunadai kiasi kikubwa.

Hata kwenye suala hili la Afya ni muhimu kuilindi nchi yetu lakini tutazame kwa sababu mazingira ya kupimwa ni hayo hayo na kama ni kipimo hicho hicho. Kwa hiyo, na sisi tuangalie wanadai kiasi gani ili sisi tusipoteze watu sasa wakawa wanakwenda kupita safari ndefu kumbe wangeweza kupita hapa nchini na tukaweza kufanya nao biashara.

Waheshimiwa Wabunge hawa ndio waliokuwa wanataka ufafanuzi. Kifungu kinaaafikiwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

|                                                    |                  |
|----------------------------------------------------|------------------|
| Kifungu 1002 - Finance and Accounts Unit.....      | Sh.1,103,292,000 |
| Kifungu 1003 - Foreign Affairs Office Zanzibar.... | Sh.1,018,886,000 |
| Kifungu 1004 - Policy and Planning Unit.....       | Sh.1,508,048,000 |
| Kifungu 1005 - International Cooperation.....      | Sh.996,182,000   |
| Kifungu 1006 - Europe and America.....             | Sh.962,699,000   |
| Kifungu 1007 - Asia and Australia.....             | Sh.867,892,000   |
| Kifungu 1008 - Africa.....                         | Sh.1,864,648,000 |
| Kifungu 1009 - Regional Cooperation.....           | Sh.991,900,000   |
| Kifungu 1010 - Protocol.....                       | Sh.4,632,140,000 |

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

|                                                                                      |                   |
|--------------------------------------------------------------------------------------|-------------------|
| Kifungu 1011 - <i>Legal Services Unit</i> .....                                      | Sh.2,125,698,000  |
| Kifungu 1012 - <i>Government Communication Unit</i> .....                            | Sh. 515,426,000   |
| Kifungu 1013 - <i>Middle East Division</i> .....                                     | Sh. 726,480,000   |
| Kifungu 1014 - <i>Internal Audit Unit</i> .....                                      | Sh. 546,044,000   |
| Kifungu 1015 - <i>Procurement Management Unit</i> .....                              | Sh. 545,012,000   |
| Kifungu 1016 - <i>Information and Communication Technology Unit</i> .....            | Sh. 599,784,000   |
| Kifungu 1017 - <i>Diaspora Engagement and Opportunity</i> .....                      | Sh. 638,911,000   |
| Kifungu 1018 - <i>Economic Infrastructure Social Support Services Division</i> ..... | Sh. 789,484,000   |
| Kifungu 1019 - <i>Political, Defence and Security Affairs</i> .....                  | Sh. 661,628,000   |
| Kifungu 1020 - <i>Trade, Investment and Productive Sector Division</i> .....         | Sh. 858,764,000   |
| Kifungu 2001 - <i>Embassy of Tanzania - Addis Ababa</i> .....                        | Sh. 2,581,637,000 |
| Kifungu 2002 - <i>Embassy of Tanzania - Berlin</i> .....                             | Sh. 3,888,400,000 |
| Kifungu 2003 - <i>Embassy of Tanzania - Cairo</i> .....                              | Sh. 2,563,179,000 |
| Kifungu 2004 - <i>Embassy of Tanzania - Kinshasa</i> .....                           | Sh. 3,792,194,000 |
| Kifungu 2005 - <i>High Commission of Tanzania - Abuja</i> .....                      | Sh. 4,546,362,000 |
| Kifungu 2006 - <i>High Commission of Tanzania - London</i> .....                     | Sh. 3,905,063,000 |
| Kifungu 2007 - <i>High Commission of Tanzania - Lusaka</i> .....                     | Sh. 1,727,067,000 |
| Kifungu 2008 - <i>High Commission of Tanzania - Maputo</i> .....                     | Sh. 2,271,753,000 |
| Kifungu 2009 - <i>Embassy of Tanzania - Moscow</i> .....                             | Sh. 4,038,220,000 |
| Kifungu 2010 - <i>High Commission of Tanzania - New Delhi</i> .....                  | Sh. 3,522,804,000 |
| Kifungu 2011 - <i>Permanent Mission to The UN - New York</i> .....                   | Sh. 5,262,145,000 |
| Kifungu 2012 - <i>High Commission of Tanzania - Ottawa</i> .....                     | Sh. 3,138,054,000 |
| Kifungu 2013 - <i>Embassy of Tanzania - Paris</i> .....                              | Sh. 3,660,648,000 |

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

|                                                                        |                   |
|------------------------------------------------------------------------|-------------------|
| Kifungu 2014 - <i>Embassy of Tanzania - Beijing</i> .....              | Sh. 3,763,808,000 |
| Kifungu 2015 - <i>Embassy of Tanzania - Rome</i> .....                 | Sh. 3,815,474,000 |
| Kifungu 2016 - <i>Embassy of Tanzania - Stockholm</i> .....            | Sh. 3,991,557,000 |
| Kifungu 2017 - <i>Embassy of Tanzania - Tokyo</i> .....                | Sh. 3,339,629,000 |
| Kifungu 2018 - <i>Embassy of Tanzania - Washington</i> .....           | Sh. 3,761,579,000 |
| Kifungu 2019 - <i>Embassy of Tanzania - Brussels</i> .....             | Sh. 4,785,384,000 |
| Kifungu 2020 - <i>Permanent Mission to The UN - Geneva</i> .....       | Sh. 5,974,498,000 |
| Kifungu 2021 - <i>High Commission of Tanzania -Kampala</i> .....       | Sh. 2,393,478,000 |
| Kifungu 2022 - <i>High Commission of Tanzania - Harare</i> .....       | Sh. 2,219,787,000 |
| Kifungu 2023 - <i>High Commission of Tanzania - Nairobi</i> .....      | Sh. 4,575,194,000 |
| Kifungu 2024 - <i>Embassy of Tanzania - Riyadh</i> .....               | Sh. 3,246,519,000 |
| Kifungu 2025 - <i>High Commission of Tanzania - Pretoria</i> .....     | Sh. 3,528,698,000 |
| Kifungu 2026 - <i>Embassy of Tanzania - Kigali</i> .....               | Sh.1,298,420,000  |
| Kifungu 2027 - <i>Embassy of Tanzania - Abu-Dhabi</i> .....            | Sh. 4,941,369,000 |
| Kifungu 2028 - <i>Embassy of Tanzania - Bujumbura</i> .....            | Sh. 2,071,617,000 |
| Kifungu 2029 - <i>Embassy of Tanzania - Muscat</i> ..                  | Sh. 2,793,286,000 |
| Kifungu 2030 - <i>High Commission of Tanzania - Lilongwe</i> .....     | Sh. 1,712,641,000 |
| Kifungu 2031 - <i>Embassy of Tanzania - Brasilia</i> .....             | Sh. 3,583,555,000 |
| Kifungu 2032 - <i>High Commission of Tanzania - Kuala Lumpur</i> ..... | Sh. 2,630,509,000 |
| Kifungu 2033 - <i>Embassy of Tanzania - The Hague</i> .....            | Sh. 3,324,992,000 |
| Kifungu 2034 - <i>Embassy of Tanzania - Moroni</i> ....                | Sh. 2,407,549,000 |
| Kifungu 2035 - <i>Embassy of Tanzania-Kuwait</i> .....                 | Sh.1,897,477,000  |



|                                                            |                   |
|------------------------------------------------------------|-------------------|
| Kifungu 2036 - <i>Embassy of Tanzania - Algiers</i> .....  | Sh. 2,756,857,000 |
| Kifungu 2037 - <i>Embassy of Tanzania - Ankara</i> ....    | Sh. 3,663,312,000 |
| Kifungu 2038 - <i>Embassy of Tanzania - Khartoum</i> ..... | Sh. 2,365,965,000 |
| Kifungu 2039 - <i>Embassy of Tanzania - Seoul</i> .....    | Sh. 5,442,978,000 |
| Kifungu 2040 - <i>Embassy of Tanzania - Tel-Aviv</i> ....  | Sh. 3,749,010,000 |
| Kifungu 2041 - <i>Embassy of Tanzania - Doha</i> .....     | Sh.3,139,275,000  |
| Kifungu 2042 - <i>Embassy of Tanzania - Havana</i> ..      | Sh. 3,075,214,000 |
| Kifungu 2043 - <i>Embassy of Tanzania - Windhoek</i> ..... | Sh. 2,944,231,000 |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda Kitabu cha Nne, Matumizi ya Maendeleo.

## KITABU CHA NNE

### MIPANGO YA MAENDELEO

#### FUNGU 34 – WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI

Kifungu 1004 - *Policy and Planning Unit*.....Sh.13,500,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**NAIBU SPIKA:** Bunge linarejea.

*(Bunge Linarejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mtoa hoja Taarifa.

## T A A R I F A

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 naomba kutoa Taarifa kuwa Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwamba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono na sasa nitawahoji. *(Makofi)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Yalipitishwa na Bunge)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Tukae Waheshimiwa Wabunge.

Nichukue fursa hii kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wao wote kwa kazi nzuri wanayoifanya na nimesikia Wabunge wengi hapa wakiwapongeza.

Tunawapongeza pia kwa kuleta bajeti nzuri ambayo Bunge imepitisha kama mlivyoomba.

Wakati mkieleza kuhusu hoja yenu hii, mmeeleza mambo mengi na Wabunge wana matamania pia mengi nayo yameshaelezwa. Mengine mmeyatolea ufafanuzi lakini hata yale ambayo hamkupata fursa ya kupata ufafanuzi ni dhahiri mtaleta kwa maandishi kama mlivyoahidi.

Mengine waliyoyatoa ni ushauri, kwa hiyo, si kwamba yanahitaji ufafanuzi lakini ni ushauri ambao tunaamini mtaufanyia kazi katika kuboresha mahusiano yetu sisi kama nchi na nchi nyingine huko nje. Lakini pia Wabunge wamesisitiza sana kuhusu diplomasia ya kiuchumi.

Kwa hiyo, ni vizuri na ninyi mkalichukua kwa uzito huo ambao Wabunge wameeleza. Tunaamini kwa sababu Bunge limeidhinisha fedha kama mlivyoomba mtaenda kuyafanyia kazi yale yote mliyoahidi kwenye bajeti yenu kwamba mtayafanyia kazi na tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa hizo ahadi mlizozitoa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo la wageni ambao tuko nao humu Bungeni mchana huu ama sasa imeshakuwa jioni, lakini wageni hawa ni wanafunzi 67 ambao ni Wanachama wa Jumuiya ya Vijana wa Chama vha Mapinduzi (UVCCM) Kata ya Kikuyu Kaskazini kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Katibu wa UVCCM Kata ya Kikuyu Kaskazini Ndugu Isaka B. Ngongi, karibuni sana vijana wetu. Nafikiri mmepata fursa ya kujifunza mambo mengi namna Bunge linavyoendesha kazi. *(Makofi)*

Sasa kabla sijasimama hapa, walisimama Waheshimiwa Wabunge wawili wakiomba Mwongozo nitawapa dakika chache, watoe maelezo yao ambayo Kikanuni inavyoonekana pengine, siku ya leo katika uendeshaji kuna mahali Kanuni imevunjwa au kama sio Kanuni basi wanataka kujua kama hilo jambo linaruhusiwa ama haliruhusiwi.

Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Manyanya.

### MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JAQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaomba katika Mwongozo huu, Mwenyezi Mungu aniongoze. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Amin.

**MHE. JAQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 68(7) inayohusu jambo ambalo limetokea leo hii Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo katika *session* ya asubuhi kuna Mbunge mwanaume alisimama ndani ya Bunge lako Tukufu ambaye alitoa Mwongozo dhidi ya Mbunge mwanamke, ambaye alielekeza kwamba amekaa upande wa kulia kwake na amevaa *blouse* ya njano. Akisema kwamba huyo Mbunge amevaa mavazi ambayo hayaruhusiwi na hayafai katika Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa sina nia ya kutokuheshimu maamuzi yaliyofanywa na Spika juu ya Mwongozo wake, lakini niseme tu mimi niliyesimama hapa pia ni Mjumbe wa Baraza Kuu UWT Taifa, ambaye nimechaguliwa na Wabunge wanawake ili kuwawakilisha wanawake wenzangu. Kwa misingi hiyo, jambo lolote linalotokea linalohusu labda ukatili wa kijinsia kwa mwanamke aidha, unyanyasaji, aidha, udhalilishaji, ninapaswa kusimama kama kiongozi ambaye nimepewa dhamana na wanawake wenzangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo, jambo lililotokea leo imeonesha kwamba mtoa hoja kwamba Mbunge yule hakuwa sawa, lakini niseme tu kwamba alimdanganya Spika na kwa mazingira yalivyokuwa Spika alikuwa kwenye Kiti chake na ilikuwa sio rahisi Spika

akamuambia Mbunge huyo kwamba tokeza hapa mbele tuone vazi ulizovaa kama ni sahihi au sio sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, busara za Mheshimiwa Spika, zilimuongoza kumueleza kwa utaratibu kabisa kwamba kama ndivyo basi huyo Mbunge atoke aende akabadilishe nguo. Lakini ukweli ni kwamba Mbunge huyu nguo aliyovaa ni nadhifu, Mbunge huyu nguo aliyovaa ni ya heshima na Mbunge huyu kimsingi mavazi yake siku zote ni mazuri na yuko vizuri. Ana heshimu kila mtu na anajiheshimu yeye mwenyewe na anaheshimu kazi yake na nafasi yake ya Kibunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo,....

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka Kiti chako...

Mheshimiwa Naibu Spika,...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar anaomba Mwongozo hakuna Taarifa kwenye Mwongozo. Mheshimiwa Jacqueline malizia. (*Makofi*)

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, huyu binti aliyedhalilishwa siku hii ya leo, kwanza ni kijana mdogo, lakini ni mwakilishi wa wananchi wa Jimbo. Sasa nyuma yake ana wananchi ambao leo hii wamepata taharuki kubwa sana katika Jimbo lake kwa jambo ambalo sio la kweli.

Sasa mimi ninaomba Mwongozo wako ili kesho na kesho kutwa jambo hili lisiweze kurudiwa la uonevu wa aina hii kwa sababu katika mageti yetu yote, wapo ma-*matron* ambao ndio wanatutazama tunapoingia ndani ya Bunge, wanajiridhisha na wanaturuhusu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba mwongozo wako katika hili kwamba huyu Mheshimiwa Mbunge ambaye amemdhallisha Mbunge mwenzetu mwanamke kwanza aombe radhi, aombe radhi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tunampa pole Mbunge mwenzetu ambaye amefanyiwa kitendo hicho. Leo hii kila mitandao inazungumza jambo hilo kwamba binti huyu ameonewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kuwasilisha ili huyu Mbunge aombe radhi, lakini pia naomba mwongozo wako katika hili inakuwaje. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kwa rejea mdogo wangu nadhani ametumia Kanuni za zamani, lakini mimi nisisitize juu ya suala hilo kwa Kanuni ya 76. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa jambo lililonifanya nizungumze mimi mtu mzima leo ni juu la suala hilo lililotokea. Katika jambo lililotokea leo asubuhi baada ya kuona hali iliyotokea, ilibidi nifuatilie kwa karibu sana kwenye mtandao, hivi hiyo nguo ilikuwaje, hali halisi ikoje, baadaye niliishia kusononeka, nilisononeka kwa nini! Vijana kama hao sisi wenyewe tumesema vijana waingie Bungeni, lakini hatutegemei kijana aingie Bungeni amevaa bugaluu lile tuliokuwa tunavaa sisi zamani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana lazima wachukuliwe kwa ujana wao ili mradi hizo nguo wanazovaa ziwe na heshima yake, hata jana wakati tunapitisha bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Sanaa limezungumzwa jambo hili tena wakaenda mbali zaidi mpaka wakasema jamani waacheni hata vijana wapige kiki zao. Sasa ile haikuwa kiki ilikuwa ni vazi nadhifu la kijana kabisa, kwa dhati mimi sitegemei wote sisi tutavaa vitenge, sitegemei wote sisi kila

siku tutaamka umevaa dera, kila mtu na utamaduni wake ili mradi liwe vazi la heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na hata kuna siku nilikuwa kwenye kituo cha redio moja wapo nilikuwa naongelea kwamba tunapowapokea sasa hawa vijana kuingia Bungeni kuna mambo ya kuwachukulia, kuna mambo ya kuona wao ni vijana siyo kwamba maadamu ameingia Bungeni basi ghafla yeye ameshakuwa mtu mzima kama sisi, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi labda pengine niseme tu kwamba kuomba radhi ni sawa, lakini mimi ningeshauri kwa sababu ya mazingira ya kiutu uzima pengine na yeye aliyetoa hoja kwa sababu ya uzoefu wake alitegemea atuone wote tuko vile, pengine siyo lazima sana tukamuamsha wewe omba radhi, lakini la msingi tu tuone kwamba jambo lililotendeka leo lilikuwa kwa namna moja au nyingine siyo la haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi naomba Mwongozo wangu ni huu. Kutokana na hayo tuliyoyazungumza ikijitokeza tena mambo kama haya yanajirudia rudia tena kwa kuwagusagusa wanawake, maana yake imeshakuwa sasa ni mchezo. Imekuwa ni mtindo sasa humu ndani anaweza akatokea mtu akamtukana mwanamke tusi kubwa yapo hayo, yapo! Anaongea kama utani, lakini unakuta ametaja mpaka viungo vya mwanamke humu humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hatuwezi kuendekeza tabia hizi. Tunawaomba Wabunge wote, tuna heshima na sifa sawa, kila mtu amjali mwenzake na tusipelekee viongozi wetu kuwapa taharuki kana kwamba kuna jambo baya limetokea mpaka yanatokea maamuzi mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi Mwongozo wangu niliokuwa naomba ni huo. Masuala kama haya je, ni

sahihi yawe yanatokea kienyeji, kienyeji tu humu ndani au tuache kufanya mambo ya aina hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge nilisema nitatoa nafasi kwa Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani na Mheshimiwa Stella Manyanya. Mheshimiwa Amar naona alisimama atakuwa wa mwisho kuzungumza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilichokifanya asubuhi kuomba Mwongozo ni kutokana na Kanuni ambazo tumezipitisha. Iwapo Kanuni hizi hazitafanya kazi tulizileta za nini na kuzipitisha naomba nirejeele nilichokizungumza asubuhi kupitia kanuni tusikilizane vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliomba Mwongozo kwa Kanuni...

**NAIBU SPIKA:** Hiyo kanuni Mheshimiwa Amar ngoja tuelewane vizuri Kanuni ni ya 170 na mimi ninaifahamu, kwa hiyo huna haja ya kusoma wewe eleza tu hoja yako ndiyo nimekupa hizo dakika chache ulisimama muda fulani hivi. Sasa nikaona kwa sababu wanazungumza kuhusu wewe nikupe nafasi uzungumze, huna haja ya kurejea kanuni mimi ninayo hapa naifahamu.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, mzungumzaji Mheshimiwa Ngonyani alichokieleza kwamba nimemdanganya Spika na Mheshimiwa Manyanya ameunga mkono kusema kwamba nimeleta taharuki na maamuzi yakachukuliwa na Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba niseme hivi,...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar nataka niiweke vizuri ili tusingie kwenye mjadala, mimi na wewe.



Nataka kuweka vizuri hivi, hawa wawili wameniomba mimi Mwongozo, hujanisikia mimi nawaongoza vipi katika wale walioomba, sasa ukianza kujibu hoja zao utakuwa ni kama umeshanisikia mimi na wewe si kazi yako kuwajibu. Mimi nitawajibu wao wewe ulitaka kuzungumza na mimi nini alipokuwa amesimama Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa, ni kwamba mimi la kwanza siombi radhi. La pilli, ninarudia kusema hivi kama nimesema uongo hebu hayo mavazi...

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa Amar naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge amesimama Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani nan akasimama pia Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya wote hoja yao ni moja kuhusu jambo lililotokea Bungeni humu leo asubuhi na wametoa maelezo marefu ambayo sina haja ya kurejea kwa sababu sote tumeyasikia wametupeleka kwenye kanuni ya 76 ambayo wanataka kujua kama hilo jambo linaruhusiwa ama haliruhusiwi na wakati wakitoa hayo maelezo yao Kanuni ya 170 ndiyo inayotuongoza.

Lakini Waheshimiwa Wabunge, Kanuni yetu ya 76 huwa inatoa nafasi kwa Spika kutoa Mwongozo wakati huo huo ama baadaye. Ninyi mtakumbuka Kanuni yetu hii ya 170 ukiisoma inatarajia kwamba hapa mbele lazima yule anayetaarifiwa awe na yeye ameona halafu amejiridhisha.

Kwa hiyo, Mwongozo huu ulioombwa na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi na Mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Stella Manyanya lazima mimi nikajiridhishe kwa mujibu wa Kanuni zetu na Kanuni ya 170 kama huyu Mbunge alikuwa amevunja hiyo Kanuni ama hajavunja ndipo mwongozo huo utakapotolewa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nadhani hilo mmelielewa vizuri. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 01:40 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 2 Juni, 2021 Saa Tatu Kamili Asubuhi)*